

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Moja – Tarehe 4 Mei, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

#### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH -KATIBU MEZANI:**

#### TAARIFA YA SPIKA

Kwa mujibu wa Kanuni ya 33(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, Waheshimiwa Wabunge kwa masikitiko makubwa Mheshimiwa Spika anapenda kuwalishwa kuwa Bunge letu limepatwa na msiba mwingine mkubwa wa kuondokewa na Mbunge na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga ambaye alifariki alfajiri ya kuamkia siku ya Ijumaa tarehe 1 Mei, 2020 Jijini Dodoma na kuzikwa tarehe 2 Mei, 2020 nyumbani kwake Tusamaganga, Iringa.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na mengi mazuri na muhimu aliyoafanya marehemu Mheshimiwa Balozi Mahiga mwaka 2003 mpaka 2010 akiwa Balozi wa Kudumu wa Tanzania katika Umoja wa Mataifa, alirejesha heshima ya Tanzania hadi kuwa moja ya nchi zilizounda Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa na yeze kuwa Mkuu wa Ujumbe wa Tanzania katika Baraza hilo.

Waheshimiwa Wabunge naomba sasa tusimame kwa muda wa dakika moja kama ishara ya kuomboleza kifo cha mwenzetu.

*(Hapa Wabunge walismama kwa dakika moja  
kuomboleza kifo cha  
Mhe. Balozi Dkt. Augustine Phillip Mahiga)*

**NAIBU SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Tukae. Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH -KATIBU MEZANI:**

#### **HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Hayupo. Katibu!

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH -KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 192

**Ujenzi wa Maabara za Shule – Hanang**

**MHE. DKT. MARY M. NAGU** aliuliza:-

Mwaka 2013 – 2015 Serikali ilihamasisha wananchi kujenga vyumba vya maabara katika shule mbalimbali Wilayani Hanang lakini hadi sasa maabara hizo hazijakamilika.

Je Serikali ipo tayari kutoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa maabara hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ipo tayari kuunga mkono jitihada za wananchi katika ukamilishaji wa ujenzi wa maabara za shule za sekondari kwa ajili ya masomo ya sayansi. Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/2021, Serikali imeidhinishiwa shilingi bilioni 42 kwa ajili ya ukamilishaji wa maabara zilizojengwa kwa nguvu za wananchi. Kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Hanang imeidhinishiwa Shilingi milioni 210 ambazo zitatumika kukamilisha maabara saba.

Na. 193

**Kuboresha Miundombinu ya Elimu Rufiji**

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA** aliuliza:-

Shule nyingi katika Wilaya ya Rufiji zimechakaa kwani nyingi zilijengwa wakati wa Mkoloni.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati shule hizo?

(b) Je, ni lini Serikali itaboresha miundombinu ya shule za Sekondari Muhoro na Ikwiriri ili ziwe za kidato cha Tano na Sita?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuzikarabati shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji ambapo katika mwaka wa fedha 2017/2018 Halmashauri ilipatiwa kiasi cha Shilingi milioni 259 kwa ajili ya ukarabati wa Shule ya Sekondari Utete.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 na 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imepatiwa kiasi cha Shilingi milioni 256 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili (2), matundu 10 ya vyoo na kukamilisha maboma nane (8) ya madarasa katika Shule ya Sekondari Muhoro. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Halmashauri ilipatiwa kiasi cha Shilingi milioni 60 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vitatu (3) vya madarasa katika Shule ya Sekondari Ikwiriri. Miundombinu hiyo imeboreshwa ili kuziwezesha shule hizo kuanza kudahili wanafunzi wa kidato cha tano.

Na. 194

### **Mji wa Lamadi Kupewa Hadhi ya Mamlaka ya Mji Mdogo**

**MHE. GIMBI D. MASABA** aliuliza:-

Mji wa Lamadi uliopo Wilaya ya Busega Mkoani Simiyu ni mionganoni mwa Miji yenyeye sifa za kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo.

Je, ni lini Serikali itautangaza Mji huo kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gimbi Dotto Masaba, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa miji inayokua kwa kasi ambayo inaweza kupewa hadhi ya Mamlaka za Miji Midogo ikiwemo Mamlaka ya Mji Mdogo wa Lamadi.

Hata hivyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa ni kuendeleza maeneo mapya ya utawala yaliyoanzishwa tayari kwa kuyawekea miundombinu na huduma muhimu ili yaanze kutoa huduma kwa wananchi kabla ya kuanzisha maeneo mapya ya utawala.

Na. 195

### **Serikali Kupunguza Kodi ya Huduma**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza Kodi ya Huduma (*Service Levy*) kutoka 0.03 na kuwa 0.01 ili kuleta unaafuu kwa wafanyabiashara nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ushuru wa huduma (*Service Levy*) unaotozwa kwa Mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Kifungu cha 6(u) na 7(z). Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Halmashauri zina hiari na uwezo wa kupanga kiwango cha Ushuru wa Huduma kisichozidi Asilimi 0.3 (*not exceeding 0.3 %*). Hivyo, Sheria imetoa mwanya wa kupunguza ushuru huo kulingana na mazingira ya biashara, uzalishaji na ulipaji wa kodi katika Halmashauri husika.

Na. 196

**Mafunzo ya Afya ya Uzazi Salama**

**MHE. SABREENA H. SUNGURA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawafikia Mama wa Tanzania kote kwa kuwapa mafunzo dhidi ya Afya ya Uzazi Salama?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE  
NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika juhudzi za kuboresha huduma za afya ya uzazi, ni muhimu sana wanawake wote, hasa walio katika umri wa kuzaa, miaka 15 hadi 49 wapate elimu ya afya ya uzazi salama. Mafunzo haya hujumuisha, uzazi wa mpango, umuhimu wa kuhudhuria kliniki wakati wa ujauzito, huduma za dharura kwa matatizo yatokanayo na uzazi, magonjwa ya zinaa, virusi vya UKIMWI/VVU na madhara ya madawa ya kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Afya imeendelea kutoa mafunzo ya uzazi salama kwa kupitia njia mbalimbali ikiwemo vipeperushi na mabango, vipindi vyta redio na televisheni. Katika kipindi cha Januari hadi Juni, 2019, Wizara imeweza kutumia njia hizo za kuelimisha na kutoa mafunzo na kuwafikia jumla ya wanawake 1,480,900 Tanzania Bara. Kupitia mafunzo haya, Idadi ya akinamama wanaojifungulia katika vituo vyta kutolea huduma imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 83 mwezi Machi, 2020 ikilinganishwa na asilimia 64 kwa kipindi kama hicho mwaka 2015/2016

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Wizara ni kuwa, kufikia mwaka 2020, kila mwanamke aliye katika umri wa kujifungua atakuwa amefikiwa na elimu hii. Elimu hii itasaidia akinamama kuhudhuria kliniki mapema mara tu wanapogundua ni wajawazito na pia kujifungulia katika vituo vyta kutolea huduma ili waweze kuhudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi.

Na. 197

### **Ufanisi wa Sospa Kuzuia Udhaililishaji kwa Mtoto wa Kike**

**MHE. JANET Z. MBENE** aliuliza:-

Hivi karibuni limejitokeza suala lililozua mjadala mkubwa kuhusu wanafunzi kupata mimba na kusababisha kukatisha masomo yao, mwaka 1998 Bunge lilipitisha Sheria maalum ya makosa ya kujamiihana (*SOSPA*) ambayo ilibadili sheria kadhaa na kuweka sheria inayoshughulikia makosa ya udhalilishaji wa kingono na wa kijinsia iliylenga kurudisha heshima, usalama na hadhi ya wanawake na watoto.

(a) Je mpaka sasa ni watu wangapi walioitiwa hatiani na kufungwa kifungo kilichoainishwa kwenye sheria hiyo?

(b) Je kati ya watu waliofungwa watu wazima ni wangapi na wanafunzi waliowapa mimba wanafunzi wenzao ni wangapi na wako wapi kwa sasa?

(c) Je kati ya watoto waliopo shuleni na ambao hawapo shuleni, ni wangapi waliobakwa au kurubuniwa na wangapi waliofanya nao mapenzi kwa hiari?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Zebedayo Mbene, Mbunge wa Ilaje, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa jumla ya watuhumiwa 456 wamekwishatiwa hatiani, kwa makosa hayo, kwa mujibu wa Sheria ya SOSPA na kufungwa kwa makosa hayo kwa mujibu wa sheria hiyo.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, watu wazima ni 373 na wanafunzi wallowapa mlimba wanafunzi wenzao ni 83.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Takwimu za hivi karibuni zinaonyesha kwamba katika kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba, 2019 jumla ya wanafunzi 2,839 walipewa mimba na wanafunzi 1,244 walirubuniwa na kukatizwa masomo yao. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2020, jumla ya watoto 892 walibakwa na 133 walirubuniwa na kukatizwa masomo yao

Mheshimiwa Naibu Spika, kesi zote hizo zipo katika hatua mbalimbali za kisheria ambapo zingine zimekwishahukumiwa na zingine zipo katika hatua mbalimbali za kiupelelezi.

Na. 198

**Hofu ya Maradhi ya Mlipuko kwa Wasafiri Wanaopita  
Katika Bandari Zetu**

**MHE. HAJI KHATIBU KAI** aliuliza:-

Mamlaka za Bandari ile ya Zanzibar na ya Tanzania Bara zinafanya kazi kwa ukaribu sana kwa vyombo vya mizigo vya majini na vile vinavyobeba abiria.

Je, inapotokea hofu ya maradhi ya mlipuko/kuambukiza ndani ya nchi au nje ya nchi yetu Mamlaka hizi zinajipangaje kwa abiria wanaopita katika bandari zetu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Haji Khatibu Kai, Mbunge wa Micheweni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) na Shirika la Bandari la Zanzibar (*ZPC*) zinafanya kazi kwa ukaribu sana katika kuhudumia vyombo vya mizigo na vile vinavyobeba abiria katika usafiri wa njia ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kushabihiana kwa shughuli za utoaji wa huduma, Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Zanzibar zimekuwa kiungo kikubwa cha usafiri wa abiria na mizigo kwa njia ya maji kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na magonjwa ya mlipuko/kuambukiza kama ilivyo sasa kwa ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu (*COVID-19*), *TPA* na *ZPC* wanatumia Kanuni na Miongozo mbalimbali iliyowekwa na Shirika la Afya Dunia (*International Health Regulation-2005*). Kwa kuzingatia miongozo hiyo, abiria anayepanda au kushuka katika meli hupimwa joto la mwili. Aidha, orodha ya abiria yenye taarifa za uchunguzi wa awali hutumwa kwa Maafisa Afya waliopo katika Bandari, meli inapokusudia kutia nanga.

Aidha, maeneo maalum (*isolation area*) yametengwa kwa ajili ya kumhifadhi na kumpa huduma ya kwanza abiria atakayehisiwa kuwa na ugonjwa wa mlipuko na baadaye kuhamishiwa katika vituo maalum vilivyoandalialiwa na Serikali.

Na. 199

### **Kusaidia Wakulima wa Pamba Nchini**

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI** aliuliza:-

Zao la Pamba limekuwa likikumbwa na changamoto ya bei na pembejeo mwaka hadi mwaka"-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima ambaao badala ya zao kuwaaletea tija kiuchumni limeendelea kuwatia umaskini kutokana na gharama za uzalishaji pamoja na huduma za ugani?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mbunge wa Jimbo la Busega, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inachukua hatua mbalimbali kutatua changamoto za bei, pembejeo na huduma za ugani zinazowakabili wakulima wa zao la pamba nchini ili kuwaondolea umaskini. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mfumo wa uzalishaji wa mbegu bora za pamba katika maeneo ya Igunga na Kasekese katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika Mkoani Katavi na kusajili wakulima wote wa pamba kwa ajili ya kurahisisha uratibu na kuwawezesha kupata pembejeo za zao la pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuratibu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wa pamba kwa kuagiza viuadudu kwa mfumo wa pamoja. Mfumo huo utasaidia kupatikana kwa viuadudu kwa wingi, vyenye ubora wa hali ya juu, kwa wakati na vyenye bei nafuu ili kuongeza uzalishaji na tija. Hadi kufikia mwezi Desemba 2019, jumla ya tani 31,955 za mbegu za pamba zimesambazwa kwa wakulima katika Wilaya zote zinazolima pamba na pia, hadi Mwezi Machi, 2020 chupa za

viuadudu 2,454,602 kati ya lengo la chupa 4,000,000 zimekwishasambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kupanua wigo wa utoaji wa huduma za ugani kwa kufundisha Wakulima Wawezeshaji (*Lead Farmers*) 4,532 na kuwajumuisha na Mtandao wa Maafisa Ugani uliopo ili kuwafikia wakulima wengi katika maeneo yao. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na wabia wa maendeleo wameendelea kuboresha huduma za ugani kwa kuwapatia usafiri wa pikipiki Maafisa Ugani 27 na magari kwa Maafisa Ugani 13 wa Bodi ya Pamba waliopo katika wilaya zinazozalisha zao la pamba ili kuboresha utoaji huduma za ugani kwa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matarajio ya Serikali kuwa Juhudi zote hizo zitapunguza gharama za uzalishaji na kuongeza tija kwa zao la pamba kutoka kilo 300 hadi kufikia kilo 1,000 kwa ekari na hivyo kupunguza umaskini kwa wakulima wa pamba.

Na. 200

### **Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria Kufika Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Mradi wa maji Ziwa Victoria umeshafika Nzega Mjini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza mradi huo hadi Bukene ili wananchi wa Mji wa Bukene na vijiji ambavyo bomba linapita wapate maji ya uhakika na ya kutosha?

**WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijiji (RUWASA) imeshakamilisha usanifu wa Mradi wa Maji kutoka tanki la maji lililopo Ushirika, Nzega Mjini, kwenda Mji wa Bukene na vijiji vingine 18 ambavyo bomba litapita na katika Vijiji ya Shila, Kagongwa, Shigamba, Itobo, Lakuyi, Chamwabo, Kabanga, Uduka, Usongwanhala, Kayombo, Mwamala, Kishili, Seki, Chaming'hwa, Kasela, Senge, Lububu na Udotu vilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu unatarajiwa kugharimu jumla ya Sh.10,169,540,224.22 na utakapokamilika unatarajiwa kuwanufaisha jumla ya wananchi 88,597 ifikapo mwaka 2035 wa Mji wa Bukene na vijiji 28 vilivyotajwa hapo juu. Utekeleza wa mradi huu umepangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Na. 201

**Wazawa Kuwekeza Kwenye Sekta ya  
Madini Nchini**

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA** aliuliza:-

Nchi imebarikiwa kuwa na aina nyingi sana za madini tena kwa kiwango kikubwa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wazawa kuwekeza kwenye sekta hiyo ili faida itokanayo na rasilimali hiyo ibaki nchini?

**WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa GoodLuck Asaph Mlingwa, Mbunge wa Jimbo la Ulanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kama Msimamizi Mkuu wa shughuli zote za maendeleo ya Sekta ya Madini nchini inawajibika kuandaa Sera na Sheria nzuri ya Madini ili

kuwezesha wazawa kuwekeza kwenye fursa za madini na kuchangia katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Madini ya 2009 inahimiza juu ya Ushiriki wa Serikali na Watanzania katika shughuli za uchimbaji madini. Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwasaidia na kuwaendeleza wachimbaji wadogo ikiwa ni pamoja na kuwapatia elimu ya kutambua fursa zilizopo, kutambua fursa za mikopo ya fedha na vifaa, kutenga na kugawa maeneo kwa ajili ya uchimbaji mdogo na kujenga vituo vyta mfano katika baadhi ya maeneo ya uchimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 ilifanyiwa marekebisho mwaka 2017 ili kuongeza wigo wa wazawa kushiriki katika shughuli za Sekta ya Madini. Kifungu cha 8(2) cha Sheria hiyo kinatamka wazi kuwa atakayepewa Leseni ya uchimbaji mdogo lazima awe Mtanzania na iwapo ni kampuni yenye mchanganyiko na wageni Wakurugenzi wake wote wawe ni Watanzania.

Aidha, Katika madini ya vito kama *Tanzanite* kwa sasa leseni zinatolewa kwa Watanzania tu na pale ambapo kutakuwa na uhitaji wa teknolojia ya hali ya juu katika kuchimba madini hayo kampuni yenye mchanganyiko na wageni watapewa leseni kwa umiliki wa asilimia 50 kwa 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Marekebisho ya Sheria ya Madini ya Mwaka 2017, kila mmiliki wa Leseni anapaswa kuandaa na kuwasilisha Tume ya Madini Mpango wa Manunuzi ya bidhaa na Matumizi ya huduma zipatikanazo nchini. Vilevile, wamiliki wa Leseni wanapaswa kuwasilisha Mpango wa Utoaji Huduma kwa Jamii (*CSR*) uliokubalika na kuidhinishwa na Halmashauri husika kwa kila mwaka. Hatua hizi zinalenga kuongeza manufaa ya uchimbaji kwa Watanzania.

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. RAMADHAN ISSA ABDALLAH – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimuite Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Isaac Kamwelwe.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuwasilisha hotuba yangu, naomba nifanye marekebisho kidogo ya mtiririko wa uwasilishaji. Wakati *main text* imeanza na Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, muhtasari wangu utaanza na Sekta ya Mawasiliano, itakwenda Uchukuzi na baadaye itakwenda kwenye Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utangulizi. Kufutia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano wa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, kwa mara nyingine, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote kwa ujumla wetu hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na hivyo kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa na wa mwisho wa Bunge la Kumi na Moja ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na kujadili Mpango na Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupatia ulinzi wake dhidi ya janga linalosumbua dunia kwa sasa la mlipuko wa ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu inayosababishwa na virusi vya *Corona* (*COVID- 19*).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Bunge lako Tukufu lilipatwa na simanzi kubwa kufuatia vifo vya wapendwa wetu ambao ni Mheshimiwa Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijiji; Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare (Mbunge wa Viti Maalum); Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve; na Mheshimiwa Augustine Philip Mahiga aliyekuwa Mbunge wa Kuteuliwa na Waziri wa Katiba na Sheria. Nachukua fursa hii kutoa pole kwako wewe binafsi na familia za marehemu hao, Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na viongozi na wanasiasa hao wakongwe na mahiri. Mwenyezi Mungu aziweke roho na marehemu hao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu wa marehemu na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania kwa msiba mkubwa wa wafanyakazi watano waliopoteza maisha na mmoja kujueruhwa katika ajali iliyotokea eneo la Mwakinyumbi na Gendagenda ambapo treni illigongana na kiberenge; wananchi 104 waliopoteza maisha kutokana na moto uliosababishwa na lori la mafuta Mjini Morogoro; na ajali ya lori kugongana na basi la abiria eneo la Mkuranga-Pwani ambapo abiria 21 walipoteza maisha na 14 kujueruhwa. Aidha, nawapa pole wote waliofikwa na majanga ya kupoteza ndugu zao kufuatia mvua zilizonyesha kupita kiwango katika maeneo mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka majeruhi wote na aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima na taadhima, naomba uniruhusu kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya

Muongano wa Tanzania kwa kusimamia utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 kwa umakini mkubwa na hivyo kuendelea kuiongoza nchi yetu kuwa na amani na utulivu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchanguliwa kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (*SADC*) pamoja na kuiongoza vyema Jumuiya hiyo hususani katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu inayosababishwa na virusi vya *Corona*. Vilevile nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabitii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano naoendelea kuupata wakati wote napotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu sekta ninazozisimamia. Napenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya kisekta na kitaifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kwa namna ya kipekee, naomba kuwashukuru wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Katavi na familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mbunge), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira); Mheshimiwa George Boniface Tabulavala Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba, Waziri wa Katiba na Sheria kwa kuteuliwa kwao kuwa Mawaziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge

wa Jimbo la Singida Mashariki na Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arusha Mashariki kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini katika mwaka wa fedha 2019/2020. Ushindi wao wa kishindo ni kielelezo tosha cha kuonyesha namna Chama cha Mapinduzi kinavyoendelea kuaminika na kupendwa na Watanzania. Vilevile, nampongeza Dkt. Zainab Abdi Sarafina Chaula kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa sekta ya Mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, napenda kuichukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Mbunge wa Jimbo la Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo Mheshimiwa hawa Mchafu Chakoma. Nakiri kuwa, Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mwasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuwasilisha hotuba hii, napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya sekta ya kijamii na kiuchumi kwa mwaka 2019/2020 na mwelekeo kwa mwaka 2020/2021. Nawashukuru na kuwapongeza pia Mawaziri wote walilowasilisha hotuba zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika utekelezaji wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Mwasiliano - Fungu 68, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Sekta ya Mwasiliano ilitengewa kiasi cha Sh.3,973,197,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh.2,047,259,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Sh.1,925,938,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 Sh.3,021,554,809.24 zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, Sh.1,457,738,432 zimetolewa kwa ajili ya mishahara na Sh.1,563,816,377.24 zimetolewa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi illidhinishiwa jumla ya Sh.3,629,130,373,895. Kati ya fedha hizo, Sh.85,408,131,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.3,543,722,242,895 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kilichotolewa ni Sh.53,404,102,071.14 sawa na asilimia 62.5 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, jumla ya fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa hadi mwezi Machi, 2020 ni Sh.1,464,673,641,683 sawa na asilimia 41.3 ya bajeti ya mwaka 2019/2020. Utumiaji wa fedha zilizoidhinishwa uliathiriwa na mvua kubwa zilizonyesha zaidi ya kiwango kuanzia mwezi Oktoba, 2019 ambapo zilisababisha kazi ya ujenzi wa reli ya *SGR* na ukarabati wa reli ya kati ya *Metergauge Railway* kusimama mara kwa mara kutokana na mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi - Fungu 98. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Sekta ya Ujenzi - Fungu 98 ilitengewa kiasi cha Sh. 36,264,751,504.04 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, Sh.33,788,265,000 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa sekta na taasisi zake na Sh.2,476,486,544.04 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara Sekta ya Ujenzi na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, bajeti ya matumizi ya kawaida imeongezewa wigo kutoka Sh.36,142,664,000 hadi Sh.36,264,751,504.04 sawa na ongezeko la Sh.122,087,544.04. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madai ya wazabuni mbalimbali ambayo yamehakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi mwezi Machi, 2020 jumla ya Sh.24,128,094,762.08 zilikuwa zimetolewa na Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 66.53 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo, Sh.22,111,449,258.04 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Sh.2,016,645,504.04 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya miradi ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Ujenzi ilitengewa shilingi 1,294,051,604,268.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 990,000,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 304,051,604,268.00 zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali Consolidated Fund shilingi 402,611,000,000.00 na fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zilikuwa shilingi 587,389,000,000.00. Aidha, Bajeti ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo imeongezewa wigo kutoka shilingi 990,000,000,000.00 hadi shilingi 1,713,862,494,259.91 sawa na ongezeko la shilingi 723,862,494,259.91. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni na madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri yaliyohakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya barabara ni shilingi 2,017,914,098,527.91.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi Machi, 2020 fedha zilizopokelewa ni shilingi 1,663,224,452,809.45. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,387,232,923,133.44 ni fedha za ndani na shilingi 277,991,529,676.01/275,991,529,676.01 ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizopokelewa zinajumuisha shilingi 936,146,859,501.27 kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na Shilingi bilioni 451,086,063,632.17 ni fedha za Mfuko wa Barabara.

Kwa ujumla, hadi kufikia Machi, 2020 fedha za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia 82.42 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ilani ya CCM ya mwaka 2015, kuhusu Sekta ya Mawasiliano Serikali imeweza kufikisha huduma za mawasiliano katika kata 703 zenye vijiji 2,501. Kwa ruzuku ya takribani shilingi bilioni 118. Vilevile, Serikali imejenga vituo vya kijamii vya kutoa huduma za TEHAMA, vikiwemo vituo 10 Zanzibar na vituo 8 Tanzania Bara. Aidha, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka laini milioni 39 mwaka 2015 hadi laini milioni 43 Machi, 2020 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka milioni 9 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 25 mwezi Machi, 2020. Pia watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenye tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Mkongo wa taifa wa mawasiliano Awamu ya Tatu ulikamilika June 2016, ukijumuisha ujenzi wa kituo cha Taifa cha Data cha Dar es Salaam ungwanishwaji wa Zanzibar kwenye Mkongo wa Taifa pamoja na upanuzi wa mkongo uliojengwa Awamu ya Kwanza na Pili. Aidha, kuititia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na watoa huduma binafsi, miundombinu ya Mkongo imefikishwa kwenye Ofisi za Halmashauri za Wilaya 150, Hospitali za Wilaya 150, Vituo vya Polisi 121, Vituo vya Posta 65, Mahakama 25 na kutoa huduma ya internet bure kwenye Shule za Sekondari 455.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilinunua mkondo wa mawasiliano kwa lugha ya kigeni bandwidth unayotumika katika taasisi mbalimbali za Serikali nchini kwa lengo la kupanua wigo ya matumizi ya TEHAMA hadi maeneo ya vijiji. Pia Serikali imeunganisha mifumo ya Serikali imeunganisha mifumo ya mikutano mtando video Conference Systems vilivyo unganishwa katika Mkongo wa Taifa ambapo vituo 45 vilivyounganishwa katika mikoa ya Tanzania bara na

Zanzibar. Vilevile, utekelezaji wa mradi wa shule mtandao e-Schools ambao unatekeleza mpango wa Taifa wa kuunganisha shule jumla ya shule za Sekondari za sekondari za Serikali 129 na shule za msingi 250 zilipatiwa vifaa vya TEHAMA nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2015/2020, yалиhusu ujenzi na uboreshaji wa bandari na kusafiri katika maziwa miundombinu na huduma za Reli, huduma za viwanja vya ndege na usafiri wa anga na huduma za hali ya hewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Dar es Salaam, Serikali imekamilisha ujenzi wa jengo la ghorofa 35 kwa ajili ya kuwaweka pamoja wadau wanaotoa huduma za kibandari. Aidha, kazi ya uboreshaji wa gati namba 1 – 4 na gati la kushusha magari (RoRo) imekamilika. Kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala (Ruvu), umekamilika kwa asilimia 45, ujenzi wa Bandari ya Nyamisati, ukarabati wa gati la kuhudumia mizigo ya Mwambao, ukarabati wa Mnara wa Kuongozea Meli, uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kisasa, mashine za kukagua mizigo scanners na Ununuzi wa Mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bandari ya Tanga kazi zilizofanyika ni ukarabati wa magala na gati 1 na 2, kuongeza kina lango la kuingilia bandarini, ujenzi wa gati la pangani na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo. Aidha kwa upande wa bandari ya Mtwara kazi ya ujenzi wa uazio sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 600 zimekamika na ujenzi wa gati kubwa lenye urefu wa mita mia 300 umekamilika kwa asilimia 61.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma katika maziwa ilani ya CCM imetekeliza kwa kukamilisha ujenzi wa magati ya Lushamba, Mtama, Magarini, Mwingobero, na Nyamilembe katika Ziwa Victoria gati la Kabunga katika Ziwa Tanganyika na Bandari za Kiwila na Itungi katika ziwa nyasa pamoja na kununua vifaa vya kuhudumia mizigo. Aidha katika kuboresha huduma za usafiri

katika maziwa Serikali imekamilisha ujenzi wa hatishari mbili zenye uwezo wa kubeba tani za shehena 1,000 kila moja na meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 355 na 200 za mizigo katika ziwa nyasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa Chelezo na ukarabati wa meli za MV Victoria, MV, Butiama, MV Clarias na M-Eliwimbi katika ziwa Victoria na ukarabati wa MV Sangara katika ziwa Tanganyika. Vilevile, ujenzi wa meli mpya, MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria. Ujenzi wa Meli hii umekamilika kwa asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa huduma za miundombinu ya reli ya katni, kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa reli ya Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kilomita 300 kwa asilimia 76.63 na Morogoro hadi Makutopora kilomita 422 kwa asilimia 28. Ununuzi wa vichwa kumi na moja vya treni ukarabati wa mabehewa 367 upembuzi hakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa SGR kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay kilomita 1,000, Tanga Arusha Musoma kilomita 1023, Kaliwa Mpanda kalema kilomita 360, Tabora hadi Kigoma kilomita 411, Uvinza hadi Msongati, Kilomita 156, Isaka hadi Kigali (km 356) na reli ya Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ukarabati wa reli ya Tanga hadi Moshi (Km 359) umekamilika na huduma zimeanza kutolewa Disemba 2019 na ukarabati wa reli ya Dar es Salaam hadi Isaka (Km 950) umekamilika kwa asilimia 86. Kwa upande wa TAZARA kilichofanyika ni ukarabati wa vichwa vipyta vinne (4) vya Treni ya njia kuu, vichwa vinne (4) vya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, ukarabati wa mabehewa 400 ya mizigo, uboreshaji wa Kituo cha Reli ya Mfuga na nyumba Nyumba nane (8) za watumishi kwa ajili ya kuhudumia Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kuititia wizara yangu imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu

ya barabara na madaraja kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo ni kujenga barabara zetu zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani, kujenga barabara zinazounganisha mikoa kwa kiwango cha lami, na kujenga barabara zinazokwenda kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi. Katika kipindi hicho barabara zenye urefu wa wa kilo mita 2,624.27 zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Aidha katika kipindi hicho jumla ya kilomita 82.6 za barabara za kupunguza msongamano kwenye majiji yetu zimejengwa kwa kiwango cha lami na barabara kuu zenye urefu wa kilomita 1,298.44 zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile, ukarabati wa barabara kuu zenye urefu wa kilomita 300.9 umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, jumla ya madaraja makubwa 13 yalikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Kati ya hatua hizo, madaraja makubwa nane yamekamilika, ambayo ni Daraja la Magufuli, Magara, Mlalakuwa, Momba, Lukuledi II, Mara, Sibiti na Daraja la Nyerere. Aidha, madaraja makubwa matano yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambayo ni Daraja Jipya la Selander, Mfingi, Wami, Kitengule na Ruhuhu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja makubwa nane ya Kigongo – Busisi, Sukuma, Simiyu, Mkenda, Mtera, Godegode, Malagarasi Chini na Ugalla yako kwenye hatua mbalimbali za maandalizi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nisije nikapigiwa kengengele nyingine naomba sasa nitoe taarifa ya mpango na makadirio ya mapato ya matumizi ya fedha kwa sekta ya wizara kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kwasababu ya muda nianze na shukrani.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ninayoiongoza nikianza na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa Mb Naibu Waziri (Ujenzi); Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye (Mb.), Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano); Makatibu Wakuu: Mbunifu Majengo Elius Asangalwisye

Mwakalinga (Ujenzi); Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho (Uchukuzi); Dkt. Maria Leticia Sasabo (Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano amestaafu) pamoja na Dkt. Jim James Yonaz, Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano). (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipa na juhud walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa ipasavyo. Ushirikiano wao ndio uliowezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu katika mwaka uliopita. Naomba waendeleze na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutimiza malengo tulioopangiwa na tuliojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukuwe nafasi hii kuwashukuru wafadhili wote ambao wametusupport katika mipango yetu yote ya maendeleo. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ([www.mwtc.go.tz](http://www.mwtc.go.tz)).

Mheshimiwa Naibu Spika, muhtasari wa maombi ya Fedha ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2020/2021 katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi 4,784,874,417,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,616,361,206,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, Shilingi 3,152,858,745,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na Shilingi 15,654,466,000.00 ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha upo ndani ya kitabu cha mawasilisho ya bajeti yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hotuba hii nimeambatanisha miradi ya wizara itakayotekelawa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kiambatisho namba moja hadi saba ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa

kutekelezwa miradi hiyo naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO,  
MHESHIMIWA ENG. ISACK ALOYCE KAMWELWE (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO  
NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 –  
KAMA ILIVYOWAKILISHWA MEZANI**

#### **A. UTANGULIZI**

- 1. Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa humu Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20. Aidha, kwa mara nyingine ninaomba Bunge lako Tukufu llijadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/21.
- 2. Mheshimiwa Spika**, sisi sote kwa ujumla wetu, hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uhai na afya njema na hivyo kutuwezesha kukutana leo kwa ajili ya kushiriki katika Mkutano huu wa 19 na wa mwisho wa Bunge la 11, ili kujadili utekelezaji wa majukumu ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na kujadili Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Sekta hizo kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, ninamuomba Mwenyezi Mungu aendelee kutupatia ulinzi wake dhidi ya janga linaloisumbua dunia kwa sasa la mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID -19).

- 3. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bunge lako Tukufu liliapatwa na simanzi kubwa kufuatia vifo vya wapendwa wetu amba ni Mhe. Rashid Ajali Ahkbar

aliyekuwa Mbunge wa jimbo la Newala Vijijini, Richard Mganga Ndassa aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Sumve na Mhe. Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, Mbunge wa Viti Maalum. Ninachukua fursa hii kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika, Familia za Marehemu hao, Bunge lako Tukufu, Wananchi wa Jimbo la Newala Vijijini na Watanzania kwa ujumla kwa kuondokewa na wanasiasa hao wakongwe na mahiri. Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

**4. *Mheshimiwa Spika*,** nitumie fursa hii kuwapa pole ndugu wa marehemu na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) kwa msiba mkubwa wa wafanyakazi watano (5) waliopoteza maisha na mmoja kujeruhiwa katika ajali iliyotokea eneo la Mwakinyumbi na Gendagenda ambapo treni iligongana na kiberenge, wananchi 104 waliopoteza maisha kutokana na moto ullosababishwa na lori la mafuta mjini Morogoro, ajali ya lori kugongana na basi la abiria eneo la Mkuranga - Pwani ambapo abiria 20 walipoteza maisha na 15 kujeruhiwa. Aidha, ninawapa pole wote walififikwa na majanga ya kupoteza ndugu zao kufuatia mvua zilizonyesha kupita kiwango katika maeneo mbalimbali nchini. Mwenyezi Mungu awape nafuu ya haraka majeruhi wote na aziweke roho za marehemu hao mahali pema peponi. Amina.

**5. *Mheshimiwa Spika*,** kwa heshima na taadhima ninaomba uniruhusu kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 kwa umakini mkubwa na hivyo kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa amani na utulivu. Aidha, ninampongeza Mhe. Rais kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyezeki wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) pamoja na kuiongoza vyema Jumuiya hiyo hususan katika kipindi hiki cha mlipuko wa ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID -19). Vilevile, ninawapongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wao thabiti.

**6. Mheshimiwa Spika**, ninaomba nikupongeze wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, Katibu wa Bunge, Watendaji wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano ninaoendelea kuupata wakati wote ninapotekeleza majukumu yangu ikiwa ni pamoja na kuwasilisha taarifa mbalimbali kuhusu sekta ninazozisimamia. Ninapenda kuwahakikishia kuwa, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kufikia malengo ya Kisekta na Kitaifa kwa ujumla. Vilevile, kwa namna ya pekee ninaomba kuishukuru familia yangu na wapiga kura wa Jimbo langu la Uchaguzi la Katavi kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika kutekeleza majukumu yangu kwa Watanzania.

**7. Mheshimiwa Spika**, nitumie pia fursa hii kuwapongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) na Mhe. George Boniface Taguluvala Simbachawene (Mb), Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kuteuliwa kuwa Mawaziri. Aidha, ninapenda kutoa pongezi kwa Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki na Mhe. John Danielson Pallangyo, Mbunge wa Jimbo la Arumeru Mashariki kwa kuchaguliwa kuwa Wabunge katika chaguzi ndogo zilizofanyika nchini katika mwaka wa fedha 2019/20. Ushindi wao wa kishindo ni kielelezo tosha cha kuonyesha namna Chama cha Mapinduzi kinavyoendelea kuaminika na kupendwa na Watanzania. Vilevile, ninapongeza Dkt. Zainab Abdi Seraphin Chaula kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano.

**8. Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, ninapenda kuchukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mhe. Seleman Moshi Kakoso (Mb), Mbunge wa Mpanda Vijijini na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mhe. Hawa Mchafu Chakoma (Mb). Nakiri kuwa Wizara imenufaika sana na umahiri, umakini na ushirikiano wa Kamati hiyo katika kuchambua, kushauri na kufuatilia maendeleo ya Sekta za Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ninapenda kiliarifu Bunge lako Tukufu kwamba maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yamezingatiwa katika Bajeti hii.

**9. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuwasilisha Hotuba hii, ninapenda kuwashukuru Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba zao zilizotangulia. Hotuba hizo zimeeleza kwa ujumla maendeleo ya sekta za Kijamii na Kiuchumi kwa mwaka 2019/20 na mwelekeo kwa mwaka 2020/21. Ninawashukuru na kuwapongeza pia Mawaziri wote waliowasilisha hotuba zao.

**10. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mipango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/20 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2020/21. Aidha, kabla ya kuelezea utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/20, ninapenda nitoe kwa muhtasari taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015' kwa kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano.

#### **B. UTEKELEZAJI WA MALENGO YALIYOAINISHWA KATIKA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2015 KWA KIPINDI CHA MWAKA 2016/17 – 2019/20**

##### **B-1 SEKTA YA UJENZI**

**11. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Serikali kuitia Wizara yangu imepata mafanikio makubwa katika kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja kwa kuzingatia vipaumbele ambavyo ni; Kujenga barabara zetu zinazounganisha nchi yetu na nchi jirani, kujenga barabara zinazounganisha mikoa kwa kiwango cha lami na kujenga barabara zinazokwenda kwenye maeneo yenye fursa za kiuchumi. Katika kipindi hicho, barabara zenye urefu wa jumla ya kilometra **2,624.27** zimejengwa na kukamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, jumla ya kilometra **82.6** za barabara za kupunguza msongamano wa magari katika miji zimejengwa kwa kiwango cha lami na barabara kuu zenye

urefu wa kilometra **1,298.44** zinaendelea kujengwa kwa kiwango cha lami. Vilevile, ukarabati wa barabara kuu zenye urefu wa kilometra **300.9** umekamilika.

**12. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, jumla ya **madaraja makubwa** 13 yalikuwa katika hatua mbali mbali za utekelezaji. Kati ya hayo, madaraja makubwa **nane (8)** yamekamilika, ambayo ni Daraja la Magufuli, Magara, Mlalakuwa, Mombasa, Lukuledi II, Mara, Sibiti na Daraja la Nyerere (Kigamboni). Aidha, **madaraja makubwa matano (5)** yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi, ambayo ni Daraja Jipya la Selander, Msingi, Wami, Kitengule na Ruhuhu. **Madaraja makubwa nane (8)** ya Kigongo – Busisi, Sukuma, Simiyu, Mkenda, Mtera, Godegode, Malagarasi Chini na Ugalla yako kwenye hatua mbalimbali za maandalizi ya kazi za ujenzi.

**13. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa **kilometra 4,856** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara kuu na za mikoa pamoja na madaraja mapya **12**. Aidha, upembuzi yakinifu wa kilometra **452.3** kwa ajili ya ukarabati wa barabara kuu na za mikoa kwa kiwango cha lami ulikamilika. Vilevile kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa jumla ya **kilometra 3,653.13** upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**14. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu iliendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Viwanja vya ndege vilivyokamilika ni: Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) pamoja na ukarabati na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza. Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato upo katika hatua ya maandalizi ya kuanza utekelezaji. Aidha, Viwanja vya Ndege vya Songea, Kigoma, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, Iringa na Musoma vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Vilevile, kati ya viwanja kumi na moja (11) vilivyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, viwanja **vinne (4)** vya Songea, Musoma, Moshi na Iringa vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa Viwanja **saba (7)** vilivyobaki. Viwanja hivyo ni:

Lindi, Kilwa Masoko, Singida, Tanga, Simiyu, Lake Manyara na Njombe.

**15. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 hadi 2020, Wizara yangu imekamilisha kununua jumla ya vivuko **vitatu (3)** ambavyo ni MV Tanga (Pangani – Bweni) mkoani Tanga, MV Kazi (Magogoni – Kigamboni) mkoani Dar es Salaam na MV Mwanza (Kigongo – Busisi) mkoani Mwanza, upanuzi wa Awamu ya kwanza wa Jengo la Abiria upande wa Kigamboni katika kivuko cha Magogoni – Kigamboni, Dar es Salaam. Kwa sasa ununuzi wa Kivuko cha Rugezi – Kisorya pamoja na Awamu ya Pili ya Upanuzi wa Jengo la Abiria upande wa Kigamboni unaendelea.

**16. Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imekamilisha ujenzi wa jumla ya majengo ya ofisi za Serikali **33** zikiwemo zilizojengwa katika mji wa Serikali Mtumba - Dodoma pamoja na nyumba **323** za Watumishi wa Umma katika mikoa mbalimbali. Aidha, ukarabati wa Karakana sita za kutengeneza samani katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Mwanza na Mbeya uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

## B-2 SEKTA YA UCHUKUZI

**17. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi malengo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015-2020 yanahusu ujenzi na uboreshaji wa bandari na usafiri katika maziwa; miundombinu na huduma za reli; huduma za viwanja vya ndege na usafiri wa anga; na huduma za hali ya hewa.

**18. Mheshimiwa Spika**, katika bandari ya Dar es Salaam, Serikali imekamilisha ujenzi wa Jengo la ghorofa 35 kwa ajili ya kuwaweka pamoja wadau wanaotoa huduma za kibandari. Aidha, kazi ya uboreshaji wa gati namba 1 – 4 na gati la kushusha magari (RoRo) imekamilika. Kazi nyingine zilizokamilika ni ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala (Ruvu), ujenzi wa Bandari ya Nyamisati, awamu ya kwanza ya ukarabati wa gati la kuhudumia mizigo ya Mwambao, ukarabati wa Mnara wa Kuongozea Meli, uwekaji wa mfumo wa ulinzi wa kisasa, mashine za kukagua mizigo (scanners) na Ununuzi wa Mitambo ya kuhudumia mizigo bandarini.

**19. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa bandari ya Tanga, kazi zilizofanyika ni Ukarabati wa Maghala na Gati namba 1 na 2; kuongeza kina na lango la kuingilia bandarini, ujenzi wa Gati la Pangani na ununuzi wa mitambo ya kuhudumia mizigo. Aidha, kwa upande wa Bandari ya Mtwara, kazi za ujenzi wa uzio na sakafu ngumu katika eneo la mita za mraba 600 zimekamilika na ujenzi wa gati kubwa lenye urefu wa mita 300 umekamilika kwa asilimia 61.

**20. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa huduma katika maziwa, llani ya CCM imetekelezwa kwa kukamilisha ujenzi wa Magati ya Lushamba, Ntama, Magarini, Mwigobero, na Nyamirembe katika Ziwa Victoria; Gati la Kagunga katika Ziwa Tanganyika; na bandari za Kiwira na Itungi katika Ziwa Nyasa pamoja na kununuzi vifaa vya kuhudumia mizigo. Aidha, katika kuboresha huduma za usafiri katika maziwa, Serikali imekamilisha ujenzi wa Tishari 2 zenye uwezo wa kubeba tani za shehena 1,000 kila moja na meli moja yenye uwezo wa kubeba abiria 350 na tani 200 za mizigo ya katika Ziwa Nyasa; Ujenzi wa Chelezo na ukarabati wa meli za MV. Victoria, MV. Butiama, MV. Clarias na ML. Wimbi katika Ziwa Victoria; na ukarabati wa MT. Sangara katika Ziwa Tanganyika. Vile vile, Ujenzi wa Meli mpya ya MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo umekamilika kwa asilimia 60.

**21. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa huduma na miundombinu ya reli ya Kati, kazi zilizokamilika ni pamoja na ujenzi wa Reli ya Standard Gauge kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) kwa asilimia 76.63 na Morogoro hadi Makutupora (km 422) kwa asilimia 28; ununuzi wa vichwa 11 vipyta vya Treni; ukarabati wa mabehewa 367; Upembusi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa SGR kutoka Mtwara hadi Mbambabay (km 1,000), Tanga – Arusha - Musoma (km 1,023), Kaliua - Mpanda – Karema, Tabora hadi Kigoma (km 411), Uvinza hadi Musongati (km 156), Isaka hadi Kigali (km 356) na reli ya Jijini Dar es Salaam. Aidha, ukarabati wa reli ya Tanga hadi Moshi (Km 359) umekamilika na huduma zimeanza kutolewa Disemba 2019 na ukarabati wa reli ya Dar es Salaam hadi Isaka (Km 970) umekamilika kwa asilimia

86. Kwa upande wa TAZARA iliokamilika ni ununuzi wa vichwa vipyta vinne (4) vya Treni ya njia kuu, vichwa vinne (4) vya sogeza, mabehewa mapya 18 ya abiria, ukarabati wa mabehewa 400 ya mizigo, uboreshaji wa Kituo cha Reli cha Fuga na nyumba Nyumba nane (8) za watumishi kwa ajili ya kuhudumia Mradi mkubwa wa Umeme wa Mto Rufiji.

**22. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa usafiri wa Anga, kazi zilizofanyika ni pamoja na ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania kwa kununua Ndege 11 ambapo Ndege nane (8) zimewasili na zinaendelea kutoa huduma; ufungaji wa Rada nne (4) za kuongozea Ndege, ukarabati wa Mnara wa kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Pemba, ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Julius Nyerere (JNIA), ukarabati wa Jengo la abiria KIA, Ununuzi wa Magari mapya matatu (3) ya Zimamoto, na ufungaji wa Mifumo ya kuongozea Ndege (AGL) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Tabora na Mwanza. Aidha, huduma za hali ya hewa zimeboreshwa kwa ununuzi wa Rada tatu (3) kwa ajili ya kufungwa Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma.

**23. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja vyombo mbalimbali vikiwemo vya Ulinzi na Usalama katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona (COVID - 19) kwa wageni wote wanaoingia nchini.

### **B-3 SEKTA YA MAWASILIANO**

**24. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeweza kufikisha huduma za mawasiliano katika kata **703** zenye vijiji **2,501**. Vile vile, Serikali imejenga vituo vya kijamii vya kutoa huduma za TEHAMA, vikiwemo vituo 10 Zanzibar na vituo 8 Tanzania Bara. Aidha, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka laini milioni 39 mwaka 2015 hadi laini milioni 43 Machi, 2020 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka milioni 9 mwaka 2015 hadi kufikia milioni 25 Machi, 2020.

**25. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Awamu ya III ulikamilika Juni, 2016

ukijumuisha ujenzi wa kituo cha Taifa cha Data cha Dar es Salaam, uunganishwaji wa Zanzibar kwenye Mkongo wa Taifa; pamoja na upanuzi wa Mkongo uliojengwa Awamu ya kwanza na ya pili. Aidha, kupitia utekelezaji wa mradi kwa kushirikiana na watoa huduma binafsi, miundombinu ya Mkongo imefikishwa kwenye Ofisi za Halmashauri za Wilaya 150, Hospitali za Wilaya 150, Vituo vya Polisi 121, Vituo vya Posta 65, Mahakama 25 na kutoa huduma ya intaneti bure kwenye Shule za Sekondari 455, kuanzisha mradi wa shule mtandao (e-Schools) ambao unatekeleza mpango wa Taifa wa kuunganisha shule pamoja na kuunganisha mifumo ya mikutano mtandao (Video Conference Systems) ambapo vituo 43 vimeunganishwa katika mikoa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

## **C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

### **C.1 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KISEKTA**

**26. *Mheshimiwa Spika*,** katika sehemu hii, nitaeleza kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa kila sekta kwa mtiririko, nikianzia na Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na hatimaye Sekta ya Mawasiliano.

#### **C.1.1 SEKTA YA UJENZI**

##### **Bajeti ya Matumizi ya Kawaida**

**27. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara (Ujenzi) ilitengewa kiasi cha Shilingi **36,264,751,504.04** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi **33,788,265,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi zake na Shilingi **2,476,486,544.04** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi zake. Aidha, Bajeti ya Matumizi ya kawaida imeongezewa wigo kutoka Shilingi **36,142,664,000.00** hadi Shilingi **36,264,751,504.04** sawa na ongezeko la Shilingi **122,087,544.04**. Ongezeko hili ni kwa

ajili ya malipo ya madeni ya Wazabuni mbalimbali ambayo yamehakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Hadi Machi, 2020 jumla ya **Shilingi 24,128,094,762.08** zilikuwa zimetolewa na HAZINA kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, sawa na asilimia **66.53** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,111,449,258.04** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Taasisi na **Shilingi 2,016,645,504.04** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo ya Wizara na Taasisi.

### Bajeti ya Miradi ya Maendeleo

**28. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Sekta ya Ujenzi ilitengewa **Shilingi 1,294,051,604,268.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 990,000,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 304,051,604,268.00** zilikuwa ni fedha za nje. Fedha za ndani zilijumuisha fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali (Consolidated Funds) **Shilingi 402,611,000,000.00** na fedha za Mfuko wa Barabara **Shilingi 587,389,000,000.00**. Aidha, Bajeti ya fedha za ndani za miradi ya maendeleo imeongezewa wigo kutoka **Shilingi 990,000,000,000.00** hadi **Shilingi 1,713,862,494,259.91** sawa na ongezeko la **Shilingi 723,862,494,259.91**. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni na madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri yaliyohakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hivyo, jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa ni **Shilingi 2,017,914,098,527.91**.

Hadi Machi, 2020 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi 1,663,224,452,809.45**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,387,232,923,133.44** ni fedha za ndani na **Shilingi 275,991,529,676.01** ni fedha za nje. Fedha za ndani zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi 936,146,859,501.27** kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 451,086,063,632.17** ni fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa ujumla, hadi kufikia Machi, 2020 fedha za maendeleo zilizotolewa ni sawa na asilimia 82.42 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/20.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

### Miradi ya Barabara na Madaraja

**29. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) ilipanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometa 432.30** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **13** pamoja na ukarabati wa **kilometa 56** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu.

Hadi kufikia Machi, 2020, jumla ya **kilometa 405.7** za barabara kuu zimekamilika kujengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya **kilometa 16.2** za barabara kuu zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa madaraja mawili **(2)** umekamilika na ujenzi wa madaraja **11** ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**30. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara kuititia TANROADS ilipanga kujenga kwa kiwango cha lami barabara za mikoa zenye urefu wa **kilometa 72.01** ambapo **kilometa 40.81** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometa 31.20** zilipangwa kujengwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometa 893.04** zilipangwa kukarabatiwa kwa kiwango cha changarawe ambapo kati ya hizo ilipangwa **kilometa 486.03** na madaraja **12** kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na ilipangwa **kilometa 407.01** pamoja na madaraja **15** kujengwa/kukarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Hadi Machi, 2020 jumla ya kilometra **24.23** za barabara za mikoa zilijengwa kwa kiwango cha lami na jumla ya kilometra **255.21** zilifanyiwa ukarabati kwa kiwango cha changarawe na ujenzi wa madaraja ulikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**31. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Wizara ilipanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yanahuisha matengenezo ya

kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa kilometra 32,944.31, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofii ya kilometra 5,031.14 na matengenezo ya madaraja 3,376. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na ulinzi wa hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Hadi Machi, 2020 utekelezaji wa matengenezo katika barabara kuu na za mikoa ulifikiya kilometra **17,134.14**, matengenezo ya muda maalum na sehemu korofii kilometra **2,820.08** na matengenezo ya madaraja **1,695**.

**32. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia TANROADS iliendelea na kazi ya kudhibiti uzito wa magari kwa kutumia mizani **55** ya kudumu na **17** inayohamishika katika barabara kuu za lami. Hadi kufikia Machi, 2020, magari **3,297,187** yalikuwa yamepimwa ambapo kati ya hayo, magari **948,247** sawa na asilimia **29** yalikuwa yamezidisha uzito. Jumla ya **Shilingi 3,147,619,811** zilikusanywa kutokana na tozo ya uzidishaji uzito unaoruhusiwa kupita barabarani. Aidha, Wizara inaendelea na utoaji wa vibali vya mizigo maalum nchini. Hadi Machi, 2020 jumla ya **Shilingi 13,661,292,803.00** zilikusanywa kutokana na tozo ya upitishaji wa mizigo maalum.

**33. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa miradi ya barabara hadi Machi, 2020 illikuwa ni kama ifuatavyo:

**34. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa **Barabara za Kuelekea kwenye mradi wa Kufua Umeme katika Maporomoko ya Mto Rufiji**; hadi Machi, 2020 maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara ya Bigwa – Kisaki (km 50) yalikuwa yanaendelea.

**35. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro – Dodoma (km 467.9)**, mkataba kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa barabara ya **Ubena Zomozi – Ngerengere** kwa kiwango cha lami, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika. Mkataba wa ujenzi wa kilometra 0.7 za barabara ya **Kwa**

**Mathias – Msangani (km 8.3)** umesainiwa na Mkandarasi yupo kwenye maandalizi ya awali (mobilization) ya ujenzi. Kwa upande wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Morogoro – Dodoma (km 256)**, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hizo zinaendelea.

**36. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa barabara ya **Wazo Hill – Bagamoyo – Msata** sehemu ya **Tegeta – Bagamoyo (km 46.9)**, **Mbegani – Bagamoyo (km 7.2)** na **Makofia – Mlandizi (km 36.7)**, kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi.

Kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)** na **Kisarawe – Maneromango (km 54)** zinaendelea. Mkataba wa ujenzi wa sehemu ya **Tanga – Pangani (km 50)** umesainiwa na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya awali (mobilization) ya kuanza kazi za ujenzi. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) imekubali kutoa fedha za mkopo nafuu kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Pangani na barabara za lami zenyе urefu wa kilometra 124.5 kutoka Pangani hadi Mkange. Majadiliano kuhusu mkopo huo yamekamilika na mkataba wa mkopo umesainiwa tarehe 13 Machi, 2020.

**37. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa**, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami umekamilika kwa sehemu ya **Geita – Bulyanhulu Junction (km 58.3)**, **Bulyanhulu Junction – Kahama (km 61.7)** na **Nyamirembe Port – Katoke (km 50)**. Taratibu za kutangaza zabuni za ujenzi zinasubiri upatikanaji wa fedha.

**38. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi 2020, katika barabara ya **Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Urambo – Kaliua (km 28)** ulikuwa umefikia asilimia 80 na Mhandisi Mshauri kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Uvinza – Malagarasi (km 51.1)** anaendelea na kazi ya kufanya mapitio ya usanifu na

makabrasha ya zabuni za kazi za ujenzi. Aidha, mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Chagu – Kazilambwa (km 36)** umesainiwa na Mkandarasi yuko katika maandalizi ya kuanza kazi.

**39. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa barabara ya **Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga na Bomang’ombe – Sanya Juu**, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Sanya Juu – Elerai (km 32.2)** umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami mita 800 za barabara ya **Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8)** umekamilika na ujenzi wa kilometra 1.4 katи ya kilometra 3.5 zilizobaki katika barabara ya **Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16)** umekamilika. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometra 3 zilizobaki katи ya kilometra 14 za barabara ya **Kijenge – Usa River (Nelson Mandela AIST)** kwa kiwango cha lami unaendelea na maandalizi kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Mianzini – Ngaramtoni (km 18)** yanaendelea.

**40. Mheshimiwa Spika**,mradi wa upanuzi wa barabara ya **Arusha – Moshi – Himo – Holili (sehemu ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105.0) pamoja na mizani ya Himo)**, mazungumzo katи ya Serikali na JICA kwa ajili ya kupata fedha za upanuzi wa barabara hii yanaendelea.

**41. Mheshimiwa Spika**,mradi wa barabara ya **Dodoma – Manyoni** unahusisha ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (One Stop Inspection Station - OSIS) cha Muhalala (Manyoni) pamoja na ujenzi wa mizani inayopima uzito wa magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) eneo la Nala Mkoani Dodoma. Hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Muhalala unaofadhiliwa na Jumuia ya Ulaya (EU) bado zimesimama. Serikali inaendelea na majadiliano na Mkandarasi ili kufikia maridhiano kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi. Aidha, ununuzi wa mizani ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo (Weigh in Motion - WIM) umefanyika na imejengwa kwenye eneo la Nala (Dodoma).

**42. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020, utekelezaji wa mradi wa barabara ya **Dumila – Kilosa - Mikumi** sehemu ya **Rudewa – Kilosa (km 24)** ulikuwa umefikia asilimia 20.

**43. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)**, ulikuwa umefikia asilimia 95 ambapo kilometa 106 zimejengwa kwa kiwango cha lami na kazi za ujenzi zinaendelea. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya **Matai – Kasesya (km 50)** zinasubiri upatikanaji wa fedha.

**44. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi wa **ujenzi wa madaraja makubwa** uliendelea katika mwaka wa fedha 2019/20. Hadi Machi, 2020 ujenzi wa madaraja ya Mara na Magara umekamilika. Madaraja ambayo ujenzi wake unaendelea ni pamoja na ujenzi wa nguzo za daraja la Ruhuhu (asilimia 85), Mitomoni (asilimia 75), Kitengule (asilimia 50), Msingi (asilimia 40), Selander (asilimia 34) na Wami (asilimia 53). Aidha, Mkandarasi anajienda kuanza kazi za nyongeza za kuweka lami kwenye barabara unganishi kwa daraja la Sibiti; Mkandarasi wa ujenzi wa daraja la Kigongo - Busisi amepatikana na yupo kwenye maandalizi (mobilization) ya kuanza ujenzi; taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi wa kufanya ukarabati wa daraja la Kirumi na kuanza ujenzi wa daraja la Sukuma zinaendelea na usanifu wa kina wa madaraja ya Mzinga, Mkenda na Ugalla umekamilika.

**45. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zinazoendelea ni upembusi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Mtera na Godegode pamoja na taratibu za manunuzi kwa ajili ya kuwapata Wahandisi Washauri watakaofanya upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa madaraja ya Malagarasi Chini na Mkundi. Aidha, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata mzabuni (supplier) wa madaraja ya chuma (Mabey Compact Bridges) zilikuwa katika hatua ya mwisho.

**46. Mheshimiwa Spika**, kazi ya usanifu wa awali (Preliminary Design) ili kuwezesha utaratibu wa Kusanifu na Kujenga (Design & Build) kwa daraja la Simiyu imekamilika. Hata hivyo, mpango wa ujenzi wa daraja la Simiyu pamoja na barabara ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border uliingizwa kwenye programu ya Benki ya Dunia ya kuimarisha barabara zinazounganisha bandari zilizoko ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Transport Programme - LVTP). Hadi Machi, 2020 Serikali ilikuwa imekamilisha majibu ya hoja zilizotolewa na Benki ya Dunia na inasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya kuendelea na programu hiyo.

**47. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **New Bagamoyo (Morocco Junction - Mwenge - Tegeta: km 18.3)**, kazi za upanuzi wa sehemu ya **Morocco - Mwenge (km 4.3)** zilikuwa zimefikia asilimia 44 na uboreshaji wa mifereji ya maji ya mvua sehemu ya **Mwenge - Tegeta (km 14.0)** ulikuwa unaendelea.

**48. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya **Kyaka - Bugene - Kasulo**, hadi Machi, 2020 taratibu za mapitio ya usanifu wa kina kwa sehemu ya **Bugene - Kasulo (km 124.0)**, Upembusi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu ya **Kumunazi - Kasulo (km 9)** na **Kyaka - Mutukula (km 30)** kwa upande wa Tanzania na sehemu ya **Mutukula - Masaka (km 89.1)** kwa upande wa Uganda chini ya ufadhilli wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) zilikuwa zinaendelea. Mhandisi Mshauri alikuwa anakamilisha taarifa ya mwisho. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)** baada ya kukamilika kwa upembusi yakinifu na usanifu wa kina.

**49. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 katika barabara ya **Isaka - Lusahunga - Rusumo**, kazi ya ukarabati wa sehemu ya **Ushirombo - Lusahunga (km 110)** imekamilika na kazi ya matengenezo ya dharura katika sehemu korofii kwenye sehemu ya **Lusahunga - Rusumo (km 92)** ilikuwa inaendelea. Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya **Lusahunga - Rusumo (km 92)** kwa

kiwango cha lami chini ya programu ya Development Corridor Transport Programme (DCTP). Nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi zilikuwa zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kutangaza zabuni.

Kwa upande wa Kituo cha Ukaguzi wa Pamoja (OSIS) cha Nyakanazi, kazi za ujenzi bado zimesimama. Kwa sasa Serikali inajadiliana na Mkandarasi ili kufikia maridhiano kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi.

Kwa upande wa barabara ya **Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba/Rulenge – Murugarama** na barabara ya **Rulenge – Kabanga Nickel** zenye jumla ya kilometa 141, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ulikuwa unaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**50. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **Manyoni – Itigi – Tabora**, ujenzi wa sehemu za **Manyoni – Itigi – Chaya (km 89.35)** na **Tabora – Nyahua (km 85)** umekamilika. Aidha, sehemu ya **Chaya – Nyahua (km 85.4)** kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami ilikuwa imefikia asilimia 65.

**51. Mheshimiwa Spika**, zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Msauri wa kufanya kazi za usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Mwanza/ Shinyanga Border – Mwanza** zilitangazwa upya Machi, 2020 baada ya Kampuni iliyopatikana awali kuwa na gharama kubwa.

**52. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa barabara za **kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam**; miradi inayoendelea ni ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya **Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66)** ambapo hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi wa barabara hii sehemu ya **Kibamba – Mloganzila (km 4.0)** zilikuwa zimekamilika. Aidha, ujenzi wa sehemu ya **Mloganzila – Kisopwa (km 1)** unasubiri upatikanaji wa fedha. Mradi mwagine unaoendelea ni ujenzi wa barabara ya **Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7)** ambapo hadi Machi,

2020 kazi za ujenzi wa sehemu ya **Kitunda- Kivule (km 3.2)** zilikuwa zimefikia asilimia 40.

Mkataba wa ujenzi wa barabara ya **Wazo Hill – Madale (km 6)** umeshasainiwa na Mkandarasi anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi. Kwa barabara ya **Ardhi – Makongo – Goba (km 9)**, kazi za ujenzi wa sehemu ya **Goba – Makongo (km 4)** zimekamilika. Ujenzi wa sehemu ya **Ardhi – Makongo (km 5)** unasubiri ulipaji wa fidia. Vilevile, kazi ya usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni zimekamilika kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Mjimwema – Kimbiji (km 27.0)** na Kongowe – Mjimwema – Kivukoni (km 25.1) ambapo Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Taratibu za kutangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya **Mwai Kibaki (km 9.1); Kawe round about – Garden Rd Junction (km 2.9)** zinasubiri upatikanaji wa fedha.

**53. Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya **Kidatu - Ifakara - Lupiro - Mahenge/Malinyi - Londo - Lumecha/Songea**, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kidatu - Ifakara (km 66.0)** inaendelea na imefikia asilimia 12. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara za **Ifakara - Kihansi - Mlimba - Taweta/Madeke (km 220.22)**, sehemu ya **Ifakara - Kihansi (km 126.74)** na **Ifakara - Lupiro - Malinyi - Londo - Lumecha (km 396)**.

**54. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya **Tabora - Ipole - Koga - Mpanda**, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Tabora - Sikonge (Usesula - km 30)** zimekamilika. Kwa sehemu ya **Sikonge (Usesula) - Ipole - Koga - Mpanda (km 359)**, ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Usesula - Komanga (km 108)** na barabara ya kuingia mji wa **Sikonge, (km 7.5)** umefikia asilimia 40, **Komanga – Kasinde (km 108)** na barabara ya kuingia mji wa **Inyonga (km 4.8)** umefikia asilimia 56 na **Kasinde – Mpanda (km 108)** na barabara ya kuingia mji wa **Urwira (km 3.7)** umefikia asilimia 44.5.

**55. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa barabara ya Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo na Loliondo – Mto wa Mbu umeendelea kutekelezwa ambapo hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Makutano – Sanzate (km 50)** ulikuwa umefikia asilimia 82.5. Kwa upande wa sehemu ya **Sanzate - Natta (km 40)**, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi ziliikuwa zinaendelea na ujenzi wa sehemu ya **Natta – Mugumu (km 45)** unasubiri upatikanaji wa fedha. Aidha, ujenzi wa barabara ya **Loliondo – Mto wa Mbu (sehemu ya Waso – Sale: km 49)** ulikuwa umefikia asilimia 46 na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Karatu – Mbulu - Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa (km 389)** ziliikuwa katika hatua za mwisho. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa sehemu ya **Mbulu – Hydom (km 50)**.

**56. Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya **Ibanda – Itungi/ Kiwira**, hadi Machi, 2020 kazi ya ujenzi wa barabara ya **Kikusya – Ipinda – Matema Beach (km 39)**, sehemu ya **Tenende – Matema (km 34.6)** na kilometra 10 za sehemu ya **Bujesi – Mbambo (km 15)** kwa kiwango cha lami ziliikuwa zimekamilika. Kazi za ujenzi wa kilometra 5 zilizobaki kwenye mradi wa **Bujesi – Mbambo (km 15)** na **Tukuyu – Mbambo (km 17.0)** zimeanza na ziliikuwa zimefikia asilimia 7.

**57. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa barabara ya **Nzega – Tabora (km 115)** kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, hadi Machi, 2020, taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya **Shelui – Nzega (km 110)** kwa kiwango cha lami ziliikuwa zinaendelea.

**58. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 barabara ya **Sumbawanga – Mpanda – Kanyani – Nyakanazi**, sehemu ya **Mpanda – Ifukutwa – Vikonge (km 37.65)** ujenzi umefikia asilimia 87, ambapo kilometra 28.64 zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, ujenzi wa sehemu za **Kibaoni – Sitalike (km 71.0)**, **Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.31)**, **Namanyere – New Katongoro Port (km 64.8 )** na **Vikonge – Magunga – Uvinza (km 159.0)** unasubiri upatikanaji wa fedha.

**59. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 miradi ya ukarabati wa barabara ya **Nyanguge – Musoma**, sehemu ya **Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4)** na ujenzi wa **daraja la Simiyu** ilikuwa haijaanza. Hata hivyo, miradi hii imejumuishwa kwenye programu ya Benki ya Dunia ya kuimarisha barabara zinazounganisha bandari zilizoko ukanda wa Ziwa Victoria (Lake Victoria Transport Programme - LVTP). Serikali ilikuwa inasubiri idhini (No Objection) ya Benki ya Dunia kuendelea na miradi hii.

Katika barabara ya **Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa**; sehemu ya **Bulamba – Kisorya (km 51)**, kazi za ujenzi zimekamilika kwa asilimia 84. Aidha, Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Nyamuswa – Bunda – Bulamba (km 55.0)** anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi (mobilization). Vilevile, hadi Machi, 2020 kazi za upanuzi wa barabara ya kwenda **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza (km 12)** na ukarabati wa barabara ya **Makutano – Sirari (km 83)** zimekamilika. Aidha, kwa barabara ya **Musoma – Makojo – Busekela (km 92)**, kazi za ujenzi wa sehemu ya Suguti – Kusenyi (km 5) zilikuwa zinaendelea.

**60. Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Magole – Turiani – Mziha**, unaendelea ambapo hadi Machi, 2020 ujenzi wa sehemu ya **Magole – Turiani (km 45.2)** kwa kiwango cha lami umekamilika. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa sehemu ya **Turiani – Mziha – Handeni (km 104)**.

**61. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020, mradi wa ujenzi wa barabara za juu (flyovers/interchange) na maboresho ya makutano ya barabara katika jiji la Dar es Salaam ulikuwa unaendelea. Katika kipindi hicho, ujenzi wa barabara za juu (Interchange) katika makutano ya Ubungo umefikia asilimia 70. Aidha, usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya Fire, Magomeni, Mwenge, Tabata/Mandela, Morocco, Buguruni pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Junction) ulikamilika. Hivi sasa tathmini ya fidia kwa watakaoathirika na utekelezaji wa mradi

inaendelea. Vilevile, maandalizi ya ujenzi wa Mabey Flyovers katika Jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza yanaendelea.

**62. *Mheshimiwa Spika***, katika barabara ya **Mwigumbi – Maswa - Bariadi – Lamadi**, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Maswa – Bariadi (km 49.7)** ulifikia asilimia 77.6. Aidha, ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za **Kolandoto – Mwanhuzi (km 10)**, **Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 74)** na **Isabdula (Magu) – Bukwimba – Ngudu – Ng'hungumalwa (km 10)** unasubiri upatikanaji wa fedha.

**63. *Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2020 kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Tabora - Ipole – Rungwa (km 172)**, zilikuwa zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**64. *Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2020 ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kibondo – Nyakanazi, uliendelea ambapo kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya **Kidahwe – Kasulu (km 63)** zilikuwa zimefikia asilimia 98.5 na kwa sehemu ya **Nyakanazi – Kibondo (km 50)** zimefikia asilimia 78. Aidha, mikataba minne ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Kakonko (Kabingo) – Kibondo – Kasulu – Manyovu (km 260)** imesainiwa na makandarasi wapo kwenye maandalizi ya kuanza ujenzi. Mkandarasi wa ujenzi wa sehemu ya **Nduita Junction – Kibondo (km 25.6)** amepatikana na anaendelea na maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi.

**65. *Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa mradi wa barabara ya **Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12)**, hadi Machi, 2020, kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara hii zimekamilika. Aidha, ujenzi wa **barabara za Ikulu Chamwino** ulikuwa unaendelea. Kwa upande wa barabara ya pete ya **Dodoma (km 112.3)** hatua za manunuza za kuwapata Makandarasi na Wahandisi Washauri kwa ajili ya kuanza ujenzi zilikuwa zinaendelea.

**66. *Mheshimiwa Spika***, hadi Machi, 2020 katika mradi wa ujenzi wa **daraja la Nyerere (Kigamboni) na barabara**

**unganishi**, ujenzi wa daraja umekamilika na ujenzi wa barabara unganishi za daraja unaendelea. Vilevile, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za **Tungi – Kibada (km 3.8) na Kibada – Mwasonga – Tundwisiogani – Kimbiji (km 41)** umekamilika.

**67. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa **njia za magari mazito na maegesho ya dharura katika Ushoroba wa Kati** umepangwa kujumuishwa kwenye kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara za ushoroba wa kati. Barabara hizo ni **Morogoro – Dodoma (km 260), Singida – Shelui (km 108) na Shelui – Nzega (km 110)** ambazo ziko katika hatua za manunuzi za kuwapata Wahandisi Washauri.

**68. Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya **Kimara – Kibaha (km 25.7)** unahusisha upanuzi wa sehemu ya **Kimara – Kiluvya (km 19.2)** kuwa njia nane ikijumuisha upanuzi wa madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji. Hadi Machi, 2020 kazi za upanuzi zimefikia asilimia 74.

**69. Mheshimiwa Spika**, kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara ya mzunguko ya **Pugu – Kifuru - Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34)**, kwa ajili ya kuijenga kuwa njia sita itaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

**70. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya **Tunduma – Sumbawanga**, sehemu ya **Mpemba – Isongole (km 51.2)** ulikuwa umefikia asilimia 59.36. Aidha, maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami kwa barabara ya **Ruanda – Iyula – Nyimbili (km 21)** yanaendelea.

**71. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa barabara ya **Kagoma – Lusahunga** umekamilika. Kazi za ujenzi wa kilometra 5.2 za barabara ya **Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54.0)** zimefikia asilimia 25 na kwa kilometra 8 za barabara ya **Muleba – Kanyambogo – Rubyia (km 18.5)**, kazi zimefikia asilimia 45. Aidha, Serikali inaendelea na maandalizi ya kuanza kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya

**Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136)** kwa ajili ya kuifanya ukarabati.

**72. Mheshimiwa Spika**, ujenzi na ukarabati wa barabara ya Arusha – Minjingu – Babati – Singida umekamilika. Hadi Machi, 2020 taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Singida – Shelui (km 108)** kwa ajili ya kuifanya ukarabati barabara hii zilikuwa zinaendelea.

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) na daraja la Gerezani; hadi Machi, 2020 ujenzi wa daraja la Gerezani umefikia asilimia 80. Aidha, kazi za upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa sehemu ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe pamoja na daraja la Mzinga zimekamilika.

**74. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020, katika barabara ya Msimba – Ruaha/Ikokoto – Mafinga – Igawa, kazi za ujenzi wa barabara ya Igawa – Mbarali – Ubaruku (km 16) sehemu ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) zimekamilika kwa kiwango cha lami. Aidha, hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Moronga (km 53.9) zilikuwa zimefikia asilimia 64 na Moranga – Makete (km 53.5) zilikuwa zimefikia asilimia 47. Kazi za ujenzi wa barabara ya Njombe – Lupembe – Madeke (km 125) zinasubiri upatikanaji wa fedha. Kwa upande wa barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104.0) na Makambako – Songea (km 295.0), taarifa ya mapitio ya tathimini za athari za mazingira pamoja na mali zitakazoathirika wakati wa ujenzi na ukarabati wa barabara hizi zimewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kuomba kibali cha kuendelea na taratibu za manunuzi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami. Aidha, Wahandisi Washauri wanaendelea na kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma (km 218) ikijumuisha barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe Bypass) (km 48.9) na barabara ya Mafinga – Mgololo (km 78.0).

75. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa ukarabati wa barabara ya Korogwe – Mkumbara – Same (**km 172**) umekamilika. Hadi Machi, 2020 Mhandisi Mshauri katika mradi wa barabara ya Soni – Bumbuli – Dindira – Korogwe (**km 74**) alikuwa anaendelea na kazi ya usanifu wa kina. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuanza kazi za ukarabati wa barabara za Same – Himo (**km 76**), Mombo – Lushoto (**km 32**) na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Lushoto – Magamba – Mlola (**km 34.5**).

76. **Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya Mbeya – Makongolosi, hadi Machi, 2020 kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Chunya – Makongolosi (**km 43**) zimefikia asilimia 61. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Mkiwa – Itigi – Noranga (**km 56.9**) na Mbalizi – Makongolosi (**km 50**).

77. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 katika mradi wa barabara ya Chalinze – Segera – Tanga, Mkandarasi yuko katika hatua ya maandalizi ya kuanza kazi za ujenzi wa kilometra 7 za sehemu ya Amani – Muheza (**km 36**).

78. **Mheshimiwa Spika**, mradi wa barabara ya Itoni – Ludewa – Manda hadi Machi, 2020, kazi ya ujenzi kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya Lusitu – Mawengi (**km 50**) imefikia asilimia 42.4.

79. **Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 ujenzi wa daraja jipya la Selander ulikuwa umefikia asilimia 34.

80. **Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijochini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (**km 460**), kutokana na umuhimu wa barabara hii kwa ujenzi wa Bomba la Mafuta kutoka Tanga hadi Hoima (Uganda), Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi wa barabara hii.

81. **Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya Dodoma – Mtera – Iringa hadi Machi, 2020 Mkandarasi alikuwa ameanza kazi

za ujenzi katika barabara ya Mchepuo wa Iringa (**Iringa Bypass: km 7.3**).

**82. Mheshimiwa Spika**, katika barabara ya **Dodoma – Babati**, hadi Machi, 2020 kazi ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo wa Babati (**Babati Bypass: km 12**) zilikuwa zinaendelea.

**83. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa barabara ya **Masasi – Songea – Mbamba Bay** na **Masasi – Newala – Mtwara** unaendelea. Hadi Machi, 2020 ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya **Mbinga – Mbamba Bay (km 66)** umefikia asilimia 52 na ujenzi wa barabara ya **Mtwara – Newala – Masasi (km 210)**, sehemu ya **Mtwara – Mnivata (km 50)** kwa kiwango cha lami umefikia asilimia 76. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya **Masasi – Nachingwea (km 45.0)** na barabara ya **Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 107)** zimekamilika na Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi. Kwa upande wa ujenzi wa barabara ya **Likuyufusi – Mkenda (km 122.5)**, mapitio ya usanifu wa kina na nyaraka za zabuni yamefanyika kwa asilimia 40. Kwa barabara ya **Nachingwea – Liwale (km 130)** hadi Machi, 2020 Mhandisi Mshauri anaendelea na kazi ya usanifu wa kina.

Ujenzi wa kilometra 5 za barabara ya **Kitahi – Lituhi (km 90)** kuelekea machimbo ya makaa ya mawe unaendelea na umefikia asilimia 65. Aidha, kwa upande wa barabara ya **Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)** hadi Machi, 2020 ukarabati wa barabara hii ulikuwa haujaanza. Aidha, Benki ya Dunia imeonyesha nia ya kugharamia ukarabati wa barabara ya hii chini ya programu ya Development Corridor Transport Program (DCTP) ambapo maandalizi ya utekelezaji wa programu hii yanaendelea.

**84. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya mchepuo kutoka barabara ya Bagamoyo kuingia kwenye **Chuo cha Uongozi cha Bagamoyo** pamoja na barabara za ndani ya Chuo hicho, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizo.

**85. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020, ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili hadi ya Tano, ulikuwa unaendelea ambapo ujenzi wa barabara za Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili Lot 1 (barabara) unaendelea na umekamilika kwa asilimia 3.3 na Lot 2 (majengo) unaendelea na umefikia asilimia 22. Kwa upande wa mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatoo, usanifu wa kina na uandaaji wa nyarakaa za zabuni umekamilika na kuwasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya kupata kibali cha kutangaza zabuni za ujenzi. Aidha, Serikali inaendelea kutafuta fedha za kuanza ujenzi wa Mradi wa BRT Awamu ya Nne na Tano ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya mazungumzo na Washirika wa Maendeleo.

**86. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 ujenzi wa jengo la **Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS)** ulifkia asilimia 25. Aidha, utekelezaji wa miradi ya majengo ya Ofisi za Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.

**87. Mheshimiwa Spika**, Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara. Kazi zilizopangwa kutekelezwa katika Barabara Kuu kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa **kilometra 5,602.73** za barabara ambapo hadi Machi, 2020 utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

i) **Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo/Benaco (km 183.1) – Sehemu ya Bugene – Kasulo/Benaco (km 124)**

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Aidha, kazi ya kufanya mapitio ya usanifu kwa sehemu ya Kumunazi – Kasulo (km 9), Kasulo – Bugene (km 124) na Kyaka – Mutukula (km 30) kwa kutumia fedha za Benki ya Maendeleo ya Afrika kuititia Jumuiya ya Afrika Mashariki zipo katika hatua ya mwisho.

*ii) Kufanya Mapitio na Kuandaa Miongozo (Standards and Specifications)*

Hadidu za Rejea kwa ajili ya kuanza taratibu za manunuzi za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya miongozo mbalimbali ya kufanya usanifu wa barabara zilizoandalisha miaka ya 1999 na 2000 zilikuwa zimekamilika. Serikali imeendelea kutafuta fedha za kugharamia mradi huu.

*iii) Barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92)*

Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii umekamilika na Serikali inatafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

*iv) Barabara ya Karatu – Mbulu – Haydom – Mto Sibiti – Lalago – Maswa (km 389)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa barabara hii zilikuwa zimefikia hatua ya mwisho kukamilika. Hatua inayofuata ni kuanza usanifu wa kina kabla ya kuanza ujenzi.

*v) Barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete (km 96.2)*

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

*vi) Kuimarisha Uwezo wa Maabara (Central Material Laboratory – CML) katika Kupima Vifaa vya Ujenzi na Kuanzisha Teknolojia ya Kisasa ya ‘Asphalt Mix Design’*

Tafiti sita (6) kuhusu vifaa ujenzi na matabaka ya lami (pavement) zilikuwa zinaendelea. Aidha, kazi ya uboreshaji wa maabara ili iweze kukidhi viwango vya kimataifa pamoja na mafunzo kwa wahandisi na Mafundi Sanifu kuhusu utumiaji wa Mwongozo wa Uchanganyaji Lami zilikuwa zinaendelea.

*vii) Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

*viii) Mifumo ya Kompyuta (Software) kwa Ajili ya Usanifu wa Barabara na Kuandaa Mipango ya Usafiri (Highway/Transport Planning)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mshauri Elekezi wa kutoa mafunzo juu ya mifumo ya kompyuta ya usanifu wa barabara na mipango ya usafiri zilikuwa zinaendelea.

*ix) Daraja la Kigongo - Busisi katika Barabara ya Usagara - Geita*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika na Mkandarasi alikuwa anaendelea na maandalizi ya kuanza ujenzi.

*x) Mpanda - Ugalla - Kaliua - Ulyankulu - Kahama (km 457)*

Taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

*xi) Barabara ya Ipole - Rungwa (km 172)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

*xii) Barabara ya Mtwara Pachani - Lusewa - Lingusenguse - Nalasi (km 211)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

*xiii) Barabara ya Arusha - Kibaya - Kongwa (km 430)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

*xiv) Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 91):*

Kazi za upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina imekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**xv) Kuboresha Eneo la Mlima Kitonga (km 10)**

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

**xvi) Barabara ya Dar es Salaam Road (Nanenane) – Miyuji (Arusha Road) – Mkonze (km 23)**

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

**xvii) Barabara ya Emmaus – Mlimwa – Wajenzi (km 5)**

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii imekamilika.

**xviii) Dodoma Outer Ring Road / Dodoma Bypass (Mtumba - Veyula - Nala - Matumbulu - Mtumba: km 104)**

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**xix) Barabara ya Ngaresh – Enguik (Monduli Juu) (km 104)**

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

**xx) Uchunguzi wa Kina wa Chanzo cha Mafuriko Eneo la Kibaigwa katika Barabara ya Morogoro - Dodoma**

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya uchunguzi wa kina wa chanzo cha mafuriko eneo la Kibaigwa zinaendelea.

**xxi) Uchunguzi wa Kina Kuhusu Chanzo cha Mafuriko na Kupata Ufumbuzi wa Kudumu Kwenye Daraja la Mkundi**

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi hii zinaendelea.

**xxii) Barabara ya Babati (Dareda) - Dongobeshi (km 60)**

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxiii) Barabara ya Soni – Bumbuli - Dindira - Korogwe (km 70)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo katika hatua za mwisho.

***xxiv) Barabara ya Kibaoni – Majimoto - Inyonga (km 152)***

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inaendelea.

***xxv) Barabara ya Kiranjeranje – Namichiga - Ruangwa (km 120)***

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

***xvi) Barabara ya Masaninga – Matandu – Nangurukuru – Kilwa Masoko (km 55)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliwuwa zinaendelea.

***xxvii) Barabara ya Sabasaba – Sepuka – Ndago – Kizaga (km 77)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxviii) Barabara ya Singida Urban – Iliongero – Haydom (km 93)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinaendelea.

***xxix) Daraja la Mpiji Chini na Barabara za Maingilio (km 1.7)***

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zipo katika hatua ya mwisho.

***xxx) Barabara za Mkiu – Liganga – Madaba (Km 112); Liganga – Nkomang’ombe (km 70) na Nkomang’ombe – Coal Power Plant (km 4.14)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliwuwa zipo katika hatua ya mwisho.

***xxxii) Barabara ya Mkuyuni - Nyakato (km 10)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina zilikuwa zinaendelea.

***xxxiii) Barabara ya Tarime - Mugumu (km 86)***

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

***xxxiv) Barabara ya Morogoro (Tumbaku Roundabout) – Mangae/Melela – Mikumi – Iyovi (km 156.45) na Daraja la Doma***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

***xxxv) Barabara ya Mbulu – Magugu (Mbonyu wa Mjerumani) (km 63)***

Mkataba kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa Machi, 2020. Maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea.

***xxxvi) Barabara ya Morogoro (Msamvu Roundabout) – Morogoro Centre – Bigwa Junction (km 10)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

***xxxvii) Barabara ya Buhongwa – Igoma (km 12)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

***xxxviii) Barabara ya Omurushaka – Murongo (km 125)***

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zilikuwa zinaendelea.

*xxxviii) Barabara ya Simanjiro (Orkesumet) – Kia – Mererani (Part Of Kongwa Ranch – Kiteto – Simanjiro – Kia (km 60)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xxxix) Barabara ya Babati – Orkesumet – Kibaya (km 255):*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xli) Barabara ya Singida Bypass (km 46):*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xlii) Barabara ya Songea Bypass (km 11)*

Mkataba kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa. Maandalizi ya kuanza kazi yanaendelea.

*xliii) Barabara ya Nyakato – VETA – Buswelu (km 3)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xliii) Daraja la Godegode (Meta 70) na Barabara za Maingilio (km 6) Kati ya Barabara ya Mpwapwa – Makutano na Pawaga – Lumuma*

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza.

*xliv) Barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xlv) Barabara ya Salawe – Old Shinyanga (km 64.70)*

Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina imeanza.

*xlv) Barabara ya Mpwapwa - Gulwe - Rudi - Chipogoro; Sehemu ya Kibakwe - Chipogoro (km 75.84)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ziliikuwa zinaendelea.

*xlvii) Barabara ya Kihansi - Mlimba - Madeke (km 220.22)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii zimejumuishwa kwenye mkopo nafuu wa AfDB ambao pia utatumika kujenga daraja la Pangani na barabara ya Pangani - Mkange - Tungamaa (km 124).

*xlviii) Barabara ya Ntendo - Muze - Kilyamatundu (km 200.00)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina ziliikuwa zinaendelea.

*xlix) Barabara ya Mbamba Bay - Lituhi (km 121.00)*

Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zimekamilika. Hatua inayofuata ni ya Serikali kutenga fedha za ujenzi kwa kiwango cha lami.

*i) Barabara ya Nangurukuru - Liwale (km 210.00)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina ziliikuwa zinaendelea.

*ii) Barabara ya Ushirombo - Nyikonga - Geita (Katoro) (km 59.00)*

Mkataba wa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umesainiwa mwezi Machi, 2020.

*iii) Barabara ya Makete - Ndulamo - Nkenja - Kitulo (km 42)*

Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Kina ziliikuwa zinaendelea.

## **Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

**88. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, kuhusu *ujenzi na ukarabati wa maegesho ya vivuko*, Wizara kupitia Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (TEMESA) ilipanga kuendelea na upanuzi wa eneo la maegesho ya Kigamboni katika kivuko cha Magogoni - Kigamboni mkoani Dar es Salaam, maegesho ya Bukondo na Zumacheli katika kivuko cha Chato - Nkome mkoani Geita, ujenzi wa maegesho ya Nyamisati - Mafia katika mkoa wa Pwani, ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda Mkoani Lindi na ukarabati wa maegesho ya Bugolora – Ukara (Mwanza), Rugezi – Kisorya (Mwanza), Kilambo – Namoto (Mtwara) na Utete – Mkongo (Pwani).

Hadi Machi, 2020 ujenzi wa miundombinu (jengo la abiria, ofisi na uzio) katika kivuko cha Lindi – Kitunda umekamilika. Aidha, awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya kivuko cha Kigamboni – Magogoni ilikuwa imeanza. Ujenzi wa maegesho ya Bukondo umeanza na maegesho ya Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome na Nyamisati – Mafia upo hatua ya kumpata mkandarasi.

**89. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa *ununuzi wa vivuko*, kazi zilizopangwa ni kumalizia ununuzi wa kivuko cha Nyamisati – Mafia, Bugolora – Ukara pamoja na ununuzi wa boti nne (4) kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana) na Magogoni – Kigamboni. Kazi nyingine ni ununuzi wa boti moja (1) ya uokozi kwa ajili ya Lindi – Kitunda na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA kwa ajili ya kuboresha huduma ya matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo ya Serikali.

Hadi Machi, 2020 ujenzi wa kivuko kipywa cha Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 40 na Bugolora – Ukara (Mwanza) umefikia asilimia 70. Ununuzi wa boti mpya za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana), Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi – Kitunda unaendelea. Aidha, vitendea kazi vya

karakana vimenunuliwa kwa ajili ya karakana 15 katika mikoa ya Dar es Salaam (Vingunguti), Pwani, Morogoro, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Katavi, Kigoma, Mwanza, Dodoma, Singida na wilaya za Kahama na Ifakara pamoja na karakana ya MT Depot (Dar es Salaam).

**90. *Mheshimiwa Spika*, miradi ya *Ukarabati wa Vivuko*, iliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2019/20 ni pamoja na kufanya ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV KIU, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Kome II na MV Misungwi.**

Hadi Machi, 2020 ukarabati mkubwa wa MV Kigamboni umekamilika, ukarabati wa MV Sengerema umefikia asilimia 60 na ukarabati wa MV Misungwi umefikia asilimia 35. Aidha, ukarabati wa MV Tegemeo, MV Musoma na MV Mara upo katika hatua za uchambuzi wa zabuni.

#### **Utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

**91. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kuititia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipanga kuendelea na ujenzi wa nyumba za Majaji katika mikoa ya Dar es Salaam (1), Kilimanjaro (1), Mtwara (1) na Shinyanga (1); ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi, Ikulu ya Dodoma; Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; ujenzi wa nyumba za makazi eneo la Magomeni (Magomeni Quarters) pamoja na Ikulu ya Chamwino.**

Vilevile, Wizara ilipanga kufanya ukarabati wa nyumba za Viongozi pamoja na kufanya manunuzi ya samani za nyumba za Viongozi na kwenye Ikulu Ndogo za Serikali; ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na Mamlaka ya Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA); ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI/NHC. Aidha, Wizara ilipanga kuendelea na ukarabati wa karakana za TBA katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya, Tabora na Dar es Salaam. Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana tano (5) za TEMESA zilizopo Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya na M.T

Depot Dar es Salaam; ujenzi wa karakana mpya ya kisasa ya magari Jijini Dodoma pamoja na kuanza ujenzi wa Karakana za TEMESA katika mikoa mpya ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi pamoja na kuendelea na kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri.

**92. *Mheshimiwa Spika*,** hadi Machi, 2020, ujenzi wa nyumba moja ya Jaji Jijini Dar es Salaam umekamilika, kazi za ujenzi wa nyumba 5 za Majaji zipo katika hatua mbalimbali na ujenzi wa nyumba za Makazi ya Magomeni "Quarters" umefikia asilimia 70. Ujenzi wa nyumba 50 za viongozi Dodoma haukufanyika kutokana na uhaba wa fedha na usanifu wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji mpya wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma upo kwenye hatua ya mapitio ya michoro na gharama. Aidha, awamu ya kwanza ya ukarabati wa karakana ya TBA Dodoma imekamilika kwa asilimia 90 na ukarabati wa karakana tano za TBA katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Mbeya, Dar es Salaam na Tabora upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Kwa upande wa karakana za TEMESA, ukarabati wa karakana zilizopo Mwanza na Mbeya unaendelea. Aidha, ujenzi wa karakana ya Simiyu na karakana mpya ya jijini Dodoma upo kwenye hatua za kusaini mikataba na ujenzi wa karakana za TEMESA katika mikoa mpya ya Geita, Njombe na Katavi upo katika hatua za manunuzi.

### **Usalama Barabarani na Mazingira**

**93. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea kuratibu shughuli za usalama barabarani na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara. Kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi; uanzishwaji wa mfumo wa usimamizi wa usalama wa vivuko; ukaguzi wa usalama wa barabara; mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani; kuendelea na ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo (Slow Weigh in Motion Weighbridge) Mkoani Dar es Salaam pamoja

na ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani katika vituo vya Polisi nchini. Kazi nyine ni kujenga uwezo na uelewa wa masuala ya usalama barabarani kwa umma.

**94. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 Wizara imeendelea na ukamilishaji wa malipo ya fidia ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi (*One Stop Inspection Station – OSIS*) katika maeneo ya Idofi – (Njombe), Iboya (Mbozi-Songwe) na Himo (Kilimanjaro). Ujenzi wa mizani ya kisasa ya kupima magari yakiwa kwenye mwendo mdogo (slow weigh in motion weighbridge) mkoani Dar es Salaam upo katika hatua za manunuzi. Vile vile ujenzi wa miundombinu na uwekaji wa mfumo wa upatikanaji na utoaji taarifa za ajali barabarani katika vituo vya Polisi nchini upo katika hatua za manunuzi. Aidha, Wizara imeanza kufuatilia na kutathmini utendaji kazi wa vituo vya mizani kwa kutumia mfumo wa Ufuatiliaji wa Utendaji Kazi wa Mizani kwa masaa 24 kila siku kwa juma (24/7) katika mizani 13 zilizofungwa mfumo huo. Wizara inaendelea kufunga mfumo huo kwenye mizani nyine zilizobaki kote nchini.

Kwa upande wa mazingira, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 katika Sekta ya Ujenzi. Aidha, mfumo wa TEHAMA wa ukusanyaji wa taarifa za mazingira upo kwenye hatua za manunuzi. Vile vile Wizara imeendelea kushiriki katika maandalizi ya Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira (State of Environment Report III) yanayoratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais.

#### **MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

**95. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kupitia TANROADS imeendelea kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege kama ifuatavyo:

**96. Mheshimiwa Spika**, mradi wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**, kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha

2019/20 ni ujenzi wa jengo jipya la abiria, upanuzi na ukarabati wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la kuongozea ndege pamoja na miundombinu yake (mitambo ya kuongozea ndege), ujenzi wa kituo kidogo cha umeme, ujenzi wa kituo cha uangalizi wa hali ya hewa pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingilia uwanjani na maegesho ya magari.

Hadi Machi, 2020 mradi huu ulikuwa kwenye hatua za mwisho za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayeutekeleza.

**97. Mheshimiwa Spika**, katika mradi uliokamilika wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**, lengo la mwaka 2019/20 lilikuwa ni ujenzi wa uzio. Hadi Machi, 2020 Serikali ilikuwa inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kazi hii.

**98. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Songwe**, mikataba ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege imesainiwa. Aidha, Serikali kuititia TANROADS inaendelea na taratibu za manunuzi ya kumpata Mkandarasi wa kuendeleza ujenzi wa jengo la abiria baada ya Mkandarasi aliyekuwepo kusimamishwa.

**99. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Tabora**, lengo la mradi lilikuwa ni kutekeleza awamu ya tatu ya kuboresha kiwanja. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi za ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua jengo jipya la abiria, barabara ya kuingilia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, barabara ya kiungio na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhilli (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**, lengo la mradi lilikuwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa

taa na mitambo ya kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi hizo ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhili (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

**101. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**, lengo la mradi ilikuwa ni ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani na maegesho ya magari pamoja na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege na uzio wa usalama wa kiwanja cha ndege. Hadi Machi, 2020 mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa ajili ya kazi hizo ilikuwa imesainiwa. Wizara inasubiri idhini ya Mfadhili (No Objection) ili ianze hatua za utekelezaji wa kazi hizo.

**102. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**, kazi zilizopangwa ni kusimika taa za kuongozea ndege, ujenzi wa jengo jipya la abiria, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua.

Hadi Machi, 2020, kazi za ukarabati na upanuzi ambazo zilihusisha ujenzi wa maegesho ya ndege, ujenzi wa jengo la mizigo (Cargo Terminal) pamoja na maegesho ya ndege za mizigo, jengo la kuongozea ndege, kituo cha umeme, maegesho ya magari, kusimika taa za kuongozea ndege na mfumo wa maji safi, maji taka na maji ya mvua zimekamilika. Aidha, kazi ya mapitio ya usanifu wa jengo jipya la abiria inaendelea.

**103. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Arusha**, kazi zilizopangwa ni kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege kwa meta 200 na ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad). Kazi nyiningine ni ujenzi wa uzio wa usalama, kujenga barabara mpya ya kuingilia na kutoka kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari. Hadi Machi, 2020, mradi huu upo katika hatua ya manunuzi ya Mkandarasi.

**104. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**, kazi zilizopangwa ni kufanya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege pamoja na kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege. Kazi nyingine ni na ujenzi wa barabara ya kuingilia na kutokakiwanjani na maegesho ya magari. Hadi Machi, 2020 kazi hizo zilikuwa zimekamilika kwa asilimia 33.

**105. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro**, kazi zilizopangwa ni kufanya usanifu wa kina na kuanza ukarabati na upanuzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, ujenzi wa barabara mpya ya kiungio na usimikaji wa taa za kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020, taratibu za manunuzi ya Mhandisi Mshauri kwa ajili ya usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka ndege zilikuwa zinaendelea.

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 katika mradi wa **Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa** kazi zilizopangwa zilikuwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipywa cha mikoa ya Geita na Simiyu na upanuzi na ukarabati viwanja vya ndege vya Iringa, Songea, Lindi, Lake Manyara, Tanga na Musoma. Kazi nyingine ni kumalizia ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na mradi wa kiwanja cha ndege cha Dodoma pamoja na kuanza ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi na viwanja vingine vya mikoa.

Hadi Machi, 2020, ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege, barabara ya kiungio na maegesho ya ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Geita umefikia asilimia 78. Wizara inaendelea na manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja cha Musoma. Upanuzi wa kiwanja cha ndege cha Songea umefikia asilimia 34; Awamu ya kwanza ya ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Iringa ipo kwenye hatua ya manunuzi; manunuzi wa makandarasi kwa ajili ya viwanja vya Iringa (Awamu ya II), Lake Manyara na Tanga yanayoubiri idhini (no objection) kutoka Benki ya Dunia na ulipaji wa fidia wa kiwanja cha ndege cha Dodoma

umekamilika. Ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Moshi unashubiri upatikanaji wa fedha.

**107. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ujenzi wa **Kiwanja cha Ndege cha Msalato**, kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 ni kulipa fidia kwa mali zitakazoathirika na utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya mapitio ya upembizi na usanifu wa kina.

Hadi Machi, 2020, uhakiki kwa ajili ya ulipaji wa fidia ulikuwa unaendelea. Aidha, taratibu za awali za manunuzi ya kumpata Mkandarasi na Mhandisi Mshauri zilikuwa zinaendelea.

**108. Mheshimiwa Spika**, katika **Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**, kazi zilizopangwa zilikuwa ni usanifu wa kina kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na ufungaji wa taa za kuongozea ndege. Hadi Machi, 2020 Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu.

**109. Mheshimiwa Spika**, katika mradi wa ujenzi wa **Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III)** katika **Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**, lengo lilikuwa ni kukamilisha ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal Building III), kulipa fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila waliohamishwa kupisha utekelezaji wa mradi huu pamoja na kufanya Usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria (Terminal II). Hadi Machi, 2020 ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria umekamilika. Ulipaji fidia kwa wakazi wa Kipunguni na Kigilagila na Usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria (Terminal II) unashubiri upatikanaji wa fedha.

## **UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI**

### **Bodi ya Mfuko wa Barabara**

**110. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Barabara ulipanga kukusanya jumla ya **Shilingi**

**839,127,000,000** kwa ajili ya matengenezo ya barabara nchini. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 587,389,000,000** ni kwa ajili ya matengenezo ya barabara za kitaifa (Barabara Kuu na Barabara za Mikoa) ambazo husimamiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuititia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na **Shilingi 251,738,000,000** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia barabara za Wilaya ambazo husimamiwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Kati ya fedha hizo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ilitengewa **Shilingi 58,233,735,546**, TANROADS ilitengewa **Shilingi 524,103,619,914**, TARURA ilitengewa Shilingi **224,615,837,106**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ilitengewa **Shilingi 24,957,315,234** na **Shilingi 7,216,492,200** zilitengwa kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**111. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 Bodi imekusanya na kugawanya jumla ya **Shilingi 661,114,850,437.44** sawa na **asilimia 79** ya bajeti ya mwaka. Kati ya hizo, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) ilipokea **Shilingi 45,878,807,037.32**, TANROADS **Shilingi 412,909,263,335.92**; Ofisi ya Rais – TAMISEMI **Shilingi 19,662,335,504.29**, TARURA **Shilingi 176,961,019,538.14** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 5,703,425,021.77**.

**112. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha usimamizi wa mizani nchini, Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa kushirikiana na TANROADS na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imekamilisha uweki mfumo wa kielektroniki na kamera za CCTV kwenye vituo 13 vya mizani ya kupima uzito wa magari. Mfumo huo umewezesha taasisi husika kufuatilia moja kwa moja na kwa wakati (real time) jinsi upimaji wa magari unavyoendelea kwenye vituo vya mizani nchini. Mfumo huu utakapounganishwa na Mfumo wa Bodi ya Mfuko wa Barabara (RFB Management Information System), Bodi itakuwa na uwezo wa kujua magari yaliyozidisha uzito na faini iliyotozwa muda uleule.

**113. Mheshimiwa Spika**, Bodi kuititia Mtaalam Mshauri inaendelea na utafiti kuhusu uwezekano wa kuwa na

mgawanyo mpya wa fedha za Mfuko (Allocation Formula) zinazotengwa kwa ajili ya Barabara za Kitaifa (Barabara Kuu na za Mikoa) zinazosimamiwa na TANROADS na barabara za Wilaya zinazosimamiwa na TARURA. Aidha, Bodi inaendelea na taratibu za kufanya tathmini ya mtandao wa barabara (Road inventory and condition survey) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Matokeo ya tathmini hii yatasaidia kuboresha mipango na usimamizi wa matengenezo ya barabara kikamilifu na kwa wakati.

### **Wakala wa Majengo Tanzania**

**114. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wakala wa Majengo Tanzania ulipanga kumalizia ujenzi wa nyumba 5 za majaji Tanzania Bara katika mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kagera, Mtwara, Shinyanga na Tabora; kuendelea na ujenzi wa nyumba za Makazi, Magomeni Kota; ujenzi wa nyumba 50 za Viongozi Dodoma, nyumba 5 za watumishi mikoa mipyä pamoja na ujenzi wa nyumba ya Makazi kwenye lkulu ya Chamwino, Dodoma.

Wakala vilevile ulipanga kufanya ukarabati wa nyumba za iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA); ukarabati/ Matengenezo nyumba za viongozi Jijini Dodoma; ukarabati wa Karakana za Wakala kwa mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Arusha, Mwanza, Mbeya na Dodoma pamoja na ununuzi wa samani kwa nyumba 55 za viongozi mkoani Dodoma na Mikoa mipyä. Aidha, Wakala ulipanga kuendelea kutoa huduma ya ushauri katika ujenzi na marekebisho ya majengo ya Serikali pamoja na kuendesha programu za kuwajengea uwezo Wataalam wa Ujenzi na Ushauri.

**115. *Mheshimiwa Spika*,** hadi kufikia Machi, 2020, miradi iliyotekelzwa na Wakala wa Majengo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi ya Mkandarasi katika Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ukarabati wa nyumba **34** na ujenzi wa nyumba **3**.

**116. Mheshimiwa Spika**, Wakala vilevile umefanikiwa kukarabati nyumba **139** Dar es Salaam na Mikoani, Hati Miliki **19** zimepatikana tayari kwa Mikoa ya Tabora (1), Geita (10), Kilimanjaro (1), Mwanza (2), Katavi (1), Manyara (2), Shinyanga (1) na Iringa (1). Aidha, michoro pamoja na gharama za mradi wa ujenzi wa nyumba **5** katи ya nyumba 100 za watumishi wa umma Dodoma vimeandaliwa.

**117. Mheshimiwa Spika**, Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi **47** ya Ubunifu na Ujenzi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Kigamboni umekamilika, Jengo la utawala la Ofisi ya Wilaya ya Mlele (asilimia 30), Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama (asilimia 47), Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara (asilimia 40), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya Mkalama (asilimia 51), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Ubungo (asilimia 98), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega (asilimia 95), majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato (asilimia 89), mradi wa jengo la Ofisi ya TANROADS – Dodoma (asilimia 25) na jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo (asilimia 50).

**118. Mheshimiwa Spika**, vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi 38 ya ujenzi. Baadhi ya miradi hiyo ni ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma awamu ya pili, ujenzi wa Jengo la Mionzi na Upasuaji, jengo la Maabara pamoja na banda la kuunguzia taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mko ya Simiyu ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mko Tabora na hospitali ya Rufaa ya Mko wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ukarabati wa jengo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu awamu ya kwanza (asilimia 95), ukarabati wa nyumba tisa za viongozi wa Serikali Wilaya ya Mwanga (asilimia 75), ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Madaba - Songea awamu ya pili (asilimia 63), ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mko Songwe awamu wa pili (asilimia 80), ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mko wa Iringa (asilimia 43) na ujenzi wa jengo la

maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (asilimia 95).

**119. Mheshimiwa Spika**, Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi 81 ya ushauri. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya kwanza kwenye Mji wa Serikali (Government City) Dodoma, ujenzi wa jengo la hospitali ya Wilaya ya Kilolo, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoo wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya pili ambao uko kwenye hatua za mwisho ya ubunifu, ujenzi wa Ofisi za maji Kimani na Mkoji (asilimia 65), ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda (asilimia 87), ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama (asilimia 95), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga (asilimia 85), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa pamoja na Msanzi (asilimia 100), ukarabati upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu katika mikoa mitano (asilimia 70) na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoo wa Simiyu (asilimia 25).

**120. Mheshimiwa Spika**, vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi miwili ya usimamizi. Miradi hiyo ni ujenzi wa majengo ya rada katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe ambapo ujenzi umekamilika katika mikoa mitatu isipokuwa mkoa wa Songwe (asilimia 95). Mradi mwingine ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhia nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula (National Food Reserve Agency) katika mikoa nane ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Songwe (asilimia 50).

**121. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2020, miradi iliyotekeliza na Wakala wa Majengo ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa kambi ya Mkandarasi katika Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Mwalimu Nyerere, ukarabati wa nyumba 34 na ujenzi wa nyumba 3 pamoja na ujenzi wa nyumba za makazi zenye uwezo wa kubeba kaya 656 zilizopo Magomeni Kota Dar es Salaam ambao umefika asilimia sabini (70). Aidha, ukarabati wa Karakana za TBA katika mikoa sita

(6) ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Tabora, Mbeya na Dodoma unaendelea.

**122. *Mheshimiwa Spika***, Wakala vilevile umefanikiwa kukarabati nyumba 139 Dar es Salaam na Mikoani, Hati Miliki 19 zimepatikana tayari kwa Mikoa ifuatayo:- Tabora 1, Geita 10, Kilimanjaro 1, Mwanza 2, Katavi 1, Manyara 2, Shinyanga1, Iringa 1. Aidha, michoro pamoja na gharama za mradi wa ujenzi wa nyumba 5 kati ya nyumba 100 za watumishi wa umma Dodoma vimeandaliwa.

**123. *Mheshimiwa Spika***, hadi kufikia Machi, 2020 Wakala umetekeleza jumla ya Miradi 47 ya Ubunifu na Ujenzi. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Kigamboni pamoja na Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Kigamboni umekamilika, Jengo la utawala la Ofisi ya Wilaya ya Mlele (asilimia 30), Jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Butiama (asilimia 47), Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara (asilimia 40), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya Mkalama (asilimia 51), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Ubungo (asilimia 98), Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega (asilimia 95), majengo ya hospitali ya rufaa Geita na Chato (asilimia 89), mradi wa jengo la Ofisi ya TANROADS – Dodoma (asilimia 25) na jengo la Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ubungo (asilimia 50).

**124. *Mheshimiwa Spika***, Wakala vilevile umetekeleza jumla ya miradi 38 ya ujenzi. Baadhi ya miradi hiyo ni Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, ujenzi wa Jengo la Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Tunduma awamu ya pili, ujenzi wa Jengo la Mionzi na Upasuaji, jengo la Maabara pamoja na banda la kuunguzia taka katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Simiyu ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Tabora na hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ukarabati wa jengo la Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu awamu ya kwanza (asilimia 95), ukarabati wa nyumba tisa za viongozi wa Serikali Wilaya ya Mwanga (asilimia 75), ujenzi wa jengo la Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya Madaba - Songea awamu

ya pili (asilimia 63), ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Songwe awamu wa pili (asilimia 80), ukarabati wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Iringa (asilimia 43) na ujenzi wa jengo la maktaba Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (asilimia 95).

**125. *Mheshimiwa Spika*,** Wakala pia umetekeleza jumla ya miradi 81 ya ushauri. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya kwanza kwenye Mji wa Serikali (Government City) Dodoma, ujenzi wa jengo la hospitali ya Wilaya ya Kilolo, ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tabora ambayo imekamilika. Miradi mingine ni ujenzi wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali awamu ya pili ambao uko kwenye hatua za mwisho ya ubunifu, ujenzi wa Ofisi za maji Kimani na Mkoji (asilimia 65), ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Mji wa Bunda (asilimia 87), ujenzi wa makazi ya Mkuu wa Wilaya ya Butiama (asilimia 95), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Laela Sumbawanga (asilimia 85), ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Mtowisa pamoja na Msanzi (asilimia 100), ukarabati upanuzi na ujenzi wa miundombinu ya Mahakama Kuu katika mikoa mitano (asilimia 70) na ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu (asilimia 25).

**126. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile Wakala umetekeleza jumla ya miradi miwili ya usimamizi. Miradi hiyo ni ujenzi wa majengo ya rada katika mikoa minne ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Songwe ambapo ujenzi umekamilika katika mikoa mitatu isipokuwa mkoa wa Songwe (asilimia 95). Mradi mwingine ni ujenzi wa Vihenge (Silos) vya kuhifadhi nafaka pamoja na maghala kwa ajili ya hifadhi ya chakula (National Food Reserve Agency) katika mikoa nane ya Dodoma, Katavi, Manyara, Njombe, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Songwe (asilimia 50).

### **Wakala wa Ufundu na Umembe**

**127. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara kuitia Wakala wa Ufundu na Umembe Tanzania (TEMESA) ilipanga kuendelea na kazi zifuatazo: Upanuzi wa

maegesho upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati na Mafia kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Mafia, ujenzi wa maegesho ya Kayenze na Bezi kwa ajili ya kivuko cha Kayenze – Bezi, ujenzi wa maegesho ya Mlimba na Malinyi kwa ajili ya kivuko cha Mlimba – Malinyi na maegesho ya Itungi *Port*. Kazi nyingine ni ujenzi na ukarabati wa maegesho ya Kigongo na Busisi kwa ajili ya kivuko cha Kigongo – Busisi, maegesho ya Kilambo na Namoto kwa ajili ya kivuko cha Kilambo – Namoto pamoja na maegesho ya Utete na Mkongo kwa ajili ya kivuko cha Utete – Mkongo.

Wakala vilevile ulipanga kuendelea na ujenzi wa vivuko vipyta vitakavyotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati - Mafia, Bugorola – Ukara, Kayenze – Bezi na Chato – Nkome. Aidha, Wakala ulipanga kufanya manunuvi ya boti tano (5) zitakazotoa huduma ya usafiri kati ya Lindi – Kitunda, Ukerewe (Ilungwa, Nafuba na Gana) na Magogoni – Kigamboni pamoja na manunuvi ya vitendea kazi kwa ajili ya karakana za TEMESA.

**128. Mheshimiwa Spika**, vilevile Wakala ulipanga kukamilisha ukarabati wa MV Sengerema, MV Kigamboni na MV Misungwi. Aidha, Wakala ulipanga kukarabati MV Tegemeo, MV Mara, MV Ujenzi, MV Ruhuhu na MV KIU. Wakala pia ulipanga kujenga karakana tano (5) mpya katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana mpya ya kisasa makao makuu ya Serikali (Dodoma) pamoja na kukarabati karakana tano (5) ambazo ni karakana ya Dar es Salaam (MT. Depot), Mtwara, Mbeya, Mwanza na Arusha. Aidha, Wakala ulipanga kuendelea na jukumu lake la msingi la kufanya matengenezo ya magari ambapo magari **46,604** yalipangwa kufanyiwa matengenezo. Kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa ni usimikaji na matengenezo ya mifumo ya umeme, elektroniki, viyoyozi na majokofu.

**129. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 ujenzi wa maegesho ya Kayenze na Bezi pamoja na awamu ya kwanza

ya upanuzi wa jengo la abiria katika maegesho ya Magogoni – Kigamboni upande wa Kigamboni mkoani Dar es Salaam umekamilika na awamu ya pili ya upanuzi wa jengo la abiria na eneo la maegesho ya Kigamboni imeanza. Aidha, ujenzi wa maegesho ya Mlimba na Malinyi pamoja na maegesho ya Itungi *Port* unaendelea, ujenzi wa maegesho ya Bukondo umeanza na ujenzi wa maegesho ya Zumacheli katika kivuko cha Chato – Nkome na maegesho ya Nyamisati – Mafia upo katika hatua ya kumpata mkandarasi.

**130. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa miradi ya ujenzi wa vivuko, kazi za ujenzi wa kivuko kipywa cha Kayenze – Bezi imekamilika. Aidha ujenzi wa kivuko cha Nyamisati – Mafia (Pwani) umefikia asilimia 40, Bugolora – Ukara (Mwanza) umefikia asilimia 70 na Chato - Nkome umefikia asilimia 70. Aidha, ununuzi wa boti mpya 4 za uokozi kwa ajili ya kisiwa cha Ukerewe (Ilugwa, Nafuba na Gana) na Magogoni - Kigamboni pamoja na boti moja ya uokozi kwa kivuko cha Lindi – Kitunda unaendelea.

**131. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa ukarabati wa vivuko, ukarabati mkubwa wa vivuko MV Sengerema na MV Kigamboni upo katika hatua za mwisho za kukamilika. Aidha, ukarabati wa MV Misungwi unaendelea. Vilevile Wakala upo katika hatua za uchambuzi wa zabuni kwa ajili ya ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara pamoja na boti MV KIU.

**132. *Mheshimiwa Spika*,** TEMESA imeendelea kutekeleza majukumu ya matengenezo ya magari ambapo hadi Machi, 2020 jumla ya magari **15,960** yalifanyiwa matengenezo. Aidha, miradi **392** ya umeme, miradi **474** ya viyoyozi na miradi **562** ya kieletroniki imetekelezwa. Vilevile, Wakala ulitekeleza miradi ya ushauri wa kihandisi ambapo miradi **16** ni ya umeme, **17** ya majokofu na viyoyozi na **5** ya elektroniki (ICT). Aidha, Wakala umeendelea kusimamia na kuendesha vivuko vya Serikali **30** katika vituo **20** mbalimbali nchini pamoja na kutoa huduma za ukodishaji wa magari na mitambo katika mikoa **19** na kituo kimoja cha *Government Transport Agency* (GTA).

## Bodi ya Usajili wa Wahandisi

**133. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20 Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB) iliweka malengo ya kusajili wahandisi **2,846**, mafundi sanifu **400**, Kampuni za Ushauri wa Kihandisi **23**, kusimamia mafunzo ya kujiedeleza kitaaluma kwa wahandisi wataalam na wahandisi washauri (CPD), kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (SEAP) **3,000** pamoja na kukagua shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa wenyewe kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi.

Hadi Machi, 2020, Bodi imesajili wahandisi **2,073** na Kampuni za ushauri wa kihandisi **11**. Idadi hii imefikisha jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali kuwa **27,739** na makampuni ya ushauri wa kihandisi kuwa **359**. Kati ya Wahandisi hao, **25,401** ni Wahandisi wazalendo na **2,338** ni wa kigeni. Kampuni za ushauri wa kihandisi za kizalendo ni **246** na za kigeni ni **113**. Aidha, katika kipindi hicho, Bodi ilifuta usajili kwa wahandisi watalaamu **417**, Wahandisi Washauri **46** na kampuni za ushauri wa Kihandisi **104** kwa kukiuka Sheria ya Usajili wa Wahandisi. Aidha, katika kipindi hiki, jumla ya miradi **81** ilikaguliwa. Wahandisi wa kigeni **97** walibainika kufanya kazi bila usajili ambapo kati yao **65** walikuwa na sifa na hivyo waliosajiliwa, na **32** hawakuwa na sifa na hivyo kurejeshwa kwenye nchi zao. Vilevile, Bodi ilianda warsha 4 katika kanda **4** kwa Wahandisi Wataalam wanaosimamia mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu.

**134. Mheshimiwa Spika**, vilevile, Bodi iliendesa Kiapo cha Utii kwa Taaluma (Professional Oath) ambapo jumla ya wahandisi **3,745** walipishwa. Aidha, Bodi iliendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Mafunzo kwa Vitendo kwa wahandisi wahitimu **2,796**. Jumla ya wahandisi wahitimu **7,582** wamepitia Mpango huu tangu uanzishwe mwaka 2003. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na Bodi nyingine za Sekta ya Ujenzi (CRB na AQRB) zilianda na kuadhimisha Siku ya Wahandisi 2019 (Annual Engineers' Day 2019 ambayo ilihudhuriwa na wahandisi zaidi ya **3,830**. Mada ilijojadiliwa

katika siku ya wahandisi ilikuwa ni "*wajibu wa Wadau wa Sekta ya Ujenzi katika kufikia uchumi endelevu kwa ustawi wa Jamii*".

### **Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

**135. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi ilipanga kusajili Wataalam **117** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi ilipanga kusajili kampuni **15** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Vile vile Bodi ilipanga kuwajengea uwezo wahitimu **60** katika fani za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na fani zinazoshabihiana nazo kupitia mpango maalumu wa mafunzo kwa vitendo. Bodi pia ilipanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote ya Tanzania bara na miradi ya majengo **950**. Aidha, katika kutangaza huduma zake na za wataalamu inaowaratibu.

Hadi Machi, 2020 Bodi imesajili Wataalam **75** ikiwa ni asilimia **64** ya malengo. Aidha, kampuni **16** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi zilisajiliwa ikiwa ni asilimia 107 ya malengo. Vilevile wahitimu **108** katika fani za Ubunifu Majengo, Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo walipatiwa mafunzo kupitia mpango maalumu wa mafunzo kwa vitendo ikiwa ni asilimia 180 ya malengo.

Vilevile, miradi ya ujenzi **1,254** ilikaguliwa ikiwa ni asilimia 63 ya malengo ambapo wataalam na waendelezaji wake walichukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kusimamishiwa ujenzi na kufunguliwa mashtaka mahakamani. Kazi nytingine zilizotekelizwa na Bodi ni usajili wa miradi ya majengo **555** ikiwa ni asilimia **58** ya malengo.

### **Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

**136. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Bodi ilipanga kusajili jumla ya Makandarasi wapya **900** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100**. Aidha, Bodi ilipanga kuendesha kozi nane (8) za mafunzo katika mikoa ya Dar es

Salaam, Mwanza, Mtwara, Arusha, Bukoba, Njombe, Dodoma na Morogoro.

Hadi Machi, 2020 Bodi imesajili jumla ya Makandarasi wapya **718** hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia **11,060**. Aidha, jumla ya miradi **2,711** ilikaguliwa ambapo jumla ya miradi **719** sawa na asilimia **26.5** ilipatikana na mapungufu mbalimbali yakiwemo kutozingatia afya na usalama kazini, kutosajili miradi na kufanya kazi za thamani inayozidi kiwango kinachoruhusiwa kwa daraja husika. Makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

Bodi iliendesa kozi **5** za mafunzo kuitia Mpango Maalum wa Mafunzo Endelevu kwa Makandarasi (Sustainable Structured Training Programme – SSTOP) katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kagera, Mtwara na Mwanza. Jumla ya makandarasi **441** walishiriki katika mafunzo hayo. Bodi pia iliendelea kuendesha Mfuko wa Kusaidia Makandarasi (Contractors Assistance Fund - CAF) unaotoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani walio katika daraja la chini na la kati ili kuwezesha ushiriki wa makandarasi wa ndani katika zabuni na utekelezaji wa miradi mbalimbali. Mfuko huu umeendelea kuwa na mtaji wa **Shilingi bilioni 3.75** kwa mwaka 2019/20. Aidha idadi ya wanachama wa Mfuko ilipungua kutoka **1,186** mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia **1,134** mwaka 2019/2020. Kushuka kwa idadi ya wanachama kumetokana na zoezi la kufuta makandarasi waliokosa sifa ya kuendelea na ukandarasi kwa mujibu wa sheria iliofanyiwa marekebisho mwishoni mwa mwaka 2019.

### **Baraza la Taifa la Ujenzi**

**137. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC) lilitekeleza majukumu mbalimbali ikiwemo kutoa ushauri wa kiufundi kwa wadau mbalimbali wa Sekta ya Ujenzi na kutoa mafunzo ya Usimamizi wa Mikataba katika miradi ya ujenzi kwa wadau **42** kutoka

taasisi mbalimbali za umma na binafsi. Kazi nyingine zilizofanyika ni utatuzi na usuluhishi wa migogoro ambapo hadi Machi, 2020 Baraza limefanya utatuzi wa mashauri **144** na usuluhishi wa mashauri **26** kwa njia ya *Adjudication*. Katika kipindi hiki migogoro mipyä iliyosajiliwa ilikuwa **37** kwa *Arbitration* na **8** ya *Adjudication*.

**138. Mheshimiwa Spika**, Baraza pia limeendelea kufanya tafiti kuhusu ushiriki wa wataalam washauri wa ndani (local consultants) katika kutekeleza miradi ya ujenzi, tathmini ya gharama za ujenzi wa majengo yaliyokamilika ili kupata viwango vya gharama (unit cost) ya ujenzi wa majengo ya aina mbalimbali na tathmini ya mafanikio na changamoto za utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa njia ya "Design and Build". Aidha, Baraza liliifanya ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi **42** iliyohusisha miradi ya barabara **38** na **4** ya madaraja inayotekelizwa kwa kutumila fedha za Mfuko wa Barabara inayosimamiwa na TANROADS na TARURA mkoa wa Dar es Salaam.

**139. Mheshimiwa Spika**, Baraza pia limeendelea na jukumu la kukusanya takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi kwa mwaka 2019/20 ili kuwezesha wadau wa Sekta ya Ujenzi kufuatilia ukuaji wa sekta. Aidha, Baraza liliendelea kukusanya na kuandaa bei za vifaa vya ujenzi na viwango vya mabadiliko ya bei hizo "indices" kwa ajili ya usimamizi wa mabadiliko ya bei ya miradi (Price Fluctuation Formula). Baraza limeandaa na kuchapisha nakala 1,000 za kitabu chenye taarifa za huduma ya vifaa vya ujenzi kwa mwaka 2019/20 (Directory of Construction Materials 2019/20) na lilikuwa linakamilisha uchapishaji wa Jarida la "Construction Business Journal Vol 13, Issue 1/2" la Februari 2020.

**140. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kuratibu Mpango wa kukuza uwazi na uwajibikaji "Construction Sector Transparency Initiative (CoST)" kupitia ufadhili wa *CoST International Secretariat* ambapo semina kwa taasisi nunuzi za umma na asasi za kiraia Mkoa wa Dodoma juu ya umuhimu wa uwazi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi zimetolewa.

## **Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

**141. *Mheshimiwa Spika***, Kituo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuimarisha/kuboresha sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa ujumla kwa kutumia mbinu ya ukusanyaji na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya ujenzi na uchukuzi kwa wadau.

Katika mwaka wa fedha 2019/20, Kituo kilifanya kazi zifuatazo:

- i. Kituo kimeshiriki katika mkutano mmoja wa kimataifa na mikutano miwili ya ndani ya nchi inayohusu ubunifu na usambazaji wa teknolojia katika sekta ya Ujenzi na Usafirishaji.
- ii. Kituo kilishiriki katika Mkutano wa Kamati ya Kujenga Uwezo ya SADC (Regional Technology Transfer and Capacity Building Committee) chini ya Shirikisho la Mamlaka za Barabara za nchi za SADC uliofanyika Lusaka Zambia kwenye masuala yanayohusu usambazaji wa teknolojia katika Sekta ya Ujenzi na usafirishaji.
- iii. Kituo kimeandaa na kuchapisha nakala 300 za jarida la kituo lenye mada mbalimbali zinazohusu teknolojia, usalama barabarani na agenda mbalimbali za Serikali ya Awamu ya Tano katika kukuza miundombinu ya usafirishaji. Awamu ya tatu ya jarida hilo ipo katika hatua za maandalizi
- iv. Kituo kilishirikiana na Shirikisho la Barabara Tanzania (Tanzania Road Association – TARA) kuandaa *International training on Road Safety Engineering and Audit* iliyo fanyika Dar es Salaam na Arusha.
- v. Kituo kimeendelea kutoa huduma za maktaba kuhusu Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji na kutekeleza mradi unaolenga kuboresha mifumo na njia za Kituo za utunzaji wa kumbukumbu na upashanaji wa habari za teknolojia.

### C.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI

**142. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,629,130,373,895** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

#### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**143. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) ilitengewa **Shilingi 85,408,131,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 58,337,187,000** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 27,070,944,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia Machi, 2020, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilichotolewa kwa Sekta ya Uchukuzi na Taasisi zake ni **Shilingi 53,404,102,071.14** sawa na asilimia 62.5 ya bajeti iliyoidhinishwa.

#### Bajeti ya Maendeleo

**144. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Sekta ya Uchukuzi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,543,722,242,895** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,327,716,600,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 216,005,642,895** ni fedha za Nje (mkopo) kutoka Benki ya Dunia. Hadi Machi, 2020, jumla ya fedha zilizokuwa zimetolewa ni **Shilingi 1,009,049,881,683**. Kati ya fedha zilizotolewa, **Shilingi 863,848,881,683** ni fedha za Ndani na Shilingi **145,201,000,000** ni fedha za Nje. Aidha, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* uliendelea kutumia **Shilingi 455,623,760,000** zilizobaki katika bajeti ya Mradi huo mwaka 2018/2019 ambazo ziliwekwa katika Akaunti ya Amana (Deposit). Hivyo, kwa ujumla fedha zilizotumika katika utekelezaji wa Miradi katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ni **Shilingi 1,464,673,641,683** sawa na asilimia **41.3** ya bajeti ya Maendeleo mwaka 2019/20. Utumiaji wa fedha uliathiriwa na mvua kubwa zaidi ya kiwango iliyonyesha kuanzia mwezi Oktoba, 2019 ambapo kazi za ujenzi wa reli ya SGR na

ukarabati wa reli ya kati ya *Metre Gauge* (MGR) zilisimama mara kwa mara.

## **HUDUMA ZA USAFIRI MIJINI NA VIJJINI**

### **Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Barabara**

**145. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilioanzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 3 ya Mwaka 2019, imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa abiria na mizigo mijini na vijijini inapatikana kulingana na mahitaji ya wananchi na ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya Leseni 41,826 za usafirishaji Abiria zilitolewa ikilinganishwa na Leseni 43,356 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Hii ikiwa ni upungufu wa asilimia 3.53. Kupungua kwa Leseni za Mabasi kulitokana na kupungua kwa mabasi madogo katika njia kuu; na baadhi ya mabasi kukosa sifa ya kutoa huduma na hivyo kuzuiliwa kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Leseni za Malori 94,902 zilitolewa ikilinganishwa na Leseni 84,299 zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 12.58.

**146. Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia LATRA imeendelea kudhibiti Viwango vya Tozo na nauli katika usafiri wa barabara kwa kuzingatia maboresho ya barabara kwa kiwango cha lami, kuanzishwa njia mpya na maombi maalum ya watoa huduma. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka ilifanya mapitio ya viwango vya nauli za mabasi na kuhuisha viwango hivyo kwa njia za Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Njombe, Manyara, Katavi, Dodoma, Rukwa, Kigoma na Pwani. Taarifa kuhusu viwango hivyo inapatikana kupitia tovuti ya Mamlaka ([www.latra.go.tz](http://www.latra.go.tz)). Aidha, katika kipindi hicho, Mamlaka ilifanya ufuutiliaji wa taarifa zilizoashiria kuwepo kwa ukiritimba katika utoaji wa huduma kwa njia ya Dar es Salaam – Songea kupitia Lindi ili kujiridhisha na ubora wa huduma inayotolewa, nauli na kiwango cha ushindani. Katika uchunguzi huo, ilibainika kuwa huduma inayotolewa ni ya ubora unaokubalika na nauli

zilionekana kuwa chini ya nauli elekezi iliyotolewa na Mamlaka.

**147. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuchukua hatua ili kupunguza ajali zinazoendelea kutokea. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuimarisha usalama wa huduma za usafiri wa nchi kavu, kuepuka makosa ya kibinadamu katika vivuko vya Reli na Barabara na kudhibiti waendesha pikipiki (bodaboda). Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, LATRA ilifanya kaguzi za barabarani kwa Malori, Mabasi, Pikipiki na Bajaji zipatazo 800 katika Mikoa 26. Lengo ni kubaini utekelezaji wa masharti ya Leseni na kufuatilia utendaji wa Mfumo wa Kudhibiti Mwendo kasi (Vehicle Tracking System). Mfumo huo ulibaini matukio 17,895 ya Mabasi kutembea zaidi ya mwendo unaokubalika kwa Mabasi hayo. Mabasi hayo yalichukuliwa hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuwatoza faini na kufungia baadhi ya Mabasi kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria.

**148. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Mifumo ya Kielektroniki inatumika katika usafiri wa Nchi Kavu. Utumiaji wa Mifumo hii unarahisisha utendaji kazi, kuongeza uwazi na uwajibikaji, kudhibiti mapato ya Serikali, kutoa takwimu sahihi, kupunguza gharama za uendeshaji na kusaidia kuondoa changamoto ya wapiga debe kwenye vituo vya mabasi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka iliendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Vyombo vya Uchukuzi (Vehicle Tracking System - VTS). Vyombo hivyo ni Mabasi ya masafa marefu na Treni. Lengo ni kuimarisha shughuli za udhibiti wakati wote na mahali popote vyombo hivyo vilipo. Hadi Machi, 2020, jumla ya Mabasi ya masafa marefu 4,030 na Treni tatu (3) zilikuwa zimeunganishwa kwenye mfumo huo. Kazi ya uunganishaji wa Mabasi mengine zaidi katika mfumo huu inaendelea kwa Mabasi yote yanayotoa huduma kwenye njia ndefu na fupi.

Aidha Machi 2020 LATRA ilizindua mfumo wa Tiketi za kielektroniki kwa mabasi ya Abiria.

Napenda kuwasihî wamiliki wote wa vyombo vya usafiri kuitia ushirika wao waongeze juhudî za kutoa Tiketi za Kielektroniki. Tunakoelekea, Tiketi zisizo za Kielektroniki hazitatambulika kabisa. Utaratibu huu utasaidia katika kurahisisha upatikanaji wa huduma na udhibiti wa mapato yatokanayo na huduma inayotolewa.

#### **Udhibiti wa Usafiri kwa Njia ya Reli**

**149. Mheshimiwa Spika**, usafiri kwa njia ya Reli umeendelea kudhibitiwa na LATRA. Mamlaka hii imeendelea kutoa huduma za udhibiti ili kuboresha usalama wa usafiri wa Treni nchini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka imefanya ukaguzi wa usalama wa Treni, Mabehewa ya Mizigo na Abiria, na madaraja ya Treni; ufuatiliaji wa vyanzo vya ajali za Treni na umwagikaji wa mafuta katika njia zote za Reli zinazoendeshwa na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) na Shirika la Reli (TRC). Kazi nyingine zilizotekelizwa ni ufungaji wa Mfumo wa *Vehicle Tracking System* kwenye vichwa vitatu (3) vya Treni ya TAZARA kwa ajili ya majaribio. Baada ya kukamilika kwa majaribio hayo, vichwa vyote vya Treni vitafungwa Mfumo huo ili kuboresha utendaji na kuongeza ufanisi wa usafiri wa Reli.

**150. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kujiardaa na utoaji wa huduma za usafiri wa Reli ya Kati ya *Standard Gauge* (SGR). Katika maandalizi hayo TRC limekabidhiwa orodha ya Viwango vya Ukaguzi wa mwisho wa Miundombinu ya SGR (SGR Commisioning Checklist) ili kuliandarda Shirika kutambua vipengele muhimu vya kiusalama na viwango vitakavyotumika kwenye ukaguzi wa mwisho wa SGR kabla ya kuanza kutumika. Aidha, ili kuwapa watendaji wa Shirika la Reli uelewa wa vipengele vya kiusalama vya SGR, Disemba, 2019, LATRA iliratibu zoezi la utoaji wa mafunzo ya kitaalam kwa watendaji 50 wa TRC.

#### **Huduma za Usafiri wa Treni Mijini**

**151. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kutekeleza maelekezo ya llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 katika eneo la uboreshaji wa utoaji wa huduma za usafiri

katika Jiji la Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa Magari barabaran. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya abiria 1,626,194 waliosafirishwa kwa njia ya Reli kati ya Stesheni za Dar es Salaam na Mwakanga kwa kutumia Reli ya TAZARA. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 4.3 ikilinganishwa na abiria 1,700,685 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Upungufu uliojitokeza umetokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika ussafiri wa Barabara na kufunguliwa kwa barabara ya juu eneo la TAZARA (Mfugale Flyover).

Kwa upande wa TRC, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Abiria waliohudumiwa kati ya Stesheni ya Kamata - Ubungo na Pugu ni 2,421,258 ikilinganishwa na abiria 3,077,966 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Sababu za kushuka kwa utendaji ni pamoja na kuhamishwa kwa kituo (Station) kutoka Stesheni ya Dar es Salaam kwenda Kamata ili kupisha ujenzi wa Reli ya SGR na kukamilika kwa daraja la juu la Mfugale ambalo limepunguza msongamano katika eneo la makutano la TAZARA.

### **Shirika la Reli Tanzania (TRC)**

**152. Mheshimiwa Spika**, katika Hotuba ya mwaka 2019/2020, tuliahidi kuendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza ya Mradi wa Reli ya kati kwa *Standard Gauge* kutoka Dar es salaam hadi Mwanza (Km 1,219). Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia Machi, 2020, ujenzi wa kipande cha reli kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300) umekamilika kwa asilimia 76.63. Kazi zilizotekelze wa ni pamoja na:

- i. Ujenzi wa Makalvati umekamilika kwa asilimia 97;
- ii. Ujenzi wa Madaraja umekamilika kwa asilimia 76;
- iii. Ujenzi wa Daraja refu katikati ya Jiji la Dar es Salaam lenye urefu wa kilomita 2.54 umekamilika kwa asilimia 85.04;
- iv. Kazi ya ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde (earthworks) umekamilika kwa asilimia 83.14;

v. Ujenzi wa Miundominu ya umeme kwa ajili ya kuendeshea Treni umekamilika kwa asilimia 82;

vi. Utandikaji wa Reli umekamilika kilometra 73; na

vii. Kazi ya ujenzi wa Stesheni za Dar es Salaam, Pugu, Soga, Ruvu na Ngerengere umekamilika kwa asilimia 48.08.

**153. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2020, ujenzi wa Reli sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (km 422) umekamilika kwa asilimia 28 na ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Februari, 2021. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni pamoja na utwaaji wa ardhi; ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde kwa ajili ya kujenga tuta la reli (earthworks). Aidha, majadiliano na mtoa huduma (Manufacturer) kuhusu ujenzi wa mabehewa ya abiria yatakayotumika kutoa huduma ya usafiri wa abiria kwenye reli ya *Standard Gauge* yanaendelea.

**154. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ujenzi wa vipande viliwyobaki vyta Makutupora – Tabora (km 295), Tabora – Isaka (km 133), na Isaka – Mwanza (km 250), upembuzi yakinifu na usanifu wa awali umekamilika na Serikali imepanga kuanza ujenzi huku ikiendelea na juhudini za kutafuta fedha. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na Taasisi za fedha na washirika wa maendeleo. Walioonesha nia hadi sasa ni pamoja na Benki ya Maendeleo ya Biashara (Trade Development Bank - TDB) na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

**155. Mheshimiwa Spika**, njia ya reli ya Kati inayotumika sasa (Meter Gauge Railway - MGR) ni muhimu kwa kusafirisha mizigo, abiria na bidhaa mbalimbali kuelekea katika maeneo ya kanda za Ziwa, Magharibi na Kaskazini mwa nchi yetu. Pia, njia hii inatumika kusafirisha mizigo inayoeklea nchini Uganda, DR Congo, Rwanda na Burundi. Ili reli hii iendelee kutoa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kusaidia katika ujenzi wa reli ya SGR, kazi ya ukarabati wa njia ya reli kwa kuondoa reli zote nyepesi na kuweka reli mpya zenye uzito wa ratili 80 kwa yadi kati ya stesheni ya Dar es Salaam na Isaka

imeendelea kutekelezwa. Kazi ya ukarabati wa sehemu ya Dar es Salaam hadi Kilosa (km 283) imekamilika kwa asilimia 83.7 na inatarajiwa kukamilika Juni, 2020. Aidha, sehemu ya Kilosa hadi Isaka (km 687) imekamilika kwa asilimia 85 na itakamilika mwishoni mwa Mei, 2020.

**156. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ufufuaji wa njia ya reli ya kutoka Tanga hadi Arusha (km 439), Serikali kupitia TRC inaendelea na ukarabati wa reli hii ili kutoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo. Aidha, kazi ya ukarabati wa reli imekamilika kwa kipande cha Tanga hadi Moshi (km 353) na njia inapitika. Ukarabati kwa kipande cha Moshi hadi Arusha (km 86) unaendelea na kazi ya urudishaji njia imefikia asilimia 95 wakati kazi ya kubadilisha reli zenyе uzito wa ratili 45 kwenda uzito wa ratili 60 imefikia asilimia 40. Lengo ni kukamilisha kazi hizo ifikapo Juni, 2020.

**157. Mheshimiwa Spika**, mvua zilizonyesha kuanzia Oktoba, 2019 zilileta athari kubwa katika miundombinu ya uchukuzi nchini. Kwa upande wa miundombinu ya Reli, mvua hizi ziliathiri kwa kiasi kikubwa miundombinu hiyo hususan Reli ya Kati inayotumika sasa (Meter Gauge Railway - MGR). Katika Kipindi cha Oktoba, 2019 hadi Januari, 2020, Reli ya Tanga hadi Arusha ilifungwa kutokana na uharibifu wa reli uliosababishwa na mvua katika maeneo ya Mkalamo - Korogwe Korogwe na Muheza. Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Februari 2020, huduma za usafiri wa abiria na mizigo kwa watumiaji wa Reli ya Kati kuanzia Dar es Salaam hadi Mwanza na Kigoma pia iliathirika baada ya eneo la Zuzu – Kigwe – Bahi na Kilosa – Gulwe kujaa maji kutokana na mvua. Vile ville, reli ya Kaliua hadi Mpanda ilisombwa na maji eneo la Mto Ugala na kusababisha kusitisha huduma mapema Aprili 2020. Hata hivyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuhakikisha kuwa huduma zinarejea haraka. Hatua hizo ni pamoja na kurudisha miundombinu iliyoharibiwa, kukarabati madaraja na mifereji ili kuruhusu maji kupita kwa haraka na kuendelea kufanya tafiti ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa athari za maji ya mvua.

**158. Mheshimiwa Spika**, miradi mingine iliyоendеlea kutekelezwa katika mwaka 2019/2020 ni pamoja na:

- (i) Kazi ya usanifu wa kina wa kuinua kiwango cha njia ya reli kati ya Tabora - Kigoma na Kaliua – Mpanda. Kazi hii inatarajiwa kukamilika Juni, 2020;
- (ii) Usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Uvinza - Musongati (Burundi) yenyе urefu wa Km 200 kwa *Standard Gauge*. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (iii) Kuboresha eneo la treni la kupakia/kupakua mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam na kukarabati vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (iv) Upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa njia za reli katika Jiji la Dodoma. Kazi hii inategemewa kukamilika Septemba, 2020;
- (v) Ukarabati wa mabehewa ya mizigo 200 na vichwa vya treni saba (7) vya TRC kwa ajili ya sogeza. Kazi hii inategemewa kukamilika Juni, 2020;
- (vi) Kukamilisha ujenzi wa njia ya reli kwenda bandari kavu ya Kwala, Ruvu;
- (vii) Ununuzi wa vichwa vya treni vitatu (3) ambavyo vinategemewa kufika Oktoba, 2020 na mabehewa ya mizigo 44 yanayotarajiwa kuwasili Juni, 2020; na
- (viii) Kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa reli ya Mtwara – Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga kwa Ubia kati ya Sekta Binafsi na Umma (PPP).

**159. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa utoaji wa huduma za usafiri, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TRC ilisafirisha tani 211,392 za mizigo ikilinganishwa na tani 275,843 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 23.4. Kwa upande wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, abiria 327,727 walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 421,585 waliosafirishwa

katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 22.3. Sababu za upungufu katika utoaji wa huduma ni pamoja na kufungwa kwa njia kwa saa 72 kwa wiki ili kupisha ukarabati wa njia ya reli ya kutoka Dar es Salaam hadi Isaka pamoja na kufungwa kwa njia kutokana na mafuriko katika maeneo mbalimbali ya miundombini ya reli.

### **Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

**160. *Mheshimiwa Spika*,** reli ya TAZARA ina umuhimu wa kipekee katika kuchangia maendeleo ya jamii kwa kuinua uchumi wa Tanzania na Zambia kuititia huduma za usafirishaji, upatikanaji wa ajira na kuchochaea ukuaji wa miji na biashara. Aidha, reli hii imebeba historia na mahusiano ya kidiplomasia baina ya Tanzania, Zambia na China. Kutokana na umuhimu huo, nchi wanahisa zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kuwa TAZARA inaendelea kutoa huduma. Hatua hizo kwa upande wa Tanzania ni pamoja na kuendelea na taratibu za kutunga Sheria mpya ya TAZARA ili kuimarisha utendaji; kulipa mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania; kuendelea kukarabati injini na mabehewa; kuendelea kutoa fedha za uendeshaji na uwekezaji wa TAZARA na kuendelea kufanya matengenezo makubwa ya njia ili kupunguza idadi ya sehemu zilizowekwa katazo la mwendo kasi wa treni.

**161. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TAZARA imeendelea kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam na New Kapiri Mposhi, Zambia. Katika kipindi hicho, jumla ya shehena ya tani 125,562 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 134,701 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019 sawa na upungufu wa asilimia 6.7. Upungufu huu umetokana na uchache na umadhubuti (Reliability) wa injini, nchi za Zambia na DR Congo kuanzisha tozo kwenye madini yanayosafirishwa nje ya nchi na uchaguzi wa DR Congo. Kuhusu usaferishaji wa abiria, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya abiria 661,551 wa njia ndefu walisafirishwa ikilinganishwa na abiria 673,904 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Utendaji huu ni pungufu kwa asilimia 1.8.

Ili kukabiliana na changamoto ya kushuka kwa utendaji, TAZARA ilikarabati mabehewa ya mizigo 19, mabehewa ya abiria matatu (3), kubadilisha mataruma ya zege 6,731 na mataruma ya mbao 2,647, kusambaza na kushindilia kokoto tani 9,350, na kufanya matengenezo ya kawaida ya njia na vitendea kazi.

**162. Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa katika mwaka 2017/2018, Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya kununua vipuri 42 vya Injini (Traction Motors) na mitambo ya kusalidla uzalishaji wa kokoto na mataruma ya zege (Dump Truck, Excavator and Drill Rig) katika mgodi wa kokoto ulioko Kongolo - Mbeya. Napenda kutoa taarifa kuwa, hadi Machi, 2020, vipuri 18 vya injini (Traction Motors) na mitambo mitatu (3) (Dump Truck, Excavator na Drill Rig) tayari vimepokelewa. Kazi ya kufunga vifaa na mitambo hii ili kuboresha utendaji inaendelea. Vipuri 24 vya injini viliviyobaki vitawasili nchini mwishoni mwa Mei, 2020.

**163. Mheshimiwa Spika**, Serikali za Tanzania na Zambia kwa upande mmoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa upande mwingine zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za Makubaliano ya Itifaki ya 16 ya ushirikiano wa kiufundi. Kupitia Itifaki hizi, Serikali ya China imekuwa ikitoa mikopo yenye masharti nafuu kwa TAZARA. Miradi itakayoteklezwa kupitia Itifaki ya 16 ni pamoja na ununuzi wa vipuri vya kuimarisha njia ya reli, vichwa vya treni na mabehewa.

## **USAFIGI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA MAJI**

**164. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji unaendelea kutolewa kwa ufanisi na weledi. Aidha, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inanufaika na uchumi wa bahari (blue economy) na maziwa. Lengo ni kufaidika na fursa zitokanazo na kuboresha huduma bora za kibandari na usafiri kwa njia ya maji. Katika mwaka 2019/2020, huduma za usafiri kwa njia ya maji zimeendelea kutolewa na Kampuni inayomilikiwa kwa pamoja kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), Kampuni

ya Huduma za Meli katika Maziwa (MSCL) na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) pamoja na sekta binafsi.

### **Huduma za Uchukuzi Baharini**

**165. *Mheshimiwa Spika*,** uchukuzi wa masafa marefu baharini umeendelea kutolewa na SINOTASHIP. Kampuni hii imeendelea kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania na China kwa zaidi ya miaka 50 kwa meli zake kubeba mizigo kati ya nchi hizi mbili na sehemu nyingine ulimwenguni kote. Aidha, SINOTASHIP imeendelea kutoa huduma ya uchukuzi wa mizigo wa masafa marefu baharini kwa kutumia meli yake kubwa (MV Changshun II) yenye uwezo wa kubeba tani 57,000 kwa ufanisi.

**166. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni hii ilisafirisha jumla ya tani 600,000 za shehena ya mizigo ikilinganishwa na jumla ya tani 598,000 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019.

**167. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na utendaji huo, Kampuni ya SINOTASHIP imekuwa na manufaa yafuatayo kwa Serikali yetu:

i. Kuimarisha uhusiano kati ya Tanzania na China ili kuendelea kuenzi maono yalioanzishwa na hayatı Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere na aliyekuwa Waziri Mkuu wa China Zhou Enlai;

ii. Kutoa fursa ya mafunzo kwa vitendo kwa vijana wa kitanzania wanaosoma masomo ya masuala ya uchukuzi kwa njia ya maji kutoka Vyuo vya DMI, NIT na Chuo cha Bandari; na

iii. Kukiunganisha Chuo cha Bahari (DMI) na mashirika ya meli ya China yanayohitaji vijana wa kufundisha na kuajiri kutoka Tanzania.

## Huduma za Uchukuzi Katika Maziwa

**168. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Kampuni ya Huduma za Meli kwenye Maziwa (MSCL) iliendelea kutoa huduma za uchukuzi na usafiri kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Aidha, Serikali imeendelea kuhamasisha na kuboresha utoaji wa huduma hizo kuitia sekta binafsi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni ya Huduma za Meli kwenye Maziwa ilisafirisha abiria 67,922 ikilinganishwa na abiria 79,049 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa asilimia 14.08. Sababu za kushuka kwa abiria waliosafirishwa ni pamoja na MV. Liemba kusimama kutoa huduma na idadi kubwa ya meli zikiwa katika matengenezo; hivyo, Kampuni kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria kwa kutumia Meli moja ya MV Clarias. Kuhusu usafirishaji wa mizigo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya tani za mizigo 27,576 zilisafirishwa ikilinganishwa na tani mizigo 22,773.36 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 21.1.

**169. Mheshimiwa Spika**, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Kampuni inapata watumishi wenye weledi ili kuimarisha utendaji wake. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Kampuni iliajiri watumishi wapya watano (5) na kupata kibali cha kuajiri watumishi wapya 48 wenye fani ya uendeshaji wa Meli, watumishi 12 wa kuhamia kutoka katika Taasisi nyingine za Serikali na kuazima wataalamu wanane (8) waliobobeaa katika fani ya uendeshaji meli kutoka Jeshi la Wanamaji Tanzania (Navy). Kampuni kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Serikali inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyo katika vibali vya kuongeza idadi ya wataalam, zoezi ambalo litakamilika Juni, 2020.

**170. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, MSCL iliendelea kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Ujenzi wa Meli mpya ya MV. Mwanza (Hapa Kazi tu) yenye Uwezo wa kubeba abiria 1,200 na tani 400 za mizigo katika Ziwa Victoria. Ujenzi wa Meli hii umekamilika kwa asilimia 60;

- ii. Ujenzi wa Chelezo ambao umekamilika kwa asilimia 96.5; na
- iii. Ukarabati wa Meli ya MV Victoria ambao umekamilika kwa asilimia 98 na ukarabati wa Meli ya MV Butiama uliokamilika kwa asilimia 98. Meli hizi ziko katika Ziwa Victoria.

### **Huduma za Bandari**

**171. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imeendelea kusimamia jumla ya bandari 89 zilizo katika mwambao wa bahari ya Hindi na kwenye Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Kati ya bandari hizo, bandari 18 ziko katika mwambao wa Bahari ya Hindi; bandari 31 katika Ziwa Victoria; bandari 25 katika Ziwa Tanganyika; na bandari 15 katika Ziwa Nyasa. Aidha, hadi Machi, 2020, jumla ya Bandari zisizo rasmi 694 zilitambuliwa. Kati ya hizo, bandari 240 ziko katika mwambao wa bahari ya Hindi; Bandari 329 katika ziwa Victoria, Bandari 108 katika ziwa Tanganyika na Bandari 17 katika ziwa Nyasa. Hadi sasa, Bandari 120 sawa na asilimia 17 ya Bandari zisizo rasmi zimerasimishwa.

**172. Mheshimiwa Spika,** ili kuhimili ushindani wa kimasoko, Januari, 2020, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilifanya utafiti wa kimasoko wa kufahamu mahitaji ya soko la Zambia na uwezo wa Bandari ya Beira. Kwa kuwa Zambia ni soko kubwa la Bandari ya Dar es Salaam, utafiti huu utasaidia kujua mahitaji ya wateja na wadau wengine. Lengo la utafiti huu ni kuzidi kuboresha huduma za Bandari za Tanzania na kuendelea kuongeza kiwango cha umiliki wa soko hili. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ilihudumia jumla ya tani za mapato milioni 7.137 za shehena za mizigo ikilinganishwa na tani za mapato milioni 6.934 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/2019. Utendaji huu ni sawa na ongezeko la asilimia 14. Kati ya shehena hiyo, Bandari ya Dar es Salaam ilihudumia jumla ya tani milioni 6.454 na bandari nyingine tani laki 683 za shehena. Pia, katika kipindi hicho, Kitengo cha Shehena Mchanganyiko (General Cargo) cha TPA kilihudumia makasha (TEUs) 110,193 ikilinganishwa

makasha (TEUs) 77,327 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 42.5. Kwa upande wa TICTS, Kitengo kilihudumia makasha (TEUs) 453,837 ikilinganishwa makasha (TEUs) 389,428 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019, sawa na ongezeko la asilimia 16.5.

**173. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, shehena ya nchi jirani iliyohudumiwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam ilikuwa tani milioni 5.545 ikilinganishwa na tani milioni 4.694 zilizohudumiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/19. Hili ni ongezeko la asilimia 18.1. Nchi zinazohudumiwa na Bandari zetu ni Uganda, Rwanda, Burundi, DR Congo, Zambia na Malawi. Vilevile, TPA inahudumia kwa kiasi kidogo shehena za Zimbabwe, Comoro, Sudani Kusini na Msumbiji.

**174. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Shehena ya Magari iliyohudumiwa katika Bandari ya Dar es Salaam iliongezeka hadi magari 129,714 kutoka magari 120,229 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19, sawa na ongezeko la asilimia 7.8.

**175. *Mheshimiwa Spika*,** ongezeko la mizigo na magari katika bandari za humu nchini lilitokana na kampeni zilizoendelea kufanyika katika nchi zote za jirani na kupunguza vikwazo visivyo vya kiforodha. Aidha, ili kuongeza uwezo wa bandari ya Dar es Salaam na kupunguza msongamano, kazi ya ujenzi wa Bandari Kavu eneo la Kwala, Ruvu inaendelea kutekelezwa kupitia Mkandarasi SUMA JKT na Shirika la Reli Tanzania. Kazi ya ujenzi wa yadi, njia ya reli na ofisi za muda kwenye eneo la ujenzi wa awamu ya kwanza lenye ukubwa wa hekta 5 ilianza Juni, 2019 na inatarajiwa kukamilika mwishoni mwa Mei, 2020. Mradi huu unaafuatiwa kwa pamoja na wadau wote wa Sekta ya Umma na Binafsi ili kuhakikisha kuwa uendeshaji wake unakidhi mahitaji ya wadau wote.

**176. *Mheshimiwa Spika*,** miradi ya kuboresha Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi za Dar es Salaam, Tanga na

Mtwara inaendelea kutekelezwa kwa mafanikio. Kazi zinazoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

**a. Bandari ya Dar es Salaam:**

- i. Uboreshaji wa Gati namba 5 – 7 na kuchimba lango la kuingilia Meli na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin);
- ii. Ujenzi wa Yadi ya shehena ya magari;
- iii. Ujenzi wa Bandari kavu eneo la Kwala-Ruvu (Vigwaza);
- iv. Ununuzi wa mitambo na vifaa vya kuhudumia mizigo; na
- v. Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhia mizigo.

**b. Bandari ya Tanga:**

- i. Kupanua na kuchimba lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin);
- ii. Kuongeza kina cha Bandari kutoka mita nne (4) hadi mita 15;
- iii. Maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya Gati la mafuta ghafi kutoka Uganda;
- iv. Ukarabati wa Zahanati;
- v. Ujenzi wa nyumba moja ya wafanyakazi; na
- vi. Ujenzi wa uzio katika eneo la Chongoleani.

**c. Bandari ya Mtwara:**

- i. Ujenzi wa awamu ya kwanza ya Gati la mita 300 la kuhudumia Shehena mchanganyiko (Multi-Purpose Terminal);
- ii. Ujenzi wa kituo cha mafuta;
- iii. Ukarabati wa Gati la Kilwa; na
- iv. Ujenzi wa Kinu cha kuhifadhia korosho bandarini.

**177. *Mheshimiwa Spika*,** katika bandari za kwenye Maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa, kazi zilizoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

**a. Bandari za Ziwa Victoria:**

- i. Ujenzi wa Ghala la mizigo, sehemu ya Abiria na majengo mengine katika Bandari ya Kyamkwiki na Mwigobero;
- ii. Ujenzi wa Bandari ya Kasenda iliyopo kijiji cha Mganza wilayani Chato;

- iii. Ujenzi wa Nyumba moja ya wafanyakazi katika Bandari ya Mwanza; na
- iv. Kuboresha Gati la Chato.

**b. Bandari za Ziwa Tanganyika:**

- i. Ujenzi wa Bandari ya Karema;
- ii. Ujenzi wa Barabara - Bandari ya Kagunga;
- iii. Ujenzi wa Gati za Kibirizi, Ujiji na Ofisi ya Mkuu wa Bandari-Kigoma;
- iv. Uboreshaji na upanuzi wa Bandari ya Kasanga;
- v. Ujenzi wa Miundombinu na Gati la Bandari ya Kabwe; na
- vi. Ujenzi wa miundombinu na Gati la Bandari ya Lagosa.

**c. Bandari za Ziwa Nyasa:**

- i. Ujenzi wa Nyumba ya Meneja wa Bandari;
- ii. Ujenzi wa Gati la Ndumbi; na
- iii. Ujenzi wa Uzio wa Bandari ya Itungi.

**Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Majini**

**178. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (Tanzania Shipping Agencies Corporation - TASAC) imeendelea kuratibu zoezi la utafutaji, uokozi na uchunguzi wa matukio ya ajali za usafiri wa majini. Katika juhudzi za kuimarisha zoezi la utafutaji na uokoaji katika ajali zinazotokea majini, TASAC imeendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu na majukumu ya Kituo cha Kuratibu Utafutaji na Uokoaji Majini (Maritime Rescue Coordination Centre - MRCC) kilichopo Dar es Salaam pamoja na kuratibu mafunzo ya mazoezi ya utafutaji na uokoaji. Aidha, Shirika liliendelea na jukumu la kufanya chunguzi za ajali za vyombo vyia usafiri majini ambapo jumla ya ajali na matukio ya ajali nane (8) ya vyombo vidogo (boats) yaliripotiwa na kufanyiwa uchunguzi. Katika ajali hizo, jumla ya watu 15 walipoteza maisha na wengine 43 kuokolewa. Uchunguzi ulibaini kuwa ajali hizo zilisababishwa na weledi mdogo wa waendesha boti hizo, hali mbaya ya hewa, upakiaji wa mizigo kupita uwezo na boti hizo kufanya kazi usiku. Mbali ya ajali hizo za boti, kumekuwepo na tukio moja la meli ya MV. Zuhra (No. 100224/IMO No.9880544) iliyosajiliwa Tanzania Zanzibar kupelea na

kugoa (grounding) katika miamba ya Bahari maeneo ya Kimbiji, Dar es Salaam. Katika tukio hilo mabaharia 13 waliookolewa na baadaye meli kutolewa salama kwenye miamba hiyo ambapo hakukuwa na madhara kwa binadamu wala mazingira. Pia, Shirika limeendelea kutumia taarifa za hali ya hewa kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ambapo jumla ya taarifa 874 za utabiri wa hali ya hewa zilipokelewa na kusambazwa kwa watumiaji.

**179. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa huduma za Bandari na Meli zinaendelea kuwa endelevu. Hivyo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Shirika lilipokea, kufanya tathmini na kutoa Leseni kwa watoa huduma za kibandari kama ifuatavyo:

- i. Uwakala wa Meli zilitolewa Leseni 24;
- ii. Mawakala wa Uondoshaji na Uingizaji wa shehena bandarini zilitolewa Leseni 828;
- iii. Wakusanyaji wa mizigo (Cargo Consolidators/ Deconsolidators) zilitolewa Leseni 18;
- iv. Watoa huduma ndogo ndogo bandarini (Miscellaneous Port Services) Leseni 23, hata hivyo bado kuna Leseni hai 48; na
- v. Wapimaji wa makasha (Gross Mass Verifiers) Leseni 37.

**180. *Mheshimiwa Spika*,** TASAC imeendelea kuimarisha ukaguzi wa meli ili kudhibiti usalama wa watu, mali na kulinda uchafuzi wa mazingira. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika limeendelea kudhibiti ujenzi wa meli mpya, ukarabati wa meli zilizopo, ukaguzi na utoaji vyeti vya ubora kwa meli zilizosajiliwa Tanzania Bara. Lengo ni kuhakikisha kuwa vyombo vyote vya usafiri majini vinakidhi viwango vya ubora na usalama vilivyowekwa na Sheria ya Usafiri wa Majini ya mwaka 2003 (Merchant Shipping Act, 2003). Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Shirika lilikagua ujenzi wa Meli mpya nne (4) za MV. Illemela (Mwanza), MV. Mbeya II (Kyela) na Tishari

mbili (2) za mizigo za Mamlaka ya Bandari (TPA) zinazojengwa Mombasa, Kenya. Aidha, ukaguzi wa Meli 2 zilizokarabatiwa za MV. Victoria na MV. Butiama ulifanyika. Pia, Shirika limeendelea kufanya ufuatiliaji wa kazi za wajenzi wadogo wa vyombo vidogo ili kukagua ubora wa vifaa na vyombo vinavyotumika pamoja na weledi wa waundaji wa vyombo hivyo.

**181. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali kupitia TASAC imeendelea kufanya ukaguzi wa ubora na usalama wa Meli zifanyazo kazi nchini na zinazotoka Nje ya Nchi (flag and port State control inspection). Lengo la ukaguzi huu ni kudhibiti ubora na usalama wa vyombo vinavyotoa huduma katika uchukuzi majini. Katika kipindi hicho, jumla ya kaguzi 255 kwa meli zenye ukubwa wa Tani 50 na zaidi zinazota huduma katika Pwani ya Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu zilizosajiliwa Tanzania Bara na zile zinazotoka Nje ya Nchi zilikaguliwa. Kati ya Meli zilizokaguliwa, asilimia 62.7 zilikidhi viwango vya ubora. Aidha, vyeti vya Usajili wa Meli tisa (9) za MV. Orion, MV. Nyehunge, MV. Nyehunge I, MV. Bijli, MT. Sangara, MT. Munanka, MV. Orion II, MV. Saint Mathew na MV. Wankyo vilihuishwa.

**182. *Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa Meli zinazoingia kwenye Bandari zetu zilizopo kwenye Ukanda wa Bahari ya Hindi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Bandari za Tanga, Pangani, Bagamoyo, Mtwara, Lindi, Kilwa na Mafia zilifanyiwa ukaguzi wa miundombinu ya kuongoza Meli zinapoingia bandarini. Aidha, Bandari za Dar es Salaam katika maeneo ya *General Cargo, Kurasini Oil Jetty - KoJ* na *Single Point Mooring - SPM, Tanzania International Container Terminal Services-TICTS*; na bandari za Tanga; Mtwara; Kilwa na Zanzibar zilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuimarisha ulinzi katika bandari hizo.

## **USAFIRI NA UCHUKUZI KWA NJIA YA ANGA**

### **Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga**

**183. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/2020, Wizara imeendelea kuboresha usafiri wa Anga ili kuhakikisha kuwa

Tanzania inakuwa kitovu (hub) cha usafiri wa Anga kwa nchi za Afrika Mashariki na ya Kati. Matakwa ya kiusalama na kiulinzi ya kitaifa na kimataifa yameendelea kuzingatiwa katika Viwanja vya Ndege nchini. Hii imelifanya anga la Tanzania kuwa salama na hivyo kuvutia wawekezaji katika kutoa huduma za usafiri wa Anga. Aidha, Wizara kuititia Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) ilienendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa viwanja vya Ndege vya Julius Nyerere, Kilimanjaro, Amani Abedi Karume, Dodoma, Songwe, Iringa, Mtwara, Lindi, Mwanza, Musoma, Shinyanga, Kigoma, Tabora, Bukoba, Tanga, Sumbawanga, Mpanda, Nachingwea, Kilwa Masoko na Songea. Pia, Viwanja vya Ndege vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA), Wizara ya Maliasili na Utalii, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) na Sekta Binafsi vimeendelea kudhibitiwa ili kuimarisha utoaji huduma, kukuza utalii nchini na kuendelea kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege zinafuatwa. Katika udhibiti huo, jumla ya viwanja vidogo vidogo 208 vilivyobainika kukiuka Sheria na Kanuni za uendeshaji wa Viwanja vya Ndege vimfungiwa hadi Machi, 2020 hadi vitakaporekebisha kasoro zilizojitokeza.

**184. *Mheshimiwa Spika*,** udhibiti wa usalama wa usafiri wa Anga katika Viwanja vya Ndege, Mashirika ya Ndege pamoja na watoa huduma za usafiri wa Anga umesaidia kuhakikisha kuwa viwanja vyetu havitumiki katika vitendo vya kihalifu dhidi ya usalama wa usafiri wa Anga pamoja na kudhibiti upitishaji wa madawa ya kulevyaa na nyara za Serikali. Aidha, Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja vyombo mbalimbali vikiwemo vya Ulinzi na Usalama katika kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona (COVID - 19) kwa wageni wote wanaoingia nchini.

**185. *Mheshimiwa Spika*,** pamoja na juhudii hizo, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, jumla ya Maafisa wa Usalama wa Usafiri wa Anga 423 kutoka Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar walitahiniwa na kupewa Leseni za Ukaguzi (Screeners Certificate). Wizara itaendelea kuhakikisha kuwa Maafisa wa Usalama katika Viwanja vya Ndege wanapatiwa

mafunzo stahiki na kupewa Leseni baada ya kuitia mchakato kama ulivyoainishwa kwenye Mpango wa Mafunzo wa Kitaifa wa Usalama wa Usafiri wa Anga (National Civil Aviation Security Training Programme).

**186. *Mheshimiwa Spika*,** idadi ya Abiria wanaotumia usafiri wa Anga inategemewa kuongezeka kwa asilimia 6.5 na kufikia Abiria 5,845,382 ifikapo Juni, 2020 kutoka Abiria 5,487,679 waliotumia usafiri huo katika mwaka 2018/2019. Aidha, idadi ya Abiria wanaosafiri kwenda na kutoka nje ya nchi inategemewa kupungua kutokana na janga la virusi vya Corona.

**187. *Mheshimiwa Spika*,** kukua kwa utendaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kwa kiasi kikubwa kumechangia kuongezeka kwa idadi ya Abiria wanaosafiri Ndani ya Nchi. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Juni 2020, idadi ya Abiria wanaosafiri ndani ya nchi inakadiriwa kufikia abiria 4,398,500 kutoka abiria 5,309,611 waliosafiri katika kipindi kama hicho katika mwaka 2018/2019. Huu ni upungufu wa abiria kwa asilimia 17.2. Aidha, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Juni, 2020, mizigo iliyosafirishwa nchini inakadiriwa kufikia tani 21,456.6 ikilinganishwa na tani 24,444 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2018/19. Upungufu huu ni sawa na asilimia 12.2. Pia, hadi Juni, 2020, miruko ya safari za Ndege inakadiriwa kushuka hadi miruko 179,283 kutoka miruko 234,048 ya mwaka 2018/19. Huu ni upungufu wa miniko kwa asilimia 23.4. Kushuka kwa utendaji huu katika usafirishaji wa abiria, mizigo na miruko ya Ndege kwa kiasi kikubwa kunatokana na mlipuko wa virusi vya Corona unaoendelea duniani kote.

**188. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali imeingia Mikataba mipy ya usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati yake na nchi za Mauritius, Rwanda na Hispania. Aidha, Mikataba ya BASA kati ya Tanzania na nchi za Zambia, Uturuki, Oman, Sri Lanka, Uingereza, Zimbabwe, Ethiopia, Afrika ya Kusini na Jordan ilipitiwa upya. Hivyo, hadi Machi, 2020, Tanzania ilikuwa imeingia Mikataba ya BASA na nchi 74 ikilinganishwa

na nchi 70 zilizosaini Mikataba hiyo katika mwaka 2018/2019. Kati ya Mikataba hiyo, Makampuni/Mashirika ya Ndege 22 kutoka nchi 19 yalikuwa yameanza kufanya safari za Ndege 175 kwa juma kati ya Tanzania na nchi hizo hadi kufikia Machi, 2020.

**189. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2019/20, Sekta ya Uchukuzi iliahidi kukamilisha Mradi wa kufunga Mfumo wa kuongoza Ndege kutua salama (Instrument Landing System - ILS) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume - Zanzibar. Napenda kutoa taarifa katika Bunge lako Tukufu kuwa Mradi huo uliogharimu Shilingi bilioni 4.6 chini ya Mkandarasi PEJA East Africa ya Uhlanzi umekamilika na uko katika hatua za majoribio. Hata hivyo, majoribio hayo yanayotakiwa kufanywa na Mkandarasi yamesitishwa hadi hapo janga la virusi vya Corona litakapokwisha.

**190. *Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na kukamilika kwa miradi mbalimbali, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali kuitia Mamlaka ya Usafiri wa Anga imeendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

- i. Kununua na kufunga vifaa vya mawasiliano ya sauti kati ya Marubani na waongozaji Ndege katika Viwanja vya JNIA na KIA;
- ii. Kununua na kufunga vifaa vya mawasiliano katika jengo jipya la kuongozea Ndege kituo cha Mwanza;
- iii. Ukamilishaji wa ujenzi wa uzio katika eneo la ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga;
- iv. Kufanya utafiti na hatua za awali za ununuzi na ufungaji wa Mtambo wa kuongozea Ndege kwa njia ya *Satelaiti* upande wa Magharibi mwa Nchi;
- v. Ukamilishaji wa Upembuzi Yakinifu wa ujenzi wa Chuo cha kisasa cha Usafiri wa Anga; na

vi. Ukamilishaji wa uhakiki wa vifaa vya kuongozea mienendo ya Ndege vituo vya KIA, JNIA, Zanzibar na Mwanza.

### **Huduma za Viwanja vya Ndege**

**191. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeendelea kuhudumia Viwanja vya Ndege 58 kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Usafiri wa Anga. Aidha, TAA imeendelea kuimarisha Viwanja vya Ndege ili kuboresha huduma, mapato na kuimarisha Ulinzi na Usalama viwanjani. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, TAA iliboresha Ulinzi na Usalama viwanjani kwa kununua na kufunga Mashine 15 za ukaguzi wa mizigo; milango sita (6) ya ukaguzi wa Abiria pamoja na vifaa vya mawasiliano kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA (3), Iringa (1), Songea (1), Kigoma (1), Mwanza (2), Songwe (1), Arusha (2), Bukoba (1), Tanga (1), Lindi (1) na Shinyanga (1).

**192. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kuhakikisha kuwa kila Mkoa unakuwa na Kiwanja cha Ndege. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, uthamini wa mali za Wananchi wanaotakiwa kupisha ujenzi wa viwanja vifaa vya Ndege vya Kisumba (Sumbawanga), Msalato (Dodoma), Mwada (Manyara) na Igegu (Simiyu) umekamilika. Mamlaka inaendelea na taratibu za utwaaji wa maeneo hayo kwa kushirikiana na Mikoa husika.

**193. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/2020, TAA imekamilisha maandalizi ya Programu za Ulinzi na Usalama (Safety and Security Programs) kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA, Mwanza, Songwe, Mtwara, Lindi, Nachingwea, Arusha, Lake Manyara, Kilwa Masoko, Mafia, Iringa, Dodoma, Songea na Tanga. Aidha, TAA ilitoa mafunzo ya usalama kwa wafanyakazi wa viwanja vyote vya Ndege vinavyoendeshwa na Mamlaka. Pia, Mamlaka imefanya mazoezi ya uokoaji wakati wa ajali kwa Viwanja vya Ndege vya Songwe, Iringa, Lake Manyara na Kahama na Mazoezi ya Usalama (Security Contingency Exercises) kwa Viwanja vya Ndege vya Songwe, Dodoma na Mwanza.

**194. *Mheshimiwa Spika*,** kazi ya ununuzi na ufungaji wa Mifumo ya taa za kuongozea Ndege (AGL) katika Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Songwe na Bukoba inaendelea. Mfumo wa taa za kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma upo na unaweza kutumika kwa dharura. Hata hivyo, kazi za kufunga Mfumo mpya imeanza na inatarajiwaka kukamilika Juni, 2020. Kuhusu Kiwanja cha Ndege cha Songwe, ufungaji wa taa hizo utafanyika kupitia Mradi unaoendelea wa ukarabati wa barabara ya kutua na kuruka Ndege (runway). Aidha, kazi za kufunga Mfumo wa taa za kuongozea Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba zitatekelezwa baada ya kurefushwa kwa barabara ya kuruka na kutua Ndege pamoja na ujenzi wa mnara wa kuongozea Ndege kukamilika. Kazi inayoendelea sasa ni Mhandisi Mshauri kufanya Usanifu na Upembuzi wa Kina kwa ajili ya kazi za urefushaji wa barabara ya kuruka na kutua Ndege.

**195. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa Kiwanja cha Ndege cha Arusha kinaboresha ili kuvutia watalii wengi kutumia kiwanja hicho na kuwezesha Ndege zenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 50 kutumia kiwanja hicho. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 kazi zilizotekelzwa ni pamoja na:

- i. Kujenga maegesho ya Ndege (Apron);
- ii. Kuboresha barabara ya Ndege (taxiway) ya kuingia na kutoka katika maegesho ya Ndege;
- iii. Kujenga maegesho ya Magari (Car Park);
- iv. Kufunga Mfumo wa maegesho ya Magari;
- v. Kujenga maegesho mapya ya Ndege (remote Apron);
- vi. Kuanza urefushaji wa barabara ya kutua na kuruka Ndege kwa mita 200 pamoja na maeneo ya kugeuzia (Turning bay); na
- vii. Kuanza ujenzi wa barabara mbadala ya kuingilia Gereza la Mkoa wa Arusha (Kisongo) badala ya kupita katikati ya eneo la Kiwanja cha Ndege.

**196. Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KADCO) imeendelea kukisimamia na kukiendesha Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) kwa faida bila kutegemea ruzuku ya uendeshaji kutoka Serikalini. Hata hivyo, Serikali imeendelea kutoa ruzuku kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya uboreshaji na uendelezaji wa miundombinu ya Kiwanja cha Ndege. Kwa mfano, Mradi wa uboreshaji njia ya kurukia na kutua Ndege (runway) ulipata fedha kutoka Serikalini. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, KADCO imeendelea kutoa huduma kwa Makampuni ya Ndege zenyе ratiba maalum ya safari. Makampuni hayo ni pamoja na Air Tanzania, Kenya Airways, Ethiopian Airline, Precision Air, Qatar Airways, KLM, Turkish Airlines na Rwandair. Aidha, kuna Mashirika ya Ndege za kukodi yanayofanya safari zisizokuwa na ratiba maalum yanayotoa huduma KIA. Mfano wa Mashirika hayo ni Coastal Aviation, Regional Air, Northern Air, Zurik Air, na El-Al Israel airlines.

**197. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zilizotekelizwa na KADCO katika mwaka 2019/2020 ni pamoja na:

- i. Kuboresha nyumba za Wafanyakazi, Majengo ya Mitambo na ofisi mbali mbali;
- ii. Kutoa elimu kwa Wafanyakazi katika kada mbalimbali za Ulinzi, Ufundı, Zimamoto na Mafunzo mengine ya kitaalam;
- iii. Kuboresha mazingira kwenye eneo la kiwanja na maeneo jirani kwa kupanda miti, kutoa elimu ya mazingira vijijini na kushiriki kikamilifu katika sherehe zinazohusu mazingira kitaifa na kimataifa.
- iv. Kukamilisha ununuzi wa vifaa mbalimbali nya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji huduma; na
- v. Kushiriki shughuli za kijamii na vijiji vinavyopakana na kiwanja kwa kutoa misaada. Misaada hiyo ni pamoja na Huduma za zimamoto na uokoaji, ukarabati wa nyumba za Taasisi kama Polisi na Halmashauri ya Hai na Arumeru na vijiji mbalimbali vinavyozunguka Kiwanja cha Ndege.

## Huduma za Usafiri wa Anga

**198. Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kuyashukuru Mashirika ya Ndege yanayotoa huduma ya usafiri wa Anga Ndani ya Nchi kwa kuendelea kutoa huduma. Mashirika hayo yamekuwa yanatoa huduma za usafiri wa Anga kwa Ndege za Ratiba maalumu (scheduled flight) na zisizo na ratiba maalumu (General Aviation). Kwa upande wa ratiba maalumu, Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na Precision Air zimendelea kutoa huduma za usafiri wa Anga katika vituo vingi huku Kampuni nyingine ndogo hasusan Auric na Coastal Air zikifuatia. Kwa upande wa huduma zinazotolewa kupitia ratiba zisizo maalumu, Kampuni za Auric, Coastal Air, Zanair, Air Excel, Tanzaniar, Sky aviation na Tropical air zimendelea kutoa huduma kwa ufanisi.

**199. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Serikali ilipokea Ndege mbili (2) mpya. Ndege ya kwanza ni Boeing 787 – 8 Dreamliner yenye uwezo wa kubeba abiria 262 kwa ajili ya masafa marefu iliyowasili nchini Oktoba, 2019. Ndege nyingine ni aina ya Dash 8 Q 400 yenye uwezo wa kubeba abiria 76 kwa ajili ya masafa mafupi iliyowasili nchini Disemba, 2019. Ongezeko hili la idadi ya Ndege limefanya ATCL kuwa na jumla ya Ndege 8. Ndege hizo zinajumuisha Ndege nne (4) za masafa mafupi aina ya Dash 8 Q400, Ndege mbili (2) za masafa ya kati aina ya Airbus A220 – 300 na Ndege mbili (2) za masafa marefu aina ya Boeing 787-8 Dreamliner. Aidha, Ndege hizo zimeongeza mtandao wa safari wa ATCL kutoka vituo vitatu (3) vya ndani ya nchi na kituo kimoja (1) cha kikanda vilivyokuwepo kabla ya mwaka 2016 hadi vituo 13 ndani ya nchi na vituo saba (7) vya nje ya nchi. Ndege aina ya Dash 8 Q300 ambayo inayohitaji matengenezo makubwa inatarajiwa kupelekwa nchini Malta mara baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID -19 kuisha.

**200. Mheshimiwa Spika,** vituo vya ndani ambavyo ATCL inatoa huduma ni pamoja na Dar es Salaam, Zanzibar, Dodoma, Kilimanjaro, Mwanza, Bukoba, Kigoma, Mbeya, Tabora, Songea, Iringa, Mtwara na Mpanda. Hata hivyo,

ukarabati unaoendelea katika kiwanja cha Songea umesababisha kushindwa kuendelea kutoa huduma katika kituo cha Mtwara kutokana na uchache wa abiria. Hivyo, Safari za Mtwara na Songea zitarejea baada ya kukamilika kwa ukarabati wa kiwanja cha Songea kwa Mfumo uleule wa kuunganisha safari za vituo hivyo viwili ili kuwa na Abiria wa kutosha na tija. Kwa safari za kikanda na kimataifa, hadi Machi, 2020, ATCL ilikuwa inatoa huduma katika vituo vya Hahaya (Comoro), Entebbe (Uganda), Bujumbura (Burundi), Mumbai (India), Lusaka (Zambia), Johanessburg (Afrika Kusini) na Harare (Zimbabwe). Aidha, vibali vyote vya kuanza safari za kwenda Guangzhou, China, vimepatikana tangu Februari, 2020. Pamoja na kupata vibali vya kuanza safari za Guangzhou, pia ATCL imesaini Mkataba wa safari maalum (Charter flight) wa kubeba watalii kati ya mji wa Hangzhou, China, na Dar es Salaam. Safari hizi za China zitaanza baada ya mlipuko wa ugonjwa wa COVID – 19 kuisha.

**201. Mheshimiwa Spika**, mazingira ya utendaji kazi kwa Watumishi wa ATCL yameendelea kuboreshwa. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, mafunzo ya lazima na yale yanayofuata ratiba ya mafunzo kwa Watumishi yametolewa kwa Marubani 78, Wahandisi Ndege 127 na Wahudumu wa Ndani ya Ndege 131. Aidha, Mfumo wa mauzo wa Serikali (Government Electronic Payment Gateway - GePG) unaendelea kufanyiwa majaribio kuona kama utaweza kutumika katika mauzo ya Tiketi Ndani na Nje ya Nchi. Lengo ni kuhakikisha kuwa malipo yote ya Tiketi yanathibitiwa na kupunguza gharama za uendeshaji.

**202. Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Agosti, 2019, ATCL ilitunukiwa cheti cha kukidhi matakwa ya usalama katika uendeshaji wa shughuli za usafiri wa Anga kutoka Shirikisho la Mashirika ya Ndege Ulimwenguni (IATA). Kufuzu ukaguzi huo ni muhimu katika uendeshaji wa shughuli za Usafiri wa Anga kwani kunaongeza imani ya Wateja na Wadau muhimu wa usafiri wa Anga kwenye mashirikiano ya kibiashara.

**203. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Miradi iliyoendelea kutekelezwa ni pamoja na:

- i. Ununuzi wa Ndege moja aina ya Dash 8 Q400. Ndege hii inatarajiwa kuwasili Juni, 2020. Aidha, Ndege nyingine mbili aina ya A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili Juni, 2021;
- ii. Kufanya matengenezo ya Ndege ndogo aina ya Dash 8 Q300;
- iii. Maandalizi ya safari za Guangzoug (China) na Lubumbashi, Nairobi, Kigali na Uingereza. Utoaji wa huduma utaanza baada ya mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona kuisha;
- iv. Kukarabati Karakana za JNIA na KIMAFA ili kufanya matengenezo madogo na makubwa nchini; na
- v. Kujenga uwezo wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kuanza kutoa Mafunzo ya Wataalam wa Usafiri wa Anga nchini.

#### **HUDUMA ZA HALI YA HEWA**

**204. Mheshimiwa Spika**, huduma za Hali ya Hewa nchini zimeendelea kutolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania. Huduma hizo zinajumuisha takwimu na taarifa za hali ya hewa iliyopita, iliyopo na ijayo; tahadhari dhidi ya matukio ya hali mbaya ya hewa; klaimatolojia ya hali ya anga na mabadiliko ya hali ya hewa. Huduma hizi zinaongeza mchango katika kuendeleza sekta za kiuchumi na kijamii na kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha, Mamlaka imeendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali za hewa kuititia maonesho mbalimbali, vipindi vya redio na runinga, tovuti, blogu na semina kwa jamii.

**205. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kutekeleza program ya kukabiliana na mabadiliko ya nchi, kufuatilia mwenendo wa mabadiliko ya hali ya hewa na kutoa taarifa za mabadiliko hayo kwa wadau wa sekta mbalimbali. Aidha,

Mamlaka hutoa taarifa ya Klimatolojia ya tathmini ya hali ya hewa na mabadiliko ya hali ya hewa kila mwaka ikijumuisha tathmini ya mwelekeo wa joto na mvua pamoja na matukio ya hali mbaya ya hewa ili kujenga uelewa kwa umma juu ya athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

**206. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Hali ya Hewa imeendelea kutekeleza Mradi wa Rada tatu (3) za hali ya hewa zitakazofungwa Mtwara, Mbeya na Kigoma. Rada inayotarajija kufungwa Mtwara imewasili nchini Februari, 2020 na taratibu za kuifunga zinaendelea. Ujenzi wa rada mbili (2) zilizobaki unaendelea kutekelezwa nchini Uhlanzi. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya Rada itakayofungwa katika maeneo hayo inayohusisha ujenzi wa barabara, uazio, majengo pamoja na uwekaji wa umeme unaendelea. Kukamiliika kwa ununuzi wa Rada hizo kutaongeza ubora wa utabiri wa hali ya hewa kwani tutakuwa na jumla ya Rada tano (5) nchini.

**207. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka imeendelea na utekelezaji wa Mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa kwa Sekta ya Usafiri wa Anga kulingana na viwango vyaa kimataifa. Ugaguzi wa kimataifa uliofanyika Disemba, 2019 ulithibitisha Mamlaka kuendelea kukidhi vigezo na hivyo kuendelea kumiliki cheti cha ubora (ISO 9001:2015). Kwa upande wa usafiri kwa njia ya maji, utekelezaji wa Mfumo wa kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa katika usafiri wa majini umeanza kutekelezwa katika ofisi tano (5) za hali ya hewa zilizopo katika Bandari za Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba, Mwanza na Kigoma.

**208. Mheshimiwa Spika**, kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa katika kipindi cha Julai, 2019 na Machi, 2020 ni pamoja na:

- i. Matengenezo ya vifaa vipyaa vyaa hali ya hewa katika karakana iliyopo JNIA;
- ii. Kufanya uhakiki wa usahihi (calibration) wa vifaa vyaa hali ya hewa;

- iii. Kuhakiki Rada ya hali ya hewa iliyoko Mwanza ili kuhakikisha kuwa inaendelea kufanya kazi kwa usahihi;
- iv. Kuwajengea uwezo Wafanyakazi kwa lengo la kuboresha huduma. Jumla ya Wafanyakazi 61 walihitimu mafunzo ya muda mfupi, 51 wanaendelea na mafunzo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali na 72 wanaendelea na mafunzo ya muda mfupi; na
- v. Kutengeneza Mifumo mitatu (3) ya TEHAMA ambayo inatumika katika uangazi (Digital Meteorological Observatory), utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa Anga (MAIS) na utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa usafiri wa kwenye maji (MMIS).

### **C.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO**

#### **Ukusanyaji wa Mapato**

**209. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, kwa kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Sekta ya Mawasiliano imekusanya jumla ya **Shilingi 290,417,311,401.97** kwa mchanganuo ufuatao: TCRA imekusanya Jumla ya **Shilingi 137,059,249,584.29** kutoka kwenye vyanzo vyake. Pia katika kipindi hicho TCRA ilipeleka katika Mfuko Mkuu wa Serikali asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya **Shilingi 18,621,401,160.00** na mapato kutokana na mtambo wa TTMS **Shilingi 9,033,895,792.19**; Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) limekusanya jumla ya **Shilingi 85,710,460,445.06**; Shirika la Posta Tanzania (TPC) limekusanya jumla ya **Shilingi 24,319,843,901.52**; Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) umekusanya kiasi cha **Shilingi 25,388,181,843.00** na Tume ya TEHAMA (ICTC) imekusanya jumla ya **Shilingi 735,184,392.00**. Aidha, **Shilingi 17,204,391,236.10** zilikusanywa kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa.

**210. Mheshimiwa Spika**, Taasisi za Sekta ya Mawasiliano katika mwaka wa fedha 2017/18 zilipata faida na hivyo zimeweza kutoa gawio Serikalini la jumla ya **Shilingi 89,315,814,942.00** kwa mchanganuo ufuatao; Mamlaka ya Mawasiliano imetoea **Shilingi 85,855,814,942.00**, Shirika la Mawasiliano limetoea

**Shilingi 2,100,000,000.00**, Shirika la Posta limetoe **Shilingi 350,000,000.00**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulitoa Shilingi **1,000,000,000.00** na Tume ya TEHAMA ilitoa **Shilingi 10,000,000.00**.

### Bajeti ya Matumizi ya Kawaida

**211. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Sekta ya Mawasiliano ilitengewa kiasi cha **Shilingi 3,973,197,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,047,259,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 1,925,938,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 **Shilingi 3,021,554,809.24** zilikuwa zimetolewa na Hazina. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,457,738,432.00** zimetolewa kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,563,816,377.24** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

### Ukuaji wa Sekta ya Mawasiliano

**212. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Mawasiliano imeendelea kuwa moja ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi. Katika kipindi cha Januari hadi Disemba, 2019 Sekta ya Mawasiliano ilichangia ukuaji wa uchumi kwa **asilimia 11** ikilinganishwa na **asilimia 9.1** kwa kipindi kinachoishia **Disemba, 2018**. Aidha, kuna ongezeko kubwa la huduma kwa wananchi zinazotolewa na Serikali na pia sekta binafsi kuititia mawasiliano ya simu za kiganjani kama vile kutuma na kupokea pesa, kununua umeme, kulipia huduma za maji na ving'amuzi. Kimsingi huduma za mawasiliano zimechangia kurahisisha utendaji kazi na kuboresha maisha ya wananchi kijamii na kiuchumi kutokana na kupata huduma mbalimbali kwa uwazi, urahisi, haraka na pasipo na ubaguzi. Vilevile, ukuwaji wa sekta ya mawasiliano umesaidia Serikali kuimarisha ukusanyaji wa kodi mbalimbali na maduhuli kwa kutumia mifumo ya TEHAMA.

**213. Mheshimiwa Spika**, laini za simu za viganjani zimeongezeka kutoka **43,749,086** Julai, 2019 hadi laini **43,932,080** mwezi Machi, 2020 na idadi ya watumiaji wa intaneti iliongezeka kutoka **23,142,960** Julai, 2019 hadi kufikia **25,794,560** mwezi Machi, 2020. Vituo vya kurusha matangazo

ya redio vimeongezeka kutoka vituo **158** mwaka 2019 hadi kufikia vituo 180 mwezi Machi, 2020 na vituo vya kurusha matangazo ya runinga kwa kutumia mitambo iliyosimikwa ardhini vimeongezeka kutoka vituo **37** mwaka 2019 hadi kufikia vituo **43** mwezi Machi, 2020. Pia, watoa huduma za mawasiliano ya simu na posta wameongezeka na kuleta ushindani wenyewe tija na ufanisi nchini kwa sekta zote.

## **UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

### **Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano**

**214. *Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea kuboresha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kuhakikisha huduma za Mkongo zinapatikana kwa uhakika. Katika mwaka wa fedha 2019/20 betri zinazotumika pindi umeme unapokatika kwenye vituo sabini na moja (71) vya mkongo wa Taifa vimebadilishwa kutokana na uchakavu wa betri za awali. Hii inawezesha Mkongo wa Taifa kufanya kazi kwa masaa hadi nane pindi umeme unapokatika.

**215. *Mheshimiwa Spika***, Serikali inaendelea na maandalizi ya kufikisha huduma ya Mkongo wa Taifa katika ofisi ambazo hazina huduma ya mkongo ambapo unganishaji wa Halmashauri za Siha, Ngorongoro, Nyang'hwale, Bukombe, Mbogwe, Kyerwa, Nsimbo, Mlele, Buhigwe, Malinyi, Buchosa, Kalambo, Ushetu, Busokelo, Momba na kituo cha Manyovu uko kwenye hatua za mwisho. Uunganishwaji huu unahuishisha baadhi ya vituo vya afya, polisi, posta, mahakama na taasisi nyingine kwenye maeneo hayo ili kuboresha huduma kwa wananchi zitakazotolewa na taasisi hizo.

**216. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imekamilisha uaandaji wa Mkakati wa Taifa wa Brodibendi (National Broadband Strategy) wenyewe lengo la kuhakikisha kuwa mawasiliano ya Brodibendi yanapatikana nchini nzima. Mkakati huu umeanisha namna bora ya kufikisha huduma za inteneti vijiji, kwenye mashule, hospitali na maeneo ya umma. Aidha, Mkakati huu unasisitiza matumizi ya teknolojia ya kuanzia 3G ili wananchi waweze kupata huduma za data.

**217. *Mheshimiwa Spika***, kituo cha Taifa cha Kutunza Data cha Dar es Salaam (Internet Data Centre) kimeendelea kutoa huduma bora kwa taasisi za Serikali na taasisi binafsi. Kituo kimeweza kuongeza wateja kutoka **wateja 79** mwezi julai, 2019 hadi **wateja 107** mwezi Machi, 2020.

**UTENDAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA MAWASILIANO  
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**218. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano, imeendelea na zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria ambapo hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020 idadi ya laini zilizosajiliwa zilikuwa **37,678,816** sawa na asilimia **85.8** ya laini zote **43,932,080** zilizounganishwa mitandaoni. Laini zillizozimwa hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2020 zilikuwa **5,082,458**. Aidha, laini ambazo bado hazijasajiliwa kwa alama za vidole lakini zilisajiliwa kwa kitambulisho cha Mpiga Kura na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni laini **6,134,477**. Uhakiki unaendelea kwa kushirikiana na NIDA kwa ajili ya taratibu za kuzifungia laini ambazo hazijasajiliwa.

**219. *Mheshimiwa Spika***, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeendelea na ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za mawasiliano kwa kutumia mtambo wa Telecommunications Traffic Monitoring System (TTMS) ili kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano. Mfumo huo unawezesha kuhakiki ubora wa huduma za Mawasiliano ya simu; kutoa takwimu za mawasiliano ya simu yanayofanyika ndani na nje ya nchi (Local and International Traffic); kugundua mawasiliano ya ulaghaji (fraudulent traffic); Kubaini na kufungia simu zenye namba tambulishi zilizonakiliwa (Duplicate IMEIs) ambapo taarifa hii inapatikana kwenye rajisi ya namba tambulishi ya simu na kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 jumla ya miamala **2,502,352,515** imepita katika mitandao ya simu na jumla ya fedha zilizopita ni **Shilingi 133,493,772,366,263**.

**220. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inaendelea kusimamia uendeshaji wa mfumo wa usimamizi wa ubora wa huduma (Quality of Service) uliowekwa katika mtambo wa TTMS na kuwezesha kupatikana kwa taarifa za ubora wa mawasiliano ya simu za kimataifa pamoja na zile za ndani (Local off-net traffic) yanayofanyika kutoka katika mtandao mmoja wa mtoe huduma kwenda mtandao mwingine wa mtoe huduma hivyo kuiwezesha Mamlaka kufuatilia kwa ufanisi ubora wa huduma za mawasiliano. Vile vile, TCRA inasimamia uendeshaji wa mfumo uliowekwa katika mtambo wa TTMS na kuwezesha kupatikana kwa taarifa za ubora wa sauti kwa mawasiliano ya simu za ndani (Local off-net traffic) yanayofanyika kutoka katika mtandao mmoja wa mtoe huduma kwenda mtandao mwingine wa mtoe huduma.

**221. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia TCRA inaendelea kusimamia kwa ufanisi uendeshaji wa Mfumo wa Rajisi wa Namba Tambulishi za simu za kiganjani hivyo kuwezesha kudhibiti matumizi ya simu ambazo hazina ubora (bandia). Simu bandia haziwezi tena kuunganishwa na mtandao wowote wa simu hapa nchini. Tangu mfumo huu uanze kufanya kazi mwezi Oktoba, 2013 hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya namba tambulishi (IMEIs) zilizofungiwa ni **1,277,048**. Mfumo huo umepunguza kwa kiasi kikubwa wizi wa simu za mkononi. Mteja anapoibowi au kupoteza simu yake hutoa taarifa ya kuibiwa au kupotea kwa simu hiyo na kuifungia isiweze kutumika tena kwenye mitandao ya simu za mkononi.

**222. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano imeendelea na zoezi la kuzitambua na kuzifungia namba za simu ambazo zimekuwa zikiingiza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia za ulaghai. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 TCRA imefanikiwa kupunguza mawasiliano ya simu za kimataifa kwa njia ya ulaghai kutoka **asilimia 15** hadi kufikia chini ya **asilimia 5**. Kabla ya udhibiti huu mawasiliano kwa njia ya ulaghai yamepelekea watoa huduma kukosa mapato na hivyo Serikali kupoteza mapato.

**223. *Mheshimiwa Spika*,** Sekta ya Mawasiliano imeendelea kukua kwa kasi kutokana na mabadiliko ya Teknolojia. Mabadiliko haya yamekuja na athari mbalimbali za usalama na uhalifu katika mitandao. Athari hizo ni pamoja na uhalifu kmtandao (cyber crime), ugaidi kwenye mifumo wa mitandao (Cyber terrorism) na uharibifu wa mila na desturi (mfano picha za utupu kwenye mitandao). TCRA inaendelea kudhibiti vitendo hivi kwa kujenga uwezo kwa watumishi wake pamoja na kushirikiana kwa karibu na vyombo vyya ulinzi na usalama. Aidha, Mamlaka imeweka taratibu mahsuswi wa kushughulikia malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma. Vile vile mamlaka ya Mawasiliano inaendelea kutoa elimu juu ya wajibu na haki za watumiaji na watoa huduma za mawasiliano. Mpaka Machi, 2020, Mamlaka ilikuwa imepokea na kushughulikia jumla ya malalamiko 502.

**224. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi 2020, TCRA imetoa mafunzo juu ya usalama wa mifumo kwa wasimamizi wa mifumo kutoka taasisi mbalimbali nchini Tanzania. Pia, imefanya tathmini ya hatari na matishio ya kiusalama ya mifumo ya kompyuta na mtandao kwa lengo la kubaini mapungufu yaliyopo dhidi ya mashambulio ya mtandao (cyber-attacks) ambapo tahadhari za usalama (security alert) (137); mashauri (security advisories) (280) na taarifa kwa umma (public notice) tatu (3) za kiusalama zilitolewa ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kuimarisha usalama wa mtandao na mifumo.

**225. *Mheshimiwa Spika*,** nitoe wito kwa wananchi waendelee kutumia vizuri huduma za mawasiliano kwa kuwa zinachangia ukuaji wa uchumi na maendeleo ya taifa letu na tuepuke matumizi yasiyo sahihi ya huduma hizo kwa kutoitumia katika kufanya uhalifu na wizi kwa njia ya mtandao; vitendo vinavyoikiuka maadili, mila na desturi zetu na uvunjifu wa amani. Aidha, nawahimiza wananchi tuendelee kulinda miundombinu ya Mawasiliano kwa kuwa ni muhimu katika kukuza uchumi wetu.

## **Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

**226. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Posta limeendelea kuboresha huduma zake za usambazaji wa barua, nyaraka, na vipeto kupitia masanduku ya barua na huduma ya Posta Mlangoni kwenye maeneo yenye miundombinu ya Anwani za Makazi na Postikodi. Jitihada za Serikali zinaendelea ili kuwezesha huduma za Posta kuwafikia wananchi wengi zaidi kupitia miundombinu hiyo.

**227. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kuimarisha biashara zake ikiwemo biashara ya kubadili fedha za Kigeni (Bureau de Change). Kufikia tarehe 31 mwezi Machi, 2020 Shirika limefikisha **maduka 26** kutoka maduka **19 mwaka 2018** katika maeneo mbalimbali ya Kimkakati. Aidha, Shirika linakamilisha ufunguzi wa huduma za 'Freight and Fowarding' (shehena na usafirishaji wa mizigo) ambapo kwa sasa Shirika liko katika hatua za kuhuisha leseni ya biashara hiyo. Vilevile kwa kushirikiana na Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF), Shirika limekamilisha mradi wa kuanzisha vituo **11** vya mawasiliano 'Tele-centres' katika maeneo ya Chato, Tarime, Maswa, Lushoto, Mahenge, Newala, Mbinga, Ludewa, Ileje, Mpanda, na Sumbawanga.

**228. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeanza kuendesha mafunzo ya matumizi ya huduma ya Posta kiganjani 'Smart Posta' (mfumo au jukwaa la kidigitu unaorahisisha kuzifikia huduma zote za msingi zinazotolewa na Shirika la Posta Tanzania na kuwezesha kufanya malipo kupitia mtandao) kwa majiji mawili ya majoribio (Dar es Salaam na Dodoma).

**229. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Posta limeunganisha **ofisi 161** katika mfumo wa uendeshaji wa kielekitroniki ambaao huwezesha huduma zote kutolewa kimtandao. Shirika pia limeunganisha ofisi hizo katika Mfumo wa Malipo wa Kielekitroniki wa Serikali (GePG). Vilevile, Shirika linaendelea kuimarisha vituo vya kutolea intaneti kwa wananchi ambavyo vinasaidia jamii kupata huduma kupitia mtandao kama vile matokeo ya mitihani, nafasi za mafunzo mbalimbali, nafasi za ajira na taarifa mbalimbali.

**230. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeanza ukarabati na kubadilisha muonekano wa majengo yake kulingana na mabadiliko ya Nembo ya kulitambulisha Shirika (**Let's Go!**). Mpaka sasa ofisi za Zanzibar pamoja na majengo saba ya Ofisi kuu za mikoa (Morogoro, Dodoma, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam na Arusha) yamefanyiwa ukarabati na kubadilishwa mwonekano wake. Aidha, zoezi hili ni endelevu kwa majengo yote nchi nzima kulingana na upatikanaji wa fedha na mpango wa maendeleo wa Shirika. Maandalizi yanaendelea kwa ajili ya kuanza ukarabati wa majengo ya ofisi kuu za mikoa ya Singida, Mtwara, Mara, Lindi, Songea, Iringa, Shinyanga na Sumbawanga.

**231. Mheshimiwa Spika**, Shirika linaendelea kuendesha Kituo cha Huduma Pamoja (Jamii Centre) katika Posta Kuu ya Dar es Salaam ambacho kinawezesha upatikanaji wa huduma za kiserikali mahali pamoja. Upanuzi wa kituo hiki na uongezaji wa huduma zinazotolewa unaendelea kufanywa. Aidha, Shirika linaendelea kuboresha majengo na kuweka muonekano mzuri. Katika mwaka 2019/20 Shirika limekamilisha uboreshaji wa majengo yake katika mikoa ya Dodoma, Arusha, Morogoro, Kigoma, Kagera, Dar es Salaam na Mjini Magharibi kwa upande wa Zanzibar, tayari kwa utoaji wa huduma hii. Aidha, katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa wateja na mali zao unaimarika kamera za ulinzi (CCTV) zimenunuliwa na kufungwa katika Ofisi za Mjini Magharibi Zanzibar na mikoa ya Dodoma, Kigoma, Kagera, Mwanza, Kilimanjaro na Tanga.

### **Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

**232. Mheshimiwa Spika**, Shirika limefanikiwa kuongeza idadi ya wasambazaji wakubwa wa muda wa maongezi kutoka 7 hadi 17 kufikia mwezi machi, 2020 ili kuhakikisha muda wa maongezi unapatikana nchi nzima. Aidha Shirika limeendelea kuboresha upatikanaji wa muda wa maongozi kwa kuwaelimisha na kuwaunganisha wateja wake na huduma ya T-pesa ili waweze kununua muda wa maongezi kupitia T-pesa kila wanapohitaji bila kulazimika kufika ofisi za Shirika au wakala.

**233. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kupata faida na kuondoka katika Mashirika yaliyokuwa yakijidesha kwa hasara. Kwa mwaka wa fedha 2018/19 Shirika limepata faida baada ya kodi ambayo ni zaidi ya Shilingi **bilion 6** na hivyo linatarajia kutoa gawio kwa Serikali baada ya taratibu za ndani kukamilika. Vilevile, Shirika limeendelea kusimamia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano nchi nzima kwa Ufanisi ambapo makampuni ya Simu, sekta binafsi, Serikali na Taasisi zake zinanufaika na huduma hizo za Mkongo.

**234. Mheshimiwa Spika**, Shirika limeendelea kutoa huduma za fedha kwa njia ya mtandao kupitia TTCL Pesa (T-PESA) ambapo tangu ilipoanzishwa mwezi Julai, 2017 hadi mwezi Februari, 2020 ilikuwa na jumla ya watumiaji wa huduma hiyo **796,421** na jumla ya **mawakala 22,364**. Ili kutanua wigo wa biashara, T-Pesa imeunganishwa kwenye mfumo wa malipo wa Serikali wa GePG, benki na watoa huduma za mawasiliano wengine.

#### **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**235. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imesaini mikataba na makampuni ya simu ili kupeleka huduma za mawasiliano katika **kata 252** zenye **vijiji 555** na wakazi zaidi ya **milioni 3** ambapo huduma za mawasiliano zinatarajiwa kuwa tayari katika maeneo hayo ifikapo Oktoba, 2020. Hatua hii ni mwendelezo wa utekelezaji wa miradi iliyotangulia ambapo Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeshapeleka huduma za mawasiliano katika **kata 704** zenye **vijiji 2,501** na wakazi zaidi ya **milioni 5** Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

**236. Mheshimiwa Spika** Serikali iko kwenye maandalizi ya kupeleka mawasiliano katika **kata 38** kwenye maeneo ya mipakani na yenye uhitaji maalum ambayo yatapatiwa mawasiliano katika tenda awamu ya tano (5) ambayo itatekelezwa na Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL). Kazi hii inatarajiwa kuanza mwezi Aprili, 2020.

**237. Mheshimiwa Spika** Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano imefanya malipo ya fedha za ununuzi wa vifaa vya TEHAMA

kwa ajili ya taasisi ya MOI na Hospitali ya Taifa MUHIMBILI ili kuunganisha hospitali katika mtandao na ukaguzi wa Hospitali na vituo vitakavyohusika. Hospitali zitakazounganishwa ni MOI, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Morogoro na Hospitali ya Mkoa Ruvuma.

**Tume ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICTC)**

**238. *Mheshimiwa Spika*,** Tume imefanya majoribio (pilot) ya usajili wa wataalam wa TEHAMA kuanzia tarehe 26 Juni, 2019 kupitia mfumo wa kielektroniki wa kusajili wataalam wa TEHAMA. Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2019 jumla ya **maombi 1,559** yalisajiliwa katika Mfumo wa Kielektroniki wa IPRS. Jumla ya maeneo 29 ya ubobezi (specialization) ambayo yamegawanywa katika makundi 11 yamebainishwa. Mwongozo wa kisera umeandaliwa na umeainisha madaraja manne ya utaalam wa TEHAMA (professional categories) ambayo ni *ICT Consultant, ICT Professional, ICT Graduate na ICT Technician*. Serikali imeanza hatua za awali za kutunga Sheria mahsus kwa ajili ya usajili na uendelezaji wa wataalam wa TEHAMA nchini kote.

**239. *Mheshimiwa Spika*,** Tume ilifanya kongamano la Tatu la Mwaka la TEHAMA (Tanzania Annual ICT Conference, TAIC) tarehe 23 hadi 25 Oktoba, 2019 jjini Dar es Salaam ambapo zaidi ya watu 400 kutoka ndani na nje ya nchi; kampuni saba kutoka nje ya Tanzania, kumi za hapa nchini pamoja na taasisi za Serikali zilishiriki maonesho na kujenga mashirikiano ya kibiashara na utoaji huduma za TEHAMA. Kupitia mikutano hii, Tume ya TEHAMA imeweza kukuza fursa za uwekezaji na mashirikiano ya kibiashara katika TEHAMA baina ya wajasiriamali wadogo na wakubwa pamoja na kubaini masuala yanayohitaji mikakati ya kisera ili nchi iweze kunufaika kiuchumi na maendeleo ya ukuaji wa TEHAMA duniani.

**240. *Mheshimiwa Spika*,** Tume imeanzisha kituo cha kuwaendeleza watengeneza bidhaa za TEHAMA inayoitwa *SoftCenter*. Kituo cha hicho kimeanzishwa kupitia mradi wa kutengeneza bidhaa za TEHAMA kutokana na TEHAMA zinazofikia mwisho wa mtumizi unaotekelizwa na Tume ya

TEHAMA; ni mpango wa Serikali wa kuendeleza vijana wa kitanzania wanaojihusisha na utengenezaji wa bidhaa za TEHAMA. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 bidhaa za vikundi Sita (6) vya kijasiriamali ziliikuwa zimesajiliwa na kushiriki program ya kuziendeleza. Tume pia imewezesha ushiriki wa bidhaa za TEHAMA zilizotengenezwa na vijana wa kitanzania kupitia kituo cha *SoftCenter* katika maonesho ya Nanenane Morogoro na SADC Dar es Salaam mwezi Agosti 2019; Kongamano la Tatu la Mwaka la TEHAMA Tanzania (TAIC) mwezi Oktoba, 2020; Wiki ya Viwanda Tanzania iliyofanyika Dar es Salaam mwezi Desemba, 2019 na tamasha la kuendeleza bidhaa za TEHAMA huko Luxembourg lilioitwa *Catapult: Inclusion Africa* mwezi Machi, 2020 ambalo liliandaliwa na *Luxembourg House of Financial Technology*. Mpango huu umewezesha bidhaa za kampuni zinazoshiriki mpango wa *SoftCenter* kuwafikia walengwa, kupata washirika wa kiblashara na kujulikana katika soko la bidhaa za TEHAMA.

**241. *Mheshimiwa Spika***, Tume imeendelea kutekeleza program ya kuwezesha wahitimu wa program za TEHAMA kutoka vyuo mbalimbali. Programu hii ilianza kutekelezwa Agosti 2019. Vijana sita (6) wamenufaika na program hii, wawili kati yao wamepata ajira katika Kampuni nyingine nchini.

#### **Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)**

**242. *Mheshimiwa Spika***, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) ni taasisi yenye jukumu la kulinda na kutetea maslahi ya watumiaji wa huduma za mawasiliano zinazodhibitiwa kisheria na TCRA. Katika mwaka 2019/20 Baraza limeendelea kutoa elimu na kuhamasisha watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano juu ya fursa na masuala muhimu kwa watumiaji wakiwemo Wanafunzi wa Sekondari, vyuo na watumiaji wenye mahitaji maalum (viziwi, wasioona na walemau wa viungo) ambapo idadi ya watumiaji takriban **3470** walifikiwa. Aidha, kupitia Maadhimisho ya wiki ya mtumiaji mwezi Machi, 2020 Baraza limewafikia watumiaji takribani **12,542**.

**243. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020 Baraza limeanzisha kamati za watumiaji katika Mkoa wa Kusini Pemba na kuendelea kushauriana na Kamati zingine 11 katika mikoa ya Arusha, Tanga, Morogoro, Mbeya, Iringa, Mwanza, Kagera, Mtwara, Lindi, Mjini Magharib na Dodoma. Aidha, Kamati ziliwafikia Watumiaji takribani **48,769** kutoka makundi ya vijana, wajasiriamali, wanawake, viongozi wa dini na Serikai za Mitaa pamoja na Watumiaji wenye mahitaji maalum. Katika Maadhimisho ya nanenane; Kamati katika mikoa ya Arusha, Lindi, Mbeya, Morogoro na Tanga zilihamasisha na kupokea maoni kutoka kwa watumiaji takriban **13,760**.

**244. Mheshimiwa Spika**, Baraza limeendelea kuwakilisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kuwasilisha maoni, taarifa na kushauriana na Mamlaka ya Mawasiliano. Aldha, Baraza limeshauriana na watoa huduma za mawasiliano kuhusu masuala yanayogusa watumiaji ikiwemo changamoto zitokanazo na huduma za vifurushi vya inteneti na sauti na kushauriana na Shirika la Posta Tanzania.

## C.2 TAASISI ZA MAFUNZO

**245. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inasimamia vyuo vya mafunzo vifuatavyo:  
**Chuo cha Ujenzi Morogoro (Morogoro Works Training Institute – MWTI)**

**246. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/20, Chuo cha Ujenzi kilipanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,200** wa fani za Barabara na Ulaguzi wa Madaraja, Majengo, Magari, Mfumo wa Umeme na Elektroniki. Chuo kilipanga kutoa pia mafunzo ya Madereva wa magari ya Umma (Public Professional Drivers), Madereva wa magari ya abiria (PSV), fani za ufunzi mbalimbali (Basic Artisans), Madereva wa awali, Madereva wa Magari ya Abiria, utengenezaji wa Mitambo (Plant Mechanics) na uendeshaji wa mitambo (Plant Operation) pamoja na Nguvukazi stahiki (Labour Based Technology). Aidha, Chuo kilipanga kutoa mafunzo kwa

makandarasi wanaotekeleza shughuli za ukarabati wa barabara, majengo na umeme hasa kwa wale makandarasi wa kazi maalum (Specialized Contractors) wa Daraja la I – III na waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi katika madaraja ya kuanzia IV - VII.

Hadi Machi, 2020 jumla ya wanafunzi **888** wa fani za ufundi stadi wa kozi za barabara na madaraja, majengo, Nguvukazi stahiki (Labour Based Technology), umeme, udereva wa mitambo, uchoraji majengo pamoja na udereva wa awali na magari ya abiria walipatiwa mafunzo. Aidha, Chuo kiliendelea na ukarabati wa majengo, ununuzi wa samani, ukarabati wa zana za kufundishia na magari, kikitangaza Chuo pamoja na kununua vifaa vya kufundishia.

### **Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi Mbeya (Appropriate Technology Training Institute - ATI)**

**247. Mheshimiwa Spika**, Chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kuratibu, kutoa na kuendeleza matumizi stahiki ya teknolojia ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara nchini.

**248. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2020 Chuo kimefanikiwa kuandaa na kuendesha mafunzo ya ukarabati na matengenezo ya barabara za changarawe, kozi maalumu ya vikundi vya wanawake na vijana katika kozi ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami; kufanya ukarabati wa miundombinu ya Chuo ili kuboresha huduma kwa watendaji wake na washiriki wa kozi; pamoja na kutoa mafunzo kwa njia ya vitendo kupitia barabara za mafunzo ambapo kilomita 1.2 zilikarabatiwa katika Halmashauri ya Rungwe na kilomita 21 zilizo chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS) Mbeya zilifanyiwa matengenezo ya kawaida kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo. Katika kutekeleza mafunzo ya vitendo wananchi wapatao 428 wamenufaika pamoja na kupata ujuzi wa kukarabati na kutengeneza barabara kwa kutumia Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi. Aidha, mita 40 ziliwekwa tabaka la lami (Single Surface Dressing) katika Barabara ya Lugombo, Mbeya.

Chuo vilevile kimeendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi hapa nchini kwa kushiriki kwenvye semina ya kimataifa ilioandalishi na Tanzania Roads Association (TARA) Mkoani Arusha, maonesho ya Nane nane kikanda yaliyofanyika Mkoa wa Mbeya na mukutano wa mwaka wa mashauriano wa pamoja kati ya Bodi za Usajili wa Wakandarasi (CRB), Wahandisi (ERB) na Wasanifu na Wakadiriaji Majenzi (AQRB). Aidha, Chuo kilifanya ziara ya kuhamasisha matumizi ya teknolojia stahiki ya nguvukazi na kutangaza shughuli za Chuo katika ofisi za Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Morogoro, Lindi na Mtwara ambapo jumla ya Halmashauri ishirini na saba (27) zilitembelewa na kuhamasishwa. Chuo vilevile kimeendelea na maandalizi ya marekebisho ya miundombinu ya Chuo ili kukidhi mahitaji ya uanzishwaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).

### **Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

**249. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimeendelea kutoa mafunzo ya Uujuzi na Utaalamu (Certificates of Competency) masuala ya usafiri majini kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Shirika la Bahari Duniani (IMO). Aidha, Chuo hiki kinaendeshwa kwa kuzingatia Ubora wa Viwango vya Kimataifa yaani ISO 9001:2015. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, DMI ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kutoa kozi ndefu 21 ambapo Wanafunzi 1,126 walidahiliwa katika mwaka wa masomo 2019/20. Aidha, jumla ya Wanafunzi 1,266 walidahiliwa kwa mafunzo ya kozi fupi za awali katika taaluma ya bahari;
- (ii) Kununua Boti ndogo ya mafunzo ili kuboresha elimu kwa vitendo katika kozi fupi za usalama baharini;
- (iii) Kukamilisha taratibu za kumpata Mtaalamu Mwelekezi wa kupanga matumizi bora ya Ardhi (Master Plan) katika eneo la Chuo lililopo Mkuranga na Sokoine Drive;

- (iv) Kukamilisha uboreshaji wa Mitaala 18 na kuandaa Mitaala mipyä ya fani mbalimbali katika Sekta ya Bahari ikiwemo fani za utafiti na uchimbaji wa Gesi na Mafuta baharini;
- (v) Kuanza kutoa mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika taaluma ya Uchumi wa Usafirishaji wa Shehena Baharini na Lojistiki; na
- (vi) Kupeleka Walimu wanane (8) nchini China kwa ajili ya masomo ya juu kwenye fani ya Bahari ambapo Walimu wawili (2) wanasoma Shahada ya uzamivu (PhD) na sita (6) Shahada ya uzamili.

### **Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

**250. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2019/2020. Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa wataalamu wa uchukuzi ili kuimarishwa utoaji huduma katika Usafiri kwa njia ya Anga, Maji, Reli na Barabara. Katika mwaka 2019/2020, Chuo kilitoa kozi ndefu 24 ikilinganisha na kozi 21 zilizotolewa katika mwaka wa masomo 2018/2019. Kozi hizi zilidahili jumla ya Wanafunzi 3,561 ikilinganishwa na Wanafunzi 2,877 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 24. Kutokana na ubora wa taaluma na mafunzo yanayotolewa katika Chuo hiki, hadi, Machi, 2020, Chuo kilikuwa na jumla ya Wanafunzi 7,694 ikilinganishwa na Wanafunzi 6,688 waliokuwepo katika kipindi kama hiki katika mwaka. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 15. Aidha, katika mwaka 2019/2020, jumla ya Wanafunzi 1,966 walihitimu mafunzo yao katika kozi ndefu ikilinganishwa na Wanafunzi 1,550 waliohitimu katika mwaka wa masomo 2018/2019. Hili ni ongezeko la asilimia 27.

**251. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeanzisha Kituo cha Umahiri katika Taaluma ya Mafunzo ya Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji (Center of Excellence in Aviation and Transport Operations - CEATO) kilichoko chini ya Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Lengo la kuanzisha kituo hiki ni kukiwezesha Chuo kufundisha wataalamu wabobezi wa Sekta ndogo za usafiri

wa Anga, Reli, Barabara na usafiri kwa njia ya Maji. Kazi ya kuandaa Mitaala sita (6) ya kufundisha wataalamu hawa imekamilika na sasa iko kwenye hatua za mwisho za kupata Ithibati kutoka Baraza la Taifa la Elimu la Ufundsi (NACTE) na Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA).

**252. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali inatambua uwepo ya changamoto za ajali za barabarani na usalama katika uchukuzi. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imepata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ili kuanzisha Kituo cha Kikanda cha Umahiri wa Mafunzo ya Usalama Barabarani (Regional Centre of Excellence in Road Safety). Kituo hiki kitawajengea uwezo zaidi wataalamu wa masuala ya usalama barabarani. Pia, kituo kitafanya tafiti mbalimbali ili kushauri namna bora ya kusaidia kupunguza ajali za barabarani. Chuo kinaendelea na taratibu za kuanzisha Kituo hiki.

**253. *Mheshimiwa Spika*,** kwa upande wa uboreshaji wa miundombinu na mazingira ya kufundishia na kufanyia kazi, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Chuo kimeendelea kukamilisha upanuzi wa majengo ya utawala na uhasibu; na ujenzi wa jengo jipya la ghorofa mbili (Aviation Complex) ambalo litakuwa na madarasa, ofisi za Wahadhiri, Ukumbi wa Mikutano, Maabara pamoja na Karakana ya Ndege.

#### **Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam (CATC)**

**254. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali imeendelea kuhakisha kuwa Chuo cha Usafiri wa Anga Dar es Salaam kinaendelea kuboreshwa ili kukidhi matakwa ya kitaifa na kimataifa. Chuo hiki ambacho kimepata Ithibati ya Kudumu ya Shirika la Usafiri wa Anga Duniani Oktoba, 2019, kina ushirikiano wa karibu na Umoja wa Vyuo vya Tasnia ya Usafiri wa Anga vya Afrika (The Association of African Aviation Training Organisations - AATO). Aidha, Chuo kimeendelea kudahili wanafunzi kutoka nchi za Uganda, Botswana, Namibia, Eswatini, Zambia, Burundi, Rwanda, Somalia, Nigeria, Liberia, Sierra Leone na Guinea Conakry. Aidha, sehemu kubwa ya wahitimu wa

Chuo hiki ni kutoka nje ya Tanzania ambapo kati ya wanafunzi 1,395 waliohitimu mafunzo katika mwaka 2018/2019, wazawa ni 55 na waliotoka nje ya nchi ni 1,340.

### **Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma**

**255. *Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ili kuweka mazingira bora ya ufundishaji. Katika mwaka 2019/2020, jumla ya Wanafunzi 68 walidahiliwa ikilinganishwa na wanafuzi 58 waliodahiliwa katika mwaka 2018/2019. Kati ya hao, wanafunzi 14 walikuwa ngazi ya Cheti na 54 ngazi ya Diploma. Aidha, jumla ya wanafunzi 57 walihitimu mafunzo yao ambapo wanafunzi 30 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Cheti na 27 walihitimu mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya Diploma.

### **C.3 MASUALA MTAMBUKA**

#### **Ushirikishwaji wa Wanawake Katika Kazi za Barabara**

**256. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu kazi za ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara ikiwa ni pamoja na elimu juu ya Mwongozo wa Ushirikishwaji Wanawake katika kazi za barabara. Kazi nyingine ilikuwa ni kutoa mafunzo kwa wanawake Makandarasi **20** kutoka Mikoa ya Tabora, Kigoma, Katavi na Rukwa kuhusu usimamizi wa mikataba, teknolojia ya nguvukazi na namna bora ya ujazaji zabuni yaliyofanyika mkoani Kigoma. Lengo ni kuwajengea uwezo wa kumudu ushindani katika kazi za ukandarasi na hatimaye kuwezesha makampuni yao kupanda madaraja. Wizara vilevile iliratibu na kuendesha mafunzo mkoani Morogoro kwa wanawake **50** waliotoka katika vikundi na kampuni kutoka mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Singida, Shinyanga, Songwe, Ruvuma, Manyara na Tanga ili kuwapa ujuzi wa kushiriki katika kazi za barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvukazi.

## **Maboresho ya Sheria za Kisekta**

**257. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara iliendelea na kazi ya kupitia sheria zinazohusu sekta kwa lengo la kuainisha maeneo yenye mapungufu na yanayohitaji kufanyiwa marekebisho. Sheria zinazofanyiwa mapitio ni pamoja na Sheria ya Barabara Sura ya 167, Sheria ya Baraza la Taifa la Ujenzi Sura ya 162, Sheria ya Usajili wa Makandarasi Sura ya 263, Sheria ya Usajili wa Wahandisi Sura ya 63 na Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi Sura ya 269. Baada ya mapitio na marekebisho ya Sheria kufanyika, Wizara itafanya mapitio ya Kanuni na Sheria Ndogondoggo zilizotungwa chini ya Sheria hizo ili kuleta ufanisi wenye tija wakati wa utekelezaji wake.

## **Ushiriki wa Wizara Katika Jumuiya Mbalimbali za Kimataifa**

**258. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2019/20, Wizara imeendelea kushiriki katika mikutano inayohusu Sekta ya Ujenzi katika Jumuiya za Kimataifa na Kikanda hususan Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya za Utatu (COMESA, EAC and SADC Tripartite Free Trade Area).

**259. *Mheshimiwa Spika*,** kutokana na ushiriki wa Wizara katika mikutano hiyo, tumeweza kupata mafanikio mbalimbali ikiwemo kupata fedha kutoka NEPAD-IPPF/AfDB kwa ajili ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na ujenzi wa miradi ya barabara ya Lusahunga – Rusumo/Kayonza – Kigali inayounganisha Tanzania na Rwanda; barabara ya Nyakanazi – Kasulu – Manyovu/Rumonge – Rutunga – Bujumbura inayounganisha Tanzania na Burundi; na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Bugene – Kasulo – Kumnazi na Kyaka – Mutukula – Masaka inayounganisha Tanzania na Uganda. Aidha, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kutekeleza miradi mbalimbali ya barabara kupitia program zifuatazo: ***Development Corridors Transport Project - DCTP***, Miradi itakayotekelzwa chini ya programu hii ni ukarabati

wa barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200); ukarabati wa barabara ya Lusahunga – Rusumo (km 92); ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295); ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe (Ruaha National Park) - km104 na ujenzi wa Viwanja vya ndege vya Iringa, Lake Manyara na Tanga. Kuhusu **Lake Victoria Transport Programme** - **LVTP** miradi itakayotekelawa ni pamoja na upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Musoma Port Access na Nansio - Rugezi Port access. Kazi nyingine ni kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ukarabati wa barabara ya Mara /Simiyu Border – Nyanguge (km 100.4) na mapitio ya Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina pamoja na ujenzi wa barabara ya Nyamuswa – Bunda – Bulamba - Kisorya (km 106) na Bukoba - Bukoba Port Access. Aidha, Programu ya **Lake Tanganyika Transport Programme** (**LTTP**) miradi itakayotekelawa chini ya programu ya **LTTP** ni upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Kagwira – Karema (km 112) na ujenzi wa barabara ya Mpanda (Vikonge) – Uvinza (km 159).

**260. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Jumuiya ya Maendeleo Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), baadhi ya masuala muhimu yanayojadiliwa ni pamoja na:

i. Uwianishaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango kuhusu usafirishaji wa mizigo mizito kwa magari makubwa kwa njia ya barabara. Majadiliano hayo yamehusisha Jumuiya za Utatu (COMESA, EAC and SADC Tripartite Free Trade Area) ambapo lengo kuu ni kurahisisha ufanyaji wa biashara katika Jumuiya tatu kwa kuwanisha viwango vya usafirishaji wa mizigo pamoja na ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi wa Magari.

ii. Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya barabara iliyojumuishwa katika Mpango Kamambe wa Uendelezaji wa Miundombinu kwa Nchi Wanachama wa SADC. Miradi hiyo ni ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea (km 295) na ujenzi wa barabara ya Kidatu – Ifakara – Malinyi – Londo – Lumecha (km 496) kwa kiwango cha lami.

## Rasilimali watu na Maendeleo ya Watumishi

**261. Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jumla ya watumishi **520**. Katika mwaka wa fedha 2019/20, watumishi **24** walistaafu; mmoja **(1)** aliacha kazi na mmoja **(1)** aliachishwa kazi. Watumishi waliostaafu kazi kwa mujibu wa Sheria waligharamiwa na Wizara kuhudhuria mafunzo ya kujiandaa na maisha baada ya kustaafu kazi wakati mafao yao yanaandaliliwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF). Aidha, Wizara imewaendeleza watumishi wake kitaaluma kwa kuwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi ikiwa ni pamoja na kutumia fursa mbalimbali za wafadhili. Hadi Machi, 2020, jumla ya watumishi **179** wamehudhuria mafunzo. Kati ya hao, watumishi **21** walishiriki mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi na watumishi **158** walishiriki mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

## Masuala Mengine Yaliyoteklezwa na Wizara

**262. Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kukabiliana na mlipuko wa maambukizi ya ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayotokana na virusi vya corona (COVID - 19) tangu kugundulika kwa virusi hivyo nchini China Disemba, 2019. Hatua hizo ni pamoja na:

- i. Kuendelea kuhamasisha watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake kuhusu kufuata miongozo inayotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto;
- ii. Kutoa elimu endelevu kwa wafanyakazi wanaohudumia abiria na ndege katika viwanja vyote vya ndege na vituo vya mabasi nchini;
- iii. Kutoa huduma ya vifaa kinga na vitakasa mikono kwa abiria wanaoingia na kutoka kwenye vyombo vya moto vya abiria na viwanja vya ndege;
- iv. Kutoa taarifa sahihi kwa wateja kuhusiana na kuwepo/ kutokuwepo kwa safari zao za ndege;

- v. Kutoa huduma ya usafiri wa treni ya abiria ya mijini kwa siku za Jumamosi ili kupunguza msongamano wa abiria;
- vi. Kushirikiana na Jeshi la Polisi (Kitengo cha Usalama barabarani) kuhakikisha kuwa mabasi ya mijini hayazidishi abiria (level seat), Mabasi ya UDART yanabebe abiria kwa kiwango cha asilimia 60 tu, Mabasi ya masafa marefu yanabebe abiria kulingana na idadi ya viti ndani ya basi; na
- vii. Kuendelea kutunza mazingira ndani na nje ya vyombo vya usafiri wa Umma.

**263. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara imeendelea kutoa elimu kwa Umma kuhusu Sera na Mipango inayosimamiwa na Wizara pamoja na kuzitunza na kuhifadhi barabara zetu, kuzingatia Sheria na Kanuni za Matumizi ya Barabara. Aidha, Wizara imeendelea kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuongeza ufanisi na kutoa huduma kwa wakati. Mfumo wa utoaji wa vibali vya kusafirisha mizigo isiyo ya kawaida (Abnormal Loads Permit System ALPS) kwa njia ya kielektroniki unaendelea kutoa huduma kwa wasafirishaji nchini na nje ya nchi. Tovuti ya Wizara imeboreshwa ili kuhakikisha kuwa wananchi wengi wanapata taarifa mbalimbali zinazohusiana na Sekta ya Ujenzi. Wizara pia ipo katika hatua za maandalizi ya uundaji wa mifumo ya usimamizi na ufuutiliaji wa shughuli za Wizara pamoja na Taasisi zake. Mifumo hiyo ni “Intergrated Infrastructure Management System (IIMS)” na “Ferry Management System (FMS)”.

#### **C.5 CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA NA MIKAKATI YA KUZITATUA**

**264. *Mheshimiwa Spika*,** katika utekelezaji wa majukumu yake, Wizara ilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Changamoto hizo ni pamoja na mahitaji makubwa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Miundombinu na utoaji wa huduma za uchukuzi. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali inaendelea kujadiliana na wawekezaji mbalimbali ikiwa ni pamoja na Taasisi za fedha ili kupata mikopo yenye masharti

nafuu kwa ajili ya kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo. Aidha, Serikali inaendelea kushawishi Sekta Binafsi kuwekeza katika uendelezaji na uboreshaji wa miradi ya uchukuzi.

**265. *Mheshimiwa Spika*,** vilevile, kuna changamoto ya tishio la homa inayosababishwa na virusi vya Corona (COVID 19). Hali hii imeleta hofu kubwa katika Sekta ya Uchukuzi hususan kwenye Bandari na Viwanja vya Ndege hivyo kuathiri Utendaji wa Taasisi zinazotoa huduma katika maeneo hayo. Wizara inaendelea kuchukua tahadhari katika vituo vya Mipakani, Viwanja vya Ndege na maeneo ya Bandari ili kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona. Aidha, vifaa vya kinga vimeendelea kutolewa kwa wafanyakazi katika maeneo hayo pamoja na utoaji wa elimu kwenye vyombo vya usafiri.

**266. *Mheshimiwa Spika*,** changamoto nyingine ni uvamizi, uharibifu na hujuma kwa Miundombinu ya Reli, hususan Reli zenyewe, Mataruma, Vifungio na Madaraja. Wizara itaendelea kushirikiana na vyombo vya Dola pamoja na jamii inayozunguka maeneo ya Reli ili kusimamia Sheria zilizopo kuhusu uharibifu huo pamoja na kutoa elimu na hamasa kwa jamii inayopakana na maeneo ya Reli ili kuelewa umuhimu wa Reli na kuwa walinzi wa miundombinu hiyo.

**267. *Mheshimiwa Spika*,** kuna changamoto ya Mabadiliko ya hali ya hewa (Climate Change) yanayosababisha Mifumo ya hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu kutokana na mafuriko. Kwa kutambua hili, Wizara imeendelea kupanua Mtandao wa Rada za Hali ya Hewa, kuongeza vifaa na kupanua Mtandao wa vituo vya hali ya hewa nchini kwa lengo la kuboresha utoaji wa utabiri na tahadhari juu ya matukio ya hali mbaya ya hewa na kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa.

#### **D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA SEKTA ZA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

**268. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2020/21 ni wa tano (5) na wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 –20/21). Katika mwaka wa fedha 2020/21, Mpango na Bajeti ya Wizara umelenga kuzingatia vipaumbele ambavyo ni Miradi iliyoainishwa kwenye llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 na llani ya Chama cha Mapinduzi ya Awamu zilizopita; Miradi iliyoainishwa kwenye Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Miradi iliyoainishwa kwenye malengo ya Mpango Mkakati wa Wizara; Miradi iliypopo kwenye ahadi mbalimbali za Viongozi wa Serikali tangu Awamu ya Kwanza; Miradi ambayo Washirika wa Maendeleo wameonesha nia ya kutoa fedha za utekelezaji ambapo Serikali inatakiwa kutoa mchango wake (Counterpart Fund); Miradi ya Kimkakati (kama vile ya ulinzi wa mipakani, inayoelekea kwenye vivutio vya utalii, Bwawa la kufua umeme la Nyerere, ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge*, ufufuaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania na ujenzi na ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu) inayohusu barabara, madaraja, bandari, viwanja vya ndege, reli na vivuko ambayo itakuwa na matokeo makubwa katika Sekta nyineza za kiuchumi; Miradi ya Makao Makuu ya Nchi kama vile miradi ya barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Dodoma, uwanja wa ndege wa Msalato, treni za abiria mijini (commuter trains), nyumba za Watumishi wa Umma na majengo ya Serikali.

**269. Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kutekeleza miradi yote kwa uwazi na kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma ili kupusha kuwepo kwa vitendo vya rushwa. Aidha, Wizara itachukua hatua stahiki dhidi ya watakaobainika kukiuka sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

#### D.1.1 SEKTA YA UJENZI

**Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**270. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekta ya Ujenzi kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni **Shilingi**

**38,774,425,000.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 36,420,026,000.00** ni Bajeti ya Mishahara na **Shilingi 2,354,399,000.00** ni Bajeti ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Sekta ya Ujenzi imetengewa jumla ya **Shilingi 1,577,586,781,000.00** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,252,222,598,000.00** ni fedha za ndani na Shilingi **325,364,183,000.00** ni za fedha za nje.

Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Na.1.** Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo ni kama ifuatavyo:

#### **MRADI WA KUJENGA UWEZO (INSTITUTIONAL CAPACITY BUILDING)**

**271.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 302.50** fedha za ndani kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi wa Sekta ya Ujenzi kwa kuwapatia mafunzo na vitendea kazi vya ofisi kwa ajili ya kuboresha utendaji wa Sekta ya Ujenzi.

#### **MIRADI YA VIVUKO, UJENZI WA NYUMBA NA MAJENGO YA SERIKALI**

##### **Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko**

**272.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi Ujenzi na Ukarabati wa Vivuko na Maegesho ya Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,785.11** kama ifuatavyo:

##### **i) Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko**

**273.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 2,868.82** zimetengwa kwa ajili ya upanuzi wa jengo la abiria na maegesho ya Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia; ujenzi na ukarabati wa maegesho nane **(8)** ya Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita,

Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Kigongo – Busisi; ujenzi wa ofisi, jengo la abiria na uzio kwenye vituo **10** vya vivuko (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakaliro, Misome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma, na Kinesi)pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ngara – Nyakiziba na Muleba – Ikuza. Lengo ni kuwezesha abiria na magari kupanda na kushuka kwenye vivuko nyakati zote za mwaka.

#### **ii) Ujenzi wa Vivuko Vipya**

**274. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa **Shilingi milioni 6,748.62** kwa ajili ya kukamilisha manunuzi na ujenzi wa vivuko vipya vya Nyamisati – Mafia na Bugolora – Ukara; kuanza manunuzi ya Kivuko kipyta cha Kisorya – Rugezi, boti 1 ya uokozi kwa ajili ya Utete – Mkongo pamoja na ununuzi wa vifaa vya karakana za TEMESA.

#### **iii) Ukarabati wa Vivuko**

**275. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi Ukarabati wa Vivuko umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 4,167.67** kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa Vivuko MV Tegemeo (Mwanza), MV Musoma (Mara), MV Mara (Mara), MV Misungwi (Mwanza), MV Sengerema (Mwanza), MV Ujenzi (Mwanza), MV Kigamboni (Dar es Salaam), MV Kome II (Mwanza) na boti ya uokozi MV KIU (Mwanza). Kazi nyingine ni kuanza ukarabati wa MV Nyerere (Mwanza), MV Kilombero I (Morogoro) na MV Kilombero II (Morogoro).

#### **Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

**276. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 66,870.38** kwa ajili ya kutekeleza miradi ifuatavyo:

#### **i) Ujenzi wa Nyumba za Viongozi**

**277. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 6,991.66** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **20** za Viongozi Dodoma pamoja na kuendelea na ujenzi wa nyumba **6** za Majaji katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Kagera na Tabora.

**ii) Ujenzi wa nyumba 150 za Watumishi wa Umma**

**278.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10,500.00** zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba **150** za Watumishi wa Umma Jijini Dodoma na mikoa mingine.

**iii) Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano**

**279.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka fedha 2020/21 mradi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano katika Mji mpya wa Serikali Mtumba – Dodoma, umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,598.04** kwa ajili ya kukamilisha usanifu na kuanza ujenzi.

**iv) Ujenzi wa Nyumba za Makazi Eneo la Magomeni (Magomeni Quarters)**

**280.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 14,650.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa nyumba za Makazi za waliokuwa wakazi wa Magomeni *Quarters*, Dar es Salaam.

**v) Ukarabati wa Nyumba na Manunuzi ya Samani kwa Ajili ya Nyumba za Viongozi**

**281.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 14,290.20** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za viongozi na ununuzi wa samani. Kazi zilizopangwa ni ukarabati wa nyumba 40 za viongozi Dodoma na nyumba 30 mikoa mingine, ukarabati wa nyumba 400 zilizokua zinamilikiwa na iliyokuwa Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma (CDA) zilizohamishiwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), ukarabati wa nyumba zilizokuwa zinamilikiwa na TAMISEMI na NHC zilizohamishiwa TBA katika mikoa 20 pamoja na ununuzi wa samani za nyumba za Ikulu na Ikulu Ndogo za Serikali.

**vi) Kujenga Uwezo wa Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi na Huduma za Ushauri**

**282.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 1,271.52** zimetengwa kwa ajili ya

kuwajengea uwezo Wabunifu Majengo (Architects) na Wakadiriaji Majenzi (Quantity Surveyors) kuititia Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), Huduma za Ushauri pamoja na maandalizi ya viwango vya msawazo (*standards and specifications*) kwa ajili ya kazi na miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali pamoja na samani.

**vii) Ujenzi na Ukarabati wa Karakana za TEMESA na TBA**

**283. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 8,138.96** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa karakana kumi na moja (11) za TEMESA zilizopo Tabora, Mwanza, Arusha, Mtwara, Mbeya, M.T Depot Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti. Kazi nyingine ni kuendelea na ujenzi wa karakana za TEMESA katika Mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi na ujenzi wa karakana mpya ya magari jijini Dodoma. Kazi nyingine ni ukarabati wa karakana za TBA sita (6) katika mikoa ya Tabora, Arusha, Mwanza, Dodoma, Mbeya na Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa kiwanda kipyga cha kutengeneza samani.

**viii) Ufutiliaji na Tathmini kwenye Miradi ya Ujenzi na Ukarabati wa Nyumba na Majengo ya Serikali**

**284. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 830.00** zimetengwa kwa ajili ya ufutiliaji na tathmini (monitoring and evaluation) kwenye miradi ya ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali.

**ix) Ununuzi wa Karakana Sita (6) Zinazohamishika (Mobile Workshops)**

**285. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa karakana sita zinazohamishika kwa ajili ya matengenezo ya magari ya Serikali katika wilaya ambazo ziko mbali na makao makuu ya mikoa.

x) Kusanifu na Kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari

286. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 3,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Ufuatiliaji wa Matengenezo ya Magari.

xi) Kuanzisha Karakana za Wilaya Pamoja na Kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Magari

287. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 600.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi na ukarabati wa karakana sita za wilaya (Same, Simanjiro, Masasi, Ukerewe, Chato na Kyela) pamoja na kusimika mifumo ya usimamizi wa taarifa za ukarabati wa magari.

#### MIRADI YA BARABARA NA MADARAJA

288. *Mheshimiwa Spika*, miradi ya barabara na madaraja itakayotekelezwa katika mwaka wa fedha 2020/21 ni kama ifuatavyo:

##### Barabara ya Soni - Bumbuli - Dindira - Korogwe (km 74)

289. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 840.00** kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

##### Barabara ya Mtwara - Newala - Masasi (km 221)

290. *Mheshimiwa Spika*, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Mtwara - Newala - Masasi kwa sehemu ya Mtwara - Mnivata (km 50) na maandalizi ya kuanza ujenzi wa sehemu ya Mnivata - Tandahimba (km 50).

##### Barabara ya Likuyufusi - Mkenda (km 122.50)

291. *Mheshimiwa Spika*, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,590.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi wa sehemu ya barabara hiyo yenye urefu wa kilometra 10.

**Barabara ya Nachingwea – Liwale (km 130)**

**292. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 250.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nachingwea - Liwale.

**Barabara ya Ubena Zomozi - Ngerengere (km 11.6)**

**293. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 730.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ubena – Zomozi – Ngerengere kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga (km 24)**

**294. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 950.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya TAMCO – Vikawe – Mapinga.

**Barabara ya Makofia – Mlandizi (km 36.7)**

**295. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara ya Makofia – Mlandizi imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Musoma - Makojo - Busekela (km 92)**

**296. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,625.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kongwa Jct – Mpwapwa – Gulwe – Kibakwe (km 98)**

**297. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,650.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muhutwe – Kamachumu – Muleba (km 54)**

**298. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,080.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Iringa – Ruaha National Park (km 104)**

**299.** *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka wa fedha 2020/21, barabara hii imetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Iringa – Msembe - Ruaha National Park kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Muheza – Amani (km 36)**

**300.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,590.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mtwara – Mingoyo – Masasi (km 200)**

**301.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya ukarabati wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 189)**

**302.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 5,420.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kibaoni – Majimoto – Inyonga (km 152) na Ntendo – Muze – Kilyamatundu sehemu ya Ntendo – Muze (km 37) kwa kiwango cha lami.

**Daraja la Kigongo - Busisi na Barabara Uganishi**

**303.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 21,295.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi (km 3.2) na barabara unganishi.

**Daraja la Mzinga**

**304.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Mzinga.

**Daraja la Ugalla**

**305.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 250.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa Daraja la Ugalla.

### **Daraja la Kitengule na Barabara Uganishi**

**306. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Kitengule pamoja na barabara uganishi zenyе urefu wa kilometra 18.

### **Barabara ya Morogoro - Dodoma (km 260.0) Pamoja na Daraja la Mkundi**

**307. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,125.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ukarabati wa barabara ya Morogoro – Dodoma pamoja na Daraja la Mkundi.

### **Daraja Jipya la Wami**

**308. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 3,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Wami liliopo mkoani Pwani.

### **Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4)**

**309. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 22,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Njombe – Makete – Isyonje sehemu ya Njombe – Moronga (km 53.9) na Moronga – Makete (km 53.5). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Isyonje – Makete (km 50) kwa kiwango cha lami.

### **Barabara ya Omugakorongo - Kigarama - Murongo (km 105)**

**310. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 8,000.00** zimetengwa kwa ajili ya fidia na kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

### **Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145)**

**311. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 7,430.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara za Masasi – Nachingwea (km 45.0) na Nanganga – Ruangwa – Nachingwea (km 100.0) sehemu ya Nanganga – Ruangwa (km 53.2) kwa kiwango cha lami.

### Barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2)

**312. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 5,310.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Mpemba – Isongole (km 51.2). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Ruanda – lyula – Nyimbili (km 21.0) na kuanza ujenzi kwa utaratibu wa *Design and Build* barabara ya Katumbasongwe - Kasumulu - Ngana – lleje (km 90.10) kwa kiwango cha lami.

### Barabara ya Tanga - Pangani - Makurunge (km 174.5)

**313. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 50,800.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tanga - Pangani (km 50). Kati ya hizo, fedha za ndani ni **Shilingi milioni 7,000.00** na **Shilingi milioni 43,800.00** ni fedha za nje. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Pangani – Mkange (km 124.5) kwa kiwango cha lami na Daraja la Pangani.

### Barabara ya Kisarawe – Maneromango (km 54)

**314. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 1,400.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

### Barabara ya Geita – Bulyanhulu – Kahama (km 120)

**315. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,500.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Geita – Bulyanhulu Jct (km 58.3), Bulyanhulu Jct – Kahama (km 61.7) na Uyogo – Nyamilangano – Nyandekwa – Kahama (km 54).

### Barabara ya Nyamirembe Port – Katoke (km 50)

**316. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Geita – Nzera (km 54)**

**317. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii.

**Barabara ya Arusha - Moshi - Himo - Holili (km 199.51)**

**318. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 4,800.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kijenge – Usa River (km 20). Aidha, fedha hizi zitahusisha maandalizi ya kuanza ujenzi wa barabara ya Mianzini – Ngaramtoni (km 18.0) kwa kiwango cha lami na upanuzi wa barabara ya Tengeru – Moshi – Himo (km 105) pamoja na ujenzi wa Mizani ya Himo.

**Barabara za Kuelekea Kwenye Mradi wa Kufua Umeme Katika Maporomoko ya Mto Rufiji (Access Roads To Rufiji Hydropower Project)**

**319. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,179.00** kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha changarawe wa barabara za Bigwa – Matombo – Mvuha (km 70), Maneromango - Vikumburu - Mloka (km 100) na Kibiti – Mloka - Mtemele – Rufiji. Aidha, mradi huu utahusisha ukarabati kwa kiwango cha changarawe sambamba na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Ubena Zomozi - Mvuha - Kisaki - Mtemele Jct (km178) ikiwa ni mandalizi ya kuijenga kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dar es Salaam – Chalinze – Morogoro (km 152.3)**

**320. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,810.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati (*overlay*) wa barabara ya Mlandizi – Chalinze (km 44) na ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kwa Mathiasi (Morogoro Road) – Msangani (km 8.3).

**Barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (km 54.1)**

**321. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 80.00** kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati na upanuzi wa

barabara ya Wazo Hill – Bagamoyo – Msata (Tegeta – Bagamoyo Section) (km 46.9) na barabara ya Mbegani – Bagamoyo (km 7.2).

**Barabara ya Usagara – Geita – Buzirayombo – Kyamyorwa (km 110)**

**322. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kulipa sehemu ya malipo ya Makandarasi kwa sehemu za Uyovu – Bwanga (km 43) na Bwanga – Biharamulo (km 67).

**Barabara ya Nyakahura - Kumubuga - Rulenge - Kabanga Nickel Road (km 141)**

**323. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 30.00** kwa ajili ya kuendelea na kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Nyakahura – Kumubuga – Murusagamba na Kumubuga – Rulenge – Kabanga Nickel (km 141) ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7)**

**324. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 25,440.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 10,440.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 15,000.00** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Urambo – Kaliua (km 28), Kazilambwa – Chagu (km 42) na kuanza ujenzi wa kwa kiwango cha lami sehemu ya Uvinza – Malagarasi (km 51.1).

**Barabara ya Ifakara - Kihansi - Mlimba - Madeke - Kibena (Njombe) (km 220)**

**325. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara ya Kibena – Lupembe (km 50) kwa kiwango cha lami na maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Ifakara – Kihansi (km 50) na Lupembe – Madeke (km 50).

**Barabara ya Karatu - Mbulu - Haydom - Sibiti River - Lalago - Maswa (km 389)**

**326. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,000.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya Karatu – Mbulu – Hydom – Sibiti River – Lalago – Maswa sehemu ya Mbulu – Hydom (km 50).

**Barabara ya Marangu – Tarakea – Rongai – Kamwanga / Bomang’ombe – Sanya Juu (km 84.80)**

**327. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,700.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Kwa Sadala – Masama – Machame Junction (km 16) na Kiboroloni – Kiharara – Tsuduni – Kidia (km 10.8).

**Barabara ya Tukuyu – Mbambo – Katumba (km 80.3)**

**328. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,850.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Tukuyu – Mbambo (km 34.6). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu za Bujesi – Mbambo (km 26.0) na Mbambo – Ipinda (km 19.7).

**Barabara ya Dodoma – Manyoni (km 127) na Barabara ya Mchepuo Kuingia Manyoni Mjini (km 4.8)**

**329. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 160.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi (One Stop Inspection Station – OSIS) cha Muhalala (Manyoni).

**Barabara ya Tabora - Mambali - Bukene - Itobo (km 114)**

**330. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Namanyere - Katongoro - New Kipili Port (km 64.80)**

**331. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 310.00** kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Dumila – Kilosa – Mikumi (km 119)**

**332. *Mheshimiwa Spika*,** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,520.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Rudewa – Kilosa (km 24) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kilosa – Ulaya – Mikumi (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112)**

**333. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha wa 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Sumbawanga – Matai – Kasanga Port (km 112) na kuanza ujenzi wa barabara ya Matai – Kasesya (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Ujenzi wa Madaraja Makubwa**

**334. *Mheshimiwa Spika*,** mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,185.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya kuanza ukarabati wa daraja la Kirumi (Mara); kuendelea na ujenzi wa Daraja la Sibiti (Singida) na barabara zake unganishi, Daraja la Msingi (Singida), Daraja la Ruhuhu (Ruvuma) na Daraja la Sukuma (Mwanza). Aidha, kazi nyingine ni kufanya mapitio ya usanifu na ujenzi wa Daraja la Mirumba (Katavi); ujenzi wa Daraja la Simiyu (Mwanza), Daraja la Kiegeya (Morogoro), Daraja la Sanza (Singida) na Daraja la Mkenda (Ruvuma). Vilevile, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Daraja la Mtera (Iringa/Dodoma), Daraja la Godegode (Dodoma) na Daraja la Mitomoni (Ruvuma); kuanza upembuzi yakinifu na Usanifu wa Kina wa Daraja la Malagarasi Chini (Kigoma) na kununua Vipuri vyaa Daraja la vyuma la dharura (Emergency Steel Bridge Parts).

**Barabara ya New Bagamoyo (Kawawa Jct – Tegeta (km 17.2)**

**335. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 11,363.89** zimetengwa ambapo fedha za ndani ni **Shilingi milioni 260.00** na fedha za **nje Shilingi milioni 11,103.89** kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa sehemu ya Morocco – Mwenge (km 4.3) na kuboresha mifereji ya maji ya mvua kwenye sehemu ya Mwenge – Tegeta (km 14).

**Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 222.10)**

**336. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 2,010.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha mapitio ya usanifu wa barabara za Kumunazi - Bugene – Kasulo (km 133) na Kyaka - Mutukula (km 30) ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Isaka – Lusahunga (km 392.0)**

**337. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 2,740.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kituo cha Pamoja cha Ukaguzi – OSIS cha Nyakanazi pamoja na kuanza ukarabati wa sehemu ya Lusahunga – Rusumo na Nyakasanza - Kobero (km 150).

**Barabara ya Manyoni – Itigi – Tabora (km 259.7)**

**338. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 23,364.47** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, ambapo **Shilingi milioni 650.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 22,714.47** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Nyahua – Chaya (km 85.4) kwa kiwango cha lami.

**Barabara za Mikoa (km 630.62)**

**339. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 48,880.96** zimetengwa kwa ajili ya barabara za mikoa na madaraja katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kati ya hizo, **Shilingi milioni 48,500** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 380.96** ni fedha za nje. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni ukarabati wa jumla ya **kilometa 589.31** kwa kiwango cha changarawe, kujenga kilometa **41.31** kwa kiwango cha lami na ujenzi na ukarabati wa madaraja/Makalavati **24**. Kazi nyingine ni kuwezesha mafunzo kwa vitendo kwa Wahandisi Wahitimu (Structured

Engineers Apprenticeship Programme - SEAP). Orodha ya miradi ya barabara za Mikoa itakayotekelezwa kwa kutumia fedha za Bajeti ya Maendeleo kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali imeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

**Barabara ya Mwanza/Shinyanga Border – Mwanza (km 102)**

**340. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 310.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili kuifanyia ukarabati barabara hii.

**Mradi wa Kuondoa Msongamano Barabara za Dar es Salaam (km 152.16)**

**341. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,070.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Banana – Kitunda – Kivule – Msongola (km 14.7) na Wazo Hill – Madale (km 6.0); kuanza ujenzi wa barabara za Kibamba – Kisopwa – Kwembe – Makondeko (km 14.66) sehemu ya Mloganzila – Mloganzila Citizen (km 4.0), Ardhi – Makongo (km 5.0), Kongowe – Mjimwema – Kivukoni Ferry Road (One Lane Widening), Mji Mwema – Kimbiji – Pembamnazi (km 27.0) na Goba – Matosa – Temboni (km 6.0) pamoja na kuanza upanuzi wa barabara ya Mwai Kibaki (km 9.1) na Kongowe – Mji Mwema – Kivukoni (km 25.1).

**Barabara ya Nyamuswa – Bunda – Kisorya (km 106)**

**342. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 4,790.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Nansio – Kisorya – Bunda – Nyamuswa (sehemu ya Kisorya – Bulamba (km 51) na Nyamuswa – Bunda - Bulamba (km 55) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kolandoto - Lalago - Ng'oboko - Mwanhuzi (km 84)**

**343. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 2,500.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara za Kolandoto – Mwanhuzi (km 10) na Lalago – Ng'oboko – Mwanhuzi (km 74).

### **Barabara ya Ndundu – Somanga (km 60)**

**344. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 10.00** zimetengwa kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi wa ujenzi wa barabara hii.

### **Barabara ya Kasulu – Manyovu (km 68)**

**345. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 11,000.09** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68). Kati ya hizo **Shilingi milioni 2,570.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,430.09** ni fedha za nje.

### **Barabara ya Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road Lot1 & 2 (km 112.3)**

**346. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 41,097.73** zimetengwa katika mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 22,830.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 18,267.73** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya mzunguko ya Dodoma (Dodoma City Outer Dual Carriageway Ring Road) sehemu ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Dry Port (km 52.3), sehemu ya Ihumwa Dry Port – Matumbulu – Nala (km 60.0) na kulipa fidia kwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa barabara ya Makulu Jct. - Ntyuka R/About - Image R/About - Bahi R/About. Kazi nydingine ni kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Ntyuka Jct. - Mvumi Hospital - Kikombo Junction (km 76.07) na barabara ya Kikombo Jct. - Chololo - Mapinduzi (JWTZ HQ) (km 18). Aidha, mradi huu utahusisha maandalizi ya upanuzi wa barabara kuu zinazoingia katikati ya mji wa Dodoma (km 200) zinazohusisha barabara ya Dodoma - Morogoro (km 50), Dodoma - Iringa (km 50), Dodoma - Singida (km 50) na Dodoma - Arusha (km 50).

### **Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/ Songea (km 464)**

**347. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 105.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Kidatu – Ifakara

(km 68) na kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Ifakara – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha (km 396.0).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Koga – Mpanda (km 383.00)**

**348.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 33,518.44** zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 2,080.00** ni fedha za ndani na fedha za nje **Shilingi milioni 31,438.44** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu za Usesula – Komanga (km 115.5), Komanga – Kasinde (km 112.8) na Kasinde – Mpanda (km 111.7).

**Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235)**

**349.** *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 12,160.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu za Makutano – Sanzate (km 50.0) na Waso – Sale Jct. (km 50.0). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi kwa sehemu za Sanzate – Natta (km 40.0), Natta – Mugumu (km 45.0) na Tarime – Mugumu (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Ibanda – Itungi Port (km 26)**

**350.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 13,395.20**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 7,843.26** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Shilingi milioni 5,551.94** kwa ajili ya ukarabati wa sehemu ya Ibanda – Itungi Port (km 26) kwa kiwango cha lami na kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Pamoja cha Ukaguzi mpakani Songwe/Kasumulu (Songwe/Kasumulu - Tanzania/Malawi Border - OSBP). Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa sehemu ya Iponjola - Kiwira Port (km 6).

**Barabara ya Nzega – Tabora (km 289.7)**

**351.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,020.00** kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami wa barabara ya Shelui – Nzega (km 110.0) na kuanza ujenzi wa barabara za Nzega – Kagongwa (km 65.0).

**Barabara ya Sumbawanga – Mpanda – Nyakanazi (km 432.56)**

**352. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 14,320.00** katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mpanda – Ifukutwa – Vikunge (km 30) na kuanza ujenzi sehemu za Kibaoni – Sitalike (km 71.0) na Kizi – Lyambalyamfipa – Sitalike (km 86.3) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Nyanguge – Musoma/ Usagara – Kisesa Bypass (km 202.25)**

**353. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi milioni 903.00** zimetengewa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara ya Musoma – Makojo – Busekela (km 92). Kazi nyingine ni kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu ya Nyanguge – Simiyu/Mara Border (km 100.4) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Magole – Mziha – Handeni (km 149.2)**

**354. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 6,280.00** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kilometra 50 za barabara ya Turiani – Mziha – Handeni (km 104).

**Ujenzi wa Barabara za Juu (Flyovers) Jijini Dsm na Barabara Uunganishi**

**355. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 5,731.94**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 180.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 5,551.94** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya Ubungo (Ubungo Interchange) pamoja na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuboresha makutano ya barabara katika maeneo ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, *Fire* pamoja na makutano ya barabara za Kinondoni/Ali Hassan Mwinyi na Selander (Ali Hassan Mwinyi/UN Road Jct). Aidha, kazi nyingine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa *Mabey Flyovers* katika jiji la Dar es Salaam, Dodoma na Mwanza.

**Barabara ya Mwigumbi – Maswa – Bariadi – Lamadi (km 181.8)**

**356.** *Mheshimiwa Spika*, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,519.99** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu ya Maswa – Bariadi (km 49.7). Aidha, Wizara imepanga kuanza maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Isabdula (Magu) – Kwimba Station – Ngudu – Ng’hungumalwa (km 10).

**Barabara ya Tabora – Ipole – Rungwa (Sehemu ya Ipole – Rungwa (km 172)**

**357.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,150.00** kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi (km 341.25)**

**358.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 44,966.31**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 21,250.00** ni fedha za ndani na fedha za nje ni **Shilingi milioni 23,716.31** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu (km 63) na kuendelea na ujenzi wa barabara za Nyakanazi – Kakonko (Kabingo) (km 50), Kanyani Junction – Mvugwe (km 70.5), Mvugwe – Nduta Junction (59.35), Nduta Junction – Kabingo (km 62.5) na Nduta Junction – Kibondo (km 25.9). Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa barabara ya Kibondo – Mabamba (km 35) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Kwenda Kiwanja cha Ndege cha Mafia (Mafia Airport Access Road (km 16)**

**359.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** kwa ajili ya kulipa sehemu ya madai ya Mkandarasi na Mhandisi Mshauri aliyesimamia ujenzi wa barabara hii.

### Dodoma University Road (km 16.5)

**360. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 20.00** katika mwaka wa fedha 2020/21, kwa ajili ya kulipa madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri wa barabara za kutoka Ihumwa kuelekea Chuo Kikuu cha Dodoma (km 12.0) na Barabara za Ikulu ya Chamwino (km 4.5).

### Daraja la Nyerere (Kigamboni) na Barabara Unganishi

**361. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,800.00** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara unganishi za Kigamboni (Daraja la Nyerere) – Vijibweni (km 1.5). Kazi nyingine ni kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Tungi – Kibada (km 3.8), Kibada – Mjimwema (km 1.6) na kuanza ujenzi wa barabara ya Kibada – Mwasonga – Tundwisongani Jct/Tundwisongani – Kimbiji (km 41.0) kwa kiwango cha lami.

### Barabara ya Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 215.88)

**362. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,090.00** kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Mutukula – Bukoba – Muhutwe – Kagoma (km 136.0), Bukoba Mjini – Busimbe – Maluku – Kanyangereko – Ngongo na Kanazi (Kyetema) – Ibwera – Katoro – Kyaka II (km 60.7).

### Fedha za Matengenezo na Ukarabati wa Barabara

**363. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 641,746.37** katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya matengenezo na ukarabati wa barabara, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya barabara na vivuko. Fedha hizi zinasimamiwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**Ujenzi wa Njia za Magari Mazito na Maegesho ya Dharura Katika Barabara Kuu ya Ukanda wa Kati (Providing Lane Enhancement Including Climbing Lanes, Passing Bays, Rest and Emergency Lay Bays on Central Corridor)**

**364. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 150.00** kwa ajili ya kuwzesha (facilitate) kazi za usanifu wa kina wa maeneo ya kujenga njia za magari mazito kwenye miinuko na kujenga maegesho ya dharura katika barabara kuu ya Ukanda wa Kati.

**Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji**

**365. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 9,000.00** kwa ajili ya kuendelea na upanuzi wa barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7); sehemu ya Kimara – Kibaha Mizani (km 19.2) na madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji kwa utaratibu wa kusanifu na kujenga (*Design and Build*).

**Barabara ya Kisarawe – Mlandizi (km 119.0)**

**366. Mheshimiwa Spika**, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 630.00** katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 34.0)**

**367. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya maandalizi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu za Pugu – Kifuru – Mbezi Mwisho (km 12.7) na Mbezi Mwisho – Mpiji Magoe – Bunju (km 21.3).

**Barabara ya Kagoma – Lusahunga (km 172.50)**

**368. Mheshimiwa Spika**, kiasi cha **Shilingi milioni 1,180.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu za Muleba – Kanyambogo – Rubya (km 18.5) kwa kiwango cha lami.

### **Barabara ya Singida – Shelui (km 110)**

**369. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, kiasi cha **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuanza ukarabati wa barabara hii.

### **Barabara ya Dar es Salaam – Mbagala (Kilwa Road) – Gerezani (Sehemu ya Kamata – Bendera Tatu: km 1.3)**

**370. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, zimetengwa jumla ya **Shilingi milioni 8,837.91** kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 510.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 8,327.91** ni fedha za nje. Kiasi kilichotengwa ni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja la Gerezani na maandalizi ya upanuzi wa barabara ya Mbagala Rangi Tatu – Kongowe (km 3.8).

### **Barabara ya Msimba – Ruaha Mbuyuni/Ikokoto Mafinga (km 535.25)**

**371. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 8,960.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara ya Mbarali – Ubaruku (km 8.9) kwa kiwango cha lami na kuanza ujenzi wa barabara za Rujewa – Madibira – Mafinga (km 152.0). Aidha, mradi huu utahusisha kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mafinga – Mgololo (km 78.0) na kufanya ukarabati wa barabara ya Morogoro – Iringa sehemu ya Tumbaku Jct. - Mangae/Meleta - Mikumi – lyovi (km 156.45).

### **Barabara ya Same – Mkumbara – Korogwe (km 147.5)**

**372. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 6,060.00** zimetengwa kwa ajili ya kuanza maandalizi ya ukarabati wa sehemu za Same – Himo (km 76.0) na Mombo – Lushoto (km 32.0) kwa kiwango cha lami. Aidha, kazi nyngine ni kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara za Lushoto – Magamba – Mlola (km 34.5) na Same - Kisiwani - Mkomazi (km 97) sehemu ya Same – Kisiwani (km 5.0) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Mbeya – Makongolosi (km 267.90)**

**373.** *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi milioni 11,060.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa sehemu ya Chunya – Makongolosi (km 39) na maandalizi ya ujenzi wa sehemu za Mkiwa - Itigi - Noranga (km 56.9), Mbalizi – Makongolosi (km 50) na Makongolosi – Rungwa – Noranga (sehemu ya Makongolosi – Rungwa (km 50) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (km 211)**

**374.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 12,000.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha zege kwa sehemu ya Lusitu – Mawengi (km 50) na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa sehemu ya Itoni – Lusitu (km 50).

**Ujenzi wa Daraja Jipya la Selander**

**375.** *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 48,161.93** fedha za nje zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Daraja Jipya la Selander (km 1.030) na barabara unganishi zenye jumla ya urefu wa kilometra 5.2.

**Barabara ya Handeni – Kibirashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro – Singida (km 460)**

**376.** *Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi milioni 6,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/21 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kuanzia na sehemu ya Handeni – Kibirashi (km 50.0) kwa kiwango cha lami.

**Barabara ya Makambako – Songea Na Barabara Ya Mchepuo Ya Songea (Songea Bypass) (km 295)**

**377.** *Mheshimiwa Spika*, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na usanifu wa kina wa barabara ya Mchepuo ya Songea na maandalizi ya ukarabati wa barabara ya Makambako – Songea.

### **Barabara ya Dodoma – Iringa (km 267.1)**

**378. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 3,020.00** zimetengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara ya mchepuo ya Iringa (km 7.3) na kuimarisha matabaka ya barabara ya Iringa – Dodoma.

### **Barabara ya Dodoma – Babati (km 263.4)**

**379. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 60.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya mchepuo wa Babati (Babati Bypass km 12).

### **Barabara ya Masasi – Songea – Mbamba Bay (km 343.20)**

**380. Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 22,921.82**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **15,030.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 7,891.82** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara za Mbinga – Mbamba Bay (km 66), kilometra tano (5) za barabara ya Kitai – Lituhi (km 90.0) pamoja na daraja la Mnywamaji.

### **Ujenzi wa Barabara za Chuo cha Uongozi (Uongozi Institute)**

**381. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 20.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na maandalizi ya ujenzi wa barabara ndani ya eneo la Chuo cha Uongozi Bagamoyo kwa kiwango cha lami.

### **Barabara ya Igawa – Songwe – Tunduma na Mbeya Bypass (km 273.40)**

**382. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi milioni 60.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya kuendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara za Igawa – Songwe – Tunduma (km 218), barabara ya mchepuo ya Mbeya (Uyole – Songwe km 48.9) na barabara ya Iwambi – Mbalizi (km 6.5) kwa ajili ya ujenzi na ukarabati kwa kiwango cha lami.

## **Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT Phase I – V: km 69.8)**

*383. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 51,749.43** zimetengwa kwa ajili ya mradi huu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 7,870.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 43,879.43** ni fedha za nje kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Pili. Aidha, kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tatu na Nne na kufanya maandalizi ya maboresho ya miundombinu ya mabasi yaendayo haraka iliyojengwa katika Awamu ya Kwanza katika eneo la Jangwani. Mradi huu utahusisha pia kufanya mapitio ya usanifu wa mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya Tano.

## **Ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (Institute Of Construction Technology - ICOT)**

*384. Mheshimiwa Spika*, jumla ya **Shilingi milioni 1,000.00** zimetengwa katika mwaka wa fedha wa 2020/21 kwa ajili ya usanifu na ujenzi (Design and Build) wa jengo la Makao Makuu ya Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi (ICoT).

## **Ujenzi wa Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania**

*385. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, jumla ya **Shilingi milioni 15,020.00** zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) pamoja na Ofisi za Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe, Lindi na Songwe.

## **MIRADI YA USALAMA BARABARANI NA MAZINGIRA**

*386. Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara itaendelea kutekeleza majukumu yanayohusu kuratibu na kuimarisha shughuli za usalama barabarani, mazingira na kudhibiti uzito wa magari yanayotumia barabara zetu. Mradi wa **Usalama Barabarani** umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 1,832.00** kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi, uwekaji wa miundombinu ya kisasa ya upimaji magari (Load Cell), kufanya maboresho katika

mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ajali barabarani, ukaguzi wa alama na usalama wa barabara pamoja na mapitio ya Sera ya Usalama Barabarani. Kazi nyingine ni kutoa elimu ya usalama barabarani kwa umma, pamoja na uendeshaji wa Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji Taarifa za Ajali Barabarani.

**387. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi wa **Menejimenti ya Utunzaji wa Mazingira** umetengewa **Shilingi milioni 148.00** kwa ajili ya kutoa mafunzo kuhusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na hifadhi ya mazingira katika Sekta ya Ujenzi. Kazi nyingine ni kuandaa mfumo wa kusimamia mazingira (Environmental Management System) na kutoa elimu ya weledi wa usimamizi wa mazingira hususan utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 kwa menejimenti ya Wizara. Aidha, fedha hizi zitatumika kuandaa programu za udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika sekta (Sectoral Pollution Control Programme).

#### **MIRADI YA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA VIWANJA VYA NDEGE**

**388. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21 miradi ya ujenzi wa miundombinu ya viwanja vya ndege imetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 91,885.299**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 60,737.98** ni za ndani na **Shilingi milioni 31,147.32** ni fedha za nje. Miradi ifuatayo itatekeleza:

#### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma**

**389. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 7,757.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 5,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria, maegesho ya ndege, maegesho ya magari na barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa uzio, jengo la kuongozea ndege na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

#### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mpanda**

**390. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 10.00** fedha za ndani kwa ajili ya ukarabati wa uzio wa usalama, ujenzi

wa barabara ya kuzunguka uzio na upanuzi wa jengo la abiria.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora**

**391. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,891.18**. Kat i ya fedha hizo, **Shilingi milioni 134.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Abiria, jengo la kuongozea ndege, barabara ya kuingia na kutoka kiwanjani, maegesho ya magari, uzio wa usalama pamoja na jengo la uchunguzi wa hali ya hewa.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe**

**392. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 8,900.00** kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa Jengo la Abiria, usimikaji wa taa za kuongozea ndege na ukarabati wa tabaka la juu la barabara ya kutua na kuruka ndege na barabara ya kiungio (taxiway), ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na ukarabati wa eneo la usalama kwenye barabara ya kutua na kuruka ndege (Runway End Safety Area-RESA).

### **Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza**

**393. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 3,023.40** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Jengo jipya la Abiria, ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na malipo ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi wakati wa kipindi cha uangalizi wa mradi (Defect Notification Period).

### **Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha**

**394. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 200.00** kwa ajili ya kurefusha barabara ya kuruka na kutua ndege; ujenzi wa maeneo ya kugeuzia ndege (Turning Pad), uzio wa usalama, barabara mpya ya kuingilia kiwanjani pamoja na kukarabati maegesho ya magari.

### **Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara**

**395. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/21, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 5,355.00** kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege, viungio vyake pamoja na maegesho ya ndege. Kazi zingine ni kusimika taa na mitambo ya kuongozea ndege, ujenzi wa barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na uzio wa usalama.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga**

**396. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,867.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 110.00** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, uzio wa usalama, barabara ya kuingia kiwanjani na maegesho ya magari. Kazi nyingine ni usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga**

**397. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 2,867.18**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 110** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 2,757.18** ni fedha za nje. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya kutua na kuruka ndege na viungio vyake, maegesho ya ndege, jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, jengo la uchunguzi wa hali ya hewa, barabara ya kuingia kiwanjani, maegesho ya magari na usimikaji wa taa na mitambo ya kuongozea ndege pamoja na ujenzi wa uzio wa usalama.

### **Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya Mikoa**

**398. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 18,237.98**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 17,787.98** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 450.00** ni fedha za nje kwa ajili ya ujenzi wa

viwanja vya ndege vya Geita, Songea, Iringa, Musoma, Tanga, Lake Manyara, Moshi, Lindi na kiwanja kipywa cha Simiyu. Aidha, kazi nyingine ni ujenzi wa uzio wa usalama pamoja na barabara ya kufanya ukaguzi kwenye kiwanja cha ndege cha Dodoma.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Msalato**

**399. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 39,714.20**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 20,045.60** ni fedha za ndani na **Shilingi milioni 19,668.60** ni fedha za një kwa ajili ya kuanza ujenzi wa kiwanja kipywa cha Msalato mkoani Dodoma. Aidha, kazi nyingine ni kulipa fidia kwa wakazi watakaoathiriwa na utekelezaji wa mradi huu.

### **Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba**

**400. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa kiasi cha **Shilingi milioni 10.00** fedha za ndani kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi wa jengo la watu mashuhuri (VIP Lounge), ukarabati wa meta 200 barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na usimikaji wa taa za kuongozea ndege.

### **Ujenzi wa Jengo la Tatu la Abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA)**

**401. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 52.00** kwa ajili ya kulipa madai ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa Jengo la Tatu la Abiria (Terminal III) pamoja na miundombinu yake. Aidha, kazi nyingine ni maandalizi ya Usanifu wa Kina kwa ajili ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal II).

### **FEDHA ZA MFUKO WA BARABARA**

**402. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 jumla ya **Shilingi 641,746,370,000.00** zimetengewa kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo na ukarabati wa barabara kuu

na za mikoa. Kati ya fedha hizo, TANROADS imetengewa **Shilingi 572,604,616,096.20** kwa ajili ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) imetengewa **Shilingi 63,622,735,121.80** kwa ajili ya kazi za ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara, ukarabati na ununuzi wa vivuko, usalama barabarani pamoja na usimamizi na ufuutiliaji wa miradi hiyo. Aidha, **Shilingi 5,519,081,782.00** zitatumika kugharamia uendeshaji wa Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**403. Mheshimiwa Spika**, kiasi cha **Shilingi 63,622,735,121.80** ni fedha za maendeleo kutoka Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara (Ujenzi). Kati ya hizo, **Shilingi 14,672,483,000.00** ni kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara zenyne urefu wa kilometa **7,032.9**. Kiasi cha **Shilingi 4,740,226,000.00** ni kwa ajili ya manunuzi na ukarabati wa vivuko pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko; **Shilingi 6,291,577,575.80** ni kwa ajili ya miradi ya Usalama Barabarani na Mazingira na **Shilingi 6,908,984,546.00** ni kwa ajili ya kazi za usimamizi na ufuutiliaji wa miradi inayotekelawa na Wizara (Ujenzi) pamoja na kujenga uwezo wa watumishi. Aidha, miradi ya barabara za mikoa imetengewa **Shilingi 31,009,464,000.00** kwa ajili ya kufanya ukarabati wa jumla ya kilometra **416.02** kwa kiwango cha changarawe na kujenga kilometra **23.41** kwa kiwango cha lami pamoja na ujenzi na ukarabati wa madaraja/ makalavati **27** katika mikoa mbalimbali nchini.

Mchanganuo wa miradi itakayotekelawa kwa fedha za Mfuko wa Barabara zilizotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Sekta ya Ujenzi) umeonyeshwa katika **Viambatisho Na. 3** na **4**.

**404. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 572,604,616,096.20** ni fedha za Mfuko wa Barabara ambazo zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS). Fedha hizo zitatumika kufanya matengenezo ya barabara kuu, barabara za mikoa, madaraja na uendeshaji wa mizani.

Mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo umeoneshwa katika **Viambatisho Na. 5, 5A - 5D.**

## **MPANGO WA KAZI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21**

### **Wakala wa Barabara Tanzania**

**405. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Barabara Tanzania umepanga kujenga barabara zenye urefu wa **kilometra 455.75** kwa kiwango cha lami, ujenzi wa madaraja **11** pamoja na ukarabati wa **kilometra 25** kwa kiwango cha lami katika barabara kuu. Aidha, Wakala umepanga kufanya matengenezo ya barabara kuu na barabara za mikoa ambayo yatahusisha matengenezo ya kawaida (routine and recurrent maintenance) kwa **kilometra 34,268.29**, matengenezo ya muda maalum **kilometra 4,886.67** na sehemu korofii **kilometra 743.49** pamoja na matengenezo ya madaraja **3,390**. Mpango huu pia unajumuisha shughuli za udhibiti wa uzito wa magari na hifadhi za barabara, kazi za dharura pamoja na mradi wa matengenezo ya barabara kwa mikataba ya muda mrefu.

Kwa upande wa barabara za mikoa, Wakala utajenga kwa kiwango cha lami barabara zenye urefu wa **kilometra 64.72** ambapo **kilometra 41.31** zitajengwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometra 23.41** zitajengwa kwa fedha za Mfuko wa Barabara. Aidha, **kilometra 1,005.33** zitakarabatiwa kwa kiwango cha changarawe. Kati ya hizo, **kilometra 589.31** na madaraja/makalavati **24** yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko Mkuu wa Serikali na **kilometra 416.2** pamoja na madaraja **27** yatajengwa/yatakarabatiwa kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

**406. Mheshimiwa Spika**, Wakala vilevile utaendelea na jukumu la kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege. Kazi zitakazotekelzwa ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa kiwanja kipywa cha Ndege cha Geita pamoja na ukarabati na upanuzi wa viwanja vya Ndege vya Songea,

Mtwara na Songwe. Kazi nyingine ni kuanza ujenzi wa Kiwanja kipywa cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, ukarabati na upanuzi wa Viwanja vya Ndege vya Kigoma, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Iringa, Musoma, Tanga na Lake Manyara ambavyo viro katika hatua mbalimbali za manunuzi. Aidha, Wakala utaendelea na maandalizi ya ukarabati wa Jengo la Pili la Abiria (Terminal Building II) katika kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) pamoja na ukarabati wa viwanja vya Ndege vya Lindi, Arusha, Bukoba, Moshi, Nachingwea, Dodoma na viwanja vingine mikoani.

### **Wakala wa Majengo Tanzania**

**407. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 Wakala wa Majengo Tanzania umepanga kuendelea kusimamia miradi ya nyumba za viongozi ambazo utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali ikiwemo ujenzi wa nyumba za Waheshimiwa Majaji katika mikoa mbalimbali na Ujenzi wa nyumba ya makazi ikulu Dodoma. Aidha, Wakala utaendelea kufanya matengenezo ya nyumba na ununuzi wa samani kwa nyumba za Viongozi. Aidha, Wakala utaendelea na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa samani katika nyumba za viongozi. Vilevile, Wakala utatekeza miradi ya Ukarabati wa nyumba DSM na Mikoani; Umalizaji wa Jengo la kibiashara simioni Arusha; Ujenzi wa nyumba 172 za watumishi wa umma Jijini Dodoma na mikoa mingine; Ukamilishaji wa Ukumbi wa matumizi Mbalimal-Area II Dar es Salaam; Ujenzi wa jengo la kibiashara Kyela Mbeya - EX TACOSHILI; Upatikanaji wa hati miliki za viwanja vya TBA; Ujenzi wa Ofisi ya Mkoa -Geita; na Ununuzi wa Samani katika jengo la Chimala.

### **Wakala wa Ufundu na Umeme**

**408. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wakala wa Ufundu na Umeme umepanga kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa Vivuko vya Serikali vipatavyo **32** na boti **11** ambavyo vinatarajiwaa kuvusha abiria **40,174,764**, magari **1,684,524** na tani za mizigo **428,172**.

**409. Mheshimiwa Spika**, katika miradi ya **maegesho ya vivuko**, Wakala umepanga kuendelea na upanuzi wa jengo la abiria na maegesho upande wa Kigamboni kwa ajili ya kivuko cha Magogoni – Kigamboni; ujenzi wa maegesho ya Bukondo na Zumacheli kwa ajili ya kivuko cha Chato – Nkome; ujenzi wa maegesho ya Nyamisati – Mafia kwa ajili ya kivuko cha Nyamisati – Mafia; ujenzi na ukarabati wa maegesho katika vituo 8 vya Bugolora – Ukara, Rugezi – Kisorya, Kilambo – Namoto, Utete – Mkongo, Iramba – Majita, Nyakarilo – Kome, Kasharu – Buganguzi na Kigongo – Busisi. Kazi nyiningine ni ujenzi wa miundombinu (majengo ya abiria, ofisi na uzio) kwa vituo kumi (Bugolora, Ukara, Kome, Nyakaliro, Maisome, Kaunda, Nkome, Kisorya, Musoma na Kinesi) pamoja na ujenzi wa maegesho ya vivuko vya Ngara – Nyakiziba na Muleba – Ikuza. Aidha, Wakala utaendelea na ujenzi wa miundombinu (jengo la kukatia tiketi, jengo la abiria na ofisi) kwa ajili ya kivuko kipyta cha Kayenze - Bezi mkoani Mwanza na kivuko cha Itungi Port (Mwaya - Kajunjumele) mkoani Mbeya.

**410. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **ununuzi wa vivuko**, miradi itakayotekelawa na Wakala ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa vivuko vipyta vitakavyotoa huduma ya usafiri kati ya Nyamisati – Mafia, Bugolora – Ukara na Chato – Nkome; ujenzi wa boti ‘*fibber boat*’ itakayotoa huduma ya usafiri kati ya Utete - Mkongo; ununuzi wa vitendea kazi kwa ajili ya karakana pamoja na vivuko. Kazi nyiningine ni ununuzi wa kivuko kipyta kitakachotoa huduma ya usafiri kati ya Kisorya – Rugezi, kufanya usanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi na Uendeshaji wa Vivuko vya Serikali.

**411. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **ukarabati**, Wakala umepanga kukamilisha ukarabati wa vivuko MV Tegemeo, MV Musoma, MV Mara, MV Sengerema, MV Ujenzi, MV Kigamboni, MV Misungwi na boti ya uokozi MV KIU. Aidha, Wakala unatarajia kuanza ukarabati wa vivuko MV Nyerere, MV Kilombero I, MV Kilombero II, MV Ruhuhu na MV Tanga pamoja na ukarabati wa mitambo ya karakana ya TEMESA Morogoro na mitambo ya Chuo cha Ujenzi Morogoro.

**412. Mheshimiwa Spika**, Wakala pia umepanga kujenga karakana 5 kwa ajili ya matengenezo ya magari na mitambo ya Serikali katika mikoa ya Songwe, Simiyu, Geita, Njombe na Katavi; kujenga karakana ya kisasa Jijini Dodoma na ununuzi wa karakana sita zinazohamishika (mobile workshops) pamoja na vitendea kazi vyake. Kazi nyingine ni kukarabati karakana 11 ambazo ni karakana ya MT Depot Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Tabora, Mwanza, Arusha, Kigoma, Mara, Ruvuma, Pwani na Vingunguti (Dar es Salaam); kuanzisha karakana 6 za ngazi ya wilaya (Simanjiro, Same, Chato, Masasi, Kyela na Ukerewe) pamoja na kusanifu na kusimika Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Magari.

**413. Mheshimiwa Spika**, Wakala vilevile umepanga kufanya matengenezo ya magari **45,681**, matengenezo na usimikaji wa mifumo **394** ya umeme, mifumo **1,395** ya majokofu na viyoyozi pamoja na mifumo **166** ya elektroniki. Vilevile, Wakala umepanga kutoa ushauri wa kihandisi kwa miradi ya usimikaji wa mifumo ya umeme, mitambo, elektroniki, viyoyozi na majokofu inayofikia **118** na kusimamia mifumo hiyo ipatayo **62**. Aidha, Wakala utaendelea kutoa huduma ya ukodishaji wa Mitambo ya Ujenzi wa Barabara.

#### **Bodi ya Mfuko wa Barabara**

**414. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Barabara unatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi 916,780,529,000** kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwemo tozo ya mafuta, tozo kwa magari ya kigeni yanayosafirisha mizigo nje ya nchi pamoja na faini za uzipishaji mizigo barabarani na mizigo yenye vipimo visivyo vya kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 641,746,370,000** zitagawanywa kwa ajili ya matengenezo ya barabara kuu na za mikoa, ukarabati wa barabara za mikoa, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, udhibiti wa uzito wa magari, usalama barabarani na mazingira, matengenezo na ukarabati wa vivuko pamoja na kujenga uwezo wa Wizara na Taasisi zinazosimamia masuala ya Barabara na Vivuko chini ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Fungu 98 -Ujenzi). Aidha, **Shilingi 275,034,159,000** zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Wilaya zilizo chini ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI (Fungu 56).

**415. Mheshimiwa Spika**, mchanganuo wa bajeti ya Mfuko wa Barabara kwa mwaka wa fedha 2020/21 ni kama ifuatavyo: Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (Ujenzi) **Shilingi 63,622,735,121.80**, Wakala wa Barabara Tanzania **Shilingi 572,604,616,096.20**, Ofisi ya Rais, TAMISEMI **Shilingi 27,266,886,523.26** TARURA **Shilingi 245,401,978,709.34** na Bodi ya Mfuko wa Barabara **Shilingi 7,884,312,549.40**.

**416. Mheshimiwa Spika**, ili kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini, Bodi kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia inatarajia kukamilisha tathmini ya mtandao wa barabara (*Road inventory and condition survey*) ili kubaini thamani, urefu na hali ya barabara nchini. Takwimu hizi zitasaidia kuandaa mkakati endelevu wa matengenezo ya barabara nchini. Vilevile, Bodi itagharimia utafiti wa teknolojia mbadala na rahisi katika matengenezo ya barabara ili kupata teknolojia nafuu ya matengenezo ya barabara itakayopunguza gharama na kuongeza ufanisi katika matumizi ya fedha za Mfuko. Aidha, Bodi itaendelea na ufuatiliaji wa ubora wa kazi za matengenezo ya barabara katika mikoa yote nchini pamoja na kuendelea kuishauri Serikali juu ya namna ya kuongeza mapato ya Mfuko kulingana na wakati muafaka.

### Bodi ya Usajili wa Wahandisi

**417. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21 Bodi imepanga kusajili wahandisi **2,300**, mafundi sanifu **210** na kampuni za ushauri wa kihandisi **20**. Bodi pia imepanga kusimamia utekelezaji wa mpango wa mafunzo kwa vitendo kwa wahandisi wahitimu **3,500**. Kati ya hao **2,796** ni wanaoendelea na mafunzo na **704** ni wapya wanaofadhiliwa na Serikali, Wafadhilli na sekta binafsi. Aidha, Bodi itaendelea kufanya kaguzi za shughuli za kihandisi nchini ili shughuli zote za kihandisi zifanywe na wahandisi waliosajiliwa na kwa kufuata maadili ya utendaji kazi za kihandisi. Vilevile, Bodi itaendelea kutembelea na kukagua miradi ya ujenzi wa barabara Tanzania Bara, ikiwa ni pamoja na barabara za Halmashauri.

Bodi vilevile itaendelea kusimamia mafunzo ya kuijendeleza kitaaluma kwa wahandisi watalaan na washauri, kwa ajili ya kuwaendeleza wahandisi kwa ujumla pamoja na kuwashawishi wahandisi watalaan waanzishe kampuni za ushauri wa kihandisi mikoani na hivyo kusogezza huduma hii muhimu karibu na watumiaji.

### **Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi**

**418. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi imepanga kusajili Wataalam **120**, katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo. Aidha, Bodi imepanga kusajili kampuni **18** za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi. Vilevile, Bodi imepanga kuendelea na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu **120** katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi.

Bodi pia imepanga kufanya ukaguzi wa miradi ya ujenzi **2,000** katika mikoa yote, Tanzania Bara na kusajili miradi ya majengo **1000**. Aidha, Bodi imepanga kuendesha mitihani ya kitaalam kwa wahitimu **120** katika fani za Ubunifu Majengo na Ukadiriaji Majenzi na fani zinazoshabihiana nazo.

Bodi vilevile itaendesha mashindano ya insha kwa wanafunzi wa sekondari, ikiwa ni njia ya kuwahamasisha kusoma masomo ya sayansi na hatimaye kusomea taaluma za ubunifu majengo, ukadiriaji majenzi na taaluma zinazoshabihiana nazo.

### **Bodi ya Usajili wa Makandarasi**

**419. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Bodi imepanga kusajili jumla ya makandarasi wapya **950** na kukagua jumla ya miradi ya ujenzi **3,100**. Aidha, Bodi inatarajia kuendesha kozi **5** za mafunzo katika mikoa ya Mwanza, Dodoma, Arusha, Dar es Salaam na Njombe. Bodi vilevile imepanga kuendesha warsha **2** za mafunzo ya ushirikiano wa ubia (Joint Venture) katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza. Bodi pia itaendeleza Mfuko maalum wa Kutoa Dhamana ya Kusaidia Makandarasi Wadogo na wa Kati

(CAF). Jitihada za kuhamasisha makandarasi wazalendo kuijunga ili kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia pia zitaendelea.

### **Baraza la Taifa la Ujenzi**

**420. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Baraza limepanga kukamilisha mapitio ya Sheria ilyoanzisha Baraza na kuandaa Kanuni za Utekelezaji wake; kuratibu na kutoa mafunzo katika Sekta ya Ujenzi, kutoa ushauri wa kiufundi na kitaalam kwa wadau wa Sekta ya Ujenzi na kuratibu utatuzi wa migogoro inayojitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi ya ujenzi.

Baraza pia litaendelea kufanya tafiti zinazohusu: kuboresha kanuni ya ukokotoaji wa mabadiliko ya gharama katika miradi ya ujenzi wa majengo nchini; kutathmini changamoto na matatizo ya ushindani wa makandarasi na Washauri wa Kitaalam wazalendo katika kutekeleza miradi ya ujenzi ukilinganisha na Makandarasi na Washauri wa Kitaalam wa kigeni; kutathmini mafanikio na changamoto katika usimamizi wa miradi ya ujenzi wa miundombinu kwa njia ya "Design and Build"; kutathmini mwenendo wa ukuaji wa Sekta ya Ujenzi nchini na mwenendo wa mahitaji ya ujuzi na weledi unaohitajika ili kutekeleza miradi ya ujenzi ipasavyo.

**421. *Mheshimiwa Spika***, Baraza pia litaendelea na wajibu wake wa kutoa huduma za ukaguzi wa kiufundi wa miradi ya ujenzi kwa wadau wa sekta ya ujenzi; ukusanyaji na utoaji wa takwimu na taarifa za Sekta ya Ujenzi pamoja na kuendelea na mchakato wa kuanzisha Kituo Maalum cha Taarifa za Sekta ya Ujenzi. Kazi nydingine ni kuratibu mpango wa kukuza uwazi na uwajibikaji (Construction Sector Transparency Initiative - CoST) katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ya umma na kuhamasisha ushiriki wa sekta isiyo rasmi katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi kwa lengo la kukuza vipato vya wananchi katika maeneo husika.

## **Kituo cha Usambazaji wa Teknolojia Katika Sekta ya Ujenzi na Usafirishaji Tanzania (Tanzania Transportation Technology Transfer Centre)**

**422. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Kituo kimepanga kuendelea na jukumu lake la kusambaza teknolojia katika sekta ya ujenzi na usafirishaji hapa nchini. Pamoja na kusambaza majarida kutoka kwa wadau, Kituo Kitaandaa, kuchapisha na kusambaza majarida yake yanayohusu teknolojia mbalimbali katika sekta ya ujenzi na usafirishaji ambayo yataandaliwa mara nne kwa mwaka. Vilevile, kituo kitaendelea kutoa huduma ya maktaba ikiwa imeboreshwa zaidi.

Aidha, kituo kimepanga kuendesha makongamano kwa kushirikiana na Mamlaka mbalimbali za barabara hapa nchini, taasisi za ufundishaji, wataalamu binafsi wa ndani na nje ya nchi na taasisi zisizo za kiserikali kwa lengo la kujadili na kutafuta majawabu ya changamoto mbalimbali zinazoikabili sekta ya barabara na uchukuzi. Majawabu yatakayopatikana yatafikishwa kwa wahandisi wetu kuitia mafunzo ya muda mfupi ambayo kituo kimepanga kuyaandaa.

### **D.1.2 SEKTA YA UCHUKUZI**

#### **Makadirio ya Ukusanyaji wa Mapato, Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

**423. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62) imetengewa jumla ya **Shilingi 3,152,858,745,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 90,710,109,000** zimetengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,062,148,636,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mgawanyo wa fedha za maendeleo pamoja na miradi iliyotengewa fedha ni kama inavyooneshwa katika **Kiambatisho Na.6**. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Shilingi 63,639,165,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000** kwa ajili

ya Matumizi Mengineyo. Katika Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa, **Shilingi 2,937,678,923,000** ni fedha za Ndani na **Shilingi 124,469,713,000** ni fedha za Nje.

**424. Mheshimiwa Spika**, ili kuendelea kuboresha huduma za usafiri na usalama wa watu na vyombo vyaya usafiri katika Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, Kampuni ya Huduma za Usafiri wa Meli katika Maziwa (MSCL) imetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 135** fedha za ndani. Fedha hizo zimetengwa ili kugharamia mipango ifuatayo:

- i. Kuendelea na ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Victoria;
- ii. Kuanza ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Ziwa Victoria (Wagon ferry);
- iii. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MV.Umoja katika Ziwa Victoria;
- iv. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MT. Nyangumi katika Ziwa Victoria;
- v. Kuanza ukarabati mkubwa wa Meli ya MT. Ukerewe katika Ziwa Victoria;
- vi. Kuanza ujenzi wa Meli mpya ya abiria na mizigo katika Ziwa Tanganyika;
- vii. Kuanza Ukarabati mkubwa wa MV. Liemba iliyo katika Ziwa Tanganyika;
- viii. Kuanza Ukarabati mkubwa wa MT. Sangara iliyo katika Ziwa Tanganyika;
- ix. Kuanza Ujenzi wa meli ya mizigo katika Ziwa Tanganyika;
- x. Kuanza Ujenzi wa Meli mpya ya mizigo katika Bahari ya Hindi; na
- xi. Kuendelea na ufungaji wa Mifumo ya TEHAMA.

**425. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **shilingi bilioni 13** zimetengwa ili kuwezesha uendeshaji na uwekaji wa miundombinu katika Jengo la Tatu la Abiria (TB III) lillo katika Kiwanja cha Ndege cha kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA). Fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kugharamia umeme, maji, vifaa vyta zimamoto, viyoyozi, madaraja ya Ndege, daraja la abiria, vyoo, maegesho, huduma za mtandao, kuboresha mazingira ya nje ya jengo la abiria, kamera na kituo cha wasindikizaji.

Aidha, jumla ya **Shilingi bilioni 3.4** fedha zinazotokana na mapato ya ndani ya TAA zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Ujenzi wa uzio wa ulinzi na usalama katika viwanja vya Ndege vya Mwanza na Dodoma;
- ii. Kukamillisha utayarishaji wa Mpango Bora wa Matumizi ya Ardhi katika viwanja vya Ndege vya Dodoma, Iringa, Geita, Tanga na Lake Manyara;
- iii. Kufanya Usanifu wa Kina kwa ajili ya ujenzi wa *Runway End Safety Area* (RESA) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere;
- iv. Kukamilisha urefushaji wa barabara ya kutua na kuruka ndege kwa mita 200 pamoja na maeneo ya kugeuzia ndege (Turning bay) katika Kiwanja cha Ndege cha Arusha.

**426. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Reli (Railway Fund) umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 289.679** fedha za ndani ili kugharamia ukarabati wa miundombinu ya Reli iliyopo, kujenga Reli mpya ya *Standard Gauge*, ukarabati wa vitendea kazi na kugharamia stadi mbalimbali kwa ajili ya Miradi ya ujenzi wa Reli. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuunda upya vichwa vya Treni 9 kwa ajili ya sogeza na njia kuu;
- ii. Kurejesha na kuimarisha huduma za usafiri wa Treni kwa Reli ya Kaskazini (Tanga – Arusha);

- iii. Kugharamia kazi za Upembuzi na Usanifu wa awali wa ujenzi wa Reli;
- iv. Ukarabati wa Karakana, Stesheni na Majengo ya Reli; na
- v. Kuchangia katika gharama za ujenzi wa Reli ya *Standard Gauge* na matengenezo ya reli ya Kati.

**427. Mheshimiwa Spika**, kuhusu ugharamiaji wa ujenzi wa reli mpya ya standard gauge, ununuzi wa injini na mabehewa ya mizigo na abiria, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya miradi ya reli, na ukarabati wa reli iliyopo jumla ya **Shilingi bilioni 2.020** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 95.0** fedha za nje kuititia Mradi wa TIRP zimetengwa ili kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Kukamilisha ujenzi wa Reli ya kati ya *Standard Gauge* kwa kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (Km 300);
- ii. Kuanza majaribio na uendeshaji wa treni ya *Standard gauge* kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro;
- iii. Kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kati kwa kipande cha Morogoro hadi Makutupora (Km 422) kwa *Standard Gauge*;
- iv. Kuanza ujenzi wa Reli ya kati kwa *Standard Gauge* kutoka Makutupora hadi Mwanza (Km 673);
- v. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge* kwa sehemu za Makutupora - Tabora (Km 294), Tabora – Isaka (Km 133) na Isaka-Mwanza (Km 246);
- vi. Kuendelea na taratibu za upatikanaji wa Mkandarasi, Mshauri Mwelekezi na utwaaji wa maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Reli mpya ya *Standard Gauge* kwa sehemu za Tabora - Kigoma (km 411), Kaliua – Mpanda - Karema (km 320), Isaka – Rusumo (km 371) na Uvinza - Musongati (km 240);
- vii. Kukamilisha kazi ya kuandaa maandiko na kutafuta wawekezaji kwa ajili ya miradi ya Mtwara – Songea –

Mbamba Bay pamoja na matawi ya kwenda Mchuchuma na Liganga na Tanga – Arusha - Musoma kwa mfumo wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Bihafsi (PPP);

viii. Kukamilisha ukarabati wa njia ya reli ya Kati iliyopo (meter gauge) kwa kutandika reli nzito za ratili 80 kwa yadi katika umbali wa Kilomita 970 kati ya Dar es Salaam na Isaka;

ix. Kuendelea na ujenzi wa madaraja na makalvati katika njia ya reli ya Tanga - Arusha;

x. Ujenzi wa sehemu ya kuunganisha treni (Marshalling yard) katika eneo la Gerezani; na

xi. Ununuzi wa vifaa ikiwemo injini 3 na mabehewa 44 ya njia ya reli ya Kati iliyopo sasa;

xii. Kukamilisha kazi ya upembuzi na usanifu wa awali na kuanza ujenzi wa reli ya Jijini Dodoma (Dodoma Commuter train);

xiii. Ununuzi wa vichwa vya treni 5, mabehewa ya abiria 60, mabehewa ya mizigo 1,430 kwa ajili ya uendeshaji wa SGR;

xiv. Ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli iliyopo; na

xv. kusafirisha tani za mizigo 672,000 na abiria 667,328 kuanzia Dar es Salaam hadi Kigoma, Mwanza na Mpanda; abiria 320,141 kwa treni ya kisasa toka Dar es Salaam hadi Morogoro na abiria 5,000,000 kwa usafiri wa treni ya mjini Dar es Salaam.

**428. Mheshimiwa Spika,** Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha utabiri wa hali ya hewa nchini kuhakikisha uwepo wa mtandao wa rada saba (7), ununuzi wa vifaa pamoja na kuimarisha miundombinu mbalimbali ya utabiri wa hali ya hewa. Katika mwaka 2020/21, **Shilingi bilioni 30** fedha za ndani zimetengwa ili kutekeleza kazi zifuatazo:

i. Ununuzi wa Rada mbili (2) za hali ya hewa;

- ii. Kununua vifaa vya hali ya hewa ikiwemo kubadilisha vifaa vinavyotumia zebaki na vitambuzi vya matukio ya radi (lightening detectors);
- iii. Kukamilisha malipo ya mwisho ya Rada mbili (2) na ujenzi wa miundombinu yake kwa ajili ya Rada hizo katika maeneo ya Mbeya na Kigoma; na
- iv. Ukarabati wa mabweni na majengo ya Utawala katika Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma.

**429. Mheshimiwa Spika**, Mradi wa kuboresha huduma za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ili iweze kutoa huduma za usafiri wa anga ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kwa ufanisi umetengewa **Shilingi milioni 450,000.00** fedha za ndani. Fedha hizi zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege mbili (2) mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner;
- ii. Kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege moja ya mizigo (freighter) aina ya Boeing 767-300. Ndege hii itasaidia kuongeza mnyororo wa thamani katika bidhaa zetu ikiwemo maua, samaki na bidhaa zitokanazo na samaki, nyama, korosho, matunda na mboga mboga;
- iii. Ununuzi wa vifaa vya kuhudumia ndege (Ground Handling Service Equipment), kulipa malipo ya mwisho na gharama za kuanzia kwa Ndege mpya mbili za aina ya A220-300 na Ndege moja aina ya Q400 zitakazopokelewa (Entry into service costs), kulipa madeni yaliyohakikiwa, ukarabati wa karakana za matengenezo ya Ndege (Hangar) zilizopo JNIA na KIMAFA, ukarabati wa nyumba 38 za Watumishi wa ATCL zilizopo KIA, ukarabati wa Jengo la ATCL makao makuu na ukarabati wa Ghala la kuhifadhi vifaa vya Ndege iliyoko JNIA; na
- iv. Kupanua mtandao wa safari za anga. Kwa safari za ndani ni kuanzisha safari za Arusha, na kurejesha safari za Songea na Mtwara. Kikanda ni kuongeza safari za Lubumbashi, DR Congo na Gatwick, London; na kurejesha safari za Afrika ya Kusini.

**430. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2020/2021, Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imelenga kuongeza kiwango cha shehena, idadi ya Meli, mapato na ziada kama ifuatavyo:  
i. Kuhudumia Shehena ya tani milioni 15.295 ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 175,300 zitakazohudumiwa na vitengo vya TPA. Aidha, Kitengo cha TICTS kinatarajia kuhudumia makasha (TEUs) 656,100;

ii. Kuhudumia jumla ya Meli 3,980 zenyе ukubwa wa (GRT) milioni 33.524. Kati ya hizo, Meli 1,283 ni za Kimataifa (Deep Sea), Meli 923 ni za Mwambao (coasters) na Meli 1,769 zitahudumiwa katika bandari za Maziwa; na

iii. Kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 1,164.406.

Aidha, ili kufikia malengo hayo, katika mwaka 2020/21 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imetenga jumla ya **Shilingi milioni 700,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 500,000** ni fedha zinazotokana na vyanzo vya Ndani ya Mamlaka na **Shilingi milioni 200,000** ni fedha za Nje za mkopo kutoka Benki ya Dunia (International Development Agency - IDA). Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:

i. Kukamilisha Mradi wa uboreshaji wa Gati Na. 5 - 7 katika Bandari ya Dar es Salaam;

ii. Kukamilisha ujenzi wa Gati moja (multipurpose terminal) lenye urefu wa mita 300 katika Bandari ya Mtwara;

iii. Kuendelea na Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Tanga;

iv. Kuanza utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Matanki ya kuhifadhi Mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam;

v. Kuanza kutekeleza Mradi wa kupanua na kuchimba Lango la kuingilia na eneo la kugeuzia Meli (entrance channel and turning basin) katika Bandari ya Dar es Salaam;

vi. Kuendelea na ununuzi wa Mitambo na vifaa mbalimbali kwa Bandari zote;

- vii. Kuendelea kuimarisha matumizi ya TEHAMA na mfumo wa usalama bandarini (Port Integrated Security System - ISS);
- viii. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala, Ruvu; na
- ix. Kuendelea na miradi ya uboreshaji wa Bandari zote.

**431. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imetenga **Shilingi bilioni 13.5** kutoka katika vyanzo vyake ili kudhibiti ubora wa huduma na miundombinu ya Usafiri wa Anga nchini. Kazi zitakazofanyika ni:

- i. Kukamilisha ufungaji wa Rada za kuongozea Ndege katika Kituo kilicho Kiwanja cha Ndege cha Songwe;
- ii. Kununua Mfumo wa Usambazaji Taarifa za Ndege kmtandao (AXIM - Aeronautical Information Exchange Modal);
- iii. Kuandaa Kanzi Data kwa ajili ya sehemu za uwanda wa Nchi unaoonesha miinuko, milima, mabonde na vizuizi (e-TOD – Electronic terrain and obstacle data) katika viwanja vya kimataifa vya Julius Nyerere, Kilimanjaro na Abeid Amani Karume;
- iv. Kununua vipuri mbalimbali kwa ajili ya Mitambo mbalimbali;
- v. Kujenga uzio katika Mtambo wa kuongozea Ndege unaotumia mawasiliano ya redio (Non-Directional Beacon-NDB katika kituo cha Songwe);
- vi. Kuandaa Mfumo wa urekebishaji wa njia za Ndege kwa ajili ya kuingia na kutoka viwanjani (DAR-FIR AIRSPACE RESTRUCTURING); na
- vii. Kuandaa michoro na uhakiki katika Viwanja vya Ndege vya Songwe, Tabora, Iringa, Chato, Dodoma, Zanzibar, Kigoma, Bukoba na Mpanda.

**432. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetenga **Shilingi bilioni 36.528** kutoka katika vyanzo vyake ili kusimamia huduma za Usafiri Ardhini. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ifuatayo:

- i. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa ardhini zinakuwa endelevu;
- ii. Kuimarisha Usalama, Ulinzi na Ubora wa huduma za usafiri wa ardhini;
- iii. Kuhakikisha mazingira endelevu sambamba na maendeleo ya huduma ya usafiri kwa jamii; na
- iv. Kuongeza uwezo wa kutekeleza majukumu kiufanisi zaidi.

**433. Mheshimiwa Spika**, Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) limetenga jumla ya **Shilingi bilioni 66.8** fedha zinazotokana na makusanyo yake ya ndani ili kutekeleza kazi mbalimbali zenye lengo la kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya maji. Kazi zitakazotekelawa ni pamoja na:

- i. Kuimarisha ushindani na kuhakikisha huduma za Usafiri kwa njia ya Maji zinakuwa endelevu;
- ii. Kuimarisha Usalama, Ulinzi na Ubora wa huduma za usafiri kwa njia ya Maji;
- iii. Kuhimiza na kutunza mazingira dhidi ya uchafuzi wa mazingira baharini utokanao na Meli na kuhakikisha mazingira endelevu;
- iv. Kuboresha Sheria, Kanuni, Sera na mahusiano ya kitaasisi katika Sekta za usafiri kwa njia ya Maji; na
- v. Kuongeza uwezo wa Shirika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

**434. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) imetenga jumla ya **Shilingi bilioni 108.4**

fedha kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri wa abiria na mizigo kati ya Tanzania, nchi za SADC na DRC; kusimamia na kuimarisha usalama wa abiria, mizigo na vyombo vya usafiri, pamoja na kuzishauri Serikali za Tanzania na Zambia kuhusu masuala yanayohusu usafiri wa Reli ya TAZARA. Fedha hizo zitatumika kutekeleza kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kutoka Shilingi bilioni 92.8 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi bilioni 95.5 mwaka 2020/2021;
- ii. Kuongeza huduma za usafirishaji wa shehena ya mizigo hadi iliyofikia tani 450,000 na abiria 800,000 kwa njia kuu;
- iii. Kukarabati Injini saba (7) za njia kuu;
- iv. Kukarabati na kuimarisha miundombinu ya njia kuu ya Reli iliyopo;
- v. Kununua mataruma ya mbao 13,000;
- vi. Kufanya matengenezo na kukarabati Injini, Mitambo, na Mabehewa ya Mizigo na Abiria; na
- vii. Kukarabati Majengo, Karakana ya Mbeya, na Kiwanda cha Kokoto na uzalishaji wa Mataruma ya Zege cha Kongolo.

**435. *Mheshimiwa Spika***, Kampuni ya Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP) imetenga **Shilingi bilioni 3.0** kutoka katika vyanzo vyake ili kuboresha utoaji huduma ya usafiri wa mizigo ya masafa marefu kwa njia ya bahari pamoja na kusimamia usalama wa Mabaharia, Mizigo na Meli. Fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kazi zifuatazo:

- i. Kuboresha ukusanyaji wa mapato kutoka Shilingi bilioni 16.9 mwaka 2019/20 hadi Shilingi bilioni 17.50 mwaka 2020/2021;
- ii. Kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 600,000 mwaka 2019/2020 na kufikia tani 610,000 ifikapo Juni, 2021;

iii. Kuongeza mapato nje ya biashara ya msingi (core business) kwa njia ya kushawishi kuongeza idadi ya Meli na mizigo itakayoingia katika Bandari nchini kutoka makasha 47,000 mwaka 2019 na kufikia makasha 50,000 mwaka 2020; na

iv. Kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni kutoka Shilingi bilioni 14.6 mwaka 2019/20 na kufikia Shilingi bilioni 12.5 mwaka 2020/21.

**436. Mheshimiwa Spika**, Kampuni ya Kuendeleza Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KADCO) imetenga **Shilingi bilioni 11.33** kutoka katika vyanzo vyake ili kuendesha na kuendeleza miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA). Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni pamoja na:

- i. Kuanza ukarabati wa njia ya kuruka na kutua Ndege (runway resurfacing);
- ii. Uwekaji wa Mfumo mpya wa Taa za kuongozea Ndege (Aeronautical Ground Lighting – AGL);
- iii. Kupima msuguano wa njia ya kurukia Ndege na magurudumu ya Ndege na kuweka alama muhimu za kuongozea Ndege;
- iv. Maboresho ya maegesho ya magari (Car Parking);
- v. Kuanza ujenzi wa uzio wa eneo la kurukia na kutua Ndege;
- vi. Kununua kifaa cha kutibu maji ya kisima cha KIA yaliyo na madini mengi ya chumvi na fluoride;
- vii. Kununua Mashine ya kukusanya na kudhibiti mapato yanayotokana na maegesho ya magari kiwanjani; na
- viii. Kununua vifaa mbalimbali vya Ulinzi na Usalama kiwanjani.

### D.1.3 SEKTA YA MAWASILIANO

**437. Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2020/21 Sekta ya Mawasiliano inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 15,654,466,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,654,466,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 11,000,000,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**438. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2020/21, Sekta ya Mawasiliano itaendelea kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Muda Mrefu ambao umetilia mkazo katika maeneo yafuatayo:

#### **TEHAMA**

- i. Kusimamia uimarishaji na uendelezaji wa mradi wa Ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ili kufikisha huduma za Mkongo kwenye nchi zote zinazopakana na Tanzania na kufikisha mkongo hadi Makao Makuu ya Wilaya zote nchini;
- ii. Kufikisha miundombinu ya Mkongo kwa watumiaji wa mwisho ikiwemo taasisi za Serikali mijini na vijiji (Last Mile connectivity) ili kuwezesha mifumo mbalimbali iliyopo kufanya kazi kwa ufanisi ikiwemo mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya serikali (GePG);
- iii. Kuweka utaratibu wa kuwezesha upatikanaji wa huduma za Intaneti kwa gharama nafuu katika maeneo ya umma;
- iv. Kuratibu ukamilishaji wa Sheria ya kulinda taarifa binafsi (Personal Data Protection Act);
- v. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa mtandao wa TEHAMA wenye kasi zaidi (National Broadband Strategy); na
- vi. Kusimamia utekelezaji wa mkakati wa kitaifa wa usalama wa mitandao (National Cyber security strategy).

#### **MAWASILIANO**

- i. Kukamilisha uhuishaji wa Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 na kuhuishwa Sheria ya Posta ya mwaka 1993 ili iendane na ukuaji wa Teknolojia na kiuchumi;

- ii. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya TEHAMA ya mwaka 2016;
- iii. Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi nchini;
- iv. Kuratibu uanzishaji wa vituo vya HUDUMA PAMOJA (One Stop Service Centres); na
- v. Kuimarisha mashirikiano na mashirika ya kimataifa na kikanda.

**Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**439. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania itatekeleza masuala yafuatayo:

- i. Kwa kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC) kuendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu Sheria, haki na wajibu wa watumiaji, kuhusu matumizi ya Mfumo mpya wa anwani za makazi na misimbo ya Posta, uhakiki wa usajili wa laini za simu za kiganjani, wajibu wa watumiaji katika masuala ya tahadhari dhidi ya uhalifu kupitia mtandao na kufanikisha ufumbuzi wa malalamiko kati ya watumiaji na watoa huduma za Mawasiliano;
- ii. Kuendelea kutekeleza usimamizi wa usalama wa mitandao ya mawasiliano kupitia TZ- CERT;
- iii. Kuendelea kusimamia na kuboresha mfumo wa usimamizi wa huduma za mawasiliano, TTMS, ili uendane na mahitaji pamoja na mabadiliko ya Teknolojia;
- iv. Kuandaa Muongozo juu ya matumizi ya utangazaji wa kidigit kwa redio na mwingiliano wa Smart Card za Vingámuzi;
- v. Kujenga Jengo la Ofisi za Shirika la Posta Afrika (Pan African Postal Union-PAPU) - Arusha, Jengo la TCRA - Dodoma na Ofisi za Zanzibar;

- vi. Kuendelea kutekeleza mifumo ya utendaji kazi (Quality Management System) ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa Mawasiliano ya simu, Posta na Utangazaji;
- vii. Kuendelea kusimamia Sekta ya mawasilino na kuhakikisha kuwa watoa huduma wote wanatoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo;
- viii. Kuendelea kuhakiki gharama na tozo mbalimbali katika matumizi ya huduma za mawasiliano;
- ix. Kuendelea kujenga uwezo wa kukabiliana na uhalifu wa matumizi mabaya ya mtandao kwa Taasisi za Ulinzi na Usalama; na
- x. Kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa leseni za huduma za mawasiliano.

**Shirika la Posta Tanzania (TPC)**

**440. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Shirika la Posta linatarajia kutekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Posta eneo la Mtumba (Awamu ya Kwanza), vituo vya kutolea huduma za Posta (Namanyere, Bariadi, Kilosa na Kondoa) na ukarabati wa majengo 30 ya Posta za wilaya na majengo 7 ya posta kuu za mikoa;
- ii) Mradi wa ununuzi wa magari kwa ajili ya kuboresha usafirishaji na ufikishaji wa mizigo, barua, nyaraka na vipeto pamoja na kuimarisha miundombinu na mifumo ya TEHAMA;
- iii) Kuandaa 'Post Office Directory' ya Shirika la Posta Tanzania;
- iv) Kufikisha huduma ya Posta Mlangoni (Last mile delivery) katika maeneo yote ambayo utoaji wa anuani za makazi na postikodi umekamilika;
- v) Kufanya ukaguzi wa ofisi na kukamilisha taratibu na maandalizi ya msingi ya miundombinu kwa ajili ya kutoa huduma ya Jamii centre, na kuanza utekelezaji wake;

- vi) Kufanya maandalizi ya msingi na kukamilisha taratibu muhimu za utekelezaji wa mradi wa Ecom-Africa katika utoaji wa huduma za biashara ya kielektroniki kuititia mtandao wa Shirika la Posta Tanzania; na
- vii) Kupanua wigo wa utoaji wa huduma ya usafirishaji wa sampuli za maabara kwa wakati.

### **Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)**

**441. *Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2020/21 Shirika la Mawasiliano Tanzania litatekeleza majukumu yafuatayo:

- i) Kupanua na kuboresha huduma kwa wateja, biashara, usambazaji na masoko kwa kuongeza matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma na uendeshaji.
- ii) Kuongeza idadi ya wateja hai (Active Customers) wa huduma mbalimbali za mawasiliano (simu na data) kutoka 1,008,455 mwezi Februari, 2020 hadi 1,800,000 kwa mwaka wa fedha 2020/21.
- iii) Kuendelea kusimamia na kuendesha Miundombinu mkakati ikiwemo Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Kituo cha Data cha Taifa (National Data Centre);
- iv) Uboreshaji wa Mifumo ya Usalama wa Mtandao kwa wateja wa Shirika. (Modernization of Broadband Traffic Management & Security);
- v) Upanuzi na uboreshaji wa Mifumo ya Mtandao Mhimili (Expansion of Core Network Systems), Usafirishaji wa Data (Expansion of Transmission/Transport Networks) na Simu za Mkononi (Expansion of Radio Access Network); na
- vi) Kuisaidia serikali katika kukusanya mapato na kuchangia katika mfumo wa fedha kwa kielektroniki kuititia kampuni tanzu ya TPesa.

## **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**442. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) utatekeleza kazi zifuatazo:

- i) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijiji ni katika kata 252 awamu ya 4 zenye vijiji 555 ili kuhakikisha kuwa huduma za wananchi zinawafikia wananchi wengi zaidi;
- ii) Kukamilisha utekelezaji wa miradi ya kufikisha huduma ya mawasiliano vijiji ni katika maeneo ya kata 38 kwenye maeneo ya mipakani na yenye uhitaji maalum awamu ya 5;
- iii) Kuboresha usikivu wa matangazo ya TBC maeneo ya mikooani na pembezoni mwa nchi;
- iv) Kutoa vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule za sekondari 150;
- v) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu 1,000;
- vi) Kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa Wanafunzi wasichana 248;
- vii) Kuendeleza ushirikiano na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili katika uunganishwaji wa mtandao wa mawasiliano katika hospitali za Serikali ili kuleta ushirikiano wa kitabibu kwa njia ya mtandao na kuondoa tatizo sugu la uhaba wa madaktari bingwa; na
- viii) Ujenzi wa Ofisi za Mfuko jijini Dodoma.

## **Tume ya TEHAMA (ICTC)**

**443. *Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2020/21, Tume ya TEHAMA itatekeleza mambo yafuatayo:

- i) Kusajili na kujenga uwezo wa wataalam wa TEHAMA wasiopungua 800;

- ii) Kuwezesha matukio ya kuvutia uwekezaji na kuendeleza miradi 10 ya TEHAMA katika kituo cha SoftCenter;
- iii) Kufanya utafiti wa kupima viashiria vya Jamii Habari (measuring Information Society and impact of digital transformation indicators) kwa kushirikina na wadau wa utafiti kutoka ndani na nje ya nchi; na
- iv) Kutekeleza Mradi wa ujenzi wa kituo cha kuendeleza ubunifu na bidhaa za TEHAMA nchini.

**Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC)**

**444. *Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha mwaka 2020/21 Baraza litaendelea kufanya yafuatayo:

- i. Kuelimisha umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma na bidhaa za mawasiliano. Baraza litaingia makubaliano na Tanzania Bus Owners Association (**TABOA**) ili kurusha documentary yenye kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano katika Mabasi yaendayo mikoani. Kupitia Makubaliano hayo Baraza linategemea kufikia watu kati ya 15,000 hadi 20,000 kwa siku na watu 500,000 kwa mwezi;
- ii. Kupokea taarifa na maoni kutoka kwa watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano na kuziwasilisha kwa taasisi husika ili kuboresha ufanisi na kupunguza changamoto kwa watumiaji;
- iii. Kuanzisha Kamati za Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano, kuendesha mikutano ya elimu na mashauriano katika mikoa ya Rukwa, Manyara, Geita na Kigoma;
- iv. Kuanzisha na kujengea uwezo vilabu vya Mawasiliano katika shule 56 za Sekondari katika mikoa 13 ya Morogoro, Mbeya, Dodoma, Iringa, Lindi, Mtwara, Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Tanga, Arusha, Mwanza, Kagera na Dar es Salaam; na

v. Baraza litaendelea kumwakilisha mtumiaji wa huduma za mawasiliano kwa kuwasilisha maoni, taarifa na kushauriana na Waziri na Mamlaka ya Mawasiliano. Aidha Baraza litaendelea kushauriana na Watoa huduma kuhusu masuala yanayomhusu mtumiaji.

## D. 2 TAASISI ZA MAFUNZO

### Chuo cha Ujenzi Morogoro

**445. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2020/21, Chuo kimepanga kufundisha jumla ya wanafunzi **1,440** katika fani za ufundi sanifu (technicians) na ufundi stadi (Basic Artisans) wa fani za barabara na ukaguzi wa madaraja, majengo, magari, utengenezaji wa mitambo (plant mechanics), uendeshaji wa mitambo (plant operations), madereva wa magari ya Umma (Public Professional Drivers), madereva wa awali (Basic driving) na madereva wa magari ya abiria (PSV), mafunzo ya kompyuta na Teknolojia ya Nguvukazi stahiki. Kazi nyingine ni pamoja na kukarabati magari, samani, majengo na miundo mbinu ya Chuo; kufanya tathmini ya mafunzo na kununua vifaa kwa ajili ya kuboresha mradi wa kuosha magari.

### Chuo cha Matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi (Appropriate Technology Training Institute – ATT) - Mbeya

**446. *Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2020/21, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo yenye lengo la kuimarisha matumizi endelevu ya teknolojia stahiki ya nguvukazi kwa kada za watendaji ili kujenga weledi na ujuzi wa kutosha katika utekelezaji wa miradi inayotumia nguvukazi. Mafunzo yatahusisha Wahandisi **10**, Mafundi Sanifu **30** na wasimamizi wa barabara **30**. Aidha, Chuo kitaendelea na utoaji wa mafunzo kwa vikundi vya vijana na wanawake ili kuimarisha matumizi endelevu ya teknolojia stahiki ya nguvukazi na kujenga weledi na ujuzi wa kutosha katika utekelezaji wa miradi inayotumia nguvukazi, lengo ni kutoa mafunzo haya kwa wanawake **50** na vijana **50**.

**447. Mheshimiwa Spika**, kazi zingine zilizopangwa ni kuendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi katika Ujenzi na ukarabati wa barabara kwa kutembelea na kutoa ushauri wa matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvukazi kwa wadau mbalimbali katika Halmashauri; kuimarisha na kuboresha utendaji wa Chuo kwa kuongeza idadi ya watumishi wa kada mbalimbali na kuwajengea uwezo kwa kushiriki kwenye mikutano na makongamano ya kitaifa, kimataifa na kikanda.

**448. Mheshimiwa Spika**, Chuo pia kimepanga kufanya matengenezo ya magari na mitambo ya mafunzo na kuongeza vifaa na huduma mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya mafunzo; kuendelea kusimamia ukarabati na matengenezo ya barabara kwa kuititia barabara za mafunzo katika utoaji wa mafunzo kwa jamii ili kuendelea kuhamasisha matumizi ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi kwa umma pamoja na kuendelea kushiriki katika uanzishaji wa Taasisi ya Teknolojia ya Ujenzi nchini inayoratibiwa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

#### **Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)**

**449. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 25.379** fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia ili kuboresha miundombinu ya Chuo, utoaji wa mafunzo na maeneo ya kufundishia. Fedha hizo zitatumika kutekeleza mipango ifuatayo:

- i. Kuanza ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Usafiri wa Anga Kitakachokuwa Katika Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro (KIA);
- ii. Kuendelea na Ujenzi wa Kituo cha Rasilimali Mafunzo kilichopo Mabibo, Dar es Salaam;
- iii. Kuanza ujenzi wa Majengo mapya sita (6) katika Kampasi ya Mabibo Dar-es- Salaam;
- iv. Ununuzi wa Ndege mbili (2) za kufundishia kozi ya urubani na vifaa mbalimbali vyaa mafunzo; na

v. Kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya kufundisha kozi za Marubani kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA).

### **Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)**

**450. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) kimetenga jumla ya **Shilingi billioni 4.842** fedha zinazotokana na vyanzo vyake vyaa mapato ili kutekeleza malengo yafuatayo:

- i. Kuongeza udahili wa wanafunzi kwenye fani mbalimbali za ujuzi (competency) na taaluma (academic) kwenye Sekta ya Bahari kutoka 1,126 hadi kufikia 1,500 kwa kozi ndefu;
- ii. Kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi kwenye Sekta ya Bahari;
- iii. Kuendeleza walimu kitaaluma katika Shahada za Uzamili, Uzamivu na kuwapatia mafunzo kwa vitendo melini (Sea time training) ili kuwaongezea sifa na uwezo wa kutoa mafunzo;
- iv. Kuanza kutoa kozi za Uhandisi katika fani za Fundi Mchundo (welding and fabrication Engineering) na *offshore Oil and Gas Engineering* ili kutoa Wataalamu wenyewe sifa kwenye Miradi ya Utafiti, Uchimbaji na Usafirishaji wa Mafuta na Gesi Baharini;
- v. Kuandaa mitaala ya Uzamili katika fani za *Marine Engineering* na *Nautical Science*; na
- vi. Kukamilisha taratibu za ununuvi wa Mkandarasi wa ujenzi wa Jengo la madarasa na ofisi katika eneo la Sokoine Drive.

### **D.3 MASUALA MTAMBUKA**

#### **Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Sekta ya Ujenzi**

**451. Mheshimiwa Spika**, ili kuongeza ushiriki wa wanawake katika kazi za ujenzi, Wizara kwa mwaka wa fedha 2020/21 imepanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake ya namna ya kuomba zabuni na kujaza zabuni kwa usahihi;

kutoa mafunzo kwa wanawake na vikundi nya wanawake juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi. Aidha, Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu kazi za sekta ya ujenzi zinazofanywa na makandarasi wanawake, ili kubaini changamoto zinazowakabili kwa lengo la kutafuta ufumbuzi pamoja na kuendelea kuelimisha umma juu ya ushirikishwaji wa wanawake katika kazi hizo.

Wizara pia imepanga kutembelea shule za Sekondari ili kuwashamasisha wasichana wanaosoma masomo ya sayansi na hisabati pamoja na kuendelea kusambaza nakala za Miongozo ya Ushirikishwaji wa Wanawake katika Kazi za Sekta ya Ujenzi.

#### **E. SHUKRANI**

**452. *Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati viongozi wenzangu katika Wizara ninayoiongoza nikianza na **Mheshimiwa Elias John Kwandikwa (Mb.)**, **Naibu Waziri (Ujenzi)**; **Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye (Mb.)**, **Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano)**; **Makatibu Wakuu: Mbunifu Majengo Elius Asangalwisye Mwakalinga (Ujenzi)**; **Mhandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho (Uchukuzi)**; **Dkt. Maria Leticia Sasabo (Aliyekuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano)** na **Dkt. Jim James Yonaz**, **Naibu Katibu Mkuu (Mawasiliano)**. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara/Vitengo; Wenyeviti wa Bodi zilizo chini ya Wizara; Viongozi wa Taasisi na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamekuwa wakinipa na juhudi walizofanya kuhakikisha kwamba tunatimiza majukumu tuliyokabidhiwa na Taifa ipasavyo. Ushirikiano wao ndio uliowezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yetu katika mwaka uliopita. Naomba waendelee na juhudi hizo katika kipindi kijacho ili tuweze kutimiza malengo tulijojiwekea.

**453. *Mheshimiwa Spika***, Washirika mbalimbali wa Maendeleo wamechangia katika utekelezaji wa Programu na Mipango mbalimbali ya Wizara. Napenda kuchukua fursa

hii kuwashukuru na kuwatambua Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini (IMO), Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO), Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO), Benki ya Kiarabu ya Maendeleo ya Afrika (BADEA), OPEC Fund, Umoja wa Nchi za Ulaya, "Third World Organization for Women in Science (TWOWS)", UNESCO, Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), Japan (JICA), Korea Kusini (KOICA), Abu Dhabi Fund, Ujerumani (KfW), Uingereza (DFID), Uhlanzi (ORIO), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Kuwait (KFAED), Uturuki, HSBC, TMEA, Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za SADC, Nchi za Urusi, Afrika Kusini, Uingereza, Marekani, Uhlanzi, Japan, India, China, Denmark, Norway, Ubelgiji, Ujerumani, Taasisi za fedha za CRDB, NSSF, PSSSF na TIB, Asasi zisizokuwa za Kiserikali; Sekta Binafsi pamoja na wengine wengi.

**454. Mheshimiwa Spika**, mwisho, nakushukuru tena wewe binafsi na Mhe. Naibu Spika. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara ([www.mwtc.go.tz](http://www.mwtc.go.tz)).

**F. MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UJENZI,  
UCHUKUZI NA MAWASILIANO KATIKA MWAKA WA FEDHA  
2020/21**

**455. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/21, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,784,874,417,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,616,361,206,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 3,152,858,745,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 15,654,466,000.00** ni kwa ajili ya Sekta ya Mawasiliano. Mchanganuo wa fedha zinazoombwa kwa kila Fungu ni kama ifuatavyo:

#### **SEKTA YA UJENZI (FUNGU 98)**

**456. Mheshimiwa Spika**, jumla ya **Shilingi 1,616,361,206,000.00** za Fungu 98 (Ujenzi) zinajumuisha **Shilingi 38,774,425,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara (Ujenzi) na Taasisi

ambapo **Shilingi 36,420,026,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 2,354,399,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Bajeti ya Maendeleo ni Shilingi **1,577,586,781,000.00** ambazo zinajumuisha **Shilingi 1,252,222,598,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 325,364,183,000.00** fedha za nje. Fedha za ndani zinajumuisha **Shilingi 641,746,370,000.00** za Mfuko wa Barabara na **Shilingi 610,476,228,000.00** za Mfuko Mkuu wa Serikali.

### **SEKTA YA UCHUKUZI (FUNGU 62)**

**457. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Uchukuzi imetengewa jumla ya **Shilingi 3,152,858,745,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya hizo, **Shilingi 90,710,109,00.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawalda ambapo **Shilingi 63,639,165,000.00** ni za Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 27,070,944,000.00** ni za Matumizi Mengineyo. Aidha, miradi ya maendeleo imetengewa **Shilingi 3,062,148,636,000.00** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,937,678,923,000.00** ni fedha za Ndani na **Shilingi 124,469,713,000.00** ni fedha za Nje.

### **SEKTA YA MAWASILIANO (FUNGU 68)**

**458. Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Mawasiliano imepangiwa jumla ya **Shilingi 15,654,466,000.00**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,654,466,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 11,000,000,000.00** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**459. Mheshimiwa Spika**, pamoja na Hotuba hii, nimeambatanisha Miradi ya Wizara itakayotekeliza katika mwaka wa fedha 2020/21 (**Kiambatisho Na. 1-7**) ikiwa ni pamoja na kiasi cha fedha kilichotengwa kutekeleza Miradi hiyo. Naomba viambatisho hivyo vichukuliwe kama sehemu ya vielelezo vya hoja hii.

**460. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso.

**MHE. SELEMANI M. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ifuatayo ni taarifa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya wizara ya ujenzi Uchukuzi Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na maoni na ushauri kuhusu makadirio na mapato na matumizi wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Taarifa hii imejikita katika uchambuzi wa Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi), Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi) na Fungu 98 (Sekta ya Mawasiliano).

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021 upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2019/2020. Kipengele hiki kinabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo ya sekta zote za Wizara ya Ujenzi Uchukuzi Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Jedwali namba 1 linaonyesha mchanganuo wa fedha zilizoidhinishwa na zilizotolewa hadi mwezi Februari, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Uchukuzi Fungu 62, katika mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishiwa jumla ya

shilingi tirioni 3.6, fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2020 tirioni 1.0 sawa na asilimia 28 ya fedha zote zilizoidhinishwa katika fungu hili kamati imeendelea kubaini kuwapo kwa changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati na kusababisha fedha za miradi kuchelewa kuanza na kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya ujenzi fungu 98 katika mwaka wa fedha 2019/20 iliidhinishwa jumla ya shilingi tirioni 1.4 hadi kufikia Februari, 2020 fedha zilizopokelewa bilioni 800.62 ambazo sawa na asilimia 62.

Hata hivyo, wakati tunachambua bajeti ya sekta hii tulipokea taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kuna fedha zilizoongezwa karibu bilioni 723 kwa ajili ya kulipa wakandarasi mbalimbali. Uchambuzi wa kamati umebaini pamoja na fedha kutolewa kwa sekta ya ujenzi kwa asilimia 62, hadi mwezi Machi, 2020 ilipokuwa ikichambua bajeti ya sekta ya ujenzi baadhi ya miradi hasa ya ujenzi wa viwanja vya ndege haikuwa imepata fedha yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanja vya ndege ambavyo havikupata fedha hiyo ni kiwanja cha ndege cha Kigoma, Mpanda, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Songwe, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, baadhi ya miradi ya barabara haikupata fedha. miradi hiyo ni pamoja na barabara ya Singida, Babati, Minjingu, Same, Mbara, Korogwe, Arusha, Namanga, Mafia *Airport*, Handeni, Mwanza, Shinyanga, Boda, Dar es Salaam, Chalinze na Morogoro *Express Way*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano - Fungu 68 mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishwa jumla shilingi bilioni 3.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi mwezi Februari, 2020 Sekta ya Mawasiliano imepokea jumla ya shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 62.4. Katika fungu hili hakukutengwa fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati ilielezwa kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zingetolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati imebaini kuwa fedha hizo za miradi ya

maendeleo hazikutolewa kama zilivyokuwa zimeahidiwa na hivyo kusababisha miradi kutokutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengwa fedha kwa ajili ya fedha za mwaka 2019/2020. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 12 hadi 19 Machi, 2020. Katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam miradi iliyotembelewa ni Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Serikali Ihumwa Dodoma, Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kati, Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Juu, Ubungo *Interchange* Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Magomeni, Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka (*BRT*), Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam na Mradi wa Ujenzi wa Daraja la Mto Wami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mambo yaliyobainika katika ziara hii ni kuhusu Wakala wa Majengo *TBA*. Baadhi ya Wizara zilizojenga ofisi zake Mtumba Dodoma kutokumlipa *TBA* ada ya ushauri ambayo kwa pamoja inadai shilingi bilioni 1.6. Kwa mwenendo huu Kamati inaona nguvu na kasi ya Wakala wa Majengo Tanzania isipolipwa hizo fedha hawataweza kufanya kazi za utendaji wake kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulitembelea ujenzi wa Reli ya Kati kiwango cha kisasa (*standard gauge*) sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro, Morogoro – Dodoma. Maendeleo ya ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa (*standard gauge*) ni mazuri kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali zimetolewa kwa wakati, fidia kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa kupisha ujenzi nazo zimetolewa kadri mradi unavyosogea. Hadi mwezi Machi, 2020 Kamati ilipotembelea mradi huu wa sehemu ya Dar es Salaam - Morogoro ujenzi umefika asilimia 75 na sehemu hii ya pili kutoka Morogoro hadi Makutupora – Dodoma ujenzi umefikia asilimia 28.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasitisiza umuhimu wa kuwa na wataalamu wa kutosha wa ndani ili wawzeze kupata usoefu na ujuzi wa kusimamia na kuendeleza reli hii wakati wataalamu wa nje watakapoondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Magomeni umefikia asilimia 70. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali ikatoa haraka kiasi kilichohitajika kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo shilingi bilioni 15 ili mradi uweze kukamilika na uweze kutoa matunda kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliendelea na ziara ya kukagua mradi wa kuangalia miundombinu ya usafiri wa mabasi yaendayo haraka (*BRT*) awamu ya pili ambako kazi imefikia asilimia mbili ukilinganisha na asilimia 15 iliyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Kamati kukagua Mradi wa Barabara za Mabasi, kuna changamoto inayoendelea kujitekeza katika awamu ya kwanza ya kipande cha Magomeni hadi *fire* ambapo Mto Msimbazi umekuwa ukijaza maji kiasi cha magari ya mradi kushindwa kupita na yale yaliyopo katika Kituo cha Mabasi kuharibika kunatokana na kuingia maji. Kamati inaona upo umuhimu mkubwa wa Serikali kujenga daraja la juu kutoka Magomenii hadi *fire* ili kuhakikisha barabara hii inapitika wakati wote.

Kuhusu baadhi ya ushauri wa mapendekezo ya Kamati yaliyozingatiwa na Serikali yameelezwa katika kipengele hiki na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021; katika mwaka wa fedha wa 2020 na 2021 Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi triliuni 4.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa fedha zinazoombwu umeonyeshwa katika jedwali Na. 2, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka 2020/2021 ni wa kuridhisha kwani fedha zimeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 16, ukilinganisha na fedha zilizokuwa zimetengwa mwaka uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa kipaumbele Sekta ya Miundombinu na kuongeza bajeti ya sekta hii kwa mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano kwa miaka minne mfululizo. Sekta hii imekuwa ikitengewa fedha kiasi cha kuridhisha ambapo mwaka 2017/2018 shilingi trillioni 4.5, 2018/2019 shilingi trillioni 4.2, 2019/2020 shilingi trillioni 4.9 na mwaka wa fedha wa 2020/2021 trillioni 4.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuangalia, fedha hizo zilizoidhinishwa ndani ya miaka minne mfululizo ni dhahiri kuwa Serikali imeipa kipaumbele cha kutosha Sekta ya Miundombinu nchini na kuharakisha maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miradi inatekelezwa katika muda uliopangwa na hatimaye wananchi wanufalike.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa ujenzi wa reli ya kati uende sambamba na ununuvi wa vichwa vyaa mabehewa ya treni ili mradi utakapokamilika mnamo mwezi Juni, 2020 sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze kufanyika. Sehemu ya pili ni kuzingatia kuwaajiri wahandisi wa kutosha wa ndani wenye fani mbalimbali muhimu na zinazohitajika katika uendeshaji wa reli pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni na utaratibu wa matumizi ya reli mpya ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalamu wa ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri yafuatayo kuhusu bandari: Serikali kwa kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Masiliano, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda, Biashara wahitishe kikao cha pamoja na wadau mbalimbali wa bandari nchini ili kubadilishana mawazo na kuona namna nzuri ya uendeshaji wa bandari nchini na kuifanya bandari iweze kujindesha kibiaishara na kuvutia wafanyabiashara wengi kuitumia jambo ambalo litaongeza mapato kwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia iharakishe kukamilisha bandari za nchi kavu katika maeneo ya Kwala, Pwani, Ihumwa Dodoma, Fela Mwanza, Katosho Kigoma, Kingori Arusha, Isaka Kahama, Nainyara Mbeya ili kupunguza gharama za wateja kusafiri mpaka Dar es Salaam kwa ajili ya kutoa mizigo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kampuni ya huduma za meli, Kamati inashauri yafuatayo: Serikali ijipange kutengeneza meli zote 14 zilizopo katika maziwa makuu ili kuiwezesha kampuni ya meli Tanzania kumudu kujidoresha kibiasara. Kutokana na uwekezaji unaofanyika sasa kukarabati na kujenga meli mpya katika Maziwa Makuu ni vyema Serikali iendelee kulipa mishahara wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi ambacho ni cha mpito mpaka kampuni hii itakapokuwa imeweza kujidoresha na kusimama vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri yafuatayo kuhusu *TAZARA*. Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya *TAZARA* kuhusu uimarishaji wa reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Serikali pia kwa kushirikiana na nchi wabia wa *TAZARA* ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka China kwa ajili ya kusaidia kuiboresha *TAZARA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania, Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia mamlaka hii angalau asilimia 50 ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili mamlaka ya Viwanja vya Ndege *TIA* iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati pamoja na uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, japokuwa kamati imefahamishwa kuwa kwa sasa *ATCL* imekuwa na marubani wa kutosha ambapo marubani 78 wamehitimu mafunzo na kupata sifa stahiki za kuendesha ndege ni muhimu sana Serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha inalinda marubani

wake wasichukuliwe na mashirika yenyeye nguvu kama vile *Emirate*.

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania (*ATCL*) kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja mara kwa mara ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote, hii itasaidia kampuni kushindana kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Ujenzi, kuhusu Wakala wa Barabara *TANROADSKamati inaendelea kusisitiza ushauri ufuatao*: Serikali itekeleze sera yake kuunganisha mikoa yote kwa barabara za lami. Baadhi ya mikoa hiyo ni Lindi - Morogoro, Morogoro - Mlimba, Madete - Njombe, Lindi - Songea, Kigoma, Katavi, Katavi- Tabora, Kigoma - Kagera, Mbeya - Makete, Njombe - Arusha, Mara. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu Kamati inajua kwamba mwaka huu kulikuwa na mvua nyngi, imependekeza Kamati Serikali itenye fedha za kutosha kwa ajili ya matengenezo ya dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa viwanja vya ndege Kamati imeshauri yafuatayo: Serikali ikamilishhe ucharaka wa ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria, mizigo pamoja na jengo la kuongezea ndege. Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishiwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vya ndege ili miradi hii iweze kukamilika.

Kuhusu Wakala wa Ufundi, Umeme TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: Wakala uendelee kukamilisha mchakato wa kuchagua karakana na kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo kwa sasa, magari yote yanayotengenezwa na Serikali mikoani yanaenda Makao Makuu kitu ambacho kinaleta usumbufu mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta ya Mawasiliano, kuhusu miradi ya anuani ya makazi na misimbo ya Posta, Kamati inasisitiza ushauri ufuatao: Serikali itoe kipaumbele kwenye mradi wa anuani za makazi na misimbo. Mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu unaimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), Kamati inaendelea kushauri na kusisitiza kuongezwa kwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki na mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama wa kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulisho vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, Kamati inaendeleza kusisitiza ushauri wake kuwa Serikali ipitie kuangalia upya taratibu na ukamilishaji wa miradi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Simu Tanzania (*TTCL*), pamoja na kuunda kikosi cha kufuatilia madeni ambayo yameripotiwa hadi tarehe 30 Machi, kufika jumla ya shilingi bilioni 30 ambayo kwa kiasi kikubwa zinadaiwa Wizara, Taasisi na Mashirika ya Serikali, Kamati inashauri Serikali isimamie *TTCL* kuhakikisha wanalipwa madeni yao wanayodai vinginevyo shirika hili litakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochaea maendeleo ya nchi. Miradi hiyo ndani ya sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nyingi ili hii yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo Kamati inaona ni muhimu sana Serikali kushirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano mkubwa walioutoa kwa kutoa michango ambayo wakati wa kupitia na kuchambua bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe katika *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa *Eng.* Isack Aloyce Kamwelwe Mbunge, akisaidiana na Manaibu; Mheshimiwa Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias John Kwandikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara, Ndugu Elias Mwakalinga, Sekta ya Ujenzi; *Eng.* Dkt. Leonard Chamuriho, Katibu Mkuu Mstaifu; *Eng.* Maria Mfasabo, Sekta ya Mawasiliano pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jimmy Yonas. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi zote, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile shukrani ziende kwa watendaji wote wa Wizara kwa Ushirikiano wanaoupatia Kamati na kutekeleza majukumu yake. Nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati ya Bunge Ndugu Michael Lucas Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati, Ndugu Hosiana John, Mkuta na Ndugu Janeth Malangu; Msaidizi wa Kamati, Ndugu Modesta Michael Kipiko pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao katika kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, naliomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya ujenzi,

Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA  
UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO KWA MWAKA WA  
FEDHA 2019/2020; PAMOJA NA MAONI NA USHAURI KUHUSU  
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO  
KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia Kanuni ya 123 ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

- a) Sehemu ya Kwanza inahusu utangulizi, sehemu hii inabainisha mpangilio wa taarifa inayowasilishwa;
- b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi unaojikita katika masuala makubwa mawili yafuatayo: -
  - i) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2019/2020. Mapitio yanajielekeza zaidi katika makusanyo ya mapato, upatikanaji wa fedha za miradi ya

maendeleo, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa Maoni na Mapendekezo ya Kamati;

ii) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Uchambuzi huu upo katika maeneo makuu matatu ambayo ni Makisio ya Ukusanyaaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 na Mambo mengine yaliyojiteze wakati wa kupitia na kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2020/2021.

c) Sehemu ya Tatu imejielekeza katika Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusiana na masuala yote yaliyofanyiwa uchambuzi katika **Fungu 62 (Sekta ya Uchukuzi)**, **Fungu 98 (Sekta ya Ujenzi)** na **Fungu 68 (Sekta ya Mawasiliano)**.

## **SEHEMU YA PILI**

### **2.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

#### **2.1 Makusanyo ya Mapato kwa Mwaka 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), liliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi 22,517,437,400** kutohana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Hadi kufikia 29 Februari, 2020, zimekusanya **Shilingi 15,273,525,046** sawa na **asilimia 68** ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, fungu 98- Sekta ya Ujenzi ilikadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 68,828,000.00** kupitia idara zenye vyanzo vya mapato. Idara hizo ni Idara ya Utawala, Idara ya Huduma za Ufundji na Kitengo cha Menejimenti ya Manunuzi. Hadi kufika mwezi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 23,790,000.00**

zilikuwa zimekusanywa sawa na **asilimia 34.56** ya malengo ya makusanyo ya sekta hii kwa mwaka wa fedha 2019/20.

## 2.2 Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kipengele hiki kinabainisha upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo kwa Sekta zote za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Jedwali Na. 1, Upatikanaji Fedha za Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano hadi Kufikia Februari, 2020**

Sekta	Fedha zilizodirisha katika Mwaka Fedha 2019/20			Fedha zilizodirisha hadi kufikia Februari, 2020		
	Matumizi ya Kawaida	Fedha za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Neza Miradi ya Maendeleo	Matumizi ya Kawaida	Fedha za Miradi ya Maendeleo	Fedha za Neza Miradi ya Maendeleo
Uchukuzi	85,408,131,000	3,327,716,600,000	216,005,642,895	53,404,102,071,14 (62%)	85,848,881,683 (29%)	145,201,000,000 (67%)
Ujenzi	36,215,250,040,04	1,081,219,351,229,52	304,651,604,280,00	22,091,947,758,04 (60%)	55,419,296,780,16 (54%)	275,991,529,676,01 (91%)
Mawasiliano	3,973,197,000	0	0	2,481,433,986 (62%)	0	0

*Chanzo: Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano 2019/2020*

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Uchukuzi (Fungu 62), katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi Triliioni 3.6 (3,629,130,373,895)**. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 85.4 (85,408,131,000)** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Triliioni 3.5 (3,543,722,242,895)** fedha za Miradi ya Maendeleo. Fedha zilizotolewa hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ni **Shilingi Triliioni 1.0 (1,009,049,881,683)** sawa na **asilimia 28** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kamati imeendelea kubaini kuwapo kwa changamoto ya kutokutolewa fedha kwa wakati kwa Sekta hii na kusababisha baadhi ya miradi kuchelewa kuanza na kukamilika kwa wakati uliopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ujenzi (Fungu 98), katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilidhinishiwa jumla ya **Shilingi Triliioni 1.4**

(1,421,516,205,501.56). Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 36.1** (36,142,664,000.00) ni fedha za Matumizi ya Kawaida na **Shilingi Triliuni 1.3 (1,385,270,955,497.52)** fedha za Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, fedha za matumizi ya kawaida imeongezewa wigo kutoka **Shilingi bilioni 36.1 (36,142,664,000.00)** zilizoidhinishwa na Bunge mpaka **Shilingi bilioni 36.2 (36,245,250,004.04)**. Hili ni ongezeko la **Shilingi milioni 102,586,004.04**. Ongezeko hili ni kwa ajili ya malipo ya madeni ya Wazabuni mbalimbali ambayo yamehakikiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 fedha zilizopokelewa ni **Shilingi bilioni 862.4 (862,410,826,456.20)** sawa na **asilimia 62**.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, pamoja na fedha kutolewa kwa Sekta ya Ujenzi kwa **asilimia 62**, hadi mwezi Machi, 2020 ilipokuwa ikichambua bajeti ya Sekta ya Ujenzi, baadhi ya miradi hasa ya ujenzi wa viwanja vyta ndege haikuwa imepata fedha yoyote. Viwanja vyta ndege hivyo ni Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Mpanda, Tabora, Shinyanga, Sumbawanga, Songwe, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, baadhi ya miradi ya barabara nayo haikupata fedha, miradi hiyo ni pamoja na barabara ya Singida-Babati-Minjingu, Same-Mkumbara-Korogwe, Arusha-Namanga, Mafia *Airport Access Road*, Korogwe-Handeni, Mwanza-Shinyanga Border, Dar es Salaam-Chalinze-Morogoro *Express Way*.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Mawasiliano (Fungu 68), mwaka wa fedha 2019/2020 iliidhinishwa jumla ya **Shilingi Bilioni 3.9 (3,973,197,000)** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi mwezi Februari, 2020 Sekta ya Mawasiliano imepokea jumla ya **Shilingi Bilioni 2.4 (2,481,463,936)** sawa na **asilimia 62.4**. Katika fungu hili hakukutengwa fedha za miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati ilielezwu kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo zingetolewa toka katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano. Kamati imebaini kuwa fedha hizo za miradi ya maendeleo hazikutolewa kama zilivyokuwa zimehaiidiwa na hivyo kusababisha miradi kutokutekelezwa.

## **2.3 Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha kwa Mwaka 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyokuwa imetengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Ziara hii ilifanyika kuanzia tarehe 12 hadi 19 Machi, 2020 katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam. Miradi iliyotembelewa ni; -

- i. Mradi wa ujenzi wa Ofisi za Serikali Ihumwa-Dodoma;
- ii. Mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kisasa (*standard guage*) sehemu ya Dar es Salaam -Morogoro na Morogoro -Dodoma;
- iii. Mradi wa ujenzi wa barabara ya juu (*Ubungo Interchange*);
- iv. Mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni;
- v. Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka (BRT)
- vi. Mradi wa ujenzi wa bandari ya Dar es Salaam; na
- vii. Mradi wa Ujenzi wa daraja la mto Wami.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya miradi iliyokuwa katika ratiba ya Kamati haikutembelewa kutohana na mlipuko wa ugonjwa wa Corona (virusi vya *Covid 19*). Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa daraja la *Selander*, Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL) na Jengo la tatu la abiria (*terminal III*) katika Kiwanja cha Kimataifa cha Julius Nyerere.

### **i) Ujenzi wa Ofisi za Serikali- Mtumba, Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, mwezi Septemba, 2016, Serikali ilifanya maamuzi ya kuhamishia shughuli za Serikali jijini Dodoma kama sehemu ya kukamilisha ndoto ya siku nyingi iliyowekwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalim Julius Kambarage Nyerere mwaka 1973. Serikali ilitenga sehemu maalum eneo la

Mtumba jijini Dodoma ambako ilielekeza yajengwe majengo ya ofisi yatakayotumiwa na Wizara mbalimbali pamoja na baadhi ya taasisi zake. Mnamo mwezi Juni, 2018, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ulielekezwa na Serikali kufanya ubunifu na usanifu wa mji huu kwa kuzingatia mahitaji ya wizara husika. Wajibu wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika mradi huu ulikuwa ni Mshauri elekezi katika hatua za awali na usimamizi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa majengo yote 21 ya awali isipokuwa la TAMISEMI yalijengwa kwa gharama ya chini ya **Shilingi Bilioni 1** (VAT ikiwemo) bila kuhusisha kazi za nje na kazi za TEHAMA. Aidha, kutokana na ufinyu wa bajeti kazi za mtandao wa viyoyozi hazikufanyika kwa majengo yote.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kubwa katika mradi wa ujenzi wa Ofisi za Serikali ni Washitiri kutokumlipa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ada ya ushauri licha ya kuwa huduma husika zimetolewa. Mpaka Kamati ilipotembelea mradi huu mwezi Machi, 2020, Kiasi cha ada ya ushauri kilicholipwa ni **Shilingi Milioni 447.9 (447,904,180.85)** na deni liliosalia ni **Shilingi Bilioni 1.26 (1,260,437,182.44)**. Kwa mwenendo huu, Kamati inaona kwamba nguvu na kasi ya Wakala wa Majengo Tanzania vinazoroteshwa, na hivyo, kuathiri moja kwa moja utendaji kazi wa Wakala hasa ukizingatia Kamati imekuwa ikishauri mara kwa mara kuwa Wakala huu uweke mkakati wa kujidesha kibiashara na kuachana na utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Spika, kiambatisho Na. 1** kinaonesha mchanganuo wa Gharama za Ada ya Ushauri zilizolipwa na zinazodaiwa na Wakala wa Majengo Tanzania kwa Wizara zilizojenga Ofisi eneo la Mtumba, Dodoma

ii) **Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kisasa (standard guage) sehemu ya Dar es Salaam- Morogoro na Morogoro – Dodoma**

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (*standard guage*) ni mazuri kwani hadi

mwezi Machi, 2020 Kamati ilipotembelea mradi huu kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300), ujenzi umefika asilimia sabini na tano (75%). Shughuli zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa makalvati, ambao umefikia asilimia 97, ujenzi wa daraja refu katikati ya jiji la Dar es Salaam lenye jumla ya km 2.54 umefikia asilimia 85, wakati ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde umefikia asilimia 83.

Vilevile, mkataba umesainiwa kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa umeme wa SGR ambapo kazi imefikia asilimia 7. Kamati imejulishwa kuwa kwa kipande cha Dar es Salaam- Morogoro kazi zote zinatarajiwaa kukamilika ifikapo Juni, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu sehemu ya pili kutoka Morogoro hadi Makutopora -Dodoma (km 422), ambapo ujenzi umefikia asilimia 28 (28%). Kazi zinazoendelea ni pamoja na ukataji wa miinuko na ujazaji wa mabonde, usanifu wa njia, ujenzi wa mahandaki, pamoja na uthamini na uhakiki wa mali za wananchi watakaopisha mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa jumla, maendeleo ya mradi kutoka Dar es Salaam -Morogoro -Dodoma ni mazuri, kwani fedha kwa ajili ya malipo mbalimbali ya mradi zinatolewa kwa wakati na hakuna madai yoyote kwa Mkandarasi. Aidha, fidia mbalimbali kwa ajili ya maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa reli zinaaendelea kutolewa kadiri mradi unavyosogea. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuwa na wataalam wa kutosha wa ndani ili waweze kuwa na ujuzi wa kutosha kusimamia na kuendeleleza reli hii.

### **iii) Mradi wa ujenzi wa barabara ya juu (*Ubungo Interchange*)**

**Mheshimiwa Spika**, Ujenzi wa barabara za juu katika makutano ya eneo la Ubungo jijini Dar es Salaam (*Ubungo Interchange*) una lengo la kupunguza msongamano wa magari, kwa kutenganisha njia za barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia kwa kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 86** na Serikali imechangia fedha za fidia kwa waathirika wa Mradi. Kwa jumla maendeleo ya

iutekelezaji wa mradi hadi kufikia tarehe 29 Februari, 2020 yamefikia asilimia 70.

Kamati imefarijika kwa kujulishwa mradi huu umeajiri wazawa wengi ambapo jumla ya wafanyakazi wote ni 960 na wazawa ni asilimia 90. Daraja linatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2020.

**iv) Mradi wa ujenzi wa nyumba za Magomeni**

**Mheshimiwa Spika**, nyumba za Magomeni zilijengwa na Wakoloni mwishoni mwa miaka ya 1940 na mwanzoni mwa miaka ya 1950 kufuatia mahitaji ya Waafrika waliokuwa wanafanya kazi maeneo ya Oysterbay, Dar es Salaam. Mnamo tarehe 06 septemba 2016, Mhe Rais Dk. John Pombe Magufuli aliwatembelea waliokuwa wapangaji wa Magomeni hizi na kutoa ahadi ya kuwajengea makazi mapya. Lengo lilikuwa kuzipatia makazi bora familia **644** za waliokuwa wakazi wa nyumba hizo kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 20 (20,000,000,000)**. Mradi unajumuisha ujenzi wa nyumba za makazi zenye huduma zote za jamii, uazio, miundombinu na mandhari ya nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa ujenzi wa mradi huu ulianza tarehe 01 Octoba, 2016 ambapo ultarajiwa kumalizika katika kipindi cha mwaka mmoja (wiki 52) yaani 31 Septemba 2017. Hata hivyo, kutokana na changamoto mbalimbali zlikwemo za kifedha, mradi ulisimama kwa vipindi tofauti kuanzia mwaka 2017. Hivyo, kwa sasa, utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia Sabini (70%) ambapo zinahitajika **Shilingi Bilioni 14 (14,742,034,302.60)** ili mradi uweze kukamilika ifikapo mwezi June, 2020.

**v) Mradi wa Miundombinu ya Mabasi yaendayo haraka (BRT)**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Usafiri wa Haraka wa Mabasi (BRT) Awamu ya Pili, ni muendelezo wa mkakakati wa kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Dar es Salaam. Mkakati huu unalenga kujenga mradi katika awamu sita ambapo awamu ya Kwanza ilihuisha ujenzi wa barabara za Morogoro kutoka

Kimara hadi Kivukoni; Kawawa kutoka Magomeni hadi Morroco; na Mtaa wa Msimbazi kutoka Fire hadi Kariakoo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea ujenzi wa miundombinu ya Usafiri wa Haraka wa Mabasi (BRT) Awamu ya Pili ambao unahusisha barabara ya Kilwa (Kamata hadi Mbagala), barabara ya Changombe/Kawawa (Magomeni hadi Mgulani) na barabara ya Sokoine (Gerezani – *City hall*). Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za mkopo kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 141.71** kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Mfuko wa pamoja wa Maendeleo ya Afrika pamoja na Serikali kuchangia kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 17.61** kwa ajili ya fidia. Hivyo, jumla kiasi cha fedha za Mradi huu ni **Dola za Kimarekani Milioni 159.32**. Eneo lilikabidhiwa kwa mkandarasi tarehe 1 Machi 2019 na alianza kazi rasmi tarehe 6 Mei 2019. Kwa sasa, Mkandarasi amekamilisha kuandaa vifaa vya ujenzi na anaendelea na kazi za awali za barabara. Kwa ujumla, kazi imefikia asilimia 2.8 ukilinganisha na asilimia 15.6 iliyopangwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Kamati kukagua mradi wa barabara za mabasi yaendayo kasi awamu ya pili, Kamati iliitaka Serikali kuangalia upya changamoto inayoendelea kujitokeza katika awamu ya kwanza kwa kipande cha Magomeni hadi *Fire ambapo* mto Msimbazi umekuwa ukijaza maji barabarani kiasi cha magari ya mradi kushindwa kupita na yale yaliyopo katika kituo cha mabasi (*depot*) kuharibika kutokana na kuingia maji.

vi) **Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Dar es Salaam**

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kamati inaipongeza Serikali kwani ilipotembelea Bandari ya Dar es Salaam mnamo mwezi Machi, 2020 ilijionea maendeleo ya miradi ya ujenzi na upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam ikiwa inaendelea vizuri.

**Mheshimiwa Spika**, Uboreshaji wa gati namba 1-7 na ujenzi wa gati jipyaa la kushushia magari.

Kamati imejionea kazi zilizokamilika bandarini hususan ujenzi wa gati la kushushia magari (*RoRo Berth*), ujenzi wa gati namba 1, 2, na 3 pamoja na eneo la kuegesha magari. Kazi zinazoendelea ni uimarishwaji na kuongeza kina cha gati namba 4,5, na 6 ambapo mwishoni mwa mwezi Machi, 2020 Mkandarasi anatarajiwa kukamilisha gati namba 4 pamoja na eneo lote la kuegesha magari yanayoshushwa katika gati la *RoRo*. Kwa ujumla kazi ya maboresho ya gati namba 1-7 pamoja na gati jipya la *RoRo* umefikia asilimia 71.2.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu upanuzi na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli. Kamati imejulishwa kuwa Mkatuba katì ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania na Mshauri Mwelekezi wa kufanya Upembuzi Yakinifu juu ya namna bora ya kupanua na kuchimba ili kuongeza kina cha lango la kuingilia meli na eneo la kugeuzia meli ulisainiwa mwezi Desemba, 2015 na kukamilika mwezi Machi, 2017. Kazi ya usanifu wa awali ilianza mwezi Desemba, 2018 na kukamilika mwezi Juni 2019. Kwa sasa hatua za manunuzi kumpata Mkandarasi wa kazi hii zinaendelea na kazi zinatarajiwa kuanza mwezi Aprili,2020 na kukamilika ndani ya miezi 30.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu kuimarisha gati namba 8-11, Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua za kufanya tathimini ya zabuni ambapo kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina inatarajiwa kuanza mwezi Mei, 2020.

Aidha, Kamati imejulishwa kuwa awamu ya pili ya mradi wa uboreshaji wa bandari itajumuisha ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta pamoja na gati la mafuta pamoja na gati la kupakulia mafuta. Vilevile itahusisha ujenzi wa gati la makasha kuanzia gati namba 12-15, ujenzi wa gati la meli za kitalii na ujenzi wa gati kwa ajili ya meli za mwambao na Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia ilijiona eneo la Kurasini *Oil Jet* ambalo lilikuwa linaandaliwa kwa ujenzi na ukarabati wa eneo linalotarajiwa kufungwa *flow meter* ambapo Kamati ilijulishwa kuwa *flow meter* ya bandari ya Dar es Salaam ni

kati ya flow meter tatu zilizoingiwa mkataba wa manunuzi kwa ajili pia ya Bandari za Tanga na Mtwara ambazo zinatarajia hadi mwezi Julai, 2020 mitambo hiyo itakuwa imefungwa.

**vii) Mradi wa Ujenzi wa daraja la mto Wami**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati litembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa daraja jipya la Wami lenye urefu wa mita 510 upana wa mita 11.85 linalojengwa na Mkandarasi *Power Construction Corporation Ltd* kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 68**. Mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 28 Juni, 2018 na tarehe ya kumaliza kazi ni 21 Oktoba, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kujenga daraja jipya kwani daraja liliopo halikidhi mahitaji ya sasa kwa kuwa ni jembamba na lenye njia moja ambayo iko kwenye miinuko mikali na kona pamoja na changamoto ya wingi wa magari na hivyo kusababisha ajali mara kwa mara.

**2.4 Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua na kupitisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, Kamati ilitoa maoni na ushauri mbalimbali. Maoni na ushauri huo uligusa masuala muhimu kama vile Bandari, Reli, Viwanja vya Ndege, Barabara na Mawasiliano. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kati ya mambo yaliyoshauriwa, yapo ambayo Serikali imeyazingatia na mengine yanaendelea kuzingatiwa. Baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni pamoja na: -

**a) Sekta ya Uchukuzi**

i) Kuhusu ushauri wa ujenzi wa Reli ya Kati kwa kuzingatia kipaumbele kwenye reli yenye matarajio ya mzigo mkubwa ili kutengeneza mazingira ya Serikali kurudisha fedha zilizotumika ndani ya muda mfupi. Kamati imefarijika kujulishwa kuwa upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli ya SGR umekamilika kwa vipande vya Isaka –

Rusumo (Km 371) Tabora – Kigoma (Km 411), Keza - Ruvubu (Km36), na Kaliua – Mpanda - Karema (Km 321). Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa reli hizo kwa kiwango cha SGR.

- ii) Kuhusu Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuijendesha kisasa kwa kufunga vyombo vyao kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufuatiliaji wa mizigo kwa wateja, udhibiti mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Kamati imejulishwa kuwa Shirika la Reli Tanzania limeanza ufungaji wa mifumo ya kielektroniki ya ukatishaji tiketi (*e-ticketing*) umeanza kutumika ambapo hadi Februari, 2020 jumla ya stesheni 71 zimefungiwa mfumo huo kwa lengo la kuboresha ukusanyaji wa mapato.
- iii) Kuhusu Serikali kushirikisha sekta binafsi au kupata mikopo yenye gharama nafuu ili kuharakisha ujenzi wa reli nchini. Kamati imejulishwa kuwa Serikali inatarajia kujenga reli ya Mchuchuma – Liganga (Km 1,092. Baada ya mshauri mwelekezi kushindwa kutekeleza kazi ya kuunadi mradi, taratibu za kuvunja mkataba zimeendelea na imeundwa Kamati ya wataalam kushughulikia chini ya utaratibu wa *PPP*. Kuhusu reli ya Tanga – Arusha – Musoma (Km 1,108) kwa mwaka 2019/2020 taratibu za kuajiri mtaalam wa uwekezaji atayeandaa andiko la kuunadi mradi kwa wawekezaji kwa mfumo wa ubia (*PPP*).
- iv) Kuhusu Serikali kurasimisha Bandari Bubu zilizopo katika mwambao wa Bandari ya Hindi na katika Maziwa Makuu ili kuongeza mapato. Kamati imejulishwa kuwa zoezi hilo limekamilika na jumla ya Bandari **437** zisizo rasmi zimetambuliwa ambapo inajumuisha bandari **132** katika mwambao wa Bahari ya Hindi, bandari **204** katika ziwa Victoria, bandari **93** katika ziwa Tanganyika na Bandari **8** katika ziwa Nyasa. Hata hivyo, tayari fedha zinaendelea kukusanya kutokana na Bandari bubu kwa kutumia vifaa vyao POS na mtandao wa POAS ambapo wastani wa **shilingi milioni mia tano (Tzs 500,000,000)** zimekuwa zikipatikana kwa mwezi.

- v) Kuhusu Serikali kuhakikisha Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki. Kamati imejulishwa kuwa hadi sasa jumla ya Viwanja vya Ndege 12 vimepata Hati Miliki. Hata hivyo, Kamati inaona kasi ya utekelezaji wa ushauri huu si yakuridhisha.
- vi) Kuhusu Shirika la Ndege la Tanzania- ATCL kujitangaza kwenye Vyombo rasmi vya Kimataifa ambavyo huonesha safari za ndege dunia nzima. Kamati imejulishwa kuwa, ATCL imeingia kwenye mfumo wa mauzo ya tiketi kimataifa (*Global Distribution System*) ambapo hadi Februari, 2020 imeweza kuuza tiketi katika jumla ya nchi 27 kupitia mfumo huo. Pia imejunga katika mitandao mikubwa minne (4) ya kuuza tiketi kimataifa ambayo ni *Galileo* uliojikita zaidi katika Bara la Afrika, Amadeus uliojikita zaidi katika Bara la Ulaya na Amerika, Traval Sky uliojikita zaidi katika nchi ya China na Sabre uliojikita zaidi pia katika Bara la Ulaya na Amerika

**b) Sekta ya Ujenzi**

**Mheshimiwa Spika**, katika Sekta ya Ujenzi, ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni;

- i) Kuhusu Wakala wa Ufundini na Umeme (TEMESA) kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri mwendo mrefu kwenda kufanya matengenezo kutokana na Wilaya zingine kuwa umbali mrefu kutoka Makao Makuu ya Mkoa.

Kamati imejulishwa kuwa, Serikali imeelekeza magari yote ya Serikali yatengenezwe katika karakana za Wakala badala ya kupelekwa katika karakana binafsi. Hivyo, Wakala umeanza kutekeleza mpango wa kusogea huduma zake katika wilaya zilizo umbali mrefu kutoka karakana za mikoa ambapo mwezi Machi, 2020, Wakala ulikuwa umeanzisha karakana mbili (2) katika Wilaya ya Kilombero katika mji wa Ifakara na katika Wilaya ya Kahama. TEMESA inatarajia kuanzisha karakana sita (6) katika Wilaya za Same, Simanjiro, Kyela, Ukerewe, Masasi na Chato.

Aidha, Serikali kupitia TEMESA imeagiza "*Mobile Workshop Truck*" sita na vitendea kazi vyake zitakazotoa huduma katika mikoa ya Dodoma, Mwanza, Tabora, Mtwara, Mbeya na Arusha.

ii) Kuhusu Serikali kuwajengea uwezo wataalam wa ndani katika miradi mikubwa inayotekelizwa, Kamati imejulishwa kuwa katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya wataalam thelathini na sita (36) kutoka katika Wizara na Taasisi zake wamejumuishwa katika ujenzi wa miradi mikubwa nchini ili kupata mafunzo kwa vitendo kwenye miradi hiyo inayohusu ukarabati wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege kupitia *TANROADS Engineering Consulting Unit (TECU)*. Aidha, Wahandisi wahitimu 120 wameshikizwa kwenye miradi kwa ajili ya kuwajengea uwezo chini.

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mpango ya kuungeza ushiriki wa wanawake katika kazi za barabara ambazo kwa kiasi kikubwa zimekuwa zikitazamwa kuwa ni kazi za wanaume. Katika mwaka fedha 2020/21 Wizara imepanga kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake ya juu ya kufanya matengenezo na ukarabati wa barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi na kuwasaidia kusajili kampuni zao za ujenzi pamoja na kufuatilia kwa karibu kazi za barabara zinazofanywa na wanawake wakandarasi.

iii) Kuhusu kununua na kujenga mizani za kisasa ambazo zinapima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (*Weight in Motion*) na kuzifunga katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa kupima magari. Kamati imejulishwa kuwa zimejengwa mizani tano za kisasa zinazopima magari yakiwa kwenye mwendo (WIM) katika vituo vyenye msongamano mkubwa wa magari vya Njuki (Singida), Nala (Dodoma), Dakawa (Morogoro), Wenda (Iringa) na Mpemba (Songwe).

### **c) Sekta ya Mawasiliano**

i) Kuhusu ushauri wa kuhakikisha minara yote iliyojengwa kwa ufadhili wa Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote

(UCSAF) inawekwa mabango yatakayoonesha ushiriki wa Serikali katika uwekezaji huo na kuifanya jamii kutambua mchango wa Serikali katika kusambaza mawasiliano nchini. Kamati imejulishwa kuwa utekelezaji wa ushauri huu umeanza ambapo hadi mwezi Aprili, 2020 minara mia moja na moja (101) iliyopo katika maeneo mbalimbali nchini imewekwa mabango kati ya minara mia saba na nne (704) na zoezi bado linaendelea.

ii) Kuhusu ushauri wa kuongeza rasilimali watu kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF ili Mfuko uweze kusimamia, kukagua na kutembelea ipasavyo maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa Minara na kuhakikisha kazí hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa. Hatua zimeanza kuchukuliwa ambapo Kamati imejulishwa kuwa kibali cha kuajiri watumishi 21 imetolewa ambapo hadi sasa watumishi 13 wameajiriwa na kuripoti kazini na inatarajiwaa ikama iliyoidhinishwa kukamilishwa kwa wafanyakazi wote wapya kujiunga na Mfuko.

iii) Kuhusu kuondolewa kwa Shirika la Posta Tanzania katika orodha ya Mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kuijidesha kwa tija. Kamati imejulishwa kuwa, Serikali kuitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imesaini Hati ya kuliondoa Shirika la Posta katika orodha ya Mashirika yanayosubiri kurekebishwa pamoja na kutoa tangazo la Serikali Na. 614 la tarehe 23 Agosti, 2019.

iv) Kuhusu umiliki wa Mikongo binafsi, ambapo baadhi ya Makampuni ya Simu yamekuwa yakimiliki Mikongo yao sambamba na Mkongo wa Taifa, Kamati imejulishwa kuwa Serikali imewasimamisha watoa huduma hao.

v) Kuhusu changamoto ya madeni ambayo TTCL inaidai Serikali na Taasis zake ambapo Kamati imekuwa ikishauri kuweka mikakati ya ukusanyaji wa madeni hayo, Kamati imejulishwa kuwa TTCL imeunda kitengo maalum cha kufuatilia madeni.

## 2.5 Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

### 2.5.1 Makisio ya Ukusanyaji wa Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Sekta ya Ujenzi (fungu 98) inatarajia kukusanya mapato ya jumla ya **shilingi 70,000,000.00** kutoka Idara ya Utawala na Rasilimali Watu, Huduma za Ufundu na Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi.

Aidha, kwa upande wa Sekta ya Mawasiliano (fungu 68) inatarajia kukusanya jumla ya **shilingi 30,000,000,000** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kutokana na mauzo ya huduma za Mkongo wa Taifa wa mawasiliano pamoja na mauzo ya vitabu vya tenda.

### 2.5.2 Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi Triliioni 4.9 (4,979,110,240,000.00)**.

**Mheshimiwa Spika**, jedwali lifuatalo linaonesha mchanganuo wa fedha zinazoombwua.

### Jedwali Na.2, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida Na Miradi ya Maendeleo kwa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

SEKTA	MATUMIZI YA KAWAIDA	MRADI YA MAENDELEO	JUMA
Ujenzi (Fungu 98)	38,774,425,000.00	1,766,303,604,000.00	1,805,078,029,000.00
Uchukuzi (Fungu 62)	90,710,109,000.00	3,067,667,636,000.00	3,158,377,745,000.00
Mawasiliano (Fungu 68)	4,654,466,000.00	11,000,000,000.00	15,654,466,000.00
JUMAKU	134,139,000,000	4,844,971,240,000	4,979,110,240,000

*Chanzo; Taarifa ya Makadirio ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2020/2021 ni yakuridhisha kwani fedha zimeongezeka kwa takribani **Shilingi bilioni 16 (15,813,410,837.00)** ukilinganisha na fedha zilizoidhinishwa mwaka wa fedha **2019/2020** ambazo zilikuwa **Shilingi Trilioni 4.9 (4,963,297,839,163.00)**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuipa kipaumbele sekta ya Miundombinu na kuongeza bajeti ya Sekta hii mwaka hadi mwaka.

**2.6 Mambo Mengine yaliyojitekeza wakati wa Kupita na Kuchambua Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka 2019/2020 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2020/2021**

a) **Sekta ya Uchukuzi**

i. **Uimarishwaji wa Mtandao wa Reli Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na dhamira ya dhati ya kufufua na kuimarisha miundombinu ya reli nchini ambapo katika kipindi cha miaka mitano yaani 2016 hadi 2020, Serikali imeweka uimarishwaji wa miundombinu ya reli kuwa kipaumbele kikuu kwani imekuwa ikitenga na kutoa fedha kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha Kimataifa (*standard gauge*). Ulinganifu wa fedha hizi umekuwa wa kuridhisha ambapo kwa miaka mitano mfululizo zimeidhinishwa na kutolewa takribani jumla ya **Shilingi Trilioni 8** ya fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha Kimataifa. Mchanganuo wa fedha hizi ni kama ifuatavyo; 2016/17 (**Trilioni 1**), 2017/18 (**Bilioni 900**), 2018/19 (**Trilioni 1.5**), 2019/20 (**Trilioni 2.5**) na 2020/21 (**Trilioni 2.1**).

**Mheshimiwa Spika**, hii ni hatua nzuri na ya kupongezwa kwani, ujenzi wa reli hii yenye kasi ya km 160 kwa saa itasaidia kurahisisha usafiri hasa wa abiria na usafirishaji wa mali ghafi hatimaye kuchochaea ukuaji wa viwanda na hata kuongeza

Pato la Taifa. [*Utekelezaji wa mradi huu unapatikana katika taarifa ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kipengele cha 2.3 (ii) na 2.4(i)*].

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuwa na uwekezaji mkubwa unaofanyika katika reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge*, ni muhimu pia kuendelea kuboresha na kuimarisha reli ya kati ya zamani (*meter guage*). Katika kufuatilia utekelezaji huu, Kamati imejulishwa kuwa njia ya reli ya kati ya zamani kwa mwaka 2020/2021 ukarabati unaendelea kwa kutandika reli nzito ya ratili 80 kwa yadi katika umbali wa Kilomita 970 kati ya Dar es Salaam na Isaka, ujenzi wa madaraja na makalvati, ujenzi wa sehemu ya kuunganisha treni (*Marshalling yard*), ununuzi wa vifaa ikiwemo ununuzi wa injini 3 na mabehewa 44.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijulishwa kuwa ukarabati wa njia ya zamani ya kipande cha Tanga-Moshi (350Km) umekamilika na huduma za usafirishaji wa mizigo ulizinduliwa mwezi Julai, 2019. Aidha, Hadi Kamati ilipokutana na Serikali mwezi Machi, 2020 ukarabati wa kipande cha Moshi-Arusha (86Km) umefikia asilimia 95.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mfuko wa reli ulianzishwa kwa lengo la kuboresha mtandao wa reli ya kati kwa kujenga reli mpya ya *standard gauge*, kukarabati reli iliyopo na kugharamia tafiti mbalimbali za njia mpya za reli. Katika mwaka 2019/2020 mfuko wa reli ilitengewa jumla ya **Shilingi bilioni 255.7** fedha za ndani. Hadi kufikia Februari, 2020, fedha za Mfuko zilizopokelewa ni jumla ya **Shilingi bilioni 159,703.28** sawa na **asilimia 62**.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Mfuko wa Reli umetengewa jumla ya **shilingi milioni 289,678.923** fedha za ndani kwa ajili ya kuunda upya vichwa vya treni 9, kurejesha na kuimarisha huduma za usafiri wa treni kwa reli ya Kaskazini (Tanga – Arusha), kugharamia kazi za upembuzi na usanifu wa awali wa ujenzi wa reli, ukarabati wa karakana, stesheni na majengo ya reli, kuchangia katika kugharamia ujenzi wa reli ya Standard Gauge, na matengenezo ya reli ya kati.

## ii. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Mamlaka hii ni kuendeleza, kuendesha shughuli za bandari, kutangaza huduma za bandari, kushirikisha na kusimamia sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini. Kutokana na jiografia ya nchi yetu ambapo imezungukwa na takribani nchi saba ambazo hazina bandari (*land locked countries*) na hivyo kuifanya Mamlaka ya Bandari kutoa huduma kwa mizigo inayoingia na kutoka ndani ya nchi na ya kuelekea nchi za Burundi, Rwanda, DR Congo, Uganda, Zambia, Malawi na Zimbambwe.

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, hatuna budi kuhakikisha kuwa changamoto mbalimbali za miundombinu ya bandari zetu inarekebishwa kwa kufanya ukarabati au kujenga upya. Vilevile kushughulikia changamoto za kiutendaji ambazo zinazorotesha na kusababisha nchi kupoteza wateja waliokuwa wakitumia bandari hususan bandari ya Dar es Salaam na kuhamia katika bandari zingine shindani za Mombasa- nchini Kenya, Beira-nchini Msumbiji, nchini Durban-Afrika Kusini na Walvis Bay-huko Namibia.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya bandari ya Dar es Salaam [*maendeleo ya bandari ya Dar es Salaam yameelezwa katika kipengele cha 2.3 (vii)*] bado upo umuhimu mkubwa wa kuhakikisha bandari zingine kuu na zile za maziwa makuu zinakuwa na mazingira ya miundombinu ya kuridhisha ili kwa pamoja na kwa kushirikiana na bandari ya Dar es Salaam kuweza kusafirisha na kupokea mzigو mkubwa jambo ambalo litaleta faida kubwa na kuimarisha uchumi wan chi hasa ukizingatia mwelekeo wa Tanzania ya viwanda.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari ya Tanga, kazi ya ukarabati wa gati Namba 2 katika Bandari ya Tanga imefikia asilimia 86. Aidha, kwa upande wa uchimbaji wa kuongeza kina cha kuingilia meli, hadi kufikia Februari, 2020, mradi umefikia asilimia 98 na kutarajiwa kukamilika Machi, 2020. Vilevile, Mamlaka ya Bandari imeendelea na maandalizi ya

ujenzi wa gati la kupokelea mafuta kutoka Uganda katika eneo la Chongoleani (Tanga).

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari ya Mtwara, ujenzi wa gati moja lenye urefu wa mita 300 linalojengwa kwa ajili ya kuhudumia shehena mchanganyiko limekamilika kwa asilimia 60 na mradi unatarajiwa kukamilika Oktoba,2020. Kukamilika kwa ujenzi wa gati hili kutasaidia sana katika kusafirisha shehena za korosho, makasha, saruji na shehena nyingine zinazotokana na bidhaa zinazotumika katika shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi baharini. Hata hivyo, ni vema mipango ya ujenzi wa magati mengine matatu ikaendelea ili kufungua fursa kubwa zaidi kwa Mtwara kwani itahudumia pia mzigo mkubwa wa wanchi za Malawi na Msumbiji kwani bandari hii ina kina kirefu, eneo kubwa la upanuzi na pia kuwa karibu zaidi na nchi hizo.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu bandari za maziwa makuu, miradi ya ujenzi wa magati, majengo ya utawala, majengo ya abiria, kuhifadhi mizigo, uongezaji wa kina, usawazishaji wa eneo, matanki ya maji, vyoo na vyumba vyta walinzi zinaendelea kujengwa katika bandari zilizopo katika Maziwa Makuu ambazo ni bandari ya Magarini-Muleba, bandari ya Nyamirembe, bandari ya Lushamba , Bandari ya Karema, Ujenzi wa Gati la Sibwesa/Kalya , Ujenzi wa Gati la Lagosa, Ujenzi wa Gati ya Kabwe – Nkasi , Ujenzi wa Gati za Mbamba Bay, Manda na Matema katika Ziwa Nyasa ambaupopo katika hatua ya upembuzi yakinifu. Mingi ya miradi hii inatarajiwa kukamilika mwaka huu 2020.

**Mheshimiwa Spika**, ni muhimu wakati ukarabati na upanuzi wa bandari unaendelea, ni muhimu pia kwa bandari zilizo katika kipaumbele vyta Serikali kama vile Bandari ya Mbegani Bagamoyo na Bandari ya Mwambani Tanga kuanza kutekelezwa. Pia kukamilisha malipo ya fidia kwa wanachi waliopisha upanuzi wa bandari hizi ili kuepuka migogoro isiyio ya lazima wakati mradi utakapoanza.

### **iii. Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwani katika mwaka 2019/2020 imeiwezesha Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL kufanya ukarabati mkubwa wa meli mbili za MV Victoria na MV Butiama katika Ziwa Victoria ambazo ukarabati wake unakamilika mwishoni mwa mwezi Machi, 2020. Pia kujenga meli mpya ya kubeba abiria na mizigo inayotarajiwa kukamilika mwezi Januari, 2021 pamoja na Chelezo katika Ziwa Victoria ikiwa ni nyenzo wezeshi ya kujengea meli na kukarabati meli zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, MSCL ilitengewa **Shilingi Bilioni 70** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 imepokea **Shilingi Bilioni 39** sawa na **asilimia 56** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Katika mwaka wa fedha (2020/2021) zimetengwa fedha kiasi cha **Shilingi Bilioni 85** za kufanya ukarabati mkubwa wa meli za MV Umoja, MV Serengeti, MT Nyangumi na MT Ukerewe katika Ziwa Victoria pamoja na Meli za MV Liemba na MT Sangara katika Ziwa Tanganyika na Bahari ya Hindi.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto kwa Kampuni ya Huduma za Meli ni uhaba wa rasilimali watu hususani kada ya watendaji wa melini (mabaharia) ambapo changamoto hii itajitokeza zaidi pindi ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli mbili zitakazokamilika. Uhaba wa vyombo (meli) kwa ajili ya kuhudumia soko kubwa la usafirishaji katika Ziwa Tanganyika na uhaba wa miundombinu kama vile Ofisi kwa ajili ya kuwezesha shughuli za utendaji wa MSCL.

### **V. Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kununua ndege kutoka ndege moja iliyokuwepo 2016 hadi kufikia ndege nane. Kuongezeka kwa ndege kumeiwezesha Kampuni ya Ndege ya Tanzania kuongeza mtandao wa safari za ndani ya nchi kutoka vituo tisa (9) hadi vituo kumi na tatu (13) ambapo kwa sasa inafanya safari

katika vituo kumi na moja (11) sababu ya kupisha maboresho ya kiwanja cha ndege cha Mtwara na Songea.

Aidha, ongezeko la ndege limewezesha ATCL kuongeza safari za Kikanda kuelekea Entebbe-Uganda, Bujumbura-Burundi, Johannesburg- Afrika Kusini, Harare-Zimbabwe na Zambia-Lusaka. Vilevile, safari za Kimataifa katika vituo vya Bangkok-Thailand, Bombay-India na pia kukamilisha taratibu zote za kuanza safari za kwenda China – Guangzhou ambapo safari zinatarajiwa kuanza kabla ya mwezi Juni, 2020. Changamoto kubwa kwa safari za Kimataifa imekuwa ugonjwa wa Corona unaoenezwa na virusi vya *Covid 19* ambapo imesababisha kusimama kwa safari zote za Kimataifa.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuendeleza juhudhi hizo mwaka wa fedha 2019/2020 zilitengwa **Shilingi Bilioni 500** ambapo hadi kufikia mwezi Februari, 2020 zimepokelewa **Shilingi Bilioni 310** sawa na **asilimia 62**. Aidha, katika mwaka 2020/21, zimetengwa **Shilingi Milioni 450,000.00** fedha za ndani kwa ajili ya kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa Ndege mbili (2) mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner, kulipa malipo ya awali ya ununuzi wa ndege moja ya mizigo (*freighter*) aina ya Boeing 767-300 na kulipa malipo ya mwisho ya Ndege mbili (2) mpya aina ya Airbus A220-300.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto ya sasa ya ugonjwa wa Corona ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri utendaji wa Shirika kwani Shirika limesimamisha safari zake za Kimataifa, Shirika limeendelea kukabiliwa na changamoto ya madeni yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma yanayofikia **Shilingi bilioni 180** ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 ATCL ilitengewa **Shilingi bilioni 35.865**. Changamoto nyingine ni ukosefu wa taa za kuongozea ndege katika baadhi ya viwanja vya ndege jambo linalosababisha ndege kutua wakati wa mchana tu.

- b) **Sekta ya Ujenzi**
  - i) **Miradi ya ujenzi wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya Ujenzi kupitia Wakala wa Barabara ina jukumu la kusimamia ujenzi, ukarabati na

matengenezo kwenye mtandao wa barabara kuu na za Mikoa zeny urefu wa jumla ya kilomita 35,000 ambapo kati ya hizo kilomita 12,786 ni barabara kuu na kilometra 22,214 ni barabara za mikoa. Lengo ni kuwezesha barabara ziweze kupitika kwa urahisi na hatimaye kusaidia ukuaji wa uchumi wa nchi kama ilivyofafanuliwa katika Mipango Mikakati ya Kitaifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo 2015, Mpango wa Taifa wa Miaka Mitano na Mikakati ya Kisekta.

**Mheshimiwa Spika**, Sekta hii kwa sasa inakabiliwa na changamoto ya mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini mfululizo ambazo kwa kaisi kikubwa zimesababisha mafuriko ambao yameharibu sana barabara na madaraja. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 fedha za dharura zilikuwa zimekadiriwa jumla ya **Shilingi bilioni 15**. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 zimetengwa jumla ya **Shilingi Bilioni 28.2** kwa ajili ya matengenezo ya dharura ya barabara. Kamati ianipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake na kuongeza fedha za dharura.

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa barabara nchini (TANROADS) umeendelea kukabiliwa na changamoto ya fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa kiasi kidogo au kutokontaktewa kwa wakati na hivyo kusababisha baadhi ya Makandarasi kusimama kufanya kazi na wengine kutekeleza kazi kwa kasi ndogo jambo ambalo linasababisha baadhi ya miradi kutokilika katika muda uliokusudiwa. Hadi kufika mwezi Machi, 2020 baadhi ya miradi ya barabara ilikuwa haijapata fedha ni Dar es Salaam-Chalinze-Morogoro Express Way, barabara ya Korogwe-Handeni, Mwanza -Shinyanga Boarder, Arusha -Namanga, Singida -Babat i-Minjingu, Same-Mkumbara-Korogwe.

Aidha, baadhi ya barabara fedha zilitolewa ni kidogo ukilinganisha na kiasi kilichoidhinishwa na muda uliobaki kabla ya kumaliza mwaka wa fedha 2019/2020. Barabara hizo ni Dodoma -Iringa, Handeni -Kibereshi -Kibaya-Singida, Kitumbi-Segera- Tanga, Msimba- Ruaha Mbuyuni-Mafinga, Kisarawe -Mlandizi, Ipole -Rungwa na Magole-Mziha-Handeni.

**Mheshimiwa Spika**, vilevile, lengo mojawapo la Sekta ya Ujenzi ni kuhakikisha Miji yote Mikuu na Mikoa inaunganishwa kwa barabara za lami. Hata hivyo, bado kuna Mikoa mingine ambayo haijaunganishwa kwa barabara za lami hususan Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Rukwa, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera, Mbeya -Makete- Njombe, Lindi- Morogoro, Lindi-Ruvuma, Arusha-Mara, Singida-Mbeya, n.k. Aidha, baadhi ya barabara za Mikoa ziko katika hali isiyoridhisha na nyingine hazipitiki wakati wa mvua hivyo kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

## **ii) Malipo ya Makandarasi na Wahandisi Washauri**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kazi kubwa inayofanywa na makandarasi na Wahandisi Washauri katika ujenzi hususan kwenye miradi ya barabara. Kamati imejulishwa kuwa hadi kufikia Februari, 2020 Serikali imetoe kiasi cha **Shilingi bilioni 615,449,139,848.53**. Aidha, deni la Makandarasi na Wahandisi Washauri wa miradi ya barabara ni **Shilingi bilioni 950**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwashirikisha makandarasi wa ndani katika ujenzi wa miradi ya barabara ambapo kiasi cha **Shilingi milioni 403,164.774** za Mfuko wa barabara zimetumika kuwalipa makandarasi wa ndani. Aidha, kuhusu changamoto ya makandarasi wa ndani kuwa na uwezo mdogo wa mtaji hivyo kushindwa kushiriki kikamilifu katika fursa za kazi kutokana na masharti ya upatikanaji wa dhamana za zabuni, dhamana za ushiriki wa kazi na mitaji ya kuwezesha kufanya kazi kutoka mabenki. Kamati imejulishwa kuwa Bodi imeendelea kuendesha Mfuko wa kusaidia Makandarasi –*Contractors Assistance Fund-CAF* ambao unatoa dhamana za zabuni na malipo ya awali kwa makandarasi wa ndani walio katika daraja la chini na la kati. Mfuko umeendelea kuwa na mtaji wa **Shilingi bilioni 3.75** kwa mwaka 2019/2020. Aidha, idadi ya wanachama imepungua kutoka 1,186 mwaka 2018/2019 hadi kufikia 1,126 mwaka 2019/2020. Idadi ya wanachama imepungua kutokana na zoezi la kufuta makandarasi waliokosa sifa kwa mujibu wa sharia.

**Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Februari, 2020 Bodi ya Usajili wa makandarsi imesajili makandarasi wapya 508 na hivyo kufanya jumla ya makandarasi waliosajiliwa kufikia 10,822. Aidha, jumla ya miradi 2,065 ilikaguliwa ambapo miradi 548 sawa na asilimia 27 ilipatikana na mapungufu mbalimbali ambapo makandarasi waliokutwa na mapungufu walichukuliwa hatua mbalimbali kwa mujibu wa sheria ikiwemo kutozwa faini, kupewa onyo, kusimamishwa kufanya biashara ya ukandarasi na kufutiwa usajili.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuwapa kipaumbele makampuni na wahandisi wazawa kwani Kamati imejulishwa kuwa hadi mwezi Februari 2020, jumla ya wahandisi waliosajiliwa katika ngazi mbalimbali ni 27,739 na makampuni ya kihandisi kuwa 359 ambapo wahandisi 25,401 ni Wahandisi wa ndani na 2,338 ni wahandisi wa kigeni. Aidha, makampuni ya ushauri wa kihandisi ya kizalendo ni 246 na ya kigeni ni 113.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Serikali inawapa kipaumbele makandarasi na wahandisi pamoja na Makampuni yao ya ndani katika utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini. Hili ni jambo jema kwani fedha na malipo mbalimbali yanayofanyika hubaki katika mzunguko wa fedha nchini na kusaidia kuinua pato la mtu mmoja mmoja na hata Taifa,

### **iii) Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

**Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Wakala wa Nyumba Tanzania ni pamoja na usimamizi na uendeshaji wa Miliki yote ya Serikali (Viwanja/maeneo ya Ardhi yaliyotengwa kwa matumizi ya Serikali, Majengo ya Ofisi za Taasisi mbalimbali za Serikali, Nyumba za Viongozi wa ngazi za juu Serikalini, Nyumba za kuwauzia Watumishi wa Umma, Nyumba za kupangisha, pamoja na uwekaji wa samani bora kwenye nyumba za Viongozi) na utoaji wa huduma za ushauri na ujenzi wa majengo ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwani kwa kuitia Wakala wa Majengo Tanzania-TBA imeweza

kufanikisha miradi mbalimbali mikubwa kama vile ujenzi wa Ofisi za Serikali Mtumba-Dodoma, Ujenzi wa Nyumba za Magomeni Kota na ujenzi na ukarabati wa nyumba za viongozi pamoja na watumishi wa umma nchini.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wakala huu, Wakala umekuwa unakabiliwa na changamoto kubwa ya malimbikizo ya madeni ya ujenzi, ushauri, pango la nyumba pamoja na mauzo ya nyumba. Kwa kiasi kikubwa Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasisi za Serikali ambapo hadi mwezi Machi, 2020 madeni yaliyohakikiwa na kuwasilishwa Hazina ili yalipwe ni jumla ya **shilingi bilioni 17**.

Changamoto zingine ni pamoja na mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi wa umma ukilinganisha na kasi ndogo ya ujenzi, riba kubwa kwenye taasis za fedha, kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika vifaa, mbinu na ubunifu kwenye sekta ya ujenzi inaugharimu Wakala fedha nydingi za kuwapatia mafunzo wataalam wake ili waendane na mabadiliko hayo na vifaa vya ujenzi vyenye gharama kubwa katika soko kusababisha kuongeza gharama za ujenzi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imebaini changamoto vongozi wengi wa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kukaimu nafasi zao za uongozi. Hali hii hairidhishi na inasababisha viongozi hao wasijiamini katika kufanya maamuzi muhimu ya taasisi.

#### **iv) Wakala wa Ufundu na Umeme (TEMESA)**

**Mheshimiwa Spika**, Wakala wa Ufundu na Umeme Tanzania (*The Tanzania Electrical Mechanical and Electronics Services Agency-TEMESA*) ni Wakala muhimu sana kwani unatoa huduma ya matengenezo ya magari, mitambo, pipipiki, mifumo ya umeme, majokofu na viyoyozi. Vilevile Wakala huu unasimamia ukodishaji wa magari na mitambo ya kusaga kokoto pamoja na kutoa ushauri katika nyanja mbalimbali za kihandisi Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwani imeelekeza

magari yote ya Serikali kutengenezwa katika karakana za TEMESA badala kupelekwa katika karakana binafsi ambazo ziliikuwa ni za gharama kubwa. Hata hivyo, ili utekelezaji huu ufanyike ni muhimu sana kwa Wakala kukamilisha kusogeza karibu karakana zake ikiwa ni pamoja na mobile workshop truck, kuajiri wataalam waliobobea katika ufundi wa magari, vifaa na mitambo ya kisasa pamoja na kuboresha mazingira ya karakana.

v) **Miradi ya Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha sekta ya usafiri wa anga, pamoja na ununuzi wa ndege, miradi mbalimbali ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika Mikoa mbalimbali kama vile Kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Kilimanjaro, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe na viwanja vya ndege vya Mikoa.

**Mheshimiwa Spika**, miradi hii inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti na kutokontaktewa fedha kwa wakati. Katika mwaka wa fedha 2019 /2020, jumla ya **Shilingi 102,192,375,000.00** zilitengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya viwanja vya ndege. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani ziliikuwa **Shilingi 40,000,000,000.00** na fedha za nje ni **Shilingi 62,192,375,000.00**. Hadi kufika mwezi Februari, 2020 jumla ya **Shilingi 61,205,521,015.40** ndizo zilizokuwa zimetolewa sawa na **asilimia 61** ya fedha zote za miradi ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Kati ya fedha hizo zilizotolewa fedha za ndani ni **Shilingi 8,413,556,960.18** sawa na **asilimia 21**. Kwa upande wa fedha za nje zilizotolewa ni **Shilingi 52,791,964,055.22** sawa na **asilimia 85**.

**Mheshimiwa Spika**, fedha zilizotolewa hadi Februari, 2020 ni kidogo ukilinganisha na miradi iliyokuwa imepangwa kutekelezwa ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa kati ya miradi kumi na tatu (13) ya viwanja vya ndege iliyokuwa imeidhinishiwa fedha 2019/2020, ni miradi minne tu (4) tu ndio iliyopata fedha ambayo ni Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, Msalato,

Mwanza na Jengo la tatu la abiria-kiwanja cha Julius Nyerere Dar es Salaam. Miradi ambayo haikuwa imepata fedha ni Kiwanja cha ndege cha Kigoma, Mpanda, Shinyanga, Tabora, Sumbawanga, Songwe, Arusha, Kilimanjaro na Bukoba.

c) **Sekta ya Mawasiliano**

i) **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa TCRA imeendelea na ujenzi wa mifumo na uratibu wa huduma za Mawasiliano kwa kutumia mtambo wa Mfumo wa kusimamia mawasiliano ya simu (*Tele-Traffic Management System-TTMS*), ambao umechangia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni zilizopo katika udhibiti wa mawasiliano na kuhakikisha Serikali inapata mapato stahiki kutokana na huduma za mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai,2019 hadi Januari, 2020 Mfumo wa TTMS pamoja na mambo mengine umewezesha kutambua mapato na takwimu za miamala ya fedha mtandao kwa mashirika yote ya simu ambapo jumla ya miamala 2,004,196,139 imepita katika mitandao ya simu na wastani wa fedha zilizopita ni **Shilingi 12,202,700,000,000**.

Aidha, katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2020, mapato kutokana na Mtambo wa TTMS ambayo yamelipwa katika mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 7,275,340,578.44**. Kwa ujumla Mfumo huu umeongeza ufanisi katika usimamizi wa Sheria ikiwa ni pamoja na kwenda sambamba na mabadiliko ya kasi yanayotokea katika Sekta ya Mawasilinao duniani.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu usajili wa laini simu, Mamlaka ya Mawasiliano kwa kushirikiana na watoa huduma za mawasiliano imeendelea na zoezi la usajili wa laini za simu kwa njia ya biometria ambapo hadi Machi, 2020 zimesajiliwa laini 35,813,455 sawa na asilimia 83.1 ya laini zote 43,072,868 zilizounganishwa mtandaoni. Aidha, kwa upande wa laini

zilizozimwa hadi kufikia tarehe 10 Machi, 2020 ni laini 5,886.286. Laini ambazo bado hazijasajiliwa kwa alama za vidole lakini zilisajila kwa kitambulisho cha mpiga kura na kitambulisho cha Mzanzibar Mkaazi ni 7,259,413.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa zoezi la usajili wa namba za simu ni endelevu kwani mahitaji ya kuwa na laini ya simu kwa ajili ya mawasiliano yataendelea kuwepo siku hadi siku, na kutokana na changamoto iliyojitokeza ya wananchi wengi kutokufikiwa ama kutokufanikisha usajili kutokana na kukosa vitambulisho vya Taifa toka NIDA na hivyo kusababisha wananchi wengi kusajili laini kwa kuazima vitambulisho ni jambo ambalo si sahihi. Ni vema sasa Mamlaka ya Mawasiliano kwa kushirikiana na NIDA pamoja na watoa Huduma kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu ili wananchi wasajili laini za simu kwa kutumia vitambulisho vyao.

### **iii) Mradi wa Postikodi na Misimbo za Posta**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ni muhimu sana kwani ni mradi ambao utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kuweza kufanyika kwa urahisi na kuokoa muda. Mionganoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na; huduma za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi, usafiri na usalama, huduma za dharura kama zima moto, magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa mradi huu, bado kumeendelea kuwapo changamoto ya kutokutolewa fedha za mradi kwa wakatai au fedha za mradi kutokutolewa kabisa. Kwa miaka minne mfululizo mwenendo wa utoaji fedha katika mradi huu sio wa kuridhisha. Katika mwaka wa Fedha 2016/2017 mradi huu uliidihiishiwa **shilingi bilioni 3** ambapo kiasi kilichotolewa kilikuwa **milioni 95** tu; katika mwaka wa fedha wa 2017/18 iliidihiishiwa **shilingi billion 3** ambapo hadi kufikia Machi 2018, hakuna kiasi chochote kilichotolewa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 iliidihiishiwa **shilingi bilioni 4** lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2019 kiasi kilichopokelewa ni **shilingi milioni 796** na mwaka wa fedha

2019/2020 mradi huu haukutengewa fedha, hata hivyo Kamati ilijulishwa kuwa fedha za maendeleo ya mradi huu zingetolewa katika fedha za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano jambo ambalo halikufanyika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Kamati haioni dhamira ya dhati ya Serikali katika kutekeleza mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa.

iv) **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF)**

**Mheshimiwa Spika**, lengo la kuanzishwa kwa Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*Universal Communication Service Access Fund- UCSAF*) ni kupeleka huduma ya mawasiliano maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara ambapo usambazaji wa Mawasiliano unafanywa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana na sekta binafsi hususan Makampuni ya simu kama vile TIGO, VODACOM, HALOTEL.

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Mawasiliano kwa wote toka kuanzishwa kwake umefanikiwa kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 704 zenye Vijiji 2,501 na wakazi zaidi ya milioni tano. Serikali kuititia UCSAF mnamo mwezi Januari, 2020 imesaini mkataba na makampuni ya simu ili kupeleka huduma za mawasiliano katika kata 252 zenye vijiji 555 na wakazi zaidi ya milioni tatu ifikapo ifikapo mwezi Oktoba, 2020. Hata hivyo, pamoja na mafaniko hayo ya usambazaji wa mawasiliano nchini, Kamati imebaini changamoto kubwa ni upungufu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kusambaza mawasiliano katika maeneo yenye uhitaji wa huduma hizo kwa wakati.

v) **Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha miaka minne, kumekuwepo na juhudhi mbalimbali za kuhakikisha TTCL inamudu ushindani wa kibiashara na kuzidi kuimarika. Jitihada hizo ni pamoja na Serikali kununua hisa asilimia 35 zilizokuwa zinamilikiwa na Kampuni ya *Bhart Airtel*; Serikali kuridhia

kubadilisha deni ililokuwa inaidai TTCL kiasi cha **Shilingi bilioni 76.6** kuwa mtaji wa Shirika; Serikali kuchukuwa deni la ada ya udhibiti ambalo TTCL ilikuwa ikidaiwa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA kiasi cha cha **shilingi bilioni 25**; TTCL kuruhusiwa kutumia rasilimali zake kama dhamana ya mkopo ambapo Shirika limechukwa dhamana ya mkopo benki ya **Shilingi bilioni 66** kat i ya **Bilioni 96** na kuwekeza katika teknolojia ya 4G LTE ya simu za mkononi; TTCL kupewa kipaumbele wakati wa kugawa masafa; na TTCL kupewa majukumu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya sekta ya mawasiliano kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na kupeleka mawasiliano vijiji kutoka Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote(UCSAF).

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 20019/2020, Shirika lilikuwa limekadiria kuzalisha na kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi Bilioni 196.8 (196,832,435,039)** kutokana na huduma za Shirika kama vile simu, data na kupangisha maeneo kwa ajili ya vyombo vya mawasiliano. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa makadiria hayo hayakufikiwa kwani Shirika hadi mwezi Februari, 2020 limekusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 60.1 (60,137,125,692.84)** sawa na **asilimia 30.5**. Kamati imefahamishwa kuwa sababu za TTCL kutokufikia lengo la makusanyo ni kutokana na kukosa fedha kwa ajili ya uwekezaji kutoka kwenye vyanzo vyake ikiwemo mkopo kutoka benki. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2020/2021, TTCL inatarajia kukopa kiasi cha **Dola za Marekani Milioni 15** kwa ajili ya uwekezaji ambao utaliwezesha Shirika kuongeza Mapato.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla hali ya utendaji wa Shirika la Mawasiliano Tanzania-TTCL bado si yakuridhisha kwani bado Shirika linakabiliwa na changamoto ya mtaji mdogo wa uwekezaji usiyoendana na mabadiliko ya teknolojia na kushindwa kukabiliana na ushindani wa soko la Mawasiliano. Changamoto zingine zinazolikabili Shirika la Mawasiliano Tanzania ni pamoja na: -

- a) Madeni ya zamani ambayo yanatokana na kutumia huduma mbalimbali ambayo mengi yao Shirika linaidai

Serikali na Taasis zake ambapo hadi mwezi Machi, 2020 kiasi cha **Shilingi billioni 30** zinadaiwa;

- b) Kutokukamilika kwa Kanuni ambazo zitatoa maelekezo ya namna ya Shirika kuendesha na kusimamia miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano;
- c) Shirika kuwa na mtaji mdogo kwa ajili ya uwekezaji na kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayokwenda sanjari na kasi ya uwekezaji;
- d) Sheria ya manunuzi kwa mashirika ya umma ambayo inaleta urasimu unaokinzana na ushindani wa kibashara; na
- e) Uharibifu na ukataji wa miundombinu ya Mkongo unaotokana na shughuli za binadamu, hujuma, na shughuli za maendeleo kama ujenzi na upanuzi wa barabara.

#### **vi) Shirika la Posta Tanzania -TPC**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka utaratibu wa kupeleka fedha kwa Shirika la Posta kwa kila kipindi cha miezi mitatu kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi wastaa fu wa liliokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki ambapo deni hilo hadi kufikia mwezi Januari 2020 limebaki **Shilingi billioni 6,521,748,190**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kuptitia Sheria ya Msamaha (*Amnesty*) kufuta deni la Shirika la **Shilingi Bilioni 12** liliokuwa limetokana na tozo, riba, na adhabu. Kamati bado inaona umuhimu wa Serikali kufuta deni liliosalia la takribani **Shilingi billioni 15** ili kupunguza mzigo wa madeni kwa Shirika na kwa kuzingatia kuwa Shirika hili bado linakabiliwa na changamoto ya kuwa na mtaji hasi na hivyo kushindwa kumudu ushindani uliopo kayika huduma ya kusafirisha barua, vipeto na rejestra ndani na nje ya nchi.

## **SEHEMU YA TATU**

### **3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

#### **3.1 Bajeti ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha mwaka hadi mwaka kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa miaka minne mfululizo Sekta hii imekuwa ikitengewa fedha kiasi cha kuridhisha ambapo mwaka 2017/2018 **Shilingi triliioni 4.5**, 2018/2019 **Shilingi triliioni 4.2**, mwaka 2019/2020 **Shilingi triliioni 4.9** na kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 **Shilingi triliioni 4.9**. Kwa kuangalia fedha hizo zilizoidhinishwa ndani ya miaka mine mfululizo, ni dhahiri kuwa, Serikali imeipa kipaumbele cha kutosha sekta ya miundombinu nchini ili kuharakisha maendeleo ya nchi. Hivyo, Kamati inazidi kusisitiza ushauri wake kuwa fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuhakikisha miradi inatekelezwa katika muda uliopangwa na hatimae wananchi wananaufaika.

#### **3.2 Sekta ya Uchukuzi**

1. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa reli nchini Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa;

a) Ujenzi wa reli ya kati uende sambamba na ununuzi wa vichwa na mabehewa ya treni, ili mradi utakapokamilika mnamo mwezi June, 2020 kwa sehemu ya Dar es Salaam hadi Morogoro huduma za usafirishaji zianze kufanyika;

b) Serikali kuzingatia kuwaajiri wahandisi wakutosha wa ndani wenye fani mbalimbali muhimu na zinazohitajika kwa uendeshaji wa reli pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali ya uendeshaji wa treni na uratibu wa matumizi ya reli mpya ili mradi utakapokamilika pawepo na wataalam wa ndani ambao watakuwa tayari kuupokea na kuusimamia vizuri;

- c) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli na kuondoa usumbufu kwa wananchi, Shirika la Reli Tanzania-TRC liweke alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi;
- d) Shirika la reli lianz kuijendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliasi wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kuijendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;
- e) Juhudi ziendelezwe kuhakikisha ujenzi wa reli nchini unafanywa kwa ushirikiano na sekta binafsi au mikopo yenye gharama nafuu kwani itasaidia kuharakisha zoezi zima la ujenzi wa reli nchini na Serikali itaweza kuweka fedha za ndani kwa ajilli ya utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo.

**2. Mheshimiwa Spika**, kuhusu Bandari Kamati inashauri yafuatayo;

- a) Serikali kwa kupitia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Waziri wa Fedha pamoja na Waziri wa Viwanda na Biashara waitishe kikao cha pamoja na wadau mbalimbali wa bandari nchini ili kubadilishana mawazo na kuona namna nzuri ya uendeshaji wa bandari nchini na kuifanya bandari iweze kuijendesha kibashara na kuvutia wafanyabiashara wengi kuitumia jambo ambalo litaongeza mapato ya Serikali;
- b) Serikali iharakishe kukamilisha bandari za nchi kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Fela-Mwanza, Katosh-Kigoma, King'ori-Arusha, Isaka-Kahama, na Inyala-Mbeya ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar es salaam kwa ajilli ya kutoa mizigo;
- c) Sulala la wadau wote wa bandari kuhamia kwenye jengo moja liwe jambo la lazima ili kurahisisha na kuongeza ufanisi wa bandari;

- d) Serikali iharakishe kutafuta mwekezaji ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza. Vile vile, Serikali ilipe fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyi ya lazima wakati mradi huu utakapoanza;
- e) Ni muhimu sana Serikali kuhakikisha mwezi Juni, 2020 kama ilivyoleza katika taarifa za utekelezaji wake kuwa inakamilisha mchakato wa kupata *flow meter* na kuifunga katika bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Na kwakuwa imeelezwa kuwa zimeagizwa *flow meter* zingine mbili za bandari ya Tanga na Mtwara, ni muhimu nazo zikamilishwe na kufungwa kwa muda ili kuweza kujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandarini;
- f) Kuhusu Bandari ya Mtwara, kasi ya uanzishwaji wa bandari ya hii iende sambamba na ujenzi wa njia ya treni; na
- g) Kwakuwa Serikali sasa imerasimisha bandari bубу na kuanza kukusanya mapato, ni vema na muhimu kuboresha mazingira ya miundombinu ya bandari hizo ili umuhimu wa urasimishaji na mapato yanayopatikana yawefeze kuonekana kwa uhalisi wake kwa wamiliki na watumiaji wa bandari hizi.

**3. Mheshimiwa Spika**, kuhusu Kampuni ya Huduma za Meli-MSCL; Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali ijipange kutengeneza meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kuijendesha kibashara;
- b) Kutohakikisha uwekezaji unaofanyika sasa wa kukarabati na ujenzi wa meli mpya katika Maziwa Makuu, ni vema Serikali iendelee kulipa mishahara ya kwa wafanyakazi wa Kampuni ya Meli Tanzania hasa kwa kipindi hiki cha mpito mpaka Kampuni hii itakapoweza kuijendesha; na
- c) Serikali iharakishe ujenzi wa meli katika ziwa Tanganyika na kukarabati meli iliyopo ya MV Liemba kwani kijiografia

bandari hii inapakana na nchi ya Kongo (Rubumbashi) ambako kuna mizigo mkubwa wa biashara ambao utaiwezesha Serikali kupata mapato.

4. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu TAZARA, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iharakishe mazungumzo baina ya nchi wabia wa reli ya TAZARA kuhusu kuimarisha reli hii kutokana na umuhimu wake katika kukuza uchumi. Serikali kwa kushirikiana na nchi wabia wa TAZARA ikamilishe itifaki ya 16 kuhusu mkopo kutoka china kwa ajili ya kusaidia kuiboresha TAZARA;

b) Serikali ikamilishe manunuzi ya injini na vipuri pamoja na mitambo ya kusaidia kuzalisha kokoto na mataluma ya zege kwenye mgodi wa kokoto uliopo Kongolo- Mbeya na kusaidia viweze kuingia nchini kwa haraka ili vianze kutumika kwa ajili ya kuongeza pato la TAZARA;

c) Serikali iharakishe mchakato wa ajira za watumishi wa TAZARA ili kupata wafanyakazi wenyewe ujuzi na weledi wa kutosha kuliongezea Shirika uwezo kwani wafanyakazi wengi wamemaliza muda wao na kustaafu;

d) Serikali ihakikishe inatoa kwa wakati fedha za ujenzi wa kipande cha reli chenye urefu wa kilometra 18 kutoka Chikola kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kuipatia TAZARA mapato ya kutosha; na

e) Kamati inaendelea kusositiza Serikali kulipa madeni yote ya wafanyakazi wastaafu wa TAZARA.

5. **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA: -

a) Kamati inaendelea kushauri Serikali kuipatia Mamlaka hii angalau **asilimia 50** ya maduhuli yatokanayo na viwanja vya ndege ili Mamlaka ya Viwanja vya Ndege- (TAA) iweze

kutekeleza majukumu yake ipasavyo na kuongeza kasi ya ujenzi na ukarabati; pamoja na, uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Aidha, Mamlaka izitumie vizuri fedha za mapato ya ndani zinazotokana na utuaji wa ndege, uegeshaji wa ndege na magari katika maegesho ya viwanja ili ziweze kutumika katika shughuli za uendeshaji wa viwanja vya ndege;

- b) Serikali ihakikishe Viwanja vyote vya Ndege na mali zake zote zinakuwa na Hati Miliki; Aidha, kuhakikisha Viwanja vya Ndege vyote vinawekewa uzio kwa ajili ya kuepusha hatari zinazotokana na wanyama au binadamu wanaokatiza katika maeneo ya viwanja vya ndege pamoja na; kuepuka migogoro ya ardhi na wananchi wanaoishi pembezoni mwa viwanja hivyo; na
- c) Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA) na wadau wengine wa viwanja vya ndege kama Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), wafanye vikao vya pamoja na kuangalia namna ya kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili katika sekta ya usafirishaji wa anga.

## **6. Mheshimiwa Spika, Kuhusu Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL**

a) Japokuwa Kamati imefahamishwa kuwa kwa sasa ATCL imekuwa na marubani wa kutosha ambapo marubani 78 wamehitimu mafunzo na kupata sifa stahiki za kuendesha ndege. Ni muhimu sana kwa Serikali kuweka mikakati ya kuhakikisha inalinda marubani wake wasichukuliwe na mashirika mengine;

b) Wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege Tanzania- ATCL kupewa mafunzo ya huduma kwa wateja, mara kwa mara, ili kuweza kutoa huduma nzuri wakati wote. Hii itasaidia Kampuni kushindana na makampuni mengine yanayofanya biashara ya usafiri wa anga; na

c) Shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake.

### **3.3 Sekta ya Ujenzi**

1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Barabara-TANROADS, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri ufuafuatao:-

a) Serikali itekeleze Sera yake ya kuunganisha Mikoa yote kwa barabara za lami. Baadhi ya Mikoa hiyo ni Lindi - Morogoro, Morogoro -Mlimba -Madeke Njombe, Lindi - Songea, Kigoma -Katavi-Tabora-Kagera, Mbeya -Makete - Njombe, Arusha-Mara. Aidha, miradi ya barabara inayoendelea ipewe kipaumbele na ile ambayo haijaanza ifanyiwe upembuzi yakinifu;

b) Serikali ijenge kwa kiwango cha lami barabara muhimu zifuatazo:-

i. Barabara zinazounganisha nchi yetu na nchi nyigine hususani Mikoa ya Kagera, Kigoma, Katavi, Ruvuma na Mtwara;

ii. Barabara zinazounganisha Makao Makuu ya Mikoa kama vile Kigoma-Kasulu-Kagera, Katavi – Kigoma – Tabora;

iii. Barabara za Kiuchumi, kama vile, Mtwara – Newala – Masasi, ambayo ni barabara inayopita katika maeneo ambayo yanazalisha korosho kwa wingi ukizingatia kwamba zao la korosho linachangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa mikoa ya kusini na nchi kwa ujumla; barabara ya Handeni - Kibereshi -Kibaya- Singida ambayo ni barabara yenye tija kiuchumi kutokana na kuwapo kwa bomba la mafuta linalounganishwa na nchi ya Uganda. Aidha, umuhimu wa makubaliano ya nchi ya Rwanda kutaka kutumia bandari ya Tanga;

iv. Barabara zinazounganisha Wilaya na Makao Makuu ya Mikoa, hizi pia zipewe kipaumbele ili kuwezesha wakulima kuweza kuyafikia masoko ya mazao; na

v. Barabara zilizohaidiwa za Marais waliostaafu na Rais aliye madarakani.

c) Serikali kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi na Bodi ya Usajili wa Makandarasi kuendelea kutoa mafunzo kwa wahandisi washauri na Makandarasi wa ndani ili waweze kusimamia na kutekeleza ujenzi wa barabara kikamilifu. Aidha, kuhamasisha wakandarasi wazalendo kujunga na kuomba zabuni kwa utaratibu wa ubia na kupata dhamana kupitia mfuko Maalum wa kutoa dhamana ya kusaidia makandarasi wadogo na wa kati. Vilevile, kuhamasisha zaidi kwa kuendelea kutoa mafunzo kwa Wahandisi na Makandarasi wanawake.

d) Sekta ya Ujenzi isimamie ipasavyo Sheria ya barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari, kama runinga, magazeti, redio na simu za mkononi. Aidha, vyombo vinavyohusika na usimamizi wa sheria ya barabara kuwa macho wakati wote na endapo kutaonekana mtu anajenga ndani ya hifadhi ya barabara kuzuiwa na kubomolewa mapema. Aidha, Wakala wa Barabara iendelee na zoezi la kuweka alama za mipaka katika maeneo ya barabara ili kuepusha usumbufu wakati maeneo hayo yanapohitajika;

e) Serikali iendelee na juhudu kufunga mizani ya kisasa zinazopima magari huku yakiwa kwenye mwendo katika vituo ambavyo vinamsongamano mkubwa wa magari kwenye mizani ili kuokoa muda, fedha na usumbufu kwa wasafiri na wasafirishaji;

f) Serikali iongeze kasi ya ujenzi wa Vituo vya Pamoja vya Ukaguzi ambavyo vinajengwa katika Ukanda wa Kati na Ukanda wa Dar es Salaam ili kurahisisha usafirishaji wa bidhaa pamoja na kuokoa muda wa mizigo kukaa barabarani;

g) Wakati wa ujenzi wa barabara ni vema wakala wa barabara wahakikishe wanaweka sehemu maalum kwa ajili ya kuvukia mifugo, kwani, maeneo mengi ambayo mifugo

inatumia kuvuka kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa barabara;

- h) Wakati wa ujenzi wa barabara zipo taasisi nyingi za Serikali zinapeleka madai kwa wakandarasi wa barabara kwa ajili ya ulipiaji malighafi zinazotumika kwenye ujenzi, kama vile Wizara ya Madini (kokoto, mawe, kifusi), Wizara ya Maji na umwagiliaji (vima vyta maji), Wizara ya Viwanda na Mazingira (uharibifu wa mazingira); pamoja na, ushuru unaotozwa na Halmashauri za mijii; gharama hizi zinaongeza gharama za ujenzi wa barabara, hivyo, Kamati inashauri Serikali isamehe kodi hizo kwani zinalipwa na Serikali na si wakandarasi; na
- i) Serikali ihakikishe inaweka mikakati ya kupunguza msongamano ya magari kwenye miji inayokua kwa kasi, kama vile, Mbeya, Mwanza, Arusha na hivi sasa Dodoma. Miji hii imekuwa ikitabiliwa na msongamano mkubwa wa magari na kusababisha kutumia muda mwingi kusafiri kutoka sehemu moja kwenda nydingine

2) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu ujenzi wa viwanja vyta ndege, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Serikali ikamilishe kwa haraka ujenzi unaoendelea wa kiwanja cha ndege cha Mwanza hasa ujenzi wa jengo la abiria, mizigo; pamoja na jengo la kuongozea ndege;
- b) Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa Viwanja vyta Ndege ili miradi hii iweze kukamilika kwa wakati na kuepuka riba ambazo hutokana na miradi kutokamilika kwa wakati;
- c) Ni muhimu Serikali iharakishe kujenga na kuimarishe Viwanja vyta Ndege vitakavyozalisha mapato na kuijendesha; kama vile, Kiwanja cha Ndege cha Moshi (kwa ajili ya Utalii), Kiwanja cha Ndege cha Iringa (kwa ajili ya Utalii) na Kiwanja cha Ndege cha Mtwara (kwa ajili ya uwekezaji);

- d) Serikali ilipe fidia mapema na kwa wakati kwa wananchi wanaopisha ujenzi mathalani kiwanja cha Ndege cha Msalato, Songea, Lake Manyara, Simiyu na Msalato; na
- e) Serikali iweke taa za kuongozea ndege hususan katika Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe-Mbeya ili ndege ziweze kutua na kuruka wakati wote.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Wakala wa Ufundu na Umeme-TEMESA, Kamati inashauri yafuatayo: -

- a) Wakala uendelee kukamilisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo;
- b) Wakala uchukue hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo, kwa kiasi kikubwa, inazidai taasisi za Serikali ili Wakala huu uweze kijidesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na
- c) Serikali iajiri wataalam waliobobea kwenye fani ya ufundu wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nydingi magari ya Serikali yamekuwa yaktengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

### **3.4 Sekta ya Mawasiliano**

- 1) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu mradi wa Anuani Makazi na Misimbo ya Posta, Kamati inasisitiza ushauri ufuatao; -
  - a) Serikali itoe kipaumbele kwa mradi wa anwani za makazi na misimbo ya posta kwani mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Aidha, Kamati inashauri Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi mkubwa;

- b) Ili mradi huu uwe wa kisasa na kuendana na wakati, ni vema wataalam wakajifunze nchi zingine na kuona namna nchi nyingine zilivyofanya na kuweka mfumo huu; na
- c) Wakati zoezi la kuweka majina ya mitaa linaendelea, ni muhimu Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka ulinzi wa nguzo dhidi ya wahalifu wanaochukua vyuma chavu.

2) **Mheshimiwa Spika**, Kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA, Kamati inashauri; -

- a) Kamati inaendelea kusisitiza kuongezwa kasi ya zoezi la usajili wa namba za simu ili kuwa na taarifa za kila mmiliki au mtumiaji wa simu kwa ajili ya usalama na kutekeleza Sheria ya Mawasiliano na Posta. Vilevile, Serikali iongeze kasi ya kutoa vitambulishao vya Taifa ili kila Mtanzania aweze kutambuliwa na kuepuka udanganyifu unaofanywa kwenye mitandao;
- b) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania- TCRA, ikabiliane na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, ambapo kumekuwa na ongezeko la uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi zikae pamoja na kuona namna ya kushughulikia changamoto ya uhalifu wa kimtandao na kuwasaidia wananchi kuwabana wahalifu bila ya kuwa na urasimu;
- c) Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania isimamie Makampuni ya Simu nchini na kudhibiti gharama za mitandao, kwani gharama za baadhi ya mitandao zipo juu ukilinganisha na mitandao mingine; na
- d) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na kuimarisha usalama wa watu na mali zao.

3) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa:-

- a) Serikali ipitie na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo ya ardhi yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia kwani fedha zitakazopatikana kutokana na malipo ya kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;
- b) Serikali iweke mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakanil ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki ya kukosa taarifa za nchi yao;
- c) Serikali izipe kipaumbele na kuhakikisha kunawekwa minara ya mawasiliano Wilaya na Halmashauri mpya zote;
- d) Serikali ihakikishe inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (*Infrastructure Sharing*) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;
- e) Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano kwa haraka;
- f) Mfuko wa Mawasiliano kutafuta vyanzo vingine vya fedha ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa fedha na kuhakikisha miradi mingi inatekelezwa na kufikia maeneo mengi yenye uhitaji wa mawasiliano kama ilivyopangwa;

- a) Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara view salama;
  - b) Kuongeza rasilimali watu kwenye Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ili Mfuko uweze kusimamia ipasavyo kwa kukagua na kutembelea maeneo ambayo Serikali imewekeza fedha kwa ajili ya ujenzi wa minara na kuhakikisha kazi hiyo imefanyika na mawasiliano yanapatikana kama ilivyokusudiwa; na
  - c) Kwa kuwa teknolojia imeendelea na wananchi wengi wamekuwa na mwamko katika huduma za TEHAMA; na hivyo, kuhitaji huduma ya *data (mtandao)*. Ni muhimu sana, minara yote illyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe na uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya (afya mtandao), elimu mtandao n.k
  - d) Serikali ifanye jitihada za kuweka na kusambaza mawasiliano nchini katika maeneo mengi zaidi hasa mipakani kwani mawasiliano ni maendeleo na hasa sasa ambako nchi yetu inawekeza katika viwanda. Kuwepo kwa mawasiliano kutarahisisha usafiri na uuzwaji wa malighafi na mazao hata kuinua kipato cha Mwananchi mmoja mmoja na hata Taifa kwa ujumla;
- 4) **Mheshimiwa Spika**, kuhusu Shirika la Posta Tanzania, Kamati inashauri Serikali iendelee kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa deni hilo kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika.
- 5) **Shirika la Simu Tanzania- (TTCL Corporation)**
- a) Pamoja na TTCL kuunda kikosi cha kufuatilia madeni ambayo yameripotiwa hadi tarehe 30 Machi, 2020 kufika

Jumla ya **Shilingi Bilioni 30** ambayo kwa kiasi kikubwa zinadaiwa Wizara/Taasisi na Mashirika ya Serikali, Kamati inaona mkakati huu bado hautakuwa na nguvu ikiwa Serikali yenyewe hajiweka mkazo kwa vyombo vyake kulipa madeni hayo. Hivyo, ni muhimu sana kwa Serikali kuchukuwa hatua na kusisitiza vyombo vyake kulipa madeni ya mawasiliano yanayodaiwa na TTCL.

b) Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa;na

c) Kwa kuwa TTCL ni Shirika la Umma, lipewe Mamlaka ya kumiliki na kuendesha Mkongo wa Taifa badala ya ilivyo sasa ambapo Mkongo unasimamiwa na kuendeshwa na TTCL lakini mapato yake yanaelekezwa Wizarani.

#### **4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, sekta ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni muhimu sana katika kuharakisha na kuchochaea maendeleo ya nchi. Miradi iliyo ndani ya Sekta hii ni mikubwa na inahitaji fedha nydingi ili yote iweze kukamilika kwa wakati uliopangwa. Hivyo, Kamati inaona ni muhimu Serikali kushirikisha Sekta binafsi katika kutekeleza miradi hii mikubwa.

#### **4.1 Shukrani**

**Mheshimiwa spika**, napenda kuwashukuru wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango waliyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti pamoja na kuandaa taarifa hii. Naomba kuwatambua wajumbe wa Kamati hii kwa kuwataja majina kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Moshi Seleman Kakoso, Mb- Mwenyekiti
2. Mhe. Hawa Mchafu Chakoma, Mb- M/ Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Matala Makani, Mb
4. Mhe. Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mb
5. Mhe. Susan Limbweni Kiwanga, Mb
6. Mhe. Joyce John Mukya, Mb

7. Mhe. Asha Mshimba Jecha, Mb
8. Mhe. Susan Chogisasi Mgongokulima, Mb
9. Mhe. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb
10. Mhe. Nuru Awadhi Bafadhili, Mb
11. Mhe. James Francis Mbatia, Mb
12. Mhe. Saul Henry Amon, Mb
13. Mhe. Ahmed Makbhuty Shabiby, Mb
14. Mhe. Dkt. Chuachua Mohamed Rashid, Mb
15. Mhe. Dkt. Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mb
16. Mhe. Bhagwanji Maganlal Meisuria, Mb
17. Mhe. Dua William Nkurua, Mb
18. Mhe. Raphael Japhary Michael, Mb
19. Mhe. Charles Muhangwa Kitwanga, Mb
20. Mhe. Rukia Kassim Ahmed, Mb
21. Mhe. Nassor Suleiman Omar, Mb
22. Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mb
23. Mhe. Munde Abdalah Tambwe, Mb
24. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb
25. Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb

**Mheshimiwa spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni na Ushauri kwa niaba ya wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kwa namna ya pekee naomba niwashukuru Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mheshimiwa Eng. Isack Alloyce Kamwelwe, (Mb) akisaidiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Justus Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias John Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch. Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Katibu Mkuu Mtsaifu Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonaz. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Vilevile, shukrani ziende kwa watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakati wote wa kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati

wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu. Michael Lucas Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Gerald Singano Magili pamoja na Makatibu wa Kamati Ndugu Hosiana John Mvunta na Ndugu Janeth Julian Malangu, Msaidizi wa Kamati Ndugu. Modesta Michael Kipiko pamoja na wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

---

**Moshi Selement Kakoso**  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE**  
**YA MIUNDOMBINU**

4 Mei, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti wetu wa Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, sitaweza kumwita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni wa Wizara ya ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa sababu taarifa hii haikuwa imewekwa mbele yetu; kwa hiyo, hawezi kuitwa kuisoma.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tutaanza uchangiaji. Nitataja majina ya Wabunge ambao watachangia kutokea

Msekwa ili kama wapo humu ndani waelekee Msekwa kupunguza kukimbiakimbia. Mheshimiwa Yahaya Omari Massare atachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Mbaraka Dau Kitwana atachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa, Msekwa; Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Msekwa; Mheshimiwa Desderius John Mipata, Msekwa; Mheshimiwa Bangwanji, Msekwa; na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Msekwa.

Baada ya kuwatangaza hao watakaochangia kutokea Msekwa tutaanza na Mheshimiwa Rashid Shangazi halafu Mheshimiwa Silinde ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuwa mzungumzaji wa kwanza katika Wizara hii. Kwanza nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri anayesimamia eneo hili la Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, lakini pamoja na wasaidizi wake, Manaibu Waziri wote wawili kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaifanya na kwa kweli kazi hii inaonekana yenze maana sana kwa Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nami nitoe mchango wangu katika maeneo kadha katika Wizara hii nikianza na eneo la mawasiliano, bado kuna shida ya mawasiliano kwa baadhi ya vijiji vyetu katika Halmashauri ya Lushoto kwa sababu ya jiografia ya milima, bado kuna maeneo ambayo hayana mawasiliano ya kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara kadhaa nimempa Mheshimiwa Naibu Waziri maeneo haya ambayo yana hilo tatizo. Kwa maana hiyo, anayo. Sasa naomba tuweke msukumo, tunaposema mawasiliano kwa wote halafu kuna watu tunawaacha nyuma katika eneo hili inakuwa hatutendi haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana yale maeneo ya Kata ya Malindi, Kijiji cha Makose ambacho bado hakina mawasiliano, Kata ya Rangwi eneo lile la Kijiji cha Longoi bado mawasiliano hayapo na Kata ya Lukosi

katika Kijiji cha Kiho na katika Kata ya Mnalo katika Kijiji cha Kikumbi ambacho kinapakana na Wilaya ya jirani ya Mkinga kwa ndugu yangu Mheshimiwa Kitandula kule bado mawasiliano siyo rafiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kwa upande wa Shirika la TTCL. Wanafanya kazi nzuri sana ambayo inahitaji kupongezwa lakini bado tunawaomba sasa na wenyewe wafike katika Milima ya Usambara. Bado hatujawaona kule kabisa. Kwa hiyo, ni vizuri wajengewe uwezo kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na wenyewe waweze kufika pale ili waweze kuboresha mawasiliano hasa haya ya kizalendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la barabara Mkoa wa Tanga, mpaka sasa hivi tunavyozungumza bado mvua zinaendelea kunyesha. Mvua hizi zimeanza tangu mwaka 2019 mwezi wa Kumi na kwa bahati nzuri Naibu Waziri Mheshimiwa Kwandikwa alifika eneo mahususi la Mlalo na kuona adha ambayo wananchi wameipata hasa baada ya mafuriko na maporomoko.

Kwa hiyo niombe sana, kupitia bajeti hii alituahidi kwamba ataangalia kila linalowezekana na shemeji yangu Waziri ananisikia hapo, kwamba angalau barabara ile ya kutoka Lushoto kwenda Lukozi mpaka Mlalo ijengwe japo kwa kiwango cha kilometra kumi kila mwaka wa bajeti ili angalau eneo hili liondokane na hiyo adha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunazungumza hivyo? Ni kwa sababu eneo hili ndiyo eneo ambalo linakwenda kwenye uzalishaji wa matunda na mbogamboga na mazao haya yanaharibika kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo inapotokea tu utelezi kidogo maana yake magari hayawezi kutembea, basi wananchi hawa wanapata hasara. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri amekuja pale ameahidi tukampiga mpaka na magoti pale na wananchi wakapiga vigelegele, naomba ahadi ile akaitimize ili na sisi mambo yetu yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili pia la barabara nikukumbushe eneo la barabara hii ya kutoka Mlalo kwenda Mng'aro, *Umba Junction* na kwenda Mkomazi na kupitia Mnazi ambako huku inakwenda kuungana na barabara inayokwenda Same Mashariki kwa mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango, naamini atakuja kuunganisha hapa. Hii nayo inaunganisha Mikoa ya Kilimanjaro na Tanga kwa hiyo ni barabara muhimu sana na pia inapita pembezoni mwa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi. Kwa maana hiyo ikikamilika moja kwa moja tu inakwenda kuleta hamasa katika ukuzaji wa utali katika eneo hili la Bonde la Umba.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kuzungumza ni kuboresha Uwanja wa Ndege wa Tanga. Nasi tunaona wivu wenzetu wa Mwanza, Songea, Mbeya na kwingineko wanapotumia hizi bombadia. Kwa hiyo na sisi tunatamani kule Tanga uwanja wetu wa mkoa ule uboreshwe ili na sisi tuweze kurahisisha shughuli hizi za usafirishaji pamoja na usafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama utafahamu hata Mradi wa Bomba la Mafuta unakwenda kuishia pale Chongoleani, Tanga. Tunaamini kwamba uwekezaji huu utavutia watu wengi na watu hawa, hasa wa kimataifa wasinge pendu kutumia muda mrefu barabarani. Kwa hiyo tunaamini kwamba uwanja wa ndege ukiboreshwu na tukapatia ndege za abiria na zenyewe zikatua katika Uwanja wa Ndege wa Tanga zitasaidia kupunguza gharama ambazo sasa hivi tunachajiwa gharama kubwa kwa sababu tunatumia hizi ndege ndogo ambazo zinaingia abiria wachache.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni uboreshaji wa Bandari ya Tanga; tunawashukuru sana. Bandari ile kina kimeongezeka na tunaona sasa meli kubwa za mafuta zinaweuka nanga pale. Niombe tu kwamba pamoja na maboresho ya kina cha bandari basi tuangalie na maeneo ya kuhifadhia mizigo. Kwa sababu bandari hii sasa inatumika zaidi kwa ukanda wa kaskazini na pia mashariki, ningetamani sana kuona kwamba tunaboresha pia miundombinu mingine

kwa maana ya ma-godown ya kuhifadhia mizigo, lakini na miundombinu mbalimbali katika eneo lile ili iweze kuvutia mizigo mingi zaidi. Ikiwezekana hata mizigo ambayo inakwenda nchi jirani za Uganda, *Southern Sudan* na Mashariki ya Kongo kuititia reli hii ambayo sasa imefufuliwa ya kutoka Tanga kwenda Kilimanjaro mpaka Arusha na baadaye tukija kwenye lile tawi la kwenda mpaka Musoma ikifika kwenye Ziwa Victoria huko naamini kwamba tutakuwa tunasafirisha shehena kubwa sana kwenda katika maeneo mbalimbali ya Ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee pia nizungumzie katika eneo hili la mawasiliano ya simu. Wenzetu wa *TCRA* walituaminisha kabisa kwamba baada ya zoezi la kuhakiki au kusajili simu kwa kutumia vidole (*biometric*), ule utapeli wa kutapeli ana sana utakuwa umekwisha, lakini naona kwamba bado hilli lipo, wananchi huko vijijini bado wanaendelea kutapeliwa. Je, *TCRA* wanakwama wapi kuwabaini matapeli wanaotuma *messages* za wizi kwa wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya idadi ya maombi niliyonayo hapa kengele itagongwa moja na kila Mbunge atakuwa amepewa dakika saba.

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa David Ernest Silinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Yahaya Omary Massare na Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza ajiandae.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ni kiungo kikuu cha uchumi katika nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mombasa wamenituma kusema haya na nasema kwa niaba yao. Kwenye ujenzi kuna *TANROADS*, kuna Uchukuzi, kuna Mawasiliano, lakini ukipitia kwenye bajeti yao utaona kuna kakifungu kadogo kanahusu *TARURA*. Sasa Halmashauri ya Mombasa tangu mwezi Desemba barabara ambazo ziko chini ya *TARURA* hazipitiki kabisa. Sasa nimeona nisipolisema hilo nitashindwa kwenda kurejesha mrejesho kwa wananchi wangu wa Mombasa. Kwa hiyo nikaona ni vizuri vilevile niliseme; *TARURA* wamepewa barabara nyngi sana, mtandao wa kilometra ambazo ziko chini ya *TARURA* ziko 108,000 na ambazo zipo kisheria zipo kama 52,000 na 56,000 bado ziko katika hatua za kuhakikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo unaweza kuangalia fedha ambayo wanapewa Sekta ya Ujenzi ambayo ni nyngi na fedha hizi ambazo ziko kwa *TARURA*. Sasa kuna barabara hapa nitazitaja baadhi ya wananchi wa Mombasa wasikie; Barabara ya Nkala – Chilulumo, imeharibika haipitiki; Barabara ya Kakozi – Ilonga, imeharibika haipitiki. Barabara hii sisi miaka yote tumeiombea ipandishwe hadhi ianze kuhudumiwa na *TANROADS* kwa sababu inaunganisha Mikoa miwili ya Songwe na Rukwa, lakini huu ni mwaka wa kumi nimekuwa nikizungumzia hii barabara na bado utendaji wa Serikali haujatekelezwa kwenye hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Iyendwe – Ikana kuunganisha Halmashauri ya Mombasa na yenewe bado haijafanyiwa kazi. Nzoka – Ipatikana, Ikana – Makamba ni barabara zilizoharikiba. Pia kuna barabara ya *TANROADS* wenewe ambayo wanaimiliki kutoka Mlowo – Kamsamba – Kilyamatundu mpaka Majiyamoto. Barabara hii kipindi cha mvua imehaibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nimeyasema haya? Ni kwa sababu *TARURA* waliomba fedha za dharura mwezi Februari, walifanya tathmini nchi nzima wakasema tuna mahitaji ya bilioni 53 kurekebisha hizi barabara za dharura. Sasa Serikali imekuja na majibu kwamba pamoja na kwamba *TARURA* mnahitaji hizi fedha kwa sasa hatuwezi kutoa kwa

sababu kuna janga la *corona* kwa hiyo sasa tuanze ku-deal na uhai wa watu. Nakumbuka kwenye Kamati ya Bajeti niliambia Serikali; mgonjwa wa *corona* wa kwanza Tanzania alipatikana tarehe 18, Machi, TARURA ilifanya tathmini mwezi Februari na walikuwa wanahitaji bilioni 53 kurejesha hali ya barabara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kigezo isiwe tu *corona* peke yake, najua *corona* ni janga la kimataifa ambalo linahitaji *collective responsibility*. Sio janga la mtu mmoja ama chama fulani cha siasa, hili ni janga letu sote. Kwa hiyo *it is a pandemic*, dunia inalia. nasi Watanzania hatupaswi kulia, tunapaswa kuchukua hatua kupambana ili kuwasaidia wananchi wetu walioko kule nje. Huo ndio wajibu wetu wa Kibunge, wajibu wa Kibunge ni kupambana mpaka dakika ya mwisho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo hilo niliona niliseme ili Serikali iweze kufanyia kazi hizo barabara, ili wananchi wangu wa Jimbo la Mombasa waweze kupata nafuu, waondokane na huu ugumu ambao unaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nahitaji kulisema kwa kifupi sana; ukiangalia Wizara ya Ujenzi, mwaka huu wanaomba 4,784,000,000,000. Hii ni sawasawa karibu na asilimia 15 ya bajeti nzima ya nchi, ni fedha nydingi sana. Siku zote huwa tunasema uwekezaji lazima uendane na matokeo ya kiuchumi. Unapowekeza sana maana yake na matokeo ya kiuchumi yaye makubwa. Ndiyo maana siku zote hapa ukisoma Wizara zinavyokuja kutuletea taarifa hapa ndani, utaona hawatuelezi kwamba tume-*invest* kiasi hiki matokeo yake ajira hizi, biashara hizi zimepatikana. Ukiwa tu na bajeti ya matumizi bila kueleza matokeo yake maana yake mwisho wa siku ndiyo huwezi kujua matokeo yake ni nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku ndiyo mtu atakwambia mmeiba fedha, mmekula fedha kwa sababu hujawapa tafsiri ya kiwango cha fedha ulichowekeza. Hiki ndicho ambacho tunataka majibu kutoka kwa Wizara ya

Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; watujibu *investment* iliyofanyika mwaka jana tunategemea itazalisha uchumi kwa kiwango gani na *investment* ambayo inawekwa mwaka huu wa fedha; Sh.4,784,000,000,000 zitaleta kitu gani katika mwaka huu wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kuna wakati mwingine hatuhitaji kutumia fedha nyngi kuwekeza kwenye upande mmoja. Wakati mwingine tunaweza tukatumia bado fursa ya *PPP*, tuwekeze kwenye *PPP* (*Public Private Partnership*); Serikali ishirikiane na Sekta Binafsi kuwekeza. Kwa mfano hapa imezungumziwa Barabara ya Dar es Salaam *Expressway*, Dar es Salaam – Morogoro. Ile barabara iliingizwa ili iingie katika mfumo wa *PPP*, ni mradi mkubwa sana na ule mradi ungeleta faida. Duniani kote, sisi wote ni mashahidi, barabara za *PPP*nyingi zinakwenda kwa mfumo wa *road toll*. Dunia imebadilika hili sasa hivi, yaani huwezi kuwa kila kitu unatoa *free*, haiwezekani kwa sababu watakushinda; watu wanaongezeka, kila siku watu wanazaliwa, huwezi, lazima ubadilishe mfumo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakumbuka mara ya mwisho Serikali ilijibu hapa kwamba ile barabara imekuwa overtaken by events kwa sababu kuna reli inapita kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, sio jambo bayu reli kupita, lakini vilevile siyo jambo bayu barabara ile kupitika kwa sababu kuna watu wana magari mazuri, wana *luxury cars*, wanataka kuwahi kuja kutembea kwenda kwingine; kwa nini isitumike hiyo kama fursa ya Serikali kupata mapato yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano mzuri ni lile Daraja la Kigamboni la *PPP* ambalo tunaona matokeo yake; makusanyo ni makubwa kwa sababu wananchi wako pale, wanalipia, wanapita. Sasa twendeni katika mfumo wa *PPP*ili kupunguza huu mzigo na hizi fedha nyngine zitakazopatikana tuziwekeze kwenye mambo mengine ikiwemo Sekta ya Afya, ikiwemo kupambana na janga hili la *corona* ili tuhakikishe tunaokoa maisha ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Silinde. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, atakayechangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza nilikuwa pia nimeshamtaja, ajiandae Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka.

Mheshimiwa Yahaya Omary Massare kutokea Msekwa.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Mheshimiwa Spika, wewe Naibu Spika, lakini Katibu wa Bunge. Kipekee kabisa nimshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kunisaidia kibali na gharama za matibabu kwenda kutibiwa katika Nchi ya India ambapo leo ninapozungumza nazungumza nikiwa na afya njema ambayo inatosha kufanya kazi hizi za Kibunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa nami ni mdau wa mambo haya ya barabara ingawaje sipo kwenye Kamati hii ya Miundombinu, nimeguswa nichangie hapa kwa kirefu kidogo kuhusu barabara ambayo inaunganisha Mikoa ya Singida na Mbeya. Sisi wananchi wa Mkoa wa Singida tumekuwa na kilio kikubwa cha muda mrefu kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Rais alifika pale yeye mwenyewe akawaambia wananchi kwamba barabara hii sasa tunajenga kwa kiwango cha lami kutokea Mkoa wa Singida. Kilometra 56.9 ambazo zilishatengewa fedha na mkandarasi akapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka ninapozungumza hapa ni mwaka wa pili kama si wa wa tatu, kwa sababu hili lilizungumzwa katika mukutano wa hadhara na wananchi

wakasikia Rais wao mpendwa, wananchi waaminifu kwa Chama cha Mapinduzi. Wamekuwa wakichagua Madiwani na Wabunge wa CCM, lakini mara hii barabara hii imeyeyuka. Sina cha kuwaambia wananchi wa Jimbo lile, labda Mheshimiwa Waziri aje na maelezo ya kutosha kuona kwamba wananchi wa Jimbo la Manyoni Magharibi wanaunganishwaje na Mkoa wa Mbeya kwa maana ya Mkoa wa Singida na Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii siku zote imekuwa ikijengwa kutokea Mbeya. Hata Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko hapo, alipofika Singida nilimililia kilio hikihiki cha barabara hii imejengwa kuanzia Mbeya – Luhanjilo kilometra 36, Luhanjilo – Chunya, kilometra 36 na inajengwa sasa kutoka Chunya kuelekeea Makongorosi, kilometra 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 22 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ameonesha tu kwamba hela zinatafutwa. Sijui lini watajenga na wao wananchi wa Mkoa wa Singida waone kwa Serikali inaonesha dhamira njema kabisa kama wao walivyo waaminifu kwamba barabara hii sasa ianze kujengwa kutokea Mkoa wa Singida. Bado kilometra 400 karibu na 13. Leo kilometra 56.9 ambazo ziliahidhiwa na zilitengewa fedha na ikatangazwa tenda na mkandarasi akapatikana zimeyeyukaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hivi tunavyozungumza barabara hii haipitiki kutoka Burungu kwenda Sanjaranda, haipitiki kutoka Sanjaranda kuja Itigi na haipitiki kutoka Itagata kwenda Mitundu na kutoka pale Kiyombo kwenda Kintanula. Barabara ni mbovu kwelikweli.

Hakuna watu wa *TANROADS* Singida kama msimamo mpaka leo hivi sijui kama wanakupa taarifa kwamba wananchi wa eneo lile wa sasa wanatembea na punda. Usafiri wao sasa magari hayaendi, wanatumia usafiri wa ajabu kwa sababu hatuna namna, tuna barabara hiyo moja tu hatuna hata mpalio wa ng'ombe kwamba tungepita pembeni. Naomba Mheshimiwa Waziri aje atuambie ni kitu

gani ambacho kinaleta shida barabara hii kutokuanza kujengwa kwa upande wa Mkoa wa Singida. Mwaka wa tano huu niko katika Bunge hili, kilio changu ni barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshiiwa Waziri alipokuwa Naibu Waziri wa Maji alikuwa mtu msikivu sana. Mimi alinisikia, watu wa Itagata wanamkumbuka kwa skimu ya umwagiliaji, watu wa Rungwe wanamkumbuka kwa bwawa, lakini alipoingia kwenye barabara sijui kuna shida gani hapo Mheshimiwa. Hebu nimwombe sasa aje na maelezo ya kutosha ili wananchi wa jimbo hili nao waone kwamba Serikali yao inawajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunayo barabara ambayo ipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi ya kuunganisha Mkoa wa Singida kupitia Mkoa wa Dodoma, Kondoa mpaka Tanga. Imezungumzwa sana kwamba wakati tunapoenda kujenga hili bomba la mafuta na barabara hii basi ijengwe, itapunguza msongamano mkubwa katika Bandari ya Dar es Salaam. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wetu wengi wataweza kutumia Bandari ya Tanga, hasa nchi jirani za Rwanda na Uganda ni rahisi zaidi kutumia Bandari ya Tanga kuliko kutumia Bandari ya Dar es Salaam. Msongamano uliopo leo Bandari ya Dar es Salaam mpaka leo tunaona Mtwara wanasoagea kuweka bandari kavu, niwapongeze kwa hili, lakini hebu waone na hili ambalo litakuwa na manufaa makubwa kwa nchi hii. Dhamira yetu ni kuona kwamba Tanzania inakuwa kweli ni nchi ambayo inahudumia hizi nchi ambazo zimetuzunguka kwa dhamira ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Mkoa wa Singida pia wana kilio cha kuunganishwa na Mkoa wa Simiyu kupitia Daraja la Sibiti. Daraja limekwisha, ndiyo kilikuwa kikwazo kikubwa; sasa hizi gharama tu za ujenzi jamani, kwa nini Mkoa wa Singida? Mbona leo tunaona Mkoa wa Kigoma, wananchi wale nao wana wivu, wanajisikia vibaya wenzao wanapounganishwa na barabara za lami. Mkoa wa Kigoma leo unaungwa na Tabora, Mkoa wa Kigoma leo unaungwa

na maeneo mengine; ni raha iliyoje na sisi wa Singida tukaanza kuungwa na Mkoa wa Mbeya na Simiyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo shida pia za mawasiliano ya simu katika maeneo yetu. Tumekuwa na ahadi nyingi toka 2017, wamekuja tu na maeleo mazuri kabisa kwamba sasa tunakwenda kukomesha tatizo la mawasiliano katika maeneo yetu ya nchi hii. Niombe sasa wafanye kazi tunapoelekea katika uchaguzi, basi tupunguze maswali magumu juu ya suala hili la mawasiliano. Naamini Wizara hii inaweza kuitia maduhuli haya ambayo yanakusanya na Serikali, kuitia *TRA*, lakini naamini Wizara ya Fedha watawapa pesa ambazo wameomba basi watulete miundombinu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru na niunge mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia mia moja japo kuna upungufu kidogo. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka na Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau ajiandae.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenijalia kuwa salama mpaka wakati huu. Pia nichukue nafasi kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri na kubwa wanayoendelea kuifanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoendelea kusimama imara katika kuwapigania wananchi wake na kupigana katika janga hili la *Corona*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Spika kwa uamuzi wa kuendelea na vikao vyetu hivi vya Bunge. Tunayo

mihimili mitatu ya dola, Serikali, Mahakama na Bunge: Mahakama hawajaahirisha kuendesha kesi Mahakamani, Serikali inaendelea kutoa huduma idara zote, Bunge ni mhimili pia muhimu kwa ajili ya kupitisha bajeti ili kuiwezesha Serikali iendelee kuwahudumia Watanzania. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu lakini kumpongeza Spika na Idara yake kwa uamuzi huu wa kuendelea na vikao vya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Waziri lakini pia ushauri wa Kamati. Ni dhahiri kwamba yapo mambo makubwa yamefanyika na tunapojadili bajeti hii tunaona ni jinsi gani ambavyo Serikali imejipanga kuendelea kuboresha miundombinu katika sekta ya usafirishaji, mawasiliano lakini pia katika kuendelea kuboresha miundombinu kwa maana ya barabara na ujenzi wa madaraja, ndio maana nikaanza kwa kupongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri inayofanywa bado zipo changamoto katika maeneo kadha wa kadha katika jimbo langu. Tunayo barabara inayotoka Dar-es-Salaam - Isaka - Ngara - Rusumo - Rwanda, inajulikana kama *Central Corridor*, yaani katika mgawanyo wa *zoning* kwenye miundombinu ya kuunganisha nchi na nchi hii ni barabara muhimu sana. Kutoka Dar-es-Salaam - Rusumo mpakani na Rwanda ni zaidi ya kilometra 1,500 lakini kipo kipande kidogo tu cha kilometra zisizozidi 91 kutoka Rusahunga - Rusumo mpakani kimechakaa kupita kawaida na muda mrefu nimekuwa nikiongelea suala hili. Kipande hiki kinafanya barabara hii ya kutoka Dar-es-Salaam - Rusumo, inayopeleka mizigo kwenda Kongo, Rwanda na Uganda isiweze kuwa *effective* vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ukiangalia *trend* ya miezi minne iliyopita magari yanayosafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar-es-Salaam kwenda Kongo na Rwanda, imeshuka kwa asilimia 40 mpaka 50. Inapokuwa magari ya kusafirisha mizigo yamepungua kwa kiasi hicho na ndio njia pekee tunayoitegemea zaidi maana yake ni kwamba hata uondoaji wa mizigo bandarini kupeleka

maeneo ambapo inatakiwa kwenda na penyewe kunakuwa na namna fulani ya kusuasua. Kama pengine ingechukua wiki moja kumaliza mizigo ambayo inatakiwa isafirishwe kuititia barabara hii maana yake inaweza ikachukua hata siku 9 mpaka 10. Kwa hiyo, kwa kipande hiki cha kilometra zisizozidi 91 kutoka Rusahunga - Rusumo tunapata hasara kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mwezi Machi, magari yanayopita kwenye barabara hiyo kwenda Rwanda na kurudi yalikuwa karibu 800, maana yake 400 kwenda na 400 kurudi, yalishuka mpaka magari karibu 56 mpaka 70. Pia yapo magari ambayo yamekuwa yakitoka Rwanda kuja Tanzania, magari ya Rwanda ambayo wanalipa *road toll* tulijikuta kwamba tumeporteza karibu milioni 50 za kila siku kutokana na malipo ambayo yanalipwa. Kwa hiyo, niombé kipande hiki cha kutoka Rusahunga - Rusumo tujaribu kukiangalia kwa mapana yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti hii nimeona zimetengwa karibu shilingi bilioni 2.7 na hii itakuwa ni pamoja na ukarabati mdogomdogo lakini pia na ujenzi wa Kituo cha Pamoja pale Nyakanazi. Kwa hiyo, utaona kwamba kama tusipokuwa na mikakati thabiti, nitaomba pengine anapokuja kuhitimisha Mheshimiwa Waziri anieleze mkakati uliopo sasa kama si kwenye bajeti hii ni wapi tunatarajia kupata fedha? Najua kwamba pia barabara hii inahusu nchi zingine kwa maana ya nchi ambazo ziko ndani ya *East Africa*, kama ni fungu linalotegemewa kutoka upande mwingine basi niweze kueleweshwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kwenye bajeti ya vivuko, nimeona tumetengewa shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuboresha maegesho Kivuko cha Rusumo Nyakiziba. Pale kuna *ferry* ya *MV Ruvuvu* lakini *ferry* hiyo kwa muda mrefu haifanyi kazi kutokana na kwamba maeneo haya yanakuwa yamejaa maji kiasi kwamba hata tutakapoweka fedha hizi ambazo zimetengwa ambazo naamini hizi ni kwa ajili ya kivuko hicho, naamini kwamba na Kivuko cha Mayenzi Kanyinya ambacho kinaunganisha Tarafa mbili za

Nyamiyaga na Rulenge itakuwa iko kwenye bajeti hii kwa sababu kivuko hicho chenyewe bajeti yake haizidi shilingi milioni 80, naamini kwamba itakuwa iko kwenye kivuko hicho. Nilishapendekeza kwamba kwa sababu kuna mradi mkubwa wa umeme wa Maporomoko ya Rusumo unaoendelea pale na kutokana na mradi unaoendelea pale inaonekana kwamba mto unakuwa unajaa kwa hiyo, inawezekana kivuko hiki kisiendelee kutumika, basi tuweke daraja badala ya kuendelea kutumia kivuko hicho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau Kitwana, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk ajandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii nitoe mchango wangu kwenye Wizara hii. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kunipa nafasi jioni hii na mimi kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kitendo alichokifanya jana cha kurudisha imani kwa wananchi kwenye mapambano haya makubwa. Mheshimiwa Rais kwa kweli amefanya jambo kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Waziri Mkuu usikatishwe tamaa na hawa askari wetu wachache waasi walioamua kukimbia vita na kujificha vichochoroni. Hawa watu wameondoka kwenye uwanja wa vita na nyumbani hawajarudi na wanajua wakirudi nyumbani watakosa maelezo wameamua kukaa vichochoroni. Mheshimiwa Waziri Mkuu hawa watu wasikukatishe tamaa, sisi tusonge mbele, wanajeshi wengine wapo tena ni wengi, jeshi imara, tunakuunga mkono sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, naomba niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Naibu Mawaziri wote wawili. Shukrani za pekee ziwaendee watendaji wote kwenye Wizara hii kwani mafanikio haya yanayoonekana kwenye Wizara hii ni kwa umoja wao kuanzia Waziri, Naibu Mawaziri na Makatibu Wakuu. Jambo hili lisingeweza kufikia hapa lilipofikia lakini ni kutokana na umoja uliopo kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu kwenye hotuba hii, naiomba Serikali kuzingatia yale yote ambayo yameelezwa na Kamati yetu kwa sababu mimi ni mjumbe wa Kamati hii. Kwa hiyo, yale yote ambayo wajumbe tumeyadadavua na kuyaleta kwenu tunaomba Serikali myazingatie sana ili lengo la Mheshimiwa Rais la kuiona Tanzania yenye uchumi wa katiliveze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna jambo hapa naomba nilichangie kwa kusistiza. Sera yetu ya Kitaifa ni kuunganisha makao makuu ya mikoa nchini na barabara za kuunganisha nchi jirani. Ni jambo jema na zuri lakini naomba niishauri Serikali, ziko barabara zinazounganisha makao makuu ya wilaya zetu na mikoa nazo hebu tujaribu kuzitupia macho kwani ni muhimu sana kwa jamii yetu. Barabara hizi ndizo zinazowawezesha wakulima wetu au wananchi wetu kwa ujumla kuhamisha mazao yao na kuyapeleka kwenye masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mazao mengi ya wakulima yanakwama au yanaharibika njiani kwa sababu ya ubovu wa barabara. Ni kweli tunakwenda kutengeneza barabara za kuunganisha mikoa yetu lakini hizi barabara zinazounganisha makao makuu ya wilaya na mikoa ambazo ndizo zinaleta mazao kwenye hizi barabara kuu tunaziweka kwenye nafasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nitoe mfano, sisi Wilaya ya Liwale tunazalisha korosho zaidi ya tani 17,000 kwa mwaka lakini mwaka huu zaidi ya kilo 800 zimeshindwa kufikia masoko na hizo tani 16,000 zilizobaki tumekwenda kuziwa kwa

bei ya hasara kwa sababu hakuna mfanyabiashara ambaye yuko tayari kwenda kununua korosho kwa bei yenye maslahi kwa Liwale kwa sababu anajua shida atakayoipata kuzihamisha zile korosho kuzileta kwenye barabara kuu. Kwa hiyo, muone namna gani wakulima wetu wanavyohangaika na kupata bei za chini kwa sababu tu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo napolizungumza hili Liwale kuna tani 800 za korosho za msimu uliopita. Leo tunaingia kwenye msimu wa ufuta lakini bado kuna korosho ziko kwa wakulima kwa sababu wafanyabiashara wameshindwa kuzifuata korosho zile kwa sababu ya ubovu wa barabara. Ni kweli kabisa nakubali kwamba mwaka huu tumekumbwa na mafuriko lakini haya mafuriko yamekuja wakati tayari sisi tumeshaathirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali kuangalia hizi barabara zinazounganisha wilaya na makao makuu ya mikoa. Sisi tuna barabara ya Nachingwea – Liwale ambayo inapitia Masasi – Lindi hajengwa na mimi huu ni mwaka wangu wa nne au wa tano niko hapa naizungumzia barabara hiyo. Mheshimiwa Waziri tafdhali hebu tuokoe sisi watu wa Liwale tuone na sisi tuko Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kuna barabara ya Nagurukuru – Liwale ambayo kwa Liwale ndiyo barabara ya kiuchumi. Barabara hii ndiyo inayopitisha korosho na ufuta na ndiyo barabara hasa sisi watu wa Liwale tunaweza kusema kwamba sasa tumefunguka, tumetoka kisiwani maana hivi navyosema barabara hii ya Nangurukuru – Liwale tangu mwezi Oktoba imejifunga. Barabara yetu pia ya Nachingwea – Liwale nayo inapita kwa kulala magari njiani mara nyingi. Kwa hiyo, uone ni namna gani barabara hizi ni muhimu. Nazungumzia umuhimu wa kuziunganisha wilaya zetu na barabara za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye hii sera ya kuunganisha mikoa bado Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi haujaunganishwa kwa barabara, hata barabara ya changarawe hakuna. Tunakuomba Mheshimiwa Waziri uone

namna ya kuunganisha Mkoa wa Lindi na Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mkoa wa Lindi unaweza kuunganishwa moja kwa moja na Mkoa wa Ruvuma kupitia Wilaya ya Liwale. Sasa hivi ukiuliza unaambiwa Mkoa wa Lindi tayari tumeuunganisha na Ruvuma kupitia barabara inayopita Mtwara lakini mjue kwamba hiyo barabara ni lazima uende Mtwara ndipo uende Songea lakini ipo barabara fupi kabisa inayotoka Lindi inakwenda moja kwa moja Liwale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema hayo machache, naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa tamko lake lile wakati akimuapisha ndugu yetu Mheshimiwa Mwigulu Mcemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria na kuwapa nguvu na ari wananchi. Kauli yake ile imeleta hamasa kubwa sana katika vita hii ya *Corona*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, nitoe salamu za pole kwa familia ya aliyekuwa Mbunge wa Mafia, kaka yangu, marehemu Mheshimiwa Esmail Abdulkarim Shah ambaye amefariki takribani wiki moja iliyopita. Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia hoja iliyoko mezani. Mheshimiwa Waziri mimi nataka niwe mkweli Mheshimiwa Rais amefanya jitihada kubwa sana katika kuiwezesha Wizara hii. Wizara hii upo wewe Mheshimiwa Waziri, Manaibu wawili, Makatibu Wakuu pale, Manaibu Katibu Wakuu na *personel* wa kutosha kabisa lakini mimi

nataka niseme ukweli mambo bado hayaendi vizuri sana. Kutokana na *interest* ya muda nitazungumzia eneo moja tu la uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukifuatilia kwa karibu sana shida ya usafiri ya Kisiwa cha Mafia toka Kilindoni kuja Nyamisati. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa jitihada zake zile za kutujengea kivuko lakini pale kivuko kimekwama, kivuko kile pamoja na kile Kivuko cha Ukara na Kivuko cha Chato hali haiendi vizuri sana kwa sababu mkandarasi pale hajalipwa pesa zake. Tuliambiwa mwezi Februari kivuko kile kitaanza kazi mpaka sasa hakijafika hata nusu. Taarifa humu ya Mheshimiwa Waziri inasema kwamba wako kwenye 40%, kwa hiyo, tuko nyuma sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Mheshimiwa Waziri nilikuja kwako kwa ajili ya kupata ile meli ya *DMYukaniambia* hii meli achana nayo tutakujengea kivuko ambacho ndio kimefika hiyo 40%. Hata hivyo, tuna shida na wananchi wa Mafia wakajiongeza kupitia wawekezaji mbalimbali imekuja meli pale ya kisasa kabisa tunataka kibali tu meli ianze kazi, leo wiki ya tatu meli ipo pale Kilindoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini taasisi zenyе mamlaka ya kutoa vibali wiki iliyopita wametoa kibali kwa boti za magogo yaani zilizotengenezwa kwa mbaо ambazo si salama lakini hii meli ya kisasa, ina *engine mbili*, ina *navigation facilities* zote, rada na kila kitu wanaambiwa kila siku kesho keshokutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikwenda kwa Mheshimiwa Waziri kumwambia akasema kwamba huwezi ku-*overrule* maelezo ya wataalam wako. Mimi nataka nikuambie wataalam wanakudanganya kwa sababu walisema ile meli ina *engine mbili*, *engine* moja mbovu kabisa, *engine* nyingine ndogo ndio ya *emergence* inafanya kazi, kwa hiyo, ni hatari kuipa kibali. Mimi nikajiongeza nikatoka Dodoma nikaenda Mafia kuiangalia meli ile nikaikagua mimi mwenyewe. Kwanza si kweli kwamba ina *engine mbili* kubwa na ndogo, ina *engine mbili* zote zina ukubwa sawa *horse power* 1,800,

kwa namna ya uhandisi wowote haziwezi kuitwa *engine* ndogo. Pili zikawashwa mbele yangu zinafanya kazi. Wamesema *pump* hazifanyi kazi, *pump* zinafanya kazi. Wamesema kwamba hakuna *life jackets*, *life jackets* zipo, lakini hawajapewa kibali mpaka leo wanahangaika wamekuwa *frustrated* wanataka kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa wale wenye maboti ya magogo wameapa kwamba ile meli mpya haitafanya kazi pale. Tunaona ushahidi huo kwa sababu afisa wa *TASAC* aliyetumwa atoke Dar es Salaam kwenda Nyamisati kukagua ametoka Dar es Salaam saa 02.00 mpaka saa 12.00 yuko Bungu kilometra 100 ana gari jipya kabisa la Serikali, anasema siwezi kuja huko kwa sababu ya giza nalala hapa nitakuja kesho. Kesho yake kaenda kakagua *engine* hazikuwashwa wala hakufanya chochote akasema nimeshaona kwaherini. Aliporudi ndiyo akaenda kuandika hiyo ripoti kwamba *engine* ile mbovu, sijui hakuna *life jackets* na kadhalika. Nimeongea na watu wa *TASAC* wakasema wanatuma timu nyngine mpya kwenda kui-*inspect* upya meli ile, toka ametumwa huyo mtu mpaka leo hajafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kupitia Bunge lako nimuombe Mheshimiwa Waziri aunde tume ya wataalam iende Mafia ikaangalie hawa *TASAC* inakuwaje meli za magogo, maboti ya magogo ambazo siyo salama zina *engine* moja tu na hiyo *engine* yenye wanakaa nayo abiria humohumo zinapewa kibali wakati meli ya kisasa ina *engine* mbili, ina *navigation facilities* zote, kuna *life jackets*, haipewi kibali? Sasa hivi imekuja hoja nyngine wanasema *life jackets* haziwaandikwa kama ni *MV*jina Fulani, ina maana hapa kuna kitu hakiko sawa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo kwa sababu hili jambo alikuwa akilifuatilia. Nataka nikumhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba watendaji wake wanamuangusha. Meli ipo, wananchi wamerundikana pale Nyamisati, wana hatari ya kupata *Corona* zaidi ya watu 400 hawawezi kusafiri kwa sababu

magogo uwezo wake ni abiria 50 wakati meli ya kisasa uwezo wake ni abiria 260 lakini hawataki kutoa kibali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah. Mheshimiwa Omary Mohamed Kigua ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, niungane na wenzangu kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ya kipekee kabisa kwa kutufanya tuendelee na shughuli zetu za Bunge tukiwa na afya njema. Pia niwaombee wale ambao wamepata mitihani ya maradhi haya na bado wako hospitalini. Mwenyezi Mungu awaponye haraka ili warudi tujumuike nao, tuendelee na shughuli zetu za Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe salamu za pole kwa wakazi wa Jimbo langu la Tanga wale ambao wamepoteza wapendwa wao na wale ambao nao wako katika mtihani wa maradhi haya, Mwenyezi Mungu awaponye na turudi katika shughuli zetu za kawaida. Nitoe ushauri hapa kidogo kwa wale wanaowekwa kwenye *quarantine* kwasababu zipo taarifa watu wanaopita katika Mpaka wa Horohoro na watu walioko katika jiji letu la Tanga kwamba wakishamaliza *quarantine* panakuwa na mtihani kidogo wa kuruhusiwa kwenda kuijunga na familia zao pamoja na upatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuchangia kwanza nitoe shukrani na pongezi kwa Serikali kwa barabara yetu ya Pangani. Najua fedha zimekwisha patikana,

mkandarasi amekwishapatikana na Taarifa nilizokuwa nazo mkandarasi ameshapata mpaka *site* ya kuweka vifaa vyake vya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tu niiombe Serikali, wananchi wetu wamekuwa na matarajio makubwa na barabara hii, lakini sasa basi barabara kama inaanza kujengwa, wale ambao kwanza walifanyiwa *evaluation* ya mashamba yao na nyumba kwa kuambiwa wasiziendeze, nashauri basi walipwe fidia kwanza kabla mradi haujafikia hatua kubwa kwa sababu wananchi wetu wale watakapokuwa wamelipwa fidia, wataweza kutumia fedha hizo kwenda kununua mashamba sehemu nyingine au viwanja sehemu nyingine wakajenga na wakaendeleza maisha yao na kuna Kata nyingi ambazo zimepitiwa na mradi huu kwa Jiji letu la Tanga, nikianza na Kata ya Msambweni, Kata ya Mazange, Mabawa, Duga, Tangasisi, Tongoni, Marungu na Kirare. Kote huku kuna wannachi ambao kwa njia moja au nyingine wameathirika na ujenzi wa barabara hii. Kwa hiyo, naomba walipwe fidia zao ili waendelee na shughuli zao za maisha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini barabara nyingine ambayo nayo pia nimekuwa nikizungumzia mara kwa mara, kuna barabara inayoanzia Mabokweni – Gombero – Daluni – Maramba hadi Korogwe. Hii barabara nayo ni muda mrefu tumekuwa tukizungumza katika vikao vya RCC vile tulikwishaomba kwamba angalau ipandishwe daraja iwe katika kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, basi namuomba Mheshimiwa Waziri, aitazame barabara hii pia. Kwanini nazizungumzia hizi barabara zimepita katika maeneo ya vijijini ambako kuna wakulima wanapata tabu sana kusafirisha mazao yao lakini najua barabara hizi zikiwa zimejengwa katika kiwango kizuri cha lami hata uchumi wa wananchi utakua, hata mapato ya Serikali yataongezeka kwasababu magari ya abiria na mizigo yakiongezeka yatatumia *diesel* na *petro*/ambayo sasa kuna kupatikana mle kodi ya mafuta,

kwa hiyo, najua mapato yataongezeka. Kwa hiyo, niiombe Serikali, barabara hizi zifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo napenda kulizungumzia ni Bandari yetu ya Tanga. Nimemsikia Mbunge mwenzangu hapa akizungumza kwamba bandari ya Tanga basi itumiwe hata na wenzetu wa Singida, nasema ni jambo zuri sana, nimpongeze kwa hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikisema siku za nyuma kwamba Bandari yetu ya Tanga ni Bandari muhimu sana na nishukuru kwamba hata kilio changu pia Mheshimiwa Waziri alikisia. Bandari yetu ilikuwa haina vifaa nya kisasa au vimechakaa, tumeppata vifaa vipyaa. Kwa mfano, tulipata *crane* ile ya *40 feet container*, tumeppata! Tukaongezewa na *crane* nyininge mbili lakini hivi ninavyozungumza nafikiri wajumbe wa Kamati ya Miundombinu nao wallkwenda kutembelea kule. Bandari yetu inaongezwa kina kwasababu ilikuwa kuna gharama kubwa ya kufuata mizigo nje ya bandari kwamba lazima utoke nje zaidi ya kilometra labda nane mpaka 10, lazima ukodishe matishari ndiyo ukachukuliwe mizigo wako lakini sasa hivi kutookana na kuchimbwa kwa kina, meli zitakuwa zinafunga *long side* ina maana gharama za uteremshaji wa mizigo, zitapungua, walilokuwa wanatumia bandari ya Mombasa, sasa watarudi katika Bandari yetu ya Tanga. Sasa hilo naona ni jambo jema sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pana tatizo moja tu, kwamba wafanyakazi wengi wa Bandari ya Tanga, wamekuwa amawanapostaafu wanakuwa basi wanalipwa kwa shida ama wanakuwa watu wa Tanga kupata ajira katika Bandari yetu inakuwa ni shida. Sasa naomba kwa sababu Bandari inaongezwa kina na vifaa vinapatikana, ina maana patahitajika wafanyakazi wengi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana, meli zitaongezeka zaidi, basi naomba watu wa Tanga nao sasa wapate ajira katika Bandari yetu ya Tanga kwasababu imekuwa wengine wanalamika, watakuja Ofisini kwangu

au wanani pigia simu, Mheshimiwa tumesikia ajira lakini tukienda tuna ambiwa ajira zimeshajaa, wengine wanasema bwana kuna watu wanakuja na vi-memo tu kutoka Dar es Saalam huko, wakija unakuta sisi hatuna nafasi. Kwa hiyo niombe watu wa Tanga nao watazamwe kwasababu *the good charity begins at home* kwamba jambo zuri linatakiwa lianzie pale nyumbani. Basi Mheshimiwa Waziri, hili liangalie. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, Bandari ya Tanga ni kiunganishi kati ya Mkoa wetu wa Tanga, nimekuwa nikisema tufanye *categories* za mizigo haswa kwasababu bandari itakuwa imejiongeza ubora wake, basi niombe mizigo yote isipitie Dar es Salaam, mizigo igawanywe kwenye bandari nyingine. Kwa mfano, mizigo ya Tanga yetu, mizigo ya Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Musoma, Bukoba, Rwanda, Burundi na Uganda, hii mizigo ingepita Bandari ya Tanga. Ina maana Bandari ile sasa ingekuwa *active*, wafanyakazi wangkuwa wanahisi nao sasa tuko kazini. Lakini tukiendelea kuitumia Bandari ya Dar es Salaam, inazidiwa inakuwa sasa mtu kama ana mizigo badala ya kutumia wiki mbili au tatu anaweza kutumia hata mwezi. Pamoja na kwamba najua sasahivi inafanya kazi masaa 24, niombe Bandari zetu nyingine nazo zifanye kazi na sizungumzii Tanga peke yake kwasababu Watanzania wote ni wamoja, niseme hata Bandari ya Mtwara, nayo pia ifanye kazi kwa mizigo ya Mtwara yenyewe, Mbeya, Songea, Ruvuma, Rukwa, Katavi mpaka Kigoma, nako pia ifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza nafikiri? Basi naomba sekunde moja tu nimalizie kitu kidogo. Jingine ni uwanja wa ndege wa kisasa, Mheshimiwa Waziri na Bombadier itue Tanga, hilo ndilo ninaloliomba. Mheshimiwa Waziri ahsante. (Makof)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, majina yako mengi sana hapa na wengine wanahitaji kuchangia. Ahsante sana, shukrani. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, atafuatiwa na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mheshimiwa Venance Mwamoto ajiandae.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kuchangia Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niungane na wenzangu wote kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambazo amekuwa akizifanya hasa kwenye Wizara hii ya Miundombinu. Ni jambo ambalo halina ubishi, tumeona vitu vingi vimefanywa kwenye Wizara hii, nikitaka kuvitaja ni vingi mno na dakika zangu ni chache, isipokuwa nibakie kusema Watanzania wanatambua kazi kubwa iliyofanywa na Rais John Joseph Pombe Magufuli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anazozifanya za kujenga nchi, Taifa kusimamia na mambo chungu nzima na kwa kazi kubwa aliyanza nayo juzi ya kumsaidia Waziri wa Afya kwenye suala zima la corona. Nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na wala usife moyo, tuko nyuma yako tunakuunga mkono, tunajua jinsi mnavyofanya kazi, tunaamini hamlali kwasababu yetu, mnahangaika kwasababu ya Watanzania lakini Mwenyezi Mungu atawalipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii pia kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu wenzetu watatu wlaiotangulia mbele za haki. Mimi kama Muislamu ninaamini Mwenyezi Mungu akikuchukua mwezi huu basi utafikia mahali pema peponi, naomba Mwenyezi Mungu na iwe hivyo kwao mwenzetu hawa Mwenyezi Mungu awapokee na awaweke mahali pema peponi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaanza kuchangia Wizara ya Ujenzi nina masikitiko yangu makubwa kwa kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni kwa matamko yake aliyyoyatoa ya kusema kwamba Wabunge wote wa CHADEMA wasiingie Bungeni kwasababu ya ugonjwa wa corona. Niseme, shujaa hakimbii vita, kama wewe ni shujaa huwezi kukimbia vita, lakini nichukue fursa hii pia kuwapongeza Wabunge hawa wa Vyama vyta Upinzani

waliomo humu ndani ya Bunge, kaka yangu Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Selasini, na Mheshimiwa Lijualikali, nawapongeza sana kwa sababu wanajua waliowaleta humu ni wapigakura wao na wamegoma kuwasaliti wapiga kura wao, wamekuja kusema matatizo ya wapiga kura wao ndani ya Bunge hili na niwaambie Wabunge wote waliotoka nje wamesaliti wapiga kura wao na wameshindwa kujiamini kwamba waliowaleta humu ni wapiga kura na wamefuata mawazo ya mtu mmoja aliywepotosha wakaacha mamilioni ya Watanzania kule wakiwa peke yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni aibu kubwa sana wenzetu waliyofanya mambo haya naamini katika bajeti hii Majimboni kwao yatakwendwa maendeleo kama Rais wetu anavyopenda kusema kila siku, Serikali haina chama kwa hiyo najua maendeleo watapelekewa lakini wajue katika kwamba kitu walichokifanya sio sahihi. Nipongeze hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa jana imetupa ari kubwa Watanzania, imetupa nguvu mpya katika ugonjwa huu wa corona na tumhakikishie tu tutaendelea kuchapa kazi kama alivyosema tuchape kazi na tutaendelea kujikinga na kufuata maelekezo yote ya wataalam wanayoyatoa katika ugonjwa huu wa corona. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiri corona ipo lakini lazima kazi ziendelee. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kujua *nature* ya Watanzania, kwa kujua Watanzania wengi mlo wao ni lazima atoke leo aende akatafute kama kuuza mitumba, kama kuuza nyanya ndiyo aje ale na watoto wake. Lakini wenzetu hawa wanataka kwamba ionekane Tanzania imeona hili jambo ni kubwa, imeliweka vizuri kwa kuweka *lockdown* lakini mambo yote yanayofanywa na Serikali, mambo makubwa yamefanywa na Serikali, tumezuia ndege na wakati ndege zinaanza tulikuwa tunawaweka hawa watu tunawatenga kwa siku 14, yote haya hatuyaoni, tumeboresha hospitali, tumetafuta vifaa, tumetenga bajeti yaani tunachukua pesa huku na huku Waziri Mkuu anakuwa anaenda kutafuta pesa ili kuwasaidia watu wa corona lakini wenzetu hawa yote hayo hawayaoni na wanaendelea kulaumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kubwa zaidi Mheshimiwa Mbewe ameamua Wabunge wa Upinzani watoke nje kwasababu ya kujitenga kwa siku 14 kwasababu tu kuna wenzetu walipata matatizo ya corona. Leo hii, mtumishi wa *TRA* akifariki ina maana *TRA* zote zifungwe nchi nzima tusikusanye mapato? *TRA* zote watu wote wakae siku 14 tusikusanye mapato? Mtumishi wa halmashauri akifariki, watendaji wa kata, watumishi wa halmashauri wote wajitenge siku 14, nia yao kubwa nchi hii isimame, nchi hii ishindwe kulipa mishahara, ishindwe kutoa huduma kwa Watanzania, waje watucheke, waje watuseme, waje watukejeli, nimuombe Mheshimiwa Rais, niwaombe viongozi, nimuombe Mheshimiwa Waziri Mkuu tusikubali kutolewa kwenye reli na Mheshimiwa mbowe, vitu wanavyovifanya ni vyta kitoto, tuko kwenye janga kubwa, Mheshimiwa Rais amesema tuungane, tuchape kazi, tuangalie kuwaelimisha watu wetu kuhusu janga la corona. Anang'ang'ania ku-*lock down* ina maana hakuna njia nyingine yoyote ya kusidia corona zaidi yak u-*lock down*. (*Makofii*)

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona nchi jirani wame-suspend wameshindwa kulipa mishahara ya watumishi lakini watu hawa wana nia kabisa ya maksudi mazima tushindwe kulipa mishahara, watoke kwenye majukwaa waseme Rais Magufuli...

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Taarifa Msewa, taarifa Msekwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde kuna taarifa kutoka Msekwa. Taarifa!

## TAARIFA

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa mzungumzaji anayezungumza. Vyama vyta Upinzani tangu tuanze bunge hili miaka mitano, havijawahi kukaa kuitisha bajeti na hili ni Bunge la bajeti.

Kwa hiyo, ni mkakati wao kutopitisha bajeti ya Serikali na ikwame.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, endelea na mchango wako.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naikubali Taarifa hiyo na mimi naamini kabisa wamekuwa siku zote wanaikataa bajeti ya Serikali lakini wanakuja kuilaumu Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza Spika wa Jamhuri ya Muungano kwa msimamo wake thabitio, nikupongeze na wewe mwenyewe Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misimamo yenu ya kukataa kufunga bunge, ni lazima tupitishe bajeti ili nchi iendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi tuko zaidi ya asilimia 80, tutaifanya kazi hii kwa moyo mmoja, tutahakikisha tunawatumikia wananchi, tuko uwanja wa vita hatutaondoka kwasababu ya corona. Tutaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu, tutaendelea kutii masharti tunayoelekezwa na Serikali lakini hatutaacha Bunge mpaka bajeti ya Bunge...

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa! Mheshimiwa Munde kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kiza Mayeye.

## TAARIFA

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba anaposema Wapinzani ajue Chama cha Wananchi CUFTupo ndani, a-specify aseme kwamba ni CHADEMA. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea Taarifa lakini najua kuna Wapinzani makini wenye nia ya kuleta upinzani wa maendeleo lakini kuna wapinzani nia yao ni kuidhoofisha Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ili waweze kutushughulikia. Niwaambie kwamba kwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli *a.k.a* chuma wamekwama! (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepata *message* moja hapa kutoka kwa Wabunge wengine wa Upinzani waliopo, kuna Mheshimiwa Latifah, Mheshimiwa Masele, Mheshimiwa Sabrina na wengineo wako Msekwa, kwa hiyo, niseme tu hii ni aibu kubwa kwa kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni. Ameaibika, amedhalilika, wamemuona kwamba kitu alichokiamua hakina maslahi kwa wapiga kura wao waliowaleta ndani ya jengo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwapongeze sana kwa moyo wao wa kujali watu waliowaleta ndani ya jengo hili na sio kama walijileta wao au walichaguliwa na kiongozi wa Upinzani waje humu, walichaguliwa na Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba tunaomba nchi yetu iendelee, tuchape kazi kama alivyosema Rais, tuna watoto tumeahidi kuwasomesha bure wanatakiwa kulipiwa ada na kuna dawa zinatakiwa zinunuliwe hospitalini kwasababu ya hiyo corona, kuna mambo chungu nzima. Leo tukisema *tu-lock down* hatutaweza kuyatimiza na tutawapa maadui zetu kicheko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Watanzania Taifa letu ni dogo sana lenye Pato dogo la kama trilioni 150, huwezi kulinganisha na Mataifa makubwa, athari iliyotokea kwetu ukilinganisha na mataifa makubwa leo hii tuna maambukizi zaidi ya 3,000,000 lakini ukiangalia Marekani wana maambukizi zaidi ya 1,000,000. Leo hii tuna vifo zaidi ya 250,000, Marekani wana vifo zaidi ya 65,000, huwezi

kulinganisha na athari yetu, ni ndogo mno! Lakini jambo hili wanali kuza kwa maslahi yao na manufaa yao binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile niendelee kuchangia Wizara ya Ujenzi, niipongeze Serikali kwa kututengea fedha Tabora – Mambali – Bukeni katika Mkoa wetu wa Tabora, barabara hii ilikuwa ni kero sana lakini Serikali imetutengea fedha safari hii naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa ujenzi wa reli Dar es salaam – Morogoro ambayo imekamilika, Morogoro – Dodoma na nitoe ushauri kidogo kwa Serikali yangu. Tutafute wabia wa kumalizia Dodoma – Tabora na Tabora – Mwanza. Nipongeze pia kwa ujenzi wa meli mpya, kwa ukarabati wa vivuko mbalimbali, kwa ukarabati wa meli ya MVButiama na Victoria vilevile hapa nitoe ushauri Serikali iongeze rasilimaliwatu kwa maana ya watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze kwa ndege lakini vilevile nitoe pongezi kubwa sasahivi Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Kilimo wameanzisha ndege ambayo inatua *KIA* ya ubebaji wa mizigo kama vile parachichi, mboga, maua, hivi ninavyoongea mimi na wewe tayari kazi hiyo imeshaanza. Hizi ndiyo juhudzi za viongozi tunaowataka wanaotuletea maendeleo. Wajasiriamali wetu sasa hivi wanaendelea kuuza vitu vyao moja kwa moja kutoka Tanzania kupeleka London, Marekani n.k kwa hiyo, nampongeza sana Waziri wa Kilimo na Waziri wetu wa Miundombinu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze sana...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa na naunga mkono hoja asilimia 100. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto. Mheshimiwa Deogratia Francis Ngalawa, ajiandae.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa jioni ya leo niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii, Naibu Waziri wawili hawa ndugu yangu Mheshimiwa Kwandikwa, Mheshimiwa Eng. ndugu yangu Nditiye, wamekuwa ni watu ambao wanafanya kazi kubwa sana. Sisi kama Waheshimiwa Wabunge, tumeshuhudia wakifanya ziara kwenye maeneo yetu na yote hii wamekuwa wakilfanya kazi hii kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini hususan katika kuwaletaa maendeleo wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kuelezea yale ambayo nimeyaona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ameeleza maeneo mengi sana, lakini katika maeneo ambayo napenda kulizungumzia ni eneo la barabara hii ambayo inaanzia Handeni – Kibirashi – Kiteto – Dodoma hadi Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, ameionta barabara hii, ametenga shilingi bilioni sita. Kwa kuanzia nadhani ni jambo jema, nampongeza katika hili. Kiuhalisia shilingi bilioni sita hazitoshii kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii. Kama walivyozungumza Waheshimiwa Wabunge, barabara hii ni ya kimkakati. Ni barabara ambayo nimezungumzia toka naingia katika Bunge hili, huu ni mwaka wa tano tunaenda sasa nimekuwa nikisimama katika Bunge hili nikiitungumzia barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni barabara ambayo inaunganisha Mikoa minne; Mikoa wa Tanga na Manyara;

na Mkoa wa Dodoma na Singida. Ni barabara ambayo hata katika hotuba Mheshimiwa Waziri ameizungumzia kwamba ni bomba la mafuta ambalo linatokea Uganda hadi Hoima Mkoani Tanga litapita. Sasa barabara hii kwa ufupi ni ni muhimu katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwamba aangalie namna ya kuongeza bajeti ya barabara hii. Shilingi bilioni sita Mheshimiwa Waziri haitoshi hata kidogo, pengine tutajenga kilometra chache sana. Ukiangalia uhalisia, kipindi hasa hiki cha mvua barabara hii haipitiki. Mheshimiwa Waziri Mkuu ni shahidi, tarehe 4 Machi, 2020 alifanya ziara katika Mkoa wa Tanga kwenye Wilaya yetu ya Kilindi...

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa, nadhani na yenyewe inatoka Msekwa

## T A A R I F A

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa kutoka Msekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nimpe taarifa Mheshimiwa Kigua kwamba asije akapotosha wananchi wakafikiri hiyo barabara inapita Dodoma Mjini. Hiyo barabara ya kutoka Handeni – Kiberashi – Kiteto – Kibaya inakuja hadi Mrijo – Chemba – Donsee – Farkwa – Kwa Mtoro hadi Puma pale Singida inapita katika Wilaya ya Chemba na siyo Dodoma Mjini. Nilitaka tu nimpe taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Kigua unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea lakini nadhani mzungumzaji hajanisikiliza vizuri. Nimesema barabara hii inaunganisha mikoa minne kwa

maana ya Mikoa ya Tanga – Manyara - Dodoma - Singida. Sikusema Dodoma Mjini. Pengine mzungumzaji hakunisikiliza vizuri na naitambua vizuri barabara hii kwamba inapita katika eneo lake la Jimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichokuwa nazungumzia barabara hii ni kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alipita barabara hii tarehe 4 akifanya ziara Jimboni kwangu, akajiona hali halisi. Nawapongeza sana Serikali, kwa kweli wamejitahidi sana kufanya marekebisho makubwa kwa njia tu ya kawaida kwa sababu barabara hii ni ya vumbi inapitika hadi leo, lakini nadhani suluhu ya kudumu kabisa ni kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafarijika kuona katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba barabara hii watajenga lakini kiasi ambacho kimetengwa cha shilingi bilioni sita hakika hakitaweza kutosha. Nilikuwa naiomba sana Serikali na Mheshimiwa Waziri kwamba wakati mwingine wanasema ni vyema ukaona mara moja kuliko kusikia mara elfu moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, hebu afanye ziara ya siku moja, apitie barabara hii kuona kwa nini Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi anaizungumzia ijengwe kwa kiwango cha lami; na kwa nini Wabunge wengine pia ambao barabara hii inapita katika maeneo yao wanaizungumzia? Wakati mwingine tuamini kwamba suala la barabara siyo lazima liwe la kiuchumi tu, hata kuwapelekea/kuwasogezea huduma wananchi ni mambo ya msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara za TARURA, wamewekewa mzigo mkubwa sana. Kuna baadhi ya barabara ambazo sasa lazima zipandishwe madaraja. Mfano ni barabara ya Kwedeswati – Muungani – Kilindi. Barabara hii inastahili sasa hivi kupanda daraja. Mheshimiwa Waziri alituma watu wake kuititia barabara zote ambazo zinastahili kupanda daraja, naomba waziangalie barabara

zote ambazo zinastahili kupanda daraja, zipande ikiwemo barabara ambayo nimeitaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda kulizungumzia, yupo Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumzia kwamba katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri hajaonesha athari za kiuchumi; *investment* hususan katika mambo ya barabara au ujenzi. Nataka nipingane katika hili. Tunapozungumzia ujenzi wa barabara maana yake ni *multiplier effect*. Ukijengewa barabara nzuri ukawenza kujenga Vituo vya Afya maana yake umeweza kuonesha *multiplier effect*. Pia tunaponunua ndege, athari yake tunaiona kwamba unaokoa muda. Kwa hiyo, *return of investment* inaonekana moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya machache naomba kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, shukrani.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Venance Mwamoto, atafuatiwa na Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, ajiandae.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi jioni ya leo. Kwanza nianze kwa kusema hofu ni dhambi. Kwa hiyo, wale wenzetu waliokimbia wametenda dhambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Neno la Mungu linasema katika Isaya 40 kwamba, "watieni moyo watu wangu, asema Bwana." Nianze kwa kukupongeza sana Mheshimiwa Waziri Kamwelwe pamoja na Mheshimiwa Nditiye na Mheshimiwa Kwandikwa kwa kazi nzuri ambazo wanafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niseme tu kwamba nitakuwa sina moyo wa shukrani nisiposema maneno haya kwamba nifikishieni ahsante nydingi sana kwa Mheshimiwa Rais, najua Waziri Mkuu yupo hapa. Wilaya ya Kilolo toka

imeanza ilikuwa haina lami, lakini Mheshimiwa Rais alipokuja pale kufungua hospitali/kuweka jiwe la msingi tulilia kilio, tukamwambia tukipata hospitali na tukawa na barabara mbovu maana yake wagonjwa hawatafika hospitali, watakufa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ninapozungumza Mkandarasi yupo kazini anajenga barabara ya kutoka Kilolo kwenda Iringa Mjini, kitu ambacho kilikuwa ni ndoto. Leo hii ninapozungumza na wewe, barabara ya kilomita 18 kutoka Dabaga kwenda Boma la Ng'ombe kazi ya upimaji inaendelea na lami itajengwa. Kwa hiyo, nashukuru kwa sababu wanasema moyo usio na shukrani hukausha mema yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba nilikuwa nafikiria Mheshimiwa Kamwelwe kwa kuwa *TANROAD* na *TARURA* kazi yake ni kujenga barabara, mngejenga umoja kusaidiana zile sehemu ambazo zina uharibifu mkubwa. Hivi sasa ninavyokwambia Wilaya ya Kilolo pamoja na neema ya kupata mvua nyngi, barabara hazipitiki. Naomba japo nyngine zitakuwa hazimgusi moja kwa moja lakini nizitaje ili na wananchi wangu wajue kwamba najua hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Kilolo – Pomelini – Ukumbi – Masege – Winome haipitiki; barabara ya kutoka Kotoo – Pomelini – Kihesa Mgagap hadi Mwatasi haipitiki; Barabara ya kutoka Boma la Ng'ombe – Inyingula – Masisiwe – Mbawi – Nyawegete haipitiki na barabara ya kutoka Mahenge – Ilingi – Magana haipitiki. Barabara ya kutoka Ruaha Mbuyuni –Msosa mpaka Nyanzwa haipitiki, barabara ya kwenda Ikula haipitiki, barabara ya Msonza – Mingisivili – Kimara haipitiki. Kwa hiyo, naomba tu siyo lazima mtoe fedha, lakini kwa sababu ninyi ni wazoefu, hata ushauri tu ule ingefaa. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Kamwelwe usichoke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama Mheshimiwa Waziri ana kumbukumbu nzuri, mwaka 2019 nilipokuwa nachangia nilisema itakapokuja kuharibika njia ya Kitonga

ikafunga, mtapita wapi? Bahati nzuri Mwenyezi Mungu akaifunga ya Dodoma, ikabidi watu watumie Kitonga. Barabara ya kutoka Kigoma wanapita Iringa wanakwenda Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna njia nilisema ukitoka Iringa ukienda Idete unakwenda Mhanga, kuna barabara ambayo inaunganisha na Morogoro, Mlimba. Kwa hiyo, mwaka 2019 tuliomba fedha na mkaahidi kwamba mngetoa ili siku moja barabara ya Kitonga na Dodoma zikifunga, barabara pekee ambayo itapitika ni ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwombwa Mheshimiwa Waziri, watu wake walishakwenda kukagua, bahati nzuri *Engineer* wa *TANROAD*, Iringa Ndugu Kindole alifika akaiona, *Engineer* wa *TANROADS* Ndugu Wambura amefika ameionna na taarifa ambazo nimezipata ni kwamba walitenga fedha kidogo. Kwa hiyo, naomba ile barabara ifunguliwe ili itakapotokea la kutokea, mvua za mwaka huu tumeziona, barabara zote zikfunga, basi tuwe na *alternative road* ya kuweza kupita badala ya kujifungia ndani. Kwa hiyo, namwombwa sana Mheshimiwa Waziri kwa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo napenda nishauri ni kuhusu *post code*. Naomba Wizara hii na Wizara ya Ardhi zishirikiane kwa sababu leo hii kwa mfano tungefanya *lockdown* nami nipo kule Peramiho, barabara haifahamiki; mtu anapotaka apelekewe chakula nyumbani kinafikaje kama hakuna namba ya nyumba na Mtaa? Wenzetu wameweza kwa sababu kunakuwa na namba ya nyumba, hata ukipiga simu tuletee Mtaa fulani, anafika. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri ashirikiane na watu wa ardhi ili mitaa iwepo na namba za nyumba, tusiwe na shida. Mtu atakaposema kwamba anakwenda sehemu fulani basi ni rahisi kufika. Sasa hivi kuna mambo ya *GPS*, akiingia kwenye *GPS* inamfikisha mpaka kule anakotaka kufika.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, kengele imeshalia.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Deogratius Francis Ngalawa atachangia kutoka Msekwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kutoa pongezi kwa Wizara hii hasa kutokana na barabara yetu ya Itoni – Njombe – Ludewa – Manda kuongezewa kile kipande cha kutoka Itoni mpaka Lusitu katika bajeti hii. Kwa kweli wananchi wa Ludewa wamekuwa na adha na kero kubwa kwenye barabara hii ya kutoka Njombe kuelekea Manda. Barabara hii imekuwa ni njema katika masuala ya kiuchumi kwa sababu maeneo yetu ni maeneo ya kilimo. Kwa hiyo, napenda kuipongeza Serikali kwa kutuongezea sasa *lot one* ya kutoka pale Itoni kuja Lusitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nizungumzie *Lot II* ambayo tayari ilishaanza toka mwaka juzi, kipande cha kutoka Lusitu kuelekea Mawengi. Kwa kweli mkandarasi yupo *site* lakini barabara ile inatengenezwa kwa kusuasua sana. Kwa sababu kimsingi kwa mujibu wa mkataba, barabara ile ilitakiwa iwe imeshaisha Desemba, 2019 lakini sasa hivi kuna *extension* ya mpaka Oktoba mwaka huu, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hiyo *extension* kutolewa, ninaamini kabisa kwa mwenendo ule, yule Mkandarasi hawezi kumaliza hiyo Oktoba, 2020. Kwa hiyo, naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Mheshimiwa Waziri na Naibu wake Mheshimiwa Kwandikwa wamefika *site*, lakini wale watu bado wanasuasua, kwa hiyo,

kuna haja ya kutengeneza msisitizo ili ile barabara iishe mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri naona kuna barabara ya lami ambayo inatoka kule Manda kuja Kandamija kilometra mbili, ile ni *Lot ya IV*. Ningependa kuiomba Serikali iongeze, kwa sababu ile *Lot ya IV* na yenye we inakuwa imeshaanza, angalau tungepewa sasa kilometra tano tano ili mwisho wa siku katika kipindi kifupi kijacho ile barabara yote iwe imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuiambia Serikali kwamba barabara ile ni muhimu sana kwa watu wa Ludewa na barabara ile ndiyo itakayofungua uchumi kwa watu wa Ludewa na Mkoa wa Njombe kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimeona barabara ya Madaba – Mkiu – Liganga – Madaba. Barabara ile mnasema kwamba upembuzi yakinifu na usanifu wa kina itaisha hivi karibuni, lakini kimsingi upembuzi na usanifu wa kina tuliambiwa uliisha toka mwaka juzi.

Kwa hiyo, nilikuwa natarajia kwenye bajeti hii tuanze ujenzi wa lami kutoka Mkiu – Liganga kwenda Madaba, kwa sababu maeneo yetu ni maeneo ya wakulima na ni maeneo ambayo yana uchumi mkubwa, Liganga na Mchuchuma zipo kule. Kwa hiyo, tuweze kwenda kwa kasi ile inayotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio kwa maana unakuta hata miradi ya Liganga na Mchuchuma inasuasua; moja kati ya vigezo ni miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, naiomba Serikali iingize kwenye mpango barabara ya Mkiu – Liganga – Madaba mpango wa ujenzi wa lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimejaribu kuona kwenye eneo la barabara kando kando ya Ziwa Nyasa, kwa kweli hela iliyotengwa ni ndogo. Tumetengewa shilingi milioni 90 tu na ile barabara ina urefu mkubwa; kilometra 139 kutoka Lupingu mpaka Matema. Kwa hiyo, naiomba Serikali na kuishauri ituongezee bajeti ili iweze kukamilika katika kipindi

kifupi kijacho kwa sababu vile vijiji vipatavyo 10 mpaka 12 havina mawasiliano ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini mpango huu wa Serikali ndiyo ambao ungefunkua lile eneo la Ziwa Nyasa kwa sababu lile ni eneo la kitalii, ni eneo la ziwa na tuna vivutio vingi; tuna tamaduni zetu nzuri nyngi ambazo zingeweza kutu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pia niapongeza Serikali katika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele imeshagonga. Ahsante sana, shukrani.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph Roman Selasini na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela ajiandae.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kabla sijachangia, kwa ridhaa yako naomba nisome neno moja kutoka Kitabu Kitakatifu; Biblia, Zaburi ya 91:5-6 nao unasema: "hutaogopa hofu ya usiku wala mshale urukao mchana, wala tauni ipitayo gizani, wala uwele uharibio, adhuhuri." (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza sana juhudzi zote zinazofanywa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa janga hili la *Corona*, zamani ikijulikana kama tauni, leo tunaita *Corona*. Ni dhahiri kwamba Mataifa yote

duniani na ndio maana tunaita ni *pandemic*; kila Taifa lina-*approach* yake namna katika kukabiliana na tatizo hili. *Approach* yetu kama Tanzania lazima tuikubali na tuisimamie, tusiige za wenzetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huo, napongeza sana hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitao jana na mfululizo, hata wiki iliyopita kwamba Watanzania tusiwe na hofu kuhusiana na janga hili la *Corona*. Wakati mwengine matabibu wanasesma, hofu inaua zaidi kuliko ugonjwa wenyewe. Unapokuwa na hofu zaidi ndipo ambapo zaidi ya asilimia 70 ya ugonjwa ambaa unaumwa unapata nafasi na mtu kuona hawezi tena kupona kwa kuwa tayari ameshajiwakea kwamba hili jambo haliwezekani, kumbe linawezekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano pamoja na Manaibu wake wote na Makatibu Wakuu wote pamoja na wasaidizi wengine katika taasisi ambazo zipo chini ya Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana nampongeza pia kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Rais wetu kwa sababu mwaka 2019 Aprili alikuja katika Jimbo langu la Busokelo na aliahidi kutengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya kutoka Katumba – Ruangwa – Mbambo – Tukuyu. Hivi ninavyozungumza, tayari kilometra 10 zimeshatengenezwa na kilometra nyingine zaidi ya 17 wanafanya maandalizi ya utengenezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri na Waziri Mkuu pia namshukuru sana, nakumbuka mwaka 2018 aliwaahidi wananchi wangu alipokuja kule Busokelo kwamba barabara hii tutahakikisha ipo kwenye llani kwa miaka zaidi ya 15 inatengenezwa. Kweli kauli zao zinaishi na leo hii wanafanya kwa vitendo. Nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna jambo hili la barabara ya kutoka Mbambo kwenda Ipinda. Alipokuja Mheshimiwa Rais nimeona kwenye bajeti, nawashukuru sana kwamba zimeshawekwa fedha za kuanzia pamoja. Katibu Mkuu wa Wizara hii *Architect* Julius Mwakalinga kwa sababu alikuwepo wakati Mheshimiwa Rais anatoa maelekezo haya, nawashukuru sana kwa sababu tayari wameshaanza. Ni mwanzo mzuri hata kama wametenga fedha ambazo siyo nydingi sana, lakini wananchi wa Busokelo wanajua kwamba kauli aliyoitamka Mheshimiwa Rais tayari imeshaanza utekelezaji wake. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali itusaidie barabara ya kuunganisha Jimbo la Busokelo na Jimbo la Makete ambayo mara nydingi nimekuwa nikisimama hapa Bungeni nikiomba kwa maana ni ya Mkoa kati ya Mkoa wa Mbeya na Mkoa wa Njombe, kupitia Vijiji na Kata za Luteba mpaka kule Makete yenye kilomita saba. Wananchi tumelima kilomita tano, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo tumeshindwa kulima hii barabara kwa sababu ya miteremko mikali na madaraja makubwa.

Niombe Serikali iweze kulisikia hili na iweze kutusaidia kwa ajili ya kukamilisha hii barabara ambayo itakuwa kiungo muhimu sanakwa Jimbo la Busokelo badala ya mwانanchi kusafiri zaidi ya kilomita 150 atasafiri kilomita zisizozidi 50 kwenda kutibiwa hospitalini ama kule Ikonda pamoja na Mkoa wa Njombe. Pia itakuwa fursa nzuri kwa Hifadhi ile ya Kitulo, kwasababu tayari inaleta watalii wengi na pia barabara hii ina historia kwasababu ilianzishwa na mkoloni Mjerumani miaka hiyo wakati akiwa anabebwa na mababu zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija katika suala zima la daraja la Mbapa; tunaiomba Serikali kwa kuwa mpo kutengeneza barabara hii ya Katumba – Rwamba – Mbamba - Tukuyu, pale wameweka daraja la chuma na kuna baadhi ya maeneo ambayo wananchi wangu wanazunguka mpaka upite Kyela ndiyo uende kwenye vile vijiji. Tunaomba lile daraja baada ya kukamilika hii barabara, basi lile daraja

lihamie katika Vijiji vya Nsanga kuunganisha na Ntaba ili wananchi wale wasizunguke kilomita zaidi ya 50 kwenda majumbani kwao ama wakati wa kutibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie hili suala zima la Bodi ya TEHAMA; mimi ni mdau muhimu katika sekta hii ya /CT na nimekuwa pia nikizungumza hapa Bungeni kwamba, bodi hii itatusaidia sana Watanzania wale waliosoma /CT ili iweze kuanzishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua muda si rafiki, lakini itoshe tu kusema naunga mkono hoja za Serikali ambazo ziko mbele yetu na kwa asilimia mia moja. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimemwita Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Kilango Malechela na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele ajiandae.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Kama ilivyo ada nachukua nafasi hii kumpa pole Spika wa Bunge na Wabungewenzangu kwa vifo hivi ambavyo vimetufika katika wiki moja hii iliyopita. Namwomba Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema awape furaha ya milele na mwanga wa milele awaaangazie wenzetu. Pia nampa pole Waziri Mkuu na timu yake kwa jinsi ambavyo wanaongoza hili janga ambalo limetupata. Unaweza kuwepo upungufu lakini wenzetu wako kazini, lazima tuwatie moyo ili waweze kuendelea na kazi yao vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kanuni ya Bunge ya namba 146(1) inaeleza kwamba wajibu namba moja wa Mbunge ni kuhudhuria vikao vya Bunge na Kamati za Bunge. Pia kanuni ndogo ya (4) na (5) inaeleza kwamba Mbunge akiwa na udhuru ni lazima apate ruhusa ya Spika na hiyo ruhusa aipate katika Ofisi ya Bunge Dodoma, au Ofisi ya Bunge Dar es Salaam. Sasa mimi niko hapa kwasababu sina ruhusa na niko hapa kwasababu naujua wajibu wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tuna matatizo lakini sisi tuna nafasi kwenye Kamati ya Uongozi ya Bunge, tuna nafasi kwenye Tume ya Utumishi ya Bunge, tuna nafasi kwenye Tume ya Kanuni ya Bunge, ambapo hoja yoyote inapita halafu inaletwa hapa. Tukishindana hapa ndio tunaweza tukachukua uamuzi, lakini hapa hakuna hoja ambayo imekwishafika ikajadiliwa tukashindwana halafu tukachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote ni kwamba hoja ikijadiliwa hapa lazima itoke Serikalini, ushauri wangu ambao ningeweza nikatoa, Serikali ituletee hoja hapa namna ambavyo hili janga liliyvo au ituletee hoja hapa kutuambia wenzetu kilichowaondolea uhai wao ni kitu hiki, kwa namna hii na hii na hii lakini mpaka sasa hivi, hivi nikifika pale Rombo nikiulizwa ehe tuambie hali ikoje nitasema nini? Au nikiambiwa enhe wenzako walikuwa kwa *corona* nitasema nini, nitakuwa napiga majungu tu. Kwasababu kwa uhakika kabisa, kwa uhalsia hakuna Mbunge anayeweza akasimama hapa akasema marehemu fulani Mbunge mwenzetu alikuwa kwa kitu hiki, nani? Asimame. Spika hajatuambia.

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo yanaendelea tu ya majungu majungu kwenye mtandao na nini na nini. Sasa mimi siyo sehemu pamoja na hayo niseme na hiki nataka kieleweke; ukishakuwa *parliamentary part*, chama kikisha kuwa ni chama cha kibunge kiko ndani ya Bunge ni sehemu ya Serikali na kwasababu hiyo ni lazima chama kijadiliane na Serikali, kujadiliana na Serikali hakuwezi kuwa usaliti hata siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachosema, huu ni Mkutano wa mwisho wa Bunge la Kumi na Moja, kama kuna haja Bunge hili lihitimishwe kabla ya muda wake wa kisheria, uko pia utaratibu tunaweza tukamwomba Mheshimiwa Rais kwa kutumia kanuni ya 30 kwamba Mheshimiwa ahirisha Bunge mapema, lakini siyo sisi tutake kutoka kabla ya wakati bila utaratibu kufanyika. Yote haya yako kwenye kanuni na kanuni zinaweza zikatumika tu kufanya kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme na niombe kwa nguvu zangu zote, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi *TARURA* ina ufinyu wa pesa na hili ndilo watu wa Rombo wamenituma. Bajeti ya *TARURA* Rombo ni milioni 700 tu na barabara zote zimevunjika na mvua zilizonyesha. Kwahiylo Mheshimiwa Waziri naomba kama inawezekana *TARURA* wakakaa na *TANROADS* vyote hivi ni vyombo vyetu, wakaona namna ambavyo *TARURA* itakavyoongezewa fedha ili iweze kurekebisha barabara ambazo zimevunjika nchi nzima na wala siyo Rombo peke yake. Vivuko vimevunjika madaraja yamevunjika nakadhalika nakadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kumwomba Mheshimiwa Wazirina hili limezungumzwa mara nyingi, miaka yote nazungumza, Rombo kuna mwingiliano mkubwa wa mitandao kati ya mitandao yetu na Kenya na hilo ya Kenya ikila, inakwenda kwenye *roaming*, kwahiylo wananchi wanaibiwa sana pesa zao. Jambo hili nimelisema mwaka 2011, 2012 na mpaka sasa hivi naendelea tu kulisema, Mheshimiwa Waziri aangalie namna ya kutatua hili tatizo. Nimeshaongea na Naibu Waziri mara nyingi akaniambia kuna ujeuri unaofanyika kwa wenzetu huko Kenya. sasa waangalie namna ya kurekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, miaka ambayo marehemu mzee Ndesamburo alikuwa hapa Bungeni alizungumza sana kuhusu reli ya Moshi na akaomba ile reli ifufuliwe iende mpaka Arusha mpaka Voi, mwaka huu nimeona treni imeleta watu Moshi, ni jambo zuri isipokuwa Mheshimiwa Waziri afanye jitihada kurekebisha kwasababu kuna maeneo mengine mataruma yameharibika, mataruma hayapo nakadhalika nakadhalika, itatusaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia kengele nakushukuru sana, nawatakia kila la kheri. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Anna Kilango Malecela, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele na Mheshimiwa Joseph George Kakunda ajiandae

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kukushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuzungumza leo ndani ya Bunge lako. Kwa unyenyekevu mkubwa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini nichukue nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo yote anayoyafanya, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu lakini nisisahau kabisa kulipongeza Baraza la Mawaziri, wanafanya jitihada sana. Pia nimalizie kwa kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Mheshimiwa *DC* wangu ambao tuko nao tunashirikiana, kufanyakazi katika Wilaya ya Same.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo naomba nizungumze hasa, naomba nizungumze barabara mbili ambazo zina historia kubwa ndani ya Bunge hili. Barabara hizi nimezungumzia Bungeni hapa Mheshimiwa Kamwelwe anisikillize vizuri, tena vizuri sana na ninauhakika na Mheshimiwa Rais atapata meseji ya haya ninayoyazungumza leo, kwa sababu naye anahistoria katika hizi barabara mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kwanza barabara ya Mkomazi – Kisiwani – Same, kilomita 97; hii ni barabara iliyoko Jimbo la Same Mashariki ninakoishi mimi na ninakotoka mimi. Barabara ya pili ni barabara ya Hedaru – Vunda - Miamba ina kilomita 42. Sasa naomba nianze hii barabara ya Mkomazi – Kisiwani - Same. Hii barabara nimeanza kuiongelea ndani ya Bunge hili mwaka 2001 nikiwa msichana kuzidi wewe, mpaka leo ni 2020 ni mama wa nguvu. Kwahiyo naomba hii barabara Mheshimiwa Kamwelwe aingalie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Waziri, nawapongeza Manaibu Waziri wote kwa jitihada kubwa walizozifanya kuitengea hii barabara bilioni tano. Kwanini nasema hivyo? Mwaka 2009 hii barabara ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami Maore kilomita tano, Ndungu kilomita tano, ilianza kuweka lami Kihurio kilomita tatu, Same kilomita tano, Kisiwani kilomita tatu. Kwahiyo Serikali ilianza tangu mwaka 2009 kuanza kuweka lami, lakini kipindi hiki Serikali

imeamua kutenga bilioni tano kwa ajili ya barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na naomba niseme ukweli kwamba CCM muwe na uhakika wa kupata kura za nguvu Wilaya ya Same shauri ya barabara hii. Hii barabara ni nzito inabeba maisha ya wananchi kuanzia Mkomazi mpaka Same. Mkomazi, Bendera, Kihurio, Ndungu, Maore, Kisiwani mpaka Same, hapa tunalima mpunga na hapa tuna Mkomazi *National Park.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi, nampongeza na Mheshimiwa Kamwelwe na Wizara kwa ujumla, lakini nampongeza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hii barabara anaipenda hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili barabara ya Hedaru – Vunda - Miamba iko Same Mashariki. Hii barabara nimeisemea hapa tangu nikiwa msichana mpaka leo ni mama wa nguvu, hii barabara ni nzito, kilomita 42. Hii barabara ina historia na Rais Magufuli tarehe 2 Machi, 2015 alikuja Kata ya Kihurio, Same akaipandisha hadhi barabara hii ikawa barabara ya mkoa ikatoka *TARURA*. Hii barabara ikajengwa kama kilomita tano au saba hivi, ikaanza kujengwa na mkoa. Mwaka 2006 hii barabara ilishushwa hadhi ikarudishwa kwa *TARURA*, *TARURA* hawezo kujenga hii barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Kamwelwe anisikilize vizuri, *TARURA* hata wafanyeje hii barabara hawaijengi, ni korofi mno, ni barabara ambayo ipo kwenye milima mirefu sana, nina uhakika aliyeweza kufika kwenye hii barabara mpaka Vunda ni Naibu Waziri wa Nishati peke yake na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alishafika kwenye hii barabara. Hii barabara haiwezi kujengwa na *TARURA*, ni barabara ambayo miundombinu inahitaji vifaa vikali na vikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, naomba niwanyenyeknee hii barabara bora wangeirudisha kwenye ile hadhi ya kuwa barabara ya mkoa au waipeleke *TANROAD*ili wale wananchi nao waishi, bila hivyo wale wananchi hawana barabara kabisa.(*Makofi*)(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika,kwa unyenyekevu mkubwa, naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anavyokwenda na huu ugonjwa wa *corona*, ina maana anawasaidia wananchi maana yake ukisemahili Bunge lifungwe, umefunga wananchi. Nchi itakwendaje bila ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana.(*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele nilikuwa nimeshamtaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph John Kakunda na Mheshimiwa Ally Mohamed Keisy ajiandae.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika,nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hotuba ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Wizara ambayo kimsingi ndiyo inayobeba sura halisi ya Taifa letu la Tanzania. Nasema hivi kwa sababu maadui wa Taifa letu ni watatu; maradhi, ujinga na umaskini. Serikali yetu ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt Magufuli, maadui hawa imewashughulikia ipasavyo. Ukiangalia kwenye Sekta ya Afya ambako maradhi ndiko yaliko, Serikali imejenga vituo vya afya, imejenga hospitali za rufaa, inatoa pesa kwa ajili ya madawa na kwaajili hiyo upande huo Serikali yetu imefanikiwa vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa ujinga Serikali yetu imefanya kazi nzuri sana, imekarabati mashule, imetoa pesa kwaajili ya elimu bila malipo. Tukija kwenye upande wa umaskini Serikali yetu kuititia Wizara yetu hii ya Ujenzi ndiyo mahali pake. Wizara hii imeifanya Tanzania ianze

kung'ara katika mataifa, Wizara hii imesababisha dunia itambue Tanzania kwamba ipo na ndyo maana hata mji wetu wa Dar es Salaam umewekwa katika ile miji ambayo wanaiita *the most beautiful and advanced cities in Africa*. Ni kitu ambacho hapo awali usingeweza kukitarajia, watu wanarusha matangazo kuonyesha Jiji letu la Dar es Salaam kwamba ni mionganoni mwa miji mizuri, inaanza kulinganishwa na miji kama Nairobi, Johannesburg, Cairo, unajua sasa kwamba kumbe na sisi tunaelekea kweli kwenye Tanzania ya uchumi wa kati na Tanzania iliyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, mhimili wa mambo yote haya ni Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwasababu tunaona *Standard Gauge Railway* inajengwa kwa kasi, viwanja vya ndege viko vya uhakika, ndege mpya kabisa za kisasa ambazo tulikuwa tunaziona kwenye mataifa yaliyoendelea *dreamliners* na vitu vingine Tanzania ndiyo mahala pale sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwahiyio nataka niseme tu kwamba ndugu yangu Mheshimiwa Kamwelwe, Mheshimiwa Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye, hongera sana kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea nayo. Pia niseme kwamba Wizara yao inavyolitendea haki Taifa la Tanzania, ndivyo hivyo hivyo wanavyowatendea haki wananchi wa Mbogwe. Kwasababu zipo barabara ambazo kwa kweli kila mara nimekuwa nikizisemea hapa nikizombea kwa Serikali ziweze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ya kutoka Butengolumasa, Ipalamasa, Mbogwe, Masumbwe ambayo hiyo hiyo tunatarajia itaunganisha Mkoa wa Shinyanga kupitia Wilaya ya Ushetu mpaka Kaliua Tabora hata Mkoa wa Katavi ambako Mheshimiwa Waziri Kamwelwe anatoka. Naomba hii barabara kwa kweli waitendee haki ili sisi wananchi wa Mkoa wa Geita tuweze kuungana na wenzetu wa Mikoa ya Tabora, Katavi, Rukwa, Songwe mpaka na kwingineko ambako inawezekana mwisho wa Bara letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa Joseph George Kakunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Mohamed Keisy na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajabu ajiandae.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wanasikonge naomba nianze kwa kutoa pole kwa Watanzania wote waliofiwa na wapendwa wao, wakiwemo viongozi ambao wametutoka hivi karibuni na leo hii hapa Bungeni Mheshimiwa Mwijage amefiwa na mjomba wake na mtoto wa mjomba wake, siku moja, hao ni ndugu kwa kweli tunawapa pole sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo huo nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa hotuba yake ya jana ambayo ni mwongozo na maelekezo kwa Watanzania wote kuhusu janga la *coronana* pia ameagiza dawa. Hii ni hatua ambayo ni kubwa sana inayoonyesha kwamba Rais wetu ni Rais ambaye ana utu na huruma kwa Watanzania wote. Ahsante sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Wizara hii ya Ujenzi, napongeza sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, msimamizi wa Serikali wa kila siku na kwa kweli kazi ambayo inafanywa kuitia sekta hizi ambazo zinaongozwa na Mheshimiwa Kamwele inaonyesha kabisa kwamba Mheshimiwa Rais amedhamiria kuchora ramani mpya ya kimaendeleo katika nchi hii inayoitwa Tanzania. Ramani huonyesha watu, barabara, reli, viwanja vya ndege, madaraja, bandari na kadhalika. Kazi inayofanywa na Wizara hii ni kazi ambayo ndani ya muda mfupi ujao, kwa yaliyofanyika, kwa yanayofanyika na kwa yatakayotekelizwa katika sekta hizi tutaandika historia mpya ya kimaendeleo ambayo itaogopwa, siyo itaogopwa na majirani tu bali itaogopwa na dunia nzima. (*Makof*)

Mheshimwa Naibu Spika, kuna mwandishi mmoja mwanafalsafa anaitwa Niccolo Machiavelli, aliandika kitabu maarufu sana chenye ushauri kwa viongozi lakini kubwa zaidi katika kitabu chake amesema viongozi wapo wa aina mbili duniani; wapo viongozi ambao wanaiishi historia lakini kuna viongozi ambao kazi yao huwa ni kuandika historia. Sisi tunaye Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ye ye kazi yake kubwa ni kuandika historia. Hii ni sifa kubwa kwa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, kule kwangu Sikonge yaliyofanyika katika miaka hii mitano ni historia kubwa sana. Barabara nyingi zimejengwa mfano barabara ya Tabora – Mpanda; Dodoma – Tabora; na kuna barabara ilikuwa imepandishwa hadhi miaka 10 iliyopita ilikuwa haijatobolewa lakini ndani ya miaka hii mitano imetobolewa kutoka Sikonge – Kipili. Pia kuna barabara ambayo inaendelea kutobolewa kutoka Inyonga kwa Mheshimiwa Kamwele kuja mpaka Kitunda. Hizi ni historia ambazo zimefanywa katika kipindi hiki. (*Makofii*)

Mheshimwa Naibu Spika, lakini changamoto zipo hasa ambazo zimeletwa na mafuriko. Mimi nawaombea Mwenyezi Mungu awape nguvu zipatikane fedha za kurudishia miundombinu ambayo watu wa *TARURA* na wadau wa barabara walikuwa wameshaitekeleza ili turudi katika hali ya kawaida. Kwa kweli miundombinu hii tukiirudisha katika hali ya kawaida tutakuwa tumefanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilichoshangaa kidogo tu ni kwamba wiki mbili zilizopita tuliletewa taarifa kwamba zinahitajika shilingi bilioni 73 kwa ajili ya kukarabati maeneo ambayo yameharibiwa na mafuriko, mimi siamini. Kichwani mwangu nilikuwa naamini kwamba zinahitajika zaidi ya shilingi bilioni 700, kama kweli zinahitajika shilingi bilioni 73 basi hawa watu wapewe hizi fedha, hata kama kutoka kwenye mafungu mengine ili kusudi turidishe hizi barabara za vijiji ni katika hali ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi yangu maalum kabla hata kengele hajaipiga, kwa kweli mimi ni mdau mkubwa sana wa Wilaya yangu ya Sikonge na Mkoa wa Tabora na vilevile ni mdau wa maendeleo ya nchi nikiwa Mchumi. Barabara kuu ambayo inaunganisha Tabora - Mbeya inaitwa Tabora - Sikonge - Ipole - Rungwa - Mbeya kupita Makongorosi na Chunya, hiyo ndiyo barabara kuu (*trunk road*) ambayo ilichorwa mwaka 1964 mpaka leo vinajengwa vipande vipande. Nafikiri kwamba barabara hii tuiwekee kipaumbele maalum kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku nilimpigia simu Mkurugenzi Mkuu wa *TANRODS*, tulikuwa tunazungumza kuhusu barabara hii, akasema ngoja tukusanye nguvu ili tuweze kupata fedha za kujenga barabara hii. Nawaombea kila la kheri Mwenyezi Mungu awawezeshe ili fedha ipatikane hatimaye barabara hiyo ijengwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, Mwenyenzi Mungu awabariki Waziri Mkuu na Waziri, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Mheshimiwa Ally Mohamed Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtataru ajiandae.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza naunga mkono hoja ya Wizara hii kwa asilimia 100, mapema kabisa, kwa kuwa kwenye Jimbo langu la Nkasi wamefanya vitu vya ajabu kabisa. Nawashukuru Mheshimiwa *Engineer Kamwele*, Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, Mheshimiwa *Kwandikwa* na *Engineer Kakoko* na Mkurugenzi wa Bandari pamoja na Bodi ya Bandari. Kusema kweli wamefanya jambo la maana sana Bandari ya Kabwe imekamilika kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Kagwe imejegwa kwa thamani ya shilingi bilioni 7.4. Kwa hiyo, sasa tumejengewa bandari lakini kitu cha ajabu bandari hiyo

imekaa kama lisanamu, hatuna meli. Kila bajeti ikija hapa tunaahidiwa meli Liemba itatengenezwa kwa shilingi bilioni 10 mwaka jana, mwaka juzi lakini mpaka leo Meli Liemba hajitatengenezwa. Tunaahidiwa meli mpya miaka sita leo hatujapata meli mpya Ziwa Tanganyika. Watu wa *TPA* wanafanya kazi ya ziada lakini usafiri katika Ziwa Tanganyika mpaka sasa hakuna. (*Makof!*)

Mheshimwa Naibu Spika, kwenye bajeti safari hii imeandikwa tena meli mpya Ziwa Tanganyika na ukarabati wa Meli ya Liemba. Naomba Mheshimiwa Waziri kwanza anza kuifufua Meli ya Liemba mapema kabla ya hiyo meli mpya maana itachukua muda mrefu, wapelekeeni hizo fedha. Mwaka jana mliahidi mtapeleka shilingi bilioni 10, nikamuona Waziri wa Fedha akasema kweli kwenye bajeti imeandikwa lakini hamjapeleka hata senti tano. Pelekeni kwanza shilingi bilioni 10 mfufue Meli ya Liemba halafu hiyo meli mpya baadaye ili wananchi wapate usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ziwa Tanganyika hamna usafiri miaka nenda miaka rudi. Naona hapa mmeandika mnafufua kwanza Meli ya Sangara, sijaona Meli ya Mwongozo hapa, kama Meli ya Mwongozo imewashinda pigeni bei. Meli ya MV Mwongozo imekaa pale miaka na miaka haina kazi yoyte iuzeni mpate fedha ya kufufua meli nyingine, haiwezi kukaa kama sanamu pale kupoteza fedha tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu kila kijiji kina mawasiliano safi lakini usikivu katika vijiji viwili bado, vijiji vyia Lyazumbi na Kizi. Kuna mnara pale lakini minara yenye we sijui namna gani bado hamna usikivu mzuri. Hata hivyo, kwenye jimbo langu Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana minara kama uyoga kote mawasiliano ni mazuri kasoro vijiji hivyo viwili, nashukuru sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kusema *TANROADS* ipunguziwe fedha zao ziende sijui wapi, hapana. Tuongeze fedha *TARURA* na *TANROADS* vilevile nao wapewe fedha na

mvua imenesha sehemu zote, nao wana barabara za vumbi zimeharibika. Barabara yangu kutoka Lyazumbi - Kabwe imeharibika ni ya *TANROADS*. Barabara toka Kilango - Namanyere imeoza kabisa ni ya *TANROADS*, haipitiki vizuri imeharibika, mvua ilikuwa kubwa mwaka huu. Nchi nzima barabara za *TANROADS* zimeharibika na za *TARURA* zimeharibika. Sasa tuseme tuchukue fedha za *TANROADS* tupeleke *TARURA*, hapana, tutafute fedha ziongezwe sehemu zote maana barabara zote zimeharibika nchi hii, hazipitiki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na maombi mengine maalum, mwambao wa Ziwa Tanganyika mvua ni kubwa maji yameongeza mita nne mpaka Bandari ya Kipili imezama, nyumba Kilando zimekwisha kabisa, kule mwambao mwa Ziwa Tanganyika hakuna nyumba tena, hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, tuwatengenezee upya ile Bandari ya Kipili na bandari ndogo ile ya Kabwe ya maboti imezama vilevile yaani maji yameongezeka mita tatu bandari zote hizi ndogo ndogo, Bandari ya Kabwe kwa sababu ilijengwa kisasa hii yenye ipo vizuri kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshukuru sana Serikali kuhusu kuweka lami barabara ya Namanyere - *Kipili Port* mmeandika hapa, sasa hii kazifanyike haraka, siyo kila wakati iko kwenye bajeti. Ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye ulikwenda mpaka kule ukaona mwenyewe hali ilivyo na nishukuru mwaka huu tena umeandika.

Mheshimiwa Naibu Spika, halafu sikuona tena kuhusu barabara kutoka Sumbawanga kuunganisha mpaka Mpanda kwa lami, Mzee Kamwele vipi tena? Mheshimiwa Rais alipokuja akasema mtapata fedha za mafisadi ili zimalize ile barabara kutoka Kibaoni kwenda Mpanda lakini kwenye bajeti hamna. Inaonyesha barabara inaishia porini tu tunaanza kupita Sumbawanga - Mpanda pale pana vumbi moja kwa moja hapapitiki. Mkao wote umeandika hapa lakini kuunganisha kwa lami kutoka Mpanda - Sumbawanga pale katikati mpaka leo bado. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga, kila bajeti ikija Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga, fidia ilishalipwa lakini haujengwi. Alipewa mkandarasi lakini mpaka leo hamna kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kuhusu *Corona*. Waheshimiwa Wabunge wengi wanazungumza habari ya *Corona*, *Corona* lakini sijasikia hata Mheshimiwa Mbunge mmoja anasema tukatwe posho ya siku mbili iende Wizara ya Afya, wote tumekaa kimya. Tunaona wengine wanachangia, wafanyabiashara wanachangia tunaona Waziri Mkuu anapokea lakini hatujaona Waheshimiwa Wabunge humu ndani tunachangia hata posho ya siku mbili kupeleka Wizara ya Afya.

Mheshimwa Naibu Spika, kazi yetu kuilaumu Serikali, Serikali haijafanya hivi na sisi Waheshimiwa Wabunge tuchange mbona michango mingine tunachanga humu Bungeni kama ya harusi? Mbona *Corona* sijasikia Mheshimiwa Mbunge anachangia humu kwamba tukatwe? Kwa hiyo, nashauri posho ya siku mbili ikatwe kwa ajili ya *Corona*. Maana ni kelele tu lakini hakuna hata Mheshimiwa Mbunge mmoja anasimama hapa anasema na sisi Waheshimiwa Wabunge tuchangie. Kwa nini Waheshimiwa Wabunge wasichangie? Ni lazima na Waheshimiwa Wabunge wachangie. Wacheza mpira huko Ulaya wanachagia lakini Waheshimiwa Wabunge humu ndani sijasikia hata kukatwa mishahara yao, kazi kulaumu Serikali, hakuna cha kulaumu Serikali na sisi tuchangie. Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge tukatwe posho ya siku mbili tuachangie *Corona*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Keissy kengele imegonga.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani.

**NAIBU SPIKA:** Hili jambo kutokea kwa Mheshimiwa Keissy huo ni muujiza mkubwa sana, lazima kuna mabadiliko makubwa sana yanaendelea. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Keissy kwa mawazo hayo. (*Kicheko*)

Nilikuwa nimeshamtaja Balozi Adadi Mohamed Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtataru, Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima ajandidate.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru kupata nafasi hii ya kuchagia hoja ambayo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kuunga na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake ya jana ambayo imewatoa hofu Watanzania wengi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuwashukuru ndugu zetu hawa wa Upinzani wakiongozwa Mheshimiwa Silinde kwa kuweza kuhudhuria kikao hiki leo kwa sababu jinsi walivyojiweka karantini *for two weeks* ina maana wiki mbili zikimalizika si watarudi humu na wakirudi humu sisi hatukuwa karantini, sasa ina maana gani? Ingekuwa na mantiki kama wangekaa kabisa moja kwa moja mpaka *Corona* iishe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia hasa kuhusu barabara ya Amani - Muheza. Barabara hii ni kilio kikubwa sana cha Wana-Muheza kwa sababu barabara hii ndiyo uchumi wa Muheza.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii yenye urefu wa kilomita 40 ni muhimu sana. Awamu zote za Serikali hii zimeshindwa kutetea barabara hii lakini Awamu hii ya Tano chini ya Mheshimiwa Rais imethubutu na imeweza kuanza ujenzi wa barabara hii ya Muheza - Amani. Nakushukuru sana Mheshimiwa Rais na namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kilio kikubwa ambacho aliambiwa na Wana-Muheza nakumbuka ni maji

pamoja na barabara hii. Kwa hiyo, *contractor* yuko *site* na ameshaanza kutengeneza *camp* kwa ajili ya kuanza ujenzi. Isipokuwa tunamwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe basi ile *advance payment* yake anapata mapema ili kazi hii isisimame aweze kuendelea moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunashukuru sana kwa sababu pamoja na barabara hii barabara yetu ya Tanga - Pangani ambayo inapita kwenye Kata yangu ya Kigombe na yenye we imetengewa fedha na kuanza matayarisho ya mwanzo kwa ajili ya ujenzi huo. Sisi watu wa Muheza na Tanga hatuna cha kuwalipa bali tunatawalipa hiyo 25 Oktoba, 2020. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la mawasiliano. Naibu Waziri Mheshimiwa Nditiye alifika Tarafa ya Amani ambapo kuna tatizo kubwa sana la mawasiliano. Alikuta TTCL wameweka 2G na aliahidi na akamwamuru Mkurugenzi Mkuu aweze kuweka 3G ambapo mawasiliano yanaweza kuwa mazuri lakini bado haijaanza kuwa *implemented*. Tunaomba kwamba suala hilo liweze kupewa umuhimu wake ili 3G ianze pamoja na kuongezwa minara kwenye Tarafa yote ya amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, treni ya abiria kutoka Dar es Salaam mpaka Arusha imeanza. Haikuweza kwenda Tanga kwa sababu kulikuwa na matatizo ya mafuriko na reli iliharibika. Sasa hivi reli ipo sawasawa na tunaomba sasa safari za abiria kutoka Dar es Salaam kwenda Tanga treni hiyo iweze kuanza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wameongelea suala la *airport* ambapo sioni kwenye makadirio ya sasa hivi kuongezwa fedha ya kuweza kupanua kiwanja kile kwa sababu tunaamini kwamba kwa sababu uchumi wa Tanga utakuwa mkubwa kwa muda mfupi tu na wawekezaji wengi watataka kuja kwa njia ya ndege na tunahitaji *Bombardier* iwe pale. Nakumbuka Mheshimiwa Waziri aliahidi kwamba ataleta *Bombardier* ambayo itakwenda Tanga, Pemba

mpaka Dar es Salaam. Tunaamini kabisa kwamba ahadi hiyo ataitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru pia kwa kuongeza kina Bandari yetu ya Tanga pamoja na kupanua yale magati 1 na 2. Hii itasaidia sana kuweka *competition* na bandari ya wenzetu ya Mombasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *road toll* ambalo limekuwa halipewa umuhimu wake mkubwa ni muhimu sasa hivi likaanza kupewa umuhimu. Mimi sijaenda nchi yoyote nikakuta hakuna *road toll* ambapo watu wanalipia barabara zile za *express* na kadhalika. Kwa hiyo, nitashukuru kama utaratibu huu utaweza kuanza kwa sababu juhudhi ambazo Serikali inafanya sasa hivi naaamini kama zingeweza kuwa *implemented* na *road toll* basi sekta binafsi ingeweza kuchangia kwa kiwango kikubwa sana na tatizo la barabara lingeweza kupungua kwa kiwango kikubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaratu atafuatiwa na Hasna Sudi Mwilima na Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii muhimu ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hakika nianze kwa kumshukuru Mwenyenzi aliyetujalia uzima na afya kukutana jioni ya leo. Kama hiyo haitoshi nimshukuru sana Rais wetu mpPENDWA Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa anayoifanya katika kuingoza nchi yetu na kwa msimamo wake thabiti kuendelea kuwahurumia wanyonge Watanzania kuititia maelekezo yake aliyoyatoa jana. Kwa hakika ile shehena kutoka Madagascar Watanzania tunaisubiri kwa hamu sana ili ije kutuponyesha kabisa tatizo

hili la *Corona*. Siku zote kiongozi anatakiwa kuwa na hekima na kusikiliza maneno yote na kuyachuja na kutoka na busara kubwa kama aliyotoka nayo jana Mheshimiwa Rais na ambayo kwa kweli imetupa faraja Watanzania wote. Tunamshukuru sana Mhesheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili katika kumshukuru Mheshimiwa Rais, sisi wana Singida juzi alitufanyia jambo kubwa. Naomba nichukue nafasi hii kumshukuru sana kwa kumteua Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Wana Singida tumefurahi sana na kwa hakika tumefarijika kwa kumleta kaka yetu kuwa mionganini mwa Serikali. Tunashukuru sana. (*Makoffii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nianze kuchangia bajeti hii ya Wizara yetu ya Ujenzi ambayo kimsingi inafanya kazi kubwa. Kama ambavyo wote tunajua ujenzi ndiyo roho ya maendeleo. Ujenzi na Mawasiliano duniani kote ndiyo ambayo inaongoza katika kuleta maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Waziri pamoja na Naibu Waziri na Makatibu Wakuu wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuratibu shughuli nzima za ujenzi na mawasiliano. Tumeona mambo mengi yamefanyika, barabara zimejengwa, reli za kisasa zinajengwa, hiyo yote ni kuonyesha dhamira ya Serikali katika kuhakikisha kwamba inabadilisha kabisa tatizo la miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shukrani hizi, nasema kwamba kwenye maeneo yetu bado kuna changamoto. Nichukue nafasi hii kwanza kuishukuru sana Serikali kwenye ile barabara inayoitwa Singida - Kwa Mtoro - Kiberashi - Tanga mwaka huu imeingizwa kwenye mpango kwa ajili ya kuanza kujengwa na wametenga shilingi bilioni sita. Kwa maana ya ujenzi wa barabara fedha hizo ni ndogo, naomba sana Serikali itafute fedha ili iweze kujenga vizuri barabara hiyo ambayo ina urefu wa kilomita 462.

Mheshimiwa Naibu Spika, najua barabara hiyo inaenda kugusa maisha ya wananchi wetu wa Kata za Siyu, Maklungu, Mungaa na Misughaa ndiyo inaenda kule kwa jirani yangu Kwa Mtoro. Nichukue nafasi hii kuiomba Serikali iweze kutenga fedha na mkandarasi apatikane ili barabara hiyo ianze kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara mwaka huu zimekatika sana ikiwepo barabara hii. Barabara nydingine ambayo pia ni ya *TANROADS*ni inayotoka Ikungi kwenda pale London mpaka inaenda kutokea Kilimatinde nayo imekufa kabisa. Kwa hiyo, niombe lifanyike jambo la dharura kuhakikisha fedha za kutosha zinapatikana kuisaidia barabara hii irudi katika hali ya kawaida na kurudisha mawasiliano kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama hiyo haitoshi wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja katika Wilaya yetu ya Ikungi, tulikuomba angalau barabara za mjini pale zipate lami hata kama ni kilomita 3. Alitoa maelekezo namshukuru sana lakini kuititia maelekezo yake yale niombe sana Serikali itusaidie kutujengea kwa lami barabara zilizopo katika Mji wa Ikungi ili zianze kuonesha sura nzuri ya mji ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi nieleze tu kwamba barabara zile nydingine za *TARURA* ninajua Serikali ni moja, barabara zimekufa kabisa mwaka huu. Barabara ile ya kutoka Ikungi, Dung'uni mpaka Makiungu, barabara ile ya kutoka pale Mungaa kwenda Lihwa mpaka Ntuntu barabara zimekufa hazipo kabisa, niombe sana wanapokuja basi watuambie namna ambavyo watasaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwenye jambo dogo na ni kubwa sisi Mkoa wa Singida tuko karibu na Makao Makuu Dodoma, sisi Singida ndiyo *backup* ya Mkoa wa Dodoma. Niombe sana uwanja wetu wa ndege, uwanja wa ndege umekuwa ukipangiliwa mipango muda mrefu angalau uweze kujengwa lakini mpaka leo ule uwanja wa ndege bado haujajengwa na haujatengewa fedha. Lakini kama ukipata dharura yoyote ya kutokutua ndege hapa

Dodoma maana yake sehemu karibu ni Singida, leo hii ukipata dharura maana yake utaenda Songwe au utarudi Dar es Salaam. Tulisema hii kwenye kamati ninaamini Mheshimiwa Waziri alituelewa, ninaomba sana nimuombe, niiombe sana Serikali iuzingatia uwanja ule tupate fedha uboreshwe ili barabara ile ikawe ni sehemu ya kuongeza uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninajua kengele imepiga nimalizie tu kwa neno dogo kwamba mtu ukimuweka kwenye goli ili akulindie goli na akaondoka ukafungwa maana yake analaumiwa yule ambaye alikuwa amekaa golini. Niwaombe Watanzania hawa walioondoka hapa ndani hawana dhamira na maendeleo yao, inapofika Oktoba hakuna sababu ya kuwachagua kwasababu hawako tayari kwa ajili ya kuleta maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja iliyopo mbele yetu, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilishamtaja Mheshimiwa Hasna Sudi Mwilima atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma, Mheshimiwa Peter Lijualikali ajiandae.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu wake kwa kazi nzuri wanazofanya katika Wizara hii japo wana changamoto kubwa sana ya mafuriko ambayo yameharibu miundombinu mingi nchini. Nianze kwanza kwa kutoa pole kwa wananchi wangu wa Ilagala kwa tatizo hili la Ziwa Tanganyika kuongezeka kina chake juu kimepelekea barabara ya Ilagala kuharibika wananchi wanatumia mitumbwi badala ya kutumia magari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa hii adha ni kubwa sana lakini niwaombe tu wananchi wangu wa Kijiji cha Kajeje, Kijiji cha Ilagala, Kijiji cha Sambala kwamba Serikali inaendelea kufanya kazi miundombinu hiyo. Kiwango kikipungua kidogo

nina imani Serikali itarekebisha hiyo miundombinu na usafari wa magari utaendelea kama kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwenye ukurusa wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 13 kuhusiana na barabara ya Uvinza – Malagarasi kilimeta 51.1. Nimeona hapa Mheshimiwa Waziri unaonesha kwamba mkandarasi yuko kwenye hatua za kupitia usanifu na makabrasha ya uzabuni. Sasa Mheshimiwa Waziri nilikuwa tu naomba nikumbushe huko nyuma kwenye bajeti ulikuja kutuambia kwamba wenzetu wa Mfuko wa Abu Dhabi walitusaidia fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii ya kilomita 51.1. Sasa Mheshimiwa Waziri hii barabara ni nyeti sana inayowezesha mizigo yote ya kutoka Dar es Salaam inayokuja Kigoma kwenda Congo, Burundi na Zambia ndiyo wanategemea barabara hii. Naomba tu Mheshimiwa Waziri kama zile fedha zipo na fedha nyingine za Serikali zipo basi mkandarasi akamilishe taratibu zote ili barabara hii iweze kukamilika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie pia barabara ya Simbokalya, hii barabara kwa muda wa miaka mingi sana inajengwa kwa kiwango cha udongo na changarawe. Sasa Mheshimiwa Waziri sijui kwanini kuna kigugumizi cha kupandisha hadhi barabara hii ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Tunaomba mlitafakari hilo kuliko kutumia kila mwaka billioni 1.9 kwenye bajeti ni bora ipandishwe hadhi ijengwe kwa kiwango cha lami hata kama itakwenda kwa faces mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kwasababu nazungumzia hiyo barabara ya Simbokalya Mheshimiwa Waziri nimeona kwenye kitabu chako hapa umezungumzia daraja la Malagarasi. Daraja la Malagarasi ndiyo daraja la Ilagala, sasa bajeti ya mwaka jana mwaka 2018/2019 ulizungumzia, mwaka 2019/2020 umezungumzia, mwaka 2020/2021 pia umezungumzia. Mheshimiwa Waziri wananchi wa Ilagala wamenituma na vijiji vyote kwa maana ya Kata ya Mwakizega, Ilagala, Sunuka, Sigunga, Herembe, Igalula, Buhingu na Kalya kwamba ni lini sasa usanifu wa daraja hili

la Malagarasi utaanza rasmi ili kupunguza ile changamoto ya kivuko ambako Mheshimiwa Waziri juzi tu umetusaidia kivuko kilikaa takribani wiki mbili bila kufanya kazi. Sasa tuondokane na masuala ya kivuko tujenge daraja kwasababu ipo kwenye bajeti mmeshaanza usanifu tuweze kuwavusha wananchi watokane na ile adha wanayoitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo nizungumzie pia barabara ya kutoka Bulimba kwenda Kijiji cha Ikuburu, Kijiji cha Lubalisi inayounganisha mpaka Mkoa wa Katavi kwenye Jimbo la Mwese. Mheshimiwa Waziri nimeshazungumza sana na wewe kuhusiana na hii barabara, hii barabara iko chini ya *TARURA*. *TARURA* hawana uwezo wa kuijenga hii barabara, hii barabara imeharibika, hii barabara ina mawe, hii barabara ina milima kwa hiyo *TARURA* fedha wanayopata ni ndogo nilishaomba kwanini isipandishwe hadhi ikawa basi ni barabara ya mkoa ili *TANROADS* waitumie hii barabara na waweze kutengeneza hii barabara wananchi wa vijiji hivi vya Ikuburu pamoja na Lubalisi na Vitongoji vya Kamatandala waweze kuitumia hii barabara sasa hivi wanapata changamoto kubwa sana katika usafiri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niunge mkono kaka yangu Mheshimiwa Keissy kuhusiana na Meli ya MV Liemba, hii Meli ya MV Liemba ni meli ambayo ina historia. Mnaweka bajeti ya kutengeneza meli mpya mizigo na meli mpya ya abiria katika Ziwa Tanganyika. Sisi wananchi wote tunaotoka kwenye Ziwa Tanganyika kwa maana ya Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Kigoma tunaomba muanze na Meli ya Liemba na Meli ya Mwongozo. Kwanza wananchi wa Ziwa Tanganyika wapate kutumia Meli ya Liemba na Meli ya Mwongozo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tunatumia meli zinazotoka Kongo ndizo zinazosafirisha mizigo, ndizo zinazobeba abiria wanaokwenda Kongo kwa maana ya Kalemi, wanaokwenda Burundi wanatumia meli za Wakongo. Sasa tuombe Meli hii ya Liemba na Meli hii ya Mwongozo muikarabati ili basi Ziwa Tanganyika angalau tupate hata

meli mbili za kuweza kubeba mizigo na kubeba abiria.  
*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana kengele imeshagonga.

**MHE. HASNA S. MWILIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Shukrani sana, ahsante. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Maftaha Nachuma anachangia kutoka Msekwa atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Lijualikali, Mheshimiwa Mary Pius Chatanda ajiandae.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana kwa wananchi wa Tanzania. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhana wataalah, Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kunipa afya njema na leo hii nimesimama ndani ya Bunge lako hili Tukufu niweze kuzungumzia machache sana yanayohusu Wizara hii ya Uchukuzi na Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza napenda kikipongeza chama changu, Chama cha Wananchi CUF kwasababu wapo Waheshimiwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi wamesimama na kuzungumza na kusema kwamba wapinzani wamekuwa ni watu ambao hawaungi mkono bajeti. Sisi Chama cha Wananchi CUF ni chama ambacho kila mwaka pale ambapo pana mambo ya msingi ya kuunga mkono tunaunga mkono lakini yale ambayo yanapaswa kushauri huwa tunaishauri Serikali. Na sisi tunasema, jana nimezungumza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Chama Profesa Ibrahim Haruna Lipumba, Profesa wa Maprofesa duniani akasema kwamba hatuvezi kukimbia bajeti kwenye wakati huu mgumu lazima tuungane na Serikali kupambana na janga hili la Corona. Kwa hiyo, sisi CUF tupo ndani ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie machache kama ifuatavyo; jambo la kwanza niliwa kusema mwaka jana hapa kwamba Serikali inafanya kazi nzuri sana na niwapongeze hawa Waheshimiwa, Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer Nditiye*, Mheshimiwa Kwandikwa wanafanya kazi kubwa sana hakuna asiyefahamu. Hawa Waheshimiwa Mawaziri ni Mawaziri ambao ni wasikivu sana, ukiwaendea hawana ubaguzi hawajali wewe ni mpinzani, wewe ni chama tawala ukiwaendea wanakusikiliaza, wanasikiliza hoja zako na wanatatua hoja zako tena kwa wakati nawapongeza sana Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna barabara ambayo niliwa kuzungumza hapa inaitwa barabara ya Uchumi, barabara ambayo Mheshimiwa Rais alikuja kusaini kule Mtwara miaka mitatu iliyopita na aliwaagiza hili barabara iweze kukamilika ndani ya miezi 18. Tangu mwaka 2017 mpaka leo hii barabara haijakamilila, ni kilometra 50 tu kutoka Mtwara Mjini kuelekea Mnivata Jimbo la Nanyamba. Hata huku penyewe Mtwara Mjini ambako immeanzia kuna maeneo mengi bado ile kampuni haijaja kumalizia ule ujenzi pale Mtwara Mjini penyewe ambako barabara inaanzia. Wameanza kujenga baada ya kilometra 10, lakini kilometra 10 kutoka Mjini penyewe eneo la Magomeni barabara ile haijaanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri kwasababu nilishapiga picha wakati fulani nikamtumia Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Manaibu wake wote wawili kwamba barabara hii tunataka ikamiliike kwasababu Mheshimiwa Rais alisisitiza sana ndani ya miezi 18 iweze kukamilika lakini haijakamiliika. Ukiwaliza wale wakandarasi wanakuambia *certificate* tayari wamesha-*raise* lakini Wizara haijawapa fedha, kwa hiyo, niombe kwamba Wizara itoe fedha kwa wakati ili hawa wakandarasi waweze kumaliza barabara hii. Ni miaka mitatu hivi sasa wakati ilisemwa ni miezi 18 lakini huu ni mwaka wa tatu barabara ya kilometra 50 haijakamiliika kutoka Mtwara Mjini kwenda Mnivata. Tunaomba mwaka huu Mheshimiwa Waziri utekeleze

barabara hii yule mkandarasi apewe fedha zake barabara hii iweze kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nilikuwa naomba kuzungumza, tumeona na wale wote ambao wanatumia barabara ya Kusini kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam inaitwa barabara ya Kibiti – Lindi. Hivi sasa ile barabara inatumia malori mengi ya kusafirisha *cement* kutoka pale Kiwanda cha Dangote Mtwara kwenda Dar es Salaam ambako kuna soko kuu. Barabara imeharibika sana na inawekwa viraka viraka lakini viraka vyenyewe vinawekwa baadhi ya maeneo tu lakini barabara ni mbovu, imekatika sana na hasa ukizingatia hili janga la mvua la mwaka huu imebomoa maeneo mengi zaidi kuliko hata vile ilivyokuwa mwaka jana. Kwa hiyo, niombe *TANROADS* Wizara iipe fedha ifanye marekebisho ya haraka barabara hii ya Kibiti – Lindi kwasababu ndiyo barabara ambayo tunaitumi sisi wananchi wa Kusini, mikoa yote ya Kusini kusafiri kwa mabasi lakini pia kusafirisha mizigo kwenda kwenye soko kuu Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine sambamba na hili niliwahi kusema hapa kwamba kutoka Mtwara mpaka kule Tanga mpaka Zanzibar tuna Bahari hii ya Hindi na Serikali imekuwa imejikita sana kutengeneza meli kule Kanda ya Ziwa, kwenye Maziwa Makuu kule, wanajenga meli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana nilisema mwaka kwamba hizi meli zinazojengwa ni lazima Serikali iweke mkakati ili barabara ya Kibiti – Lindi isibomoke wanunue meli kwa ajili ya kusafirishia mizigo ya *cement* kutoka bandari ya Mtwara kwenda Dar es Salaam na kwenda Tanga na Zanzibar na kwingineko huko duniani. Tukifanya hivi Serikali...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana kengele imeshagonga.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana nakushukuru sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Peter Lijualikali atafuatiwa...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amina Mollel.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68, kwa kuwa ili kupambana na janga hili la ugonjwa wa Corona, ni janga ambalo lipo dunia nzima ni lazima sisi kama wabunge tuwepo na tuweze kupitisha bajeti ya miundombinu lakini pamoja na bajeti nyingine zilizopo na mwisho kupitisha bajeti kuu ya Serikali. Na ili bajeti hili ipitishwe ni lazima Wabunge wawepo Bungeni kutimiza jukumu ambalo ni la kikatiba na la kikanuni. Lakini pamoja na uzalendo uliopo wa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wakiwemo pia baadhi ya Wabunge ambaao ni Wabunge kutoka Vyama vyta Upinzani yupo Mtanzania mmoja ambaye leo hii katika mitandao mbalimbali ya kijamii amewatuhumu vikali Waheshimiwa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi kwamba ni wezi na wanaiba fedha za umma ambazo ni fedha za Serikali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe tu kwamba tupo hapa kihalali, tupo hapa tukitimiza kanuni lakini pia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Bunge hili la bajeti. Ninaomba mwongozo wako kwasababu ameenda mbali zaidi pamoja na kumkashfu Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais kipenzi ambaye pamoja na janga hili bado amewatia moyo Watanzania na kuonesha dhamira ya dhati kabisa katika kulishughulikia janga hili la ugonjwa wa Corona. Kwa mwongozo wako ninaomba; je, ni halali kwa Mtanzania kulituhumu Bunge lako tukufu kwa kauli ambazo

zinalifedhehesha Bunge lako? Naomba mwongozo wako tafadhali.

**NAIBU SPIKA:** Mwongozo utajibiwa baadae, Mheshimiwa Peter Lijualikali atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha ajiandae.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii, kule Jimboni kwangu kuna ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kidatu japokuwa ujenzi unasuasua lakini Serikali ilitakiwa kutoa asilimia 10 ya fedha zote za mradi kwa ajili ya fidia. Lakini hivi ninavyokuambia jambo hili limekuwa ni la manung’ uniko sana kwa wananchi wa Kilombero. Mtu ana nyumba ina vyumba viwili, vyumba vitatu wengine vinne anapewa fidia milioni tatu, milioni tano, milioni sita, mmoja amepewa fidia shillingi 275,000. Kwa kweli nimuombe Mheshimiwa Waziri aangalie utaratibu wa fidia ziliviyotoka kwa watu wa Kilombero. Ukienda pale Muaya, ukienda Kidatu, ukienda Mkula kwa kweli kuna manung’ uniko makubwa sana. Mtu kama Daudi Kitalima ana nyumba ya vyumba vinne anapewa fidia milioni sita, kweli! Mtu ana nyumba ya vyumba saba anapewa fidia milioni nane kwa hiyo Mheshimiwa Waziri nikuombe hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TARURA*, hivi *TARURA* iliundwa ili isaidie kitu gani? Msingi ulikuwa ni nini? Ni kwamba kulikuwa na ombwe ndiyo maana ikaumbwa au ilikuwa ni kit utu kimekaa ilimradi kiwepo. Ukienda pale Ifakara barabara zimekuwa, ukienda kwa Mkurugenzi anakuambia hizi ni za dharura, ukienda *TARURA* wanakuambia hakuna fedha. Sasa *TARURA* iliundwa ili iweje Mheshimiwa Waziri kama fedha hampeleki? Waheshimiwa Wabunge wote hapa wanalamika fedha *TARURA* hawapewi barabara zinakufa, Mkurugenzi akiulizwa anasema hazimhusu, ni bora basi zikibaki kwa Mkurugenzi ili aweze kuzishughulikia. Kwa hiyo nikuombe sana hili mliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwalimu Nyerere amewahi kuongea maneno akasema” Ukweli una tabia ya kulipa kisasi”

ukidharau ukweli utakulipiza kisasi tu, na kwa maana hiyo unaangalia hili jambo la Corona na mambo ambayo tunayafanya kuna kisasi kitakuja kulipwa. Nitoe pole kwa waislamu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na msiba hapo Dar es Salaam muumini amefariki Sheikh akasema amepewa maagizo na Serikali Msikiti ufungwe kwasababu ya hiyo shida na tamko likatoka. Baadae yanakuja matamko kwamba watu waendelee kusali (*business as usual*) sasa hii maana yake ni nini? Tunakwenda kuua Taifa hili, *Corona is really*. Kama mambo ya kitaalamu yanatamkwa kitaalamu, Mheshimiwa Waziri anasimamia mambo ya kitaalamu, wataalamu wanafanya mambo ya kitaalamu halafu Mheshimiwa Rais ni Rais wetu anakuja na hoja za kisiasa. Hivi kuna haja gani ya jambo ambalo wataalamu wameshaamua kitaalamu na dunia inakubali *social distance*. Mtu anakufa kwenye msikiti Sheikh Mkoa anasema jamani hapo msikiti ufungwe kwa muda mpaka hili jambo lifanyiwe kazi yanakuja matamko mengine watu wasali tu, maana yake nini? *We are killing the nation*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe na niombe Serikali...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa!

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tunafanya mchezo kwenye Corona newaambia Watanzania ipo siku watakuja kuandamana hapa nchini. Hawatokubali mtu anakufa anaangaliwa anakufa, hawatokubali, kama tunachezea Corona, siasa kwenye Corona hii ambayo inaua, wenzetu pale Brazil walifanya utani kama huu leo wanazika maelfu kwa maelfu Rais wao alifanya utani. Nchi inasema ina Corona yeye anasema haya ni mafua tu *the same applied* hii ya kwetu, mtu anakufa msikitini BAKWATA inasema jamani huyu mtu amekufa mnaambiwa nyie mkasali tu.

Mheshimiwa Lijualikali naamini kwenye hiyo *tablet* yako unazo kanuni. kanuni ya 64 inakuongoza namna ya michango yako inatakiwa kuwa. Nilikuwa nakusikiliza kwa makini nione unaelekeea wapi. Unajaribu kuzungumza kana kwamba yule Rais uliyemtaja sijui wa wapi alifanya mzaha. Kwa hiyo, unajaribu kuona kwamba Rais pia hapa nchini amefanya mzaha; hilo halikubaliki kwa kanuni zetu. Halikubaliki. Kama una hoja yako unayotaka kuizungumza, iseme hoja yako maliza, uzingatie matakwa ya Kanuni ya 64 na makatazo yake. (*Makofî*)

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeelewa hiyo Kanuni mkumbuke hapa tunazungumzia vifo vya Watanzania, maisha ya watu. Ninachosema ni kwamba hili jambo liko wazi, Mheshimiwa Waziri alitoa maagizo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lijualikali ukisema liko wazi, unaweza wewe ukathibitisha kwamba ule Msikiti kuna mgonjwa alifariki kule kwenye Msikiti na alikufa na *Corona*. Wewe unaweza kuthibitisha?

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Shehe wa Mkoa wa Dar es Salaam alisema na wote timeshikia kwamba hapa tuna tatizo, Msikiti tufunge. Serikali imemwambia kwamba Msikiti ufungwe kwa sababu ya *issue* ya *Corona* pale Msikitini. *Clip* zipo, Shehe yupo na kila mtu kasikia.

**NAIBU SPIKA:** Sawa. Sasa ngoja Mheshimiwa Lijualikali, usiliingize Bunge kwenye jambo ambalo haliko hapa kwenye hoja zetu. Ukiniletea hiyo *clip* ya huyo Shehe; mimi sijaiona; na kwa kuwa hajiazungumzwa hapa ndani sina uwezo wa kusema niletee hiyo *clip* nione ili nikuruhusu uendelee na hicho unachofanya. Haya Shehe naye akija akasema hakusema, nawe umeshamaliza mchango wako humu ndani, hilo nalo siwezi kuliruhusu. Kwa sababu sina hiyo taarifa, wala sijaona hiyo *clip*, kama umeionna ni wewe labda na Wabunge wengine, mimi sijaiona.

Kwa hiyo, siwezi kuingiza huo mjadala wa Rais na maagizo aliyosema na wewe kuashiria kwamba Shehe alichosema ndicho kilikuwa sahihi, sijamsikia Shehe, nimemsikia Mheshimiwa Rais akitoa maagizo, akitoa ushauri, akitoa maelekezo. Tafadhali dadika zako zimebaki chache sana, changia ulichokuwa umepanga kuchangia.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, mzee wangu baba Paroko hapa Mheshimiwa Mbunge wa Rombo alisema jambo hapa kwamba watu wemefariki, Wabunge wenzetu, lakini tunafanya *ku-guess*. Watu wanafariki tunashindwa *ku-disclose the reason behind*. Kwa nini tunaficha ukweli? Tunamwoga nani? Kwa faida ya nani?

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele yako imegonga Mheshimiwa.

**MHE. PETER A. P. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaua Taifa.

**NAIBU SPIKA:** Kengele imegonga.

Tunaendelea na kumalizia Wabunge waliosalia. Mheshimiwa Mary Pius Chatanda nilikuwa nimekutaja, Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatia, halafu Mheshimiwa Desderius John Mipata.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika hii Wizara ya Ujenzi. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Manaibu Waziri na Watendaji Wakuu wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya hasa katika kipindi hiki ambacho wanapita katika majaribu makubwa ya mvua kubwa ambazo zinaharibu madaraja, barabara na kila kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii tena ya kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wangu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumpongeza kwa hotuba yake

ya jana. Hotuba yake imetulia na Mataifa mengine yameanza kusema kwamba wanahitaji hotuba hiyo iweze kutafsiriwa kwa lugha za kwao, tumesoma kwenye mitandao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme neno moja hapa kupitia kitabu cha dini anasema Yohana Mstari wa 14:1 inasema: " msifadhaike moyoni mwenu, mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Amani nawaachieni, amani yangu nawapa, niwapavyo mimi sivyo ulimwengu utoavyo. Msifadhaike moyoni mwenu wala msiwe na woga. Jipeni moyo, mimi nimeushinda ulimwengu."

Mheshimiwa Naibu Spika na Ndugu zangu Watanzania naomba niwahakikishie kwamba Mwenyezi Mungu yupo pamoja nasi katika janga hili, tusiendelee kubabaishwa na watu wachache akiwemo huyu mwingine ameingia humu ndani anaanza kueleza mambo ya Msikitini, mambo ya wapi, lazima tuendelee kumwomba Mwenyezi Mungu. Kama ye ye hamwamini Mungu, aache ye ye abaki na ushetani, sisi wengine tunaomwamini Mungu kwamba ndiye anayeweza kutusaidia kuondoa balaa hili, tutaendelea kumwomba Mungu na tutaendelea kuwaomba Viongozi wa Dini waendelee kutuombea ili jambo hili liweze kuondoka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwamba kwangu kule Korogwe barabara zangu nyingi ni za *TARURA* na kwa bahati nzuri zimeanza kuwekewea lami, lakini maeneo yale ambayo hayajaanza kuwekewa lami, nazungumza kwa sababu Ujenzi na *TARURA* ni kitu kimoja. Nawaomba sasa kwamba zile barabara nyingine ambazo muda wake wa kuanza kuwekewa lami bado, tungepewa fedha ya kutosha kwa ajili ya kujenga mitaro au mifereji kwa kiwango cha mawe ili kuzua maji ambayo yanaharibu barabara ambazo zinajengwa kwa kiwango cha changarawe. Kwa kufanya hivyo, mtakuwa mmetusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukijenga ile mifereji, watakapokuja kuweka lami barabara zile zitakuwa zimekaa

vizuri. Naomba sana kwa sababu *TARURA* na Ujenzi wako pamoja, basi naomba jambo langu hili kwa Korogwe Mjini tunaomba tuwekewe fedha za kutosha katika kujenga mifereji kwa kiwango cha mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona kwenye *Vote Na.* 2005 zimetengwa kama shilingi milioni 840/= kwa ajili ya barabara inayokwenda Soni – Bumbuli – Dindira - Korogwe kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Hata mwaka 2019 niliona walikuwa wametenga fedha. Naendelea kuiomba Serikali, basi huu upembuzi yakinifu ukamilike ili barabara hii nayo iweze sasa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena kwa Korogwe yetu na Mkoa wa Tanga, barabara ambayo inatoka Old Korogwe kwa Mndolwa – Kerenge – Magoma – Mashewa – Daruni iingizwe kwenye mpango wa upembuzi yakinifu. Barabara hii ni muhimu kiuchumi. Ikifanyiwa kazi kwa kuwekwa kwa kiwango cha lami tutawainua wananchi wa maeneo yale ya Tarafa ya Magoma kwamba nao sasa waingie kuwa na uchumi mifukoni mwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara yoyote ikishakuwa ya lami, tayari wananchi wanainuka kiuchumi. Barabara hii ina mazao ambayo yanalinwa kwenye maeneo hayo. Wananchi wakiwa na miundombinu mizuri, itawasaidia kuuza mazao yao kwenye masoko na kuwawezesha na wenyewe kuinuka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii barabara naona nimeizungumza sasa kwa mara ya pili. Mwaka 2019 nilizungumza na mwaka huu naizungumza. Nomba sana iinginzwe kwenye kiwango cha lami; kwa mfano kule Kalalani kuna mgodi kule wa dhahabu, katika barabara hii ninayoizungumza. Vilevile nilizungumza barabara ya kutoka Old Korogwe - Lwengela Darajani kutokea pale Maguzoni.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Nashukuru sana. Naomba nayo iingizwe kwenye upembuzi yakinifu. Ahsante sana. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha atafuatiwa na Mheshimiwa Desderius John Mipata na Mheshimiwa Bhagwanji Maganlan Meisuria, ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kabisa nimshukuru Mungu kwa kutupa Rais mwenye maono na mafunuo ya Kimungu. Ni jana tu Rais ametoka kuhutubia Taifa kwa kile ambacho Mungu alimfunulia kwamba wafanye moja, mbili, tatu, kuangalia kwamba vile vipimo vilivyoko maabara kama viko sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninavyoongea hapa kuna taarifa ya habari kutoka India inayosema: "*India stops using Chinese test kits which are faulty;*" na anaendelea anasema: "*after Spain taken Netherlands several Counters have received faulty Chinese supplies.*" (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni Taifa. Siyo kila kitu tunachokipokea tupokee tu, lazima tujiridhishe kama kiko sahihi. Kwa hiyo, naomba nimpongeze Mheshimiwa, tuna Rais mzuri. Siyo kwamba wewe kila kitu unapewa unakubali tu!

Mheshimiwa Naibu Spika, tupo kwenye kipindi ambacho tunafahamu Mataifa haya makubwa yanapigana kiuchumi, kuna vita ya kiuchumi inayoendelea duniani ambayo pengine inaweza ikasababisha hata haya *Corona* tunayopata pengine ni vita ya uchumi, *you never know*. Kwa hiyo, lazima tuwe makini kama Taifa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi naomba unisikilize. Kwanza naomba nikishukuru sana chama changu; Chama cha Mapinduzi. Naomba niishukuru CCM sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Tarime - Mgumu kulikuwa na Daraja la Mto Mara ambalo juzi limeondoshwa. Cha kushangaza CCM kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, ilitujengea daraja ambalo mwaka 2019 limekamilika. Mheshimiwa Waziri inabidi mje kuzindua daraja lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu alisema atakuja, sijui atakuja lini kuzindua zile daraja ambalo lipo kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi. Wananchi wa Serengeti wanafurahia, kama lile daraja lisingekuwepo, leo wangevuka vipi kwenda Tarime? Maana lile la zamani limezolewa na maji. Kwa hiyo, wanaishukuru sana CCM, nami naomba niishukuru CCM kwa kuiweka barabara ya Tarime - Mgumu kwenye llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nawaambia wananchi wa Serengeti, barabara ya Tarime - Mgumu tayari imeingia kwenye Mpango wa Serikali, kinachosubiriwa ni Serikali ipate fedha barabara ile iweze kutengenezwa kwa kiwango cha lami. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niishukuru Serikali kwa kutenga fedha na kutangaza *tenderya* barabara kuanzia Sanzate kuja Nata, kilometra 40. *Tenderinatangazwa* wakati wowote, Mkandarasi atapatikana na kazi itaanza. Naomba nikishukuru Chama cha Mapinduzi kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri; barabara hii ya kuunganisha Mkoa wa Mara na Mkoa wa Arusha ni barabara ambayo ni kiu na hitaji kubwa la watu wa Mkoa wa Mara. Juzi limekatika daraja la kuunganisha Kijiji cha Robanda na Foti Ikoma naomba niishukuru Serikali na *TANROAD* kwa kazi kubwa ambayo imefanya kurejesha mawasiliano. Ni barabara inayotuunganisha na Mkoa wa Arusha. Baada ya lile daraja kukatika hakuna mtu alikuwa anaenda Arusha, labda uzunguke Mwanza ndiyo uende Arusha. Sisi na Arusha ni majirani, tumepakana. Kutoka Serengeti kwenda Arusha ni

kilometra chache tu, ukitoka kwa mfano mpakani mwa Tabora (b), unaingia pale ni kama kilometra 51, lakini inakulazimu uzunguke Mwanza *almost* karibia kilometra 600 uende Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaomba sana Wizara, hii barabara ikamilike mapema, ni barabara ambayo ina siasa nyingi, ni barabara ambayo alliasisi Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, ikaja Awamu ya Pili, Awamu ya Tatu, Awamu ya Nne, Awamu ya Tano; ninaamini kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hii barabara itakamilika kabla hajaondoka madarakani.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye mfuko wa barabara, huu mgawanyo ambao nimeona kuna *purpose* ambayo imetengenezwa kwa ripoti ambayo pengine Tume mliounda naomba chonde chonde msigawe fedha hizi. Tunaomba tutafute fedha nyingine kwa ajili ya kuiwezesha TARURA. Ukitoa fedha hizi kutoka *TANROAD* kwamba ukaigawie TARURA, *TANROAD* ambayo inamiliki barabara ambayo *heavy tracks* zinapita pale, itakuwa ni shida kweli kweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Desderius John Mipata, atafuatiwa na Mheshimiwa, Bhagwanji Maganlal Meisuria.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nachukua nafasi hii kumshuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima. Pia nashukuru sana Bunge lako Tukufu mwaka 2018 walinipeleka matibabu India na sasa niko vizuri. Nilipata kibali na Mheshimiwa Rais lazima nimshukuru sana, niko imara na

ninachapa kazi. Nawaombea Mwenyezi Mungu awajalie sana katika majukumu yenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie kidogo kuhusu *Corona*. Mwelekeo wa kupambana na *Corona* hauwezi kufanana na nchi zote. Ni lazima nchi au jamii fulani iangalie kulingana na mazingira yake ya kiuchumi, kiutamaddni, na kijamii. Bila kuangalia hivyo, uki-*impose* jambo ambalo hawajalizoea, unaweza ukaanzisha *Corona* nyine. Kwa hiyo, hatua zinazochukuliwa na Serikali ni za kuungwa mkono na kuwa na nidhamu katika ufuutiliaji. Bila hivyo tutaweza kugombana bila sababu. Naomba tuwe wamoja zaidi katika vita hii dhidi ya *Corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua zinazochukuliwa na Mheshimiwa Rais na wataalam wetu ni muhimu na lazima tuwe makini kuzifuatilia na tuwe na nidhamu kama vile mtu anayeendesha gari kutoka Arusha kwenda Kilimanjaro kwenye *Traffic* nyangi; ukisinzia kidogo unagongwa. Tukiwa na nidhamu ya namna hiyo, Mungu atatuvusha na huku tukiwa tunaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, nimeona utendaji wa Serikali ya Awamu ya Tano umeleta mabadiliko makubwa katika nyanja mbalimbali. Mimi natokea kwenye Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*P/C*). Tumeangalia miundombinu mbalimbali iliyojengwa, tumeona bandari, tumeanza kuona ujenzi wa reli, barabara nyangi ambazo zimejengwa; ni hali ya tofauti kabisa katika kipindi ambacho tumeona hapo nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, utendaji uliotokea sasa hivi unaigeuza Tanzania kuwa ni Tanzania yenye matumaini ya kiuchumi kwa baadaye kuliko wakati wowote na ndiyo maana inatupa kiburi kuzungumza sasa kusifia utendaji wa Serikali. Zamani kipindi kama hiki ilikuwa ili wananchi wakusikie vizuri uiponde Serikali kwa sababu mambo mabaya ni mengi zaidi. Sasa ukienda Afya unaona mazuri, ukienda kwenye umeme unaona mazuri; lazima tuipongeze Serikali, inafanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mkoa wetu wa Rukwa kwenye Bodi ya Barabara tumekuja na ombi kwamba Serikali iflikirie kutujengea reli kutoka Tunduma kuja *Kasanga Port*. Eneo hili ni muhimu, litaweza kutusaidia kuchukua mizigo inayozalishwa kwenye ukanda huu wa Nyanda za Juu Kusini, lakini kuna kiwanda cha *cement* pale Mbeya. *Cement* inahitajika sana Congo na mahindi yanahitajika sana Congo. Ili uweze kupidisha, utatumia barabara hizi. Utbaumiza barabara zetu. Tukitaka kufanya biashara na Congo, unapitisha Zambia. Sasa Zambia wanatuzuia, wanaweka kodi kwenye mahindi, tunashindwa kuuza. Mwaka 2018 tulishindwa bila sababu. Kwa hiyo, mtusaidie ili iwezekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile meli tumekuwa tukiahidiwa kila wakati katika bajeti mbili mfululizo. Wamesema wenzangu, imefika wakati na Mheshimiwa Waziri wewe umetokea katika maeneo haya, unajua kilio cha meli katika maeneo yetu. Nakuomba pambana sasa, umeweka safari hii, tuione meli mpya ikijengwa na hizi za zamani zikiwa zinakarabatiwa. Wananchi wanahangaika sana katika suala la usafiri wa mwambao mwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie barabara za kwangu. Katika Bodi ya Barabara tulipitisha barabara ya Karakara ya kilometra 67 ipate hadhi iwe ya Mkoa. Vilevile barabara ya Kitosi - Wabembe, tumeshaleta kwako mara nydingi na mtaalam mmoja wa kwako alikuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba uzingatie hiyo. Barabara ya Milundikwa *junction* Kisula haipitiki, nimezungumza hata safari iliopita. Barabara ya Katongolo na Masi sasa hivi huwezi kufika, barabara ya Kitosi - Wapembe huwezi kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hiyo ya Kitosi - Wapembe Mheshimiwa Rais anajua na anaipenda. Nilienda kumlilia akiwa Waziri kama wewe, akanipa shilingi milioni 500 ndiyo ikawezesha mabasi kufika Wapembe. Leo hii barabara inaanza kufa, haipati hela kutoka Serikalini. Kwa hiyo, naomba tupate fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa daraja la Kizumbi, nimelizungumza mara kwa mara hapa. Nimekwendwa kwa Mtendaji Mkuu, nimekuja hata kwako Mheshimiwa Waziri; Kizumbi huwezi kwenda ukafika, barabara imefungwa. Sasa hatuwezi kwenda katika utaratibu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya simu katika Kijiji cha Msamba, Kijiji cha Mkilinga, Kijiji cha Izinga, Kijiji cha Kata tunapata shida katika mawasiliano mwambao mwa Ziwa Tanganyika tuna vijiji karibu vitatu, vinne, vitano, Kata ya Kala, Wampembe, Ninde pamoja na Kasapa. Tunaomba katika maeneo hayo watusaidie tuweze kupata...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Bagwanji Maganlal Meisuria, halafu Wabunge watakaofuatia baada ya hapo watachangia dakika tatu tatu; nao ni Mheshimiwa Charles John Mwijage, Mheshimiwa Flatei Massay tutamalizia na Mheshimiwa Charles Kitwanga.

Mheshimiwa Bagwanji Maganlal Meisuria.

**MHE. BAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nampongeza sana Mheshimiwa Spika katika miaka mitano ya Bunge, mmefanya kazi nzuri sana katika awamu yako katika Bunge. Namshukuru Mwenyezi Mungu na nawaombea mrudi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nataka nimpongeze Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli; Makamu wa Rais, Mama Samia Suluhu; Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote. Wamefanya kazi nzuri kabisa katika awamu hii ya Bunge na *Insha Allah* Mwenyezi Mungu atampa nguvu na uwezo na watarudi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, isitoshe Mheshimiwa Rais wa Zanzibar Ali Mohamed Shein pamoja na Makamu wa Pili wa Rais Balozi Seif Iddi anafanya kazi nzuri sana katika Zanzibar na sie tunashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa si fadhila Jimboni kwangu Chwaka kama sitawashukuru wapigakura wangu wote walionichagua kwa haki, hali na mali na roho moja na imani moja, pamoja na Wawakilishi wangu Madiwani wangu, wote pamoja wamenipenda tunafanya kazi pamoja. Nawashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme mambo mawili tu; jambo la kwanza ni la *corona*. *Corona* Mungu ameleta lakini *insha Allah* Mwenyezi Mungu ataiondoa kwa dunia nzima. Hapa Tanzania mimi nilikuwepo Dar es Salaam Jumuiya yetu ya *Ghayet Parguayyaani* Shekhe wetu alikuwa anasoma dua pamoja na Zanzibar Shekhe wetu alisoma dua, tumeondosha *corona* yote na *insha Allah* itaondoka. Hapa Kisharubaya amesoma Dua Dar Es Salaam ya *Ghayet Parguay* itaondoka *corona* Tanzania nzima pamoja na duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Zanzibar pia sisi Wahindi Baniani pia tunesoma *Arriasmaji*, tunesoma dua ya Mwenyezi Mungu ya Dini ya Baniani itaondoka *Sures* pamoja na *Sharif* wetu ameondosha hiyo *corona*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumza mambo ya Kamati yangu. Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Magufuli amefanya mambo makubwa sana katika Kamati hiyo ya Miundombinu. Mheshimiwa Rais John Joseph Magufuli amesimamia pamoja na Waziri, Naibu Waziri wote, wamesimamia barabara zote kutoka Dar es Salaam, Ubungo kuja mpaka Dodoma, Ubungo kuja mpaka Morogoro, wamesimamia barabara inapanuka na pia barabara zingine za nje za kutoka Dodoma kwenda mbele imesimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, madaraja yote vilevile wamesimamia; madaraja yalikuwa yamebomoka, Tanga

huko limebomoka. Hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam daraja lilibomoka. Tumeshuhudia, tumeona limesimamiwa na Rais wetu na hiyo Kamati yetu ya Miundombinu na kuwa itakuwa sisi tunakwenda mbele tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili *Standard Gauge*, sisi Kamati yetu nampongeza Mwenyekiti wetu na Kamati yangu yote, tumekwenda katika ziara tumesimamia na inafanyiwa kazi. Bandari ya Dar es Salaam, *Standard Gauge* ya Reli pamoja na uwanja wa ndege tumeshuhudia inafanyiwa kazi na inaingiza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niseme jambo moja, hii mitandao ya simu kwenda mpaka huko mipakani mpaka Zanzibar yote mpaka Tanzania, wanajitahidi kupata mitandao ya simu lakini wanaendelea *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, Mheshimiwa Rais wangu Dkt. John Pombe Magufuli, *insha Allah* na mie Baniani peke yangu naomba dua Kibaniiani pamoja na dini zote, atarudi katika CCM na mimi atanirudisha ndani ya Bunge hili. CCM niwe hapa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, tutamalizia na Mheshimiwa Charles Kitwanga.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kupata nafasi hii. Kwa kuwa dakika zangu ni chache, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kazi anazozifanya katika Jimbo langu, lakini pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu sana kwa sababu Jimboni kwangu juzi tumepeata gari la Wagonjwa ambalo tulilhitaji sana. Namshukuru sana limefika na litasaidia wagonjwa kule jimboni na hakika katika Janga hili la *corona* basi Mungu ataendelea kutuepusha na janga hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimeona hotuba hapa na nimeisoma vizuri, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Kamwele ndugu yangu hongera sana. Ndugu yangu Mheshimiwa Nditiye nimpongeze sana. Barabara yetu ile ya Karatu – Mbulu – Hydom Sibiti ipo katika bajeti ya mwaka huu unaopita. Nimwombe Mheshimiwa Waziri mwaka unaendelea kuyoyoma, basi tuone basi tenda inatangazwa ili angalau barabara ile ya kutoka Hospitali ile ya Hydom kwenda Mbulu Mjini kuweza kujengwa kwa kiwangocha lami. Najua kwamba aliniambia mwaka hautaisha bila jambo lolote kutokea pale, basi nimwombe kwa ajili ya uchumi wa wananchi wa Mbulu maeneo yale ya Mjini na anafahamu Karatu na barabara hii inaunganisha Mkoa ule wa Arusha na Manyara, Manyara na Singida, Singida kwenda Simiyu. Nimwombe Mheshimiwa Waziri kwa kuwa ameshaitenga na ipo inaonekana basi nimwombe mwaka huu usipite, jambo lolote litokee katika barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna minara michache ambayo tuliona kwenye bajeti, Mheshimiwa Naibu Waziri Nditiye anajua. Naomba basi ile minara iweze kumalizika kujengwa, najua iko kwenye hatua mbalimbali, kwa hiyo, ikimalizika kujengwa nafikiri ile ahadi ambayo tumeitoa tutakuwa tumekamilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu muda wangu ni mchache, nimshukuru sana na kumwombea Rais wetu ili walau aweze kupata afya njema. Nliombee Tanzania na nchi yetu hii kwa ujumla, Mungu atuepushe na ugonjwa huu wa *corona* na niwaombe Watanzania tuombe ili mambo haya ya ugonjwa yaishe, lakini pia tumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na mchango wangu unaishia hapo. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Charles Kitwangwa atafuatiwa na Mheshimiwa Atashasta Nditiye.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza nianze kwa kusema naunga mkono hoja, niipongeze sana Serikali kwenye eneo hili wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dakika zangu hizi tatu, nitoe tu zile sifa maana yake kama ningekuwa na dakika kumi, dakika sita ningezitumia kutoa pongezi, lakini kwa sababu ya huu muda mfupi nitoe tu ushauri katika mambo matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, Mheshimiwa Mfugale na *TANROADS*, wewe unazeeka, lakini tunahitaji sasa busara zako zieneee sehemu nyngi. *TANROADS* wanafanya vizuri, waweke utaratibu wa kuhakikisha na maeneo mengine kama *TAAA* wanakuwa na uwezo na ujuzi kama ilivyo *TANROADS* ili *TANROADS* wasisambae kila mahali mwishowe wakawa wamezidiwa na mzigo wakashindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niombe Wizara hii pale Bandarini, Bandari wa-*concentrate* na kazi yao ya msingi. Nashukuru sana sasa hivi wameanza kuifanikisha ile Bandari Kavu ya Kwara lakini wafanye, wahakikishe kwamba ile gati *thirteen* na *fourteen* zinasimikwa maana utafiti ninaouona na nilioufanya kidogo sasa mizigo kutoka Bandari yetu inaanza kuwa michache kuliko wale *TICS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilikuwa na mzigo, unakuja mzigo wangu ulishushiwa *TICS*, nashukuru bandari waliweza kuutoa *TICS* nikalipia *TPA*. *TICS* wazidi kuwa na asilimia chache bandari yetu iweze kuwa na asilimia kubwa ya upakuaji wa makasha. Waache mambo ya mafuta wafanye wenyewe Wataalam wa mafuta, waache mambo mengine kama wanaweza kuwasaidia *financially*, watumie Serikali wawasaidie, lakini wa-*concentrate to the desk functions*, wahakikishe bandari kavu ya Fela inajengwa, Bandari kavu zote zinajengwa, washushe uwezo wa kushusha makasha, meli iingie isitumie zaidi ya siku tatu, siku saba ni nyngi sana na wana uwezo huo ila wamejitapanya sana.

Wanafanya mambo mengi ambayo mengine wawaachie wengine, Serikali ipo watafanya hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, mvua imenyesha kila mahali kuna matatizo, tunaiomba Serikali sasa, rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mpango atafute hela sehemu nyingine yoyote. Asinyofoe pesa ambapo zipo zimepangwa kupelekwa kwenye barabara, atafutea pengine, ana uwezo, atatufanya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge hasa katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Covid-19.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya barabara, reli, bandari, mtandao wa mawasiliano na ufujuji wa Shirika la Ndege ATCL. Naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR pamoja na uboreshaji wa bandari ambao

utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. *SGR*na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika biashara ya usafirishaji wa ndani na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki tunapopambana na janga la Corona virus (Covid-19), tumejifunza umuhimu wa kuwepo kwa mikakati mbadala kama vile kufanya kazi kwa kutumia TEHAMA. Pia napongeza mkakati wa Shirika la Ndege kuanza kutumia ndege zake kusafirisha mizigo, na itawezesha usafirishaji wa mazao yetu ya kilimo kufikia masoko kirahisi na hapo hapo uhakika wa mapato kwa Shirika la Ndege hasa kipindi hiki kukiwa na upungufu wa abiria.

Napendekeza kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea hata kwa kutafuta vyanzo mbadala vya fedha kugharamia ujenzi huo kwa vile kutakuwa na fursa kubwa za usafirishaji. Pamoja na ujenzi wa *SGR*, napendekeza kuendelea na kuboresha reli ya *TAZARA* na ujenzi wa Bandari Kavu Inyala ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki ili kupunguza ghamama za kusafirisha pembejeo na mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto za Covid-19, kuna fursa nyngi hasa mahitaji makubwa ya mazao ya kilimo na Serikali iweke msukumo zaidi kwenye kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na fursa za uzalishaji mkubwa kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, napendekeza muendelezo wa uboreshaji wa barabara za Tanzania kipande cha Igawa - Tunduma; barabara ya *bypass* ya Uyole - Songwe; barabara ya Mbalizi – Shigamba – Isongole kutokana na uzalishaji wa mazao ya kilimo; barabara ya Mbalizi – Galula – Makongosi kutokana na uzalishaji mkubwa wa mazao ya kilimo na madini; na pia barabara ya Isyonje – Kikondo – Makete ambayo ni muhimu sana katika kusafirisha mazao ya kilimo ikiwemo maua, parachichi na viazi kwa soko la nje. Uboreshaji wa barabara hizi pamoja na

uwanja wa ndege wa Songwe ni muhimu sana kwa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje na kwa kiasi kikubwa utaongeza mapato ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanazozifanya katika Wizara zao. Hii ni Wizara mojawapo ambayo imetekeleza llani ya Uchaguzi ya CCM kwa kiasi kikubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya mvua nydingi zilizonyesha mwaka huu barabara nydingi zimeharibika na madaraja yameondoka. Mkoani Kagera barabara nydingi zimeharibika na hasa barabara inayoanzia Katerero kwenda Kanazi, Ibwera, Katoro kuzunguka hadi Ruzinga na ile ya Kemondo, Kanazi, Ibwera, Rubale, Ruhunga zimeharibika sana. Wananchi wanapata shida na kwингine wanatembea kwa mitumbwi. Barabara hizi zina umuhimu mkubwa kiuchumi. Naomba zitengewe fedha ili barabara hizi zitekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Kagera tunapata shida sana ya usafirishaji wa mizigo, biashara nydingi zimefungwa, vijana wanakosa ajira sababu ya ukosefu wa usafiri wa kuaminika wa kutoka Mwanza kwenda Bukoba. MV Victoria ilipelekwa kukarabatiwa je, itakamilika lini? Tunajengewa meli mpya, wananchi wanaisubiri kwa hamu, je, ni lini itakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, wanafunzi wamefunga shule na vyuo, wako majumbani kwa sababu ya ugonjwa wa Corona. Je, Mkonga wa Taifa unatusaidiaje ili wanafunzi waweze kutumia *internet* wapambane na masomo kwa bei nafuu? Kuna maeneo ambapo hakuna mtandao, je, mnasaidiaje ili kila mwafunzi hata katika maeneo haya apate mtandao tena kwa bei nafuu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIA N. KANGOYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa nafasi ya kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayofanya ya kuhakikisha nchi inakuwa na mawasiliano kuititia barabara, mitandao ya simu na hata anga. Nakupongeza Waziri kwa kuonekana maeneo mbalimbali yaliyopata changamoto ya kuharibikiwa miundombinu. Tumeshuhudia Waziri ukikesha na wakandarasi kwa ajili ya kunusuru wananchi kutokupata changamoto ya usafiri. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Wizara ya Miundombinu na Uchukuzi imesheheni mawazo na mipango mizuri sana. Ila natamani Wizara ingejikita kwenye kuhakikisha kwamba miradi ilioanzishwa inakamilika, iwe ya barabara au mitandao ya simu. Na kwa maeneo ambayo barabara zimeharibika kwa kutokana na mvua za mwanzo wa mwaka ni vyema zikatengenezwa kwa mfuko wa dharura maana hali ni mbaya sana kwa wananchi wanaosafiri na hasa wanaotegemea biashara za kusafirisha mazao kutoka vijiji kwenda mijini. Bidhaa za shamba zimepanda bei si tu kwa mazao kuharibiwa na mafuriko bali kwa sababu ya taabu iliyopo katika kusafirisha mazao hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana hili suala la miundombinu kuharibika lifanyiwe kazi mapema kabla hali haijawa mbaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wake wote pamoja na watendaji wake wote kwa

kutayarisha na hatimaye kuweza kuwasilisha katika Bunge lako tukufu kwa ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo; kwanza ni usikivu hafifu katika maeneo ya visiwa vidogo. Naipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa kuendelea na juhudzi zake za kupeleka huduma za mawasiliano nchi nzima. Lakini bado kuna usikivu hafifu katika visiwa vidogo. Kwa hivyo naomba juhudzi za makusudi zichukuliwe ili kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii. Natoa pole kwa Spika, Wabunge wenzangu na familia za Wabunge wenzetu waliofariki siku chache zilizopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila shaka wapo watakaonishangaa kwa nini nipo hapa na sikutii agizo la karantini iliyoitishwa na wenzangu. Niseme tu kwamba mambo hayo nimekuwa nikiyasikia kwenye mitandao. Kwa kawaida yangu huwasiamini sana mambo yanayoandikwa katika mitandao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natambua kwamba kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 146(1) wajibu wa kwanza wa Mbunge yeoyote ni kuhudhuria Vikao vya Bunge na Kamati zake. Natambua pia kwamba Kanuni ya 146(4) na (5) zinaweka utaratibu wa namna Mbunge anavyotakiwa kufanya kama ana udhuru wa kutohudhuria Bunge au Kamati. Kwa kuwa hayo nayajua ndio maana unaniona hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo hoja hii ya karantini haikuanzia hapa Bungeni. Hivyo Bunge halina taarifa rasmi za Serikali kuhusu hali halisi ya ugojwa huu na wala hakuna taarifa rasmi kwamba wenzetu wamefariki kwa ugonjwa huo. Hii ina maana taarifa tulizonazo hata kama

zina harufu ya ukweli sio rasmi. Nashauri Bunge liitake Serikali kuleta Bungeni taarifa rasmi ili ijadiliwe na kutokana na mjadala huo hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo huu ni Mkutano wa mwisho wa Bunge la Kumi na Moja. Kwa mujibu wa sheria ni lazima Mheshimiwa Rais avunje Bunge hili. Napenda kushauri kwamba iwapo taarifa rasmi ya Serikali au Bunge itathibitisha hali kuwa mbaya kama inavyozungumzwa Mheshimiwa Rais anaombwa kwa mujibu wa Kanuni ya 30 kulivunja Bunge kabla ya muda wake badala ya kulikimbia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kwamba wajibu wa Mbunge ni kwa Taifa, kwa jimbo lake, kwa chama chake na kwa dhamira yake. Sasa tusichukue la mwisho tukalifanya kuwa la kwanza bila utafiti wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii naiomba Wizara ishauriane na TAMISEMI ili kuona namna ya kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili *TARURA* iweze kupata fedha maana barabara nydingi sana zinazosimamiwa na *TARURA* katika Halmashauri madaraja na vivuko vimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Rombo karibu barabara zote vijijini zimevunjika na hata barabara kuu inahitaji viraka vingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mamsera-Mahida na Lower Road Holili-Tarakea ambazo ziko chini ya *TANROADS* zilikuwa katika hali nzuri lakini mvua ambazo zilifuatana uli na masika zimeziathiri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara nydingine zote ambazo ni *TARURA* zimeharibika kwa kiwango kikubwa sana. *TARURA* kwa bajeti tunayopata haina uwezo hata kidogo wa kushughulikia barabara hizi.

Narudia ombi langu kwamba *TANROADS* na *TARURA* zishirikiane maana nchi yetu ni moja vyombo hivi visiwe sababu ya wananchi kukosa huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Disemba tumeshuhudia treni ya Moshi ikisafirisha abiria. Ingawa bado reli ni mbovu, vituo vimekuwa mapagale lakini kufika mara kadhaa kunaonesha dhamira nzuri ya Serikali kuishughulikia. Namkumbuka sana aliyezua Mbunge wa Moshi Marehemu Philemon Ndesamburo Kiwelu alivyokuwa akiipigania reli hii. Mungu amlaze mahali pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu reli ya katiba kazi inayofanyika ni nzuri, lakini Serikali ianzu mapema maandalizi ya namna ya kuiendesha kwa maana ya kuandaa wataalam na watumishi muhimu na utaratibu wa uendeshaji. Reli hizi zikikamilika barabara zetu zitadumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimelalamika sana hapa Bungeni kuhusu muingiliano wa mitandao iliyopo nchini mwetu na ile ya Kenya. Karibu nusu ya wakazi wa Jimbo la Rombo wanasumbuliwa na adha hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naionomba sasa Serikali itoe tamko ni lini kero hii itamalizika.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi nydingi kwa kazi kubwa inayofanywa na Wizara, naombia nichangie kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, vivuko vya Bugorola - Ukara. Nashukuru kwa hatua iliyofikiwa, niombe pesa zitolewe mapema ili kivuko hiki kikamilike na kuanza kutoa huduma maana wananchi wanateseka sana kwa sababu MV Sabasaba haifai na inafanya wananchi kukumbuka ajali ya MV Nyerere.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, barabara ya Lugezi – Masonga; ni muhimu sana kusaidia eneo la Bulamba – Murutunguru - Bugorola mahalo limekuwa linaharibika mara kwa mara, lijengwe kwa kiwango cha lami kama ambavyo nimeombia mara kwa mara ili eneo la Ukerewe Masako uzalishaji wa samaki ni mkubwa usiathirike. Eneo hili ni chini ya kilometra 10 tu, naombia Serikali itusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu usafiri wa Nansio-Irugwa; pamoja na kutengwa pesa za kununulia boti za uokoaji maeneo ya Irugwa, Gana na Nafuba, niombe kivuko cha MV Nyerere kitakapokarabatiwa kirudishwe Ukerewe ili kifanye kazi kwenye eneo la Gana na Irugwa. Bado Ukerewe yenye visiwa zaidi ya 30 ina uhitaji mkubwa wa vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ukarabati wa magati; kutokana na wingi wa mvua, maeneo ya maegesho ya vivuko yamefukikwa na maji kiasi cha kufanya magari yashindwe kuingia na kutoka vizuri. Maegesho Haya yakarabatiwe mapema ili kuhakikisha usalama wa watumiaji.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba nzuri aliyoitao kwa Watanzania kututoa woga wa ugonjwa wa Corona. Mchango wangu katika Wizara hii ni kupongeza sana Serikali kwa ujenzi wa barabara nyingi katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hali ni nzuri sana, kuititia mradi wa *DMDP*pamoja na *flyover*mbalimbali zilizopo ikiwemo na *interchanges* ya Ubungo. Ni maendeleo makubwa sana, naipongeza sana Serikali. Ushauri wangu naomba Serikali iungane na maoni ya Kamati ya kujenga *flyover* Magomeni kupunguza athari ya mafuriko ambayo inawakosesha usafiri wananchi na kuleta athari kubwa kwa wananchi wetu. Pia nashukuru sana Serikali sasa imeanza kujenga barabara ya Nzasa - Kilungule, mkandarasi yuko *site*, naomba Serikali ikamilishe taratibu za malipo ili waanze kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Manaibu wake kwa kazi nzuri sana mlizofanya. Mungu awabariki sana kwa kazi kubwa mliyowafanyia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mungu kwa kutujalia afya njema na tunaomba Mungu azidi kutulinda dhidi ya Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba Mungu awarehemu Wabunge wenzetu waliotangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina hoja zifuatazo; kwanza, tuta la reli Mto Ugala; mvua za mwaka 2019/2020 zimeharibu tuta hilo ambalo ndio njia pekee ya reli muhimu sana kwa uchumi wa nchi na ustawi wa Watanzania, hivyo tunaomba Serikali ifanye haraka matengenezo kwa kushirikiana na *TRC* ili huduma za usafiri zirudi kama awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ni muhimu sana kwa usafiri wa abiria na mizigo ya mahitaji pia mazao ya chakula na blashara kuanzia mwezi wa tano kazi ya ubebaji inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Daraja la Mto Ugala; barabara ya Mpanda-Kaliua-Kahama kilometra 428 ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi hivyo tunaomba Serikali itenye fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja ambalo upembuzi yakinifu umefanyika, nchi kuwa na njia mbadala ni muhimu sana kwa mustakabali wa maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, fidia za barabara ya Sitalike – Mpanda; wananchi wanaoishi katika maeneo hayo bado hawajalipwa fidia zao na imekuwa muda mrefu kitu ambacho kitaongeza ghamama kwa Serikali, hivyo madai hayo ya shilingi 3.6 bilioni wanauliza lini watalipwa fedha zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho natoa shukrani na tuendelee kuomba Mungu atuepushe na Covid-19.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema. Nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa

anazozifanya kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na Tanzania, Mungu amjalie afya njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa *Engineer Kamwelwe*, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, pia niwapongeze Naibu Mawaziri Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Nditiye kwa kazi kubwa wanazozifanya usiku na mchana. Mungu awabariki sana. Pia niwapongeze watendaji wote wa Wizara hii bila kuwasahau Katibu Mkuu wa Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru Serikali kwa kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kibena - Lupembe - Madeke - Morogoro kwa kiwango cha lami kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2016/2017 mpaka 2020/2021. Niombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kuitangaza hii barabara ili mkandarasi apatikane na aenze ujenzi kwa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Njombe na Morogoro na kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Eneo hili la Lupembe ni maarufu sana kwa ajili ya uzalishashaji wa mazao ya miti kwa ajili ya mbao, nguzo na mazao mengine yatokanayo na miti au misitu. Pia mazao ya biashara kama chai na kahawa yanazalishwa na mazao mengine ni nanasi na matunda, wakati wa msimu wa mvua mazao hayo huozea mashambani kutokana na ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Jimbo la Lupembe kuna shida kubwa ya mawasiliano, naipongeza sana Serikali kwa kutuletea mnara mmoja kati ya mitano tuliyoahidiwa, tumepata mnara eneo la Nyave. Tunaomba tupewe minara ya simu katika vijiji vya Madeke, Mfriga, Kanikelele, Ninga ili Jimbo zima liwe na mawasiliano. Hii itasaidia ukuaji wa shughuli za kibiashara katika Jimbo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la Jimbo Lupembe hususani kwenye barabara ya kutoka Kibena kuelekea Lupembe mpaka Mlimba hakuna Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano. Katika eneo hili kuna Hospitali ya Wilaya ambayo ipo umbali wa kilometra 50 kutoka barabara ya

Makambako-Songea ambako Mkonga wa Taifa umepita na Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe imehamia eneo la Kidegembye ambayo ipo umbali wa kilometra 40 kutoka Kibena.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo kutokuwa na Mkonga wa Mawasiliano katika eneo hili utendaji wa Halmashauri na Hospitali kwa kukosa mifumo ya mawasiliano utaaahirika sana. Hivyo naomba kujua Serikali imejipangaje kupeleka Mkonga wa Taifa wa Mawasiliano katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe au lini tutapata Mkonga huu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kupitia mchango wangu huu wa maandishi na kuuwasilisha Serikalini ili ufanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya awamu ya tano chini ya uongozi mahiri wa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wake ikiwa ni pamoja na huyu *Engineer Isack Kamwelwe* na timu yake ya Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zote za Wizara hii kwa kazi kubwa inayofanywa katika sekta zote tatu za ujenzi, uchukuzi na mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri Kamwelwe anihakikishie ujenzi kwa kiwango cha lami barabara za Ifakara hadi Lumecha kupitia Lupiro na Londo; Mtwarapachani hadi Nalasi kupitia Lusewa na Lingusenguse; Namtumbo hadi Likuyu kupitia Mtanya; na Mtanya hadi Naikesi kupitia Mgombasi na Nangero.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, tunaomba Kivuko cha Luhuhu kihamishiwe eneo la Kastam lililoko katika Kijiji cha Magazini ili turasimishe mawasiliano ya barabara kati ya Msumbiji (Wilaya ya Mabtagho) na Tanzania (Wilaya ya Namtumbo).

Mheshimiwa Naibu Spika, na mwisho nimuombe Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla ikamilishe upelekaji wa mawasiliano ya simu na *data* katika vijiji 11 vilivyobakia ili nao wapate kuwasiliana na wenzao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza *CEO* wa *UCSAF* aliyenionesha dhamira ya dhati ya kukamilisha mawasiliano kupitia Mfuko anaousimamia na watoa huduma hususan Ttcl, Halotel, Tigo na Vodacom. Naomba dhamira hiyo izae matunda katika muda mfupi ujao. Ni Vijiji vya Likusanguse, Mtelawamwahi, Matepwende, Mtakuja, Limamu, Nambecha, Nangero, Msindo, Mtakanini, Nambehe na Lumecha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100 na naomba kuwasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuitendea haki Wizara hii, yakiwemo ujenzi wa barabara kuunganisha Mkoa na Mkoa kama ilivyo sera ya Wizara ya Ujenzi, ujenzi wa reli, upanuzi wa bandari na mengine mengi mno ambayo yameipatia sifa kubwa mno ukilinganisha na kipindi kifupi toka Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano na Serikali kuchukua madaraka chini ya Chama pendwa cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara za kiuchumi nchini, ni vyema sasa Serikali ikaanza kushughulikia barabara za kiuchumi nchini kwa sababu wakati wa mvua hazipitiki kabisa na kufanya magari hasa magari makubwa kukwama wakati wote na ndiko ziliko malighafi kwa ajili ya viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni vyema ungefanyika upembuzi yakinifu wa barabara zote za kiuchumi nchini ili yapatiwe kipaumbele cha ujenzi kwa kiwango cha lami na ikiwezekana barabara zilizo chini ya *TARURA* zihamishiwe Wizara ya Ujenzi kutokana na wakala huyu kuwa na barabara nyingi za vijijini lakini fungu dogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Mkoa wa Iringa; tunaomba Serikali itoe kipaumbele kwa ujenzi wa barabara ya mchepuko ili kuchepusha magari makubwa kupita katikati ya mji kama ilivyo katika miji mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu umekuwa na hatari kubwa sana ya kuitisha magari makubwa katikati ya mji na kuhatarisha usalama wa wanachi na kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi kukosa *parking* wanapofuata mahitaji kwa biashara zilizo kando ya barabara kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ujenzi wa reli; niendelee kuipongeza Serikali yetu kwa ujenzi wa reli nchini, ujenzi huu utakapokamilika unaweza kuponya barabara zetu nchini. Magari makubwa ya mizigo yamekuwa ndio chanzo cha uharibifu mkubwa wa barabara zetu zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni vyema reli hii ikikamilika itungwe sheria kabisa ya katazo la upitishwaji wa magari makubwa ya mizigo katika barabara zetu zote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*); pongezi kubwa sana kwa wenzetu wa *UCSAF* na kwa kuwa kitengo hiki kinaongozwa na dada yetu Justina Mashiba. Ameitendea haki taasisi hii, kwa sababu kwanza, wameweza kupeleka mawasiliano kwenye kata 562 ambazo Watanzania wanaoishi vijijiini wemeweza kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, wameweza kuboresha usikivu wa redio katika Mikoa ya Kaskazini kwa kushirikiana na TBC na sasa kumekuwa na usikivu wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, wameweza kupeleka vifaa vya TEHAMA kwa shule za Summa za sekondari na za msingi ambazo kwa kweli karibu *computer* 1500 zimegawiwa nchini ukiwemo Mkoa wa Iringa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuziunganisha Hospitali nane za Mikoa na Hospitali za *MOI* na Muhimbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, wameweza kutoa mafunzo ya TEHAMA kwa walimu zaidi ya 3000 nchini, hongera sana. Hii imesaidia hata ufundishaji kwa watoto wetu kuitia mafunzo wakati wa hili janga la Corona.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu katika vyombo vyaya usafiri sio rafiki kwa watu wenye ulemavu. Ni lini Serikali italeta sheria ili kusababisha vyombo vyaya usafiri kuweka miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu?

Mheshimiwa Naibu Spika, walemavu wamekuwa wakipata mateso makubwa sana wanapotaka kupanda katika vyombo vyaya usafiri pamoja na baiskeli zao kutoka *point* moja kwenda *point*nyingine, katika madaladala na wengine wamekuwa wakidhahikiwa kwa maneno ya kejeli. Ombi langu, ni muhimu sasa wenzetu hawa changamoto hii langaliwe upya na mkakati uwepo wa kuhakikisha wanawekewa utaratibu mzuri ili wasiendelee kuteseka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bima za maisha kwa vyombo vyaya usafiri; wananchi wanapata mateso makubwa mno wanapopata ajali katika vyombo vyaya usafiri. Ningemba sasa chombo husika *TASAC* na *SUMATRA* vitoe elimu kwa abiria wao wakati wanakagua vyombo hivyo na abiria waelekezwe hatua za kuchukua mara ajali ikitokea. Watu wengi sana hawajui la kufanya ajali inapotokea na wengi wao wamepoteza maisha, viungo na mali zao. Nitaomba Waziri anapojobu basi atutolee ufanuzi wa jumbo hilo kwa sababu wamiliki wenye mabasi wamekuwa wakiwanyanya sana abiria waliopata ajali na hivyo kushindwa kujua nini wafanye.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hiyo.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Mwenyezi Mungu kunipatia uzima na afya

na kuweza kuchangia haya kwa maslahi ya wananchi wa Mkoa wa Rukwa, wengi wao ni akinamama na watoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera kwa Rais wetu jinsi anavyojitahidi kuwafikia wanyonge wake, pamoja na wasaidizi wake wa Wizara hii wanavyomuunga mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 14 kuhusu kuboresha uwanja wa ndege; tunashukuru Serikali kukubali kukarabati Uwanja wa Ndege Sumbawanga. Ombi langu kasi ya ukarabati hairidhishi hata kidogo, eneo limekuwa pori na kuwa hatarishi kwa watembua kwa miguu, watoka mjini kwenda Sumbawanga Asilia, Adeni, Sido na kadhalika. Pamoja na mikataba ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kusaini bado shughuli haijaanza. Tunaomba Wizara kufuatilia kwa karibu zaidi kwa huyo mfadhili shughuli iweze kuanza na kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Rukwa hatuna kiwanja cha ndege cha mkoa, tunaomba Wizara kwa kipindi kijacho tufikiriwe na sisi tuwe kwenye orodha ya mikoa kwa uendelezaji wa viwanja vya ndege vya mikoa. Ni mkoa tangu mwaka 1974 na sasa tunastahili kuwa na kiwanja hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya Fungu 14 ya hotuba ya Wizara, kuhusu kufikia asilimia 95 ya ujenzi wa barabra ya Sumbawanga - Matai - *Kasanga Port (DRC-Congo)* ni vema mtuunganishe na Zambia sasa kwa barabara ya Matai - Kasesya yenye kilometra 50 kufanyiwa kazi, kwani tangu mwaka 2019/2020 tunasubiri mkandarasi, tunaomba kuongezewa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kibaoni - Muze - Mtowisa -Kilyamatundu, pamoja na kutuunga kutokea Ntendo - Muze - Kilyamatundu yenye kilometra 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba taratibu za kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya mapitio ya upembuzi yakinifu na usanifu, hili lifanyiwe kazi haraka, kwani barabara

hiyo imeharibika sana, haina madaraja kabisa na usumbufu mkubwa sasa kwa ajili ya mvua nyingi za mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunaomba *TARURA* kuongezewa fedha kwa kushughulikiwa barabara za vijijini tuunganike na shughuli za uzalishaji zifike na kisha wafikie masoko kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mungu kunipa afya njema ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni yangu naishauri Serikali fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo zitolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe miundombinu katika barabara kuu zote zijengwe kwa kiwango cha lami ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka vijijini kwenda miji mikuu kwa mauzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe na ijenge kwa umadhubuti madaraja yote ili wakati wa masika madaraja hayo yasikate mawasiliano baina ya eneo na eneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ziweke alama za usalama barabarani ili kuepusha ajali maana kuna maeneo alama hizo hazipo na zingine zimefutika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali iboreshe mizani iliyopo maeneo ya Mikese, Morogoro ili kuondoa msongamano usio wa lazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naishauri Serikali iboreshe barabara ya Chalinze hadi Mlandizi maana ni mbovu na mara kwa mara inasababisha ajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali ijenge daraja la juu maeneo ya Magomeni hadi *Fire* Mkoa wa Dar es Salaam ili kuondoa adha wanayopata wananchi kipindi cha mvua maana Mto Msimbazi huleta mafuriko na eneo la Jangwani halipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho viwanja vyatia ndege viboreshwe ili ndege ziweze kutua kwa wakati wote.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, pongezi nyingi kwa Rais, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu, Mawaziri, Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Naibu Mawaziri wa Wizara, Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Serikali kwa uchapakazi na hasa utekelezaji mzuri wa llani ya CCM. Pongezi pia kwa viongozi wote wa CCM wakiongozwa na Mtendaji Mkuu Dkt. Bashiru Ali na wana CCM wote kwa kukiwezesha chama kutembea kifua mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, michango mahsus; changamoto ya upungufu wa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara; Serikali iendelee kuboresha chanzo kilichopo ambacho ni tozo ya mafuta na kadhalika kwa *RFB* kushirikiana na *TRA* na *EWURA* kutafiti na kubaini mianya inayovujisha mapato na kuiziba haraka kama ilivyokwisha shauriwa. Serikali itafute chanzo/vyanzo vingine kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutumia vema fedha zitokanazo na chanzo kilichopo, vipaumbele vyatia aina ya barabara, kiwango na aina ya matengenezo kulingana na utaalami ikiwemo matumizi ya *RMMS* na *DROMAS* na *results* zake. Mipango mikuu ya Taifa izingative zaidi. *FYDP*, mpango wa mwaka, llani ya CCM na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bodi ya Mfuko wa Barabara ifanyiwe maboresho kwa kumjumuisha Mkurugenzi/Mtendaji Mkuu anayehusika na barabara kutoka TAMISEMI ili amsaidie

Katibu Mkuu wake ambaye kwa sasa yuko peke yake kwenye bodi. Upande wa *TANROADS* timu imetimia. Katibu Mkuu yuko pamoja na Mkurugenzi wake wa barabara. Idadi ya wajumbe inaweza kuangaliwa kwa mantiki hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uwanja wa Ndege wa Songea; kuboresha shirika la ndege ni pamoja na kuboresha viwanja vyta ndege kama ilivyopangwa kwenye *FYDP2*. Kwa kuwa tumeamua kama Taifa kuanza na viwanja vyta mikoa, nashauri ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songea uharakishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, reli ya Mtwara-Mbambabay na matawi ya Mchuchuma na Liganga. Kwa kuwa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, *FYDP2* umeitaja reli hii, lakini kwa kiwango cha kazi za awali. Nashauri sasa Serikali isonge mbele katika mradi huu kwa hatua kubwa zaidi na muhimu za ujenzi. Ushirikishaji wa wabia ama wawekezaji wenza kwa utaratibu wa *PPP*uharakishwe kwani hesabu za kiuchumi kwa reli hii hazina mashaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, utayari katika matukio ya dharura (*emergency preparedness*); hatujachelewa, tuharakishe kuwa na mpango wa kitaifa kwa ajili hii. Mafuriko, vimbunga, matetemeko na kadhalika yasitukute tukiwa hatuna utayari na hatukuiandaa (*off guard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mtandao bora unaozingatia njia mbadala (*alternative route*); mfano ni daraja la Kiyegea lilipovunjika. Tungepata nafuu kubwa kama barabara inayopita Berega kutokea Kiwanda cha Sukari Mtibwa ingekuwa imeboreshwa. Pia barabara ya Mikumi - Kilosa - Dumila. Kwa uwiano huo Sera ya Taifa ya kuunganisha mikoa kwa barabara za lami ni mojawapo ya njia za kuufanya mtandao wa barabara uwe unaojitibu wenyewe inapotokea dharura. Na kwa sababu hiyo, naomba Serikali iipe umuhimu barabara inayounganisha Mkoa wa Ruvuma na Mkoa wa Lindi bila kulazimika kuititia Mtwara ambako ni mbali. Barabara hii itakuwa njia ya mkato kwenda Dar es Salaam kuititia Nachingwea, Liwale na Nangurukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya changamoto kubwa zinazoorodheshwa katika taarifa mbalimbali za sekta ni masuala ya usalama barabarani. Katika Wilaya ya Tunduru barabara ya mchepuo (*Tunduru by-pass*) inayopita Masonya hadi Mlima Mkapunda ni ya kupunguza ajali kwa kiwango kikubwa. Pia eneo la mzunguko (*round about*) katika eneo ambapo barabara zinakutana kutoka Msumbiji, Songea na Mtwara ni muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, haja ya kulirudishia Shirika la Ndege uwezo kutokana na kuzorota kwa biashara ya usafiri wa abiria na mizigo kwa ndege kutokana na kadhia ya Corona na kutokana na hatua ya shirika letu la ndege kuanza safari za kusafirisha mizigo katika kujinasua, naipongeza Serikali na Menejimenti ya Shirika kwa ubunifu. Hata hivyo, nashauri Serikali ichukue hatua zaidi kulinusuru Shirika la Ndege ikiwa ni pamoja na kulipatia fedha za kuziba pengo kama zilivyoofanya nchi zingine. Hatua hii ichukuliwe kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania ili kuokoa uwekezaji mkubwa uliofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sayansi, teknolojia na ubunifu; katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021 mojawapo ya miradi mikubwa ya kielelezo (*flagship projects*) ni uboreshaji wa mawasiliano kwa njia ya *ICT* na pia kukuza na kuboresha utafiti. Ni vema juhudzi za Serikali kufikisha mawasiliano vijijini na kwingineko nchini zikaenda sambamba na uboreshaji wa madaraja ya mitandao kwenda mifumo ya *3G* na *4G* badala ya mitandao ambayo iko katika *2G*.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa ukuu wake naye kuniwezesha na mimi kuwepo kwenye mkutano huu niweze kuchangia hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano ya mwaka wa fedha 2020/2021. Hotuba hii inakwenda kutekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 ambayo kwa pamoja imeainisha masuala mbalimbali ya kimkakati katika sekta nzima ya uchukuzi, mawasiliano

pamoja na ujenzi. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri yenyе taswira ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni takribani miaka 120 ambapo historia iliandikwa, mwaka 1912, Serikali ya kikoloni nchini iliamua kuimarisha sekta ya usafirishaji kwa kujenga reli ambapo njia zake ziliunganisha miji hasa maeneo ya kilimo, uzalishaji na kibiasara, reli kuu kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza, hatimaye Kigoma na Tanga.

Katika uchumi wa nchi yoyote duniani, sekta ya usafirishaji ni muhimu sana, kwa hiyo, Serikali kuchukua hatua madhubuti ya kuimarisha sekta ya usafirishaji kwa kujenga reli ya kisasa (*SGR*), ni moja ya mwarobaini wa kutatua changamoto ya usafirishaji mizigo na kulinda usalama wa barabara zetu. Mageuzi makubwa ya Serikali yetu yanalenga kuwaimarisha wananchi, si tu wafanyabiashara bali hata wasafiri kwa utekelezaji wa ujenzi wa reli ya kisasa (*SGR*) yenyе kasi ya 160km/saa utakuwa na faida kubwa kwani masaa 2.5 Dar es Salaam-Morogoro na masaa tisa kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, ni dhahiri kutakuwa na furaha kubwa kwa watu kuwahi kufika Mwanza mapema badala ya saa saba usiku au kulala Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu umeleta pia faida mbalimbali kwa wafanyabiashara wa hapa nchini kwetu kwa kusambaza bidhaa mbalimbali zitakazotumika katika ujenzi huo, pamoja na wananchi kupata ajira takribani mifuko ya simenti 9,200,000 ambayo ni sawa na tani 600, nondo kilo milioni 115 sawa na tani 1500 na mataruma 1,400,000; kutoka kwa wasambazaji wa malighafi hizo takribani 500, wafanyakazi 10,000 huku asilimia 94 ya wafanyakazi hao ni Watanzania. Pia asilimia 48 ya wataalam ni Watanzania, kwa hiyo, pamoja na mradi huu kuwa nguzo imara ya usafirishaji nchini, *SGR* imekuja kutoa fursa za ajira kwa Watanzania. Pongezi nyingi sana ziende kwa Serikali yetu ya awamu ya tano kwa kuthubutu hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ilizochukua hasa kuhakikisha inaboresha bandari zetu kwa kiwango cha juu kuitendaji na kupunguza urasimu na changamoto zilizokuwepo hapo awali, kiuhalisia nchi yetu inategemewa na baadhi ya nchi jirani kupidishia mizigo yao hapa na hivyo kuliingizia Taifa fedha. Ni wajibu kuhakikisha tunatoa huduma inayokidhi viwango ili tuendelee kuwavutia watumiaji wa bandari zetu.

Hata hivyo bado kuna changamoto ya bandari bubu takribani 600, bandari hizi zimekuwa zikilikosesa Taifa mapato kwani watu wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakipitisha mizigo ya magendo katika bandari hizo bubu. Lakini nawapongeza Serikali kuptitia Mamlaka ya Bandari kwa uamuzi waliochukua wa kuzirasimisha bandari hizo ili ziweze kutambulika jambo ambalo litasaidia kuleta ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Naishauri Serikali kuendelea kuzishughulikia baadhi ya changamoto zilizopo katika sekta ya bandari ili tuendelee kuwavutia hasa watumiaji wa bandari zetu hapa nchini na sisi tuendelee kuingiza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Serikali imeendelea kusisitiza hasa katika suala zima la mawasiliano nchini kwa makampuni kuwa na uwiano sawa wa utoaji huduma, lakini bado changamoto ya upatikanaji wa mawasiliano kwa baadhi ya maeneo imekuwa ni tatizo sugu, ni wakati sasa Serikali kwa kushirikiana na wadau wa mawasiliano kufanya tafiti katika maeneo hayo na kuhakikisha mawasiliano yanapatikana, kuna baadhi ya maeneo usikivu unakuwa ni wa shida kulingana na kutokuwa na minara ya kutosha, ni vyema maeneo hayo yakaangaliwa na kuongezewa nguvu ili wananchi wapate mawasiliano, adha hii pia ipo kwenye baadhi ya maeneo Jimboni kwangu Kibaha Vijijiini, kuna maeneo mawasiliano ni ya shida, kama nilivyotangulia kusema hapo awali na kuishauri Serikali kuchukua hatua kutatua changamoto hizi, dunia sasa imebadilika sana, simu/mawasiliano yakitumika vizuri ni fursa ya kujajiri na kuijingizia kipato kwa haraka hivyo ni vyema tukahakikisha mawasiliano yanaboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hasa katika kusimamia wadau wa mawasiliano hapa nchini, naipongeza Serikali kwa kuhakikisha wadau wote wa mawasiliano wanafanya kazi kwa kufuata taratibu na sheria zilizowekwa hasa kwa kulinda hadhi na heshima ya nchi yetu. Naishauri Serikali kutosita kuchukua hatua kali kwa yejete atakayekiuka au kuvunja sheria na kutofua utaratibu uliowekwa, hili lifanyike kuanzia kwenye urushaji wa habari katika mitandao ya kijamii, huko kumekuwa na upotoshaji mkubwa wa taarifa na baadhi zimekuwa zikileta taharuki kwa wananchi, hata hivyo nichukue fursa hii kuipongeza *TCRA* kwa hatua mbalimbali ilizowahi kuchukua kwa kuwatoza faini na hata kuwafungia baadhi ya vyombo kwa kukiuka taratibu na sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaona juhudhi mbalimbali za Serikali hasa katika sekta ya ujenzi wa miundombinu ya barabara nchini, miradi mbalimbali inaendelea nchi nzima ili kuhakikisha barabara zinapitika, kuunganisha mikoa kwa mikoa ili kurahisisha shughuli za kibashara baina ya eneo moja na lingine, tukiwa na barabara zinazopitika wakati wote hasa katika vipindi vyote vya mvua na kiangazi tutakua tumetatua changamoto zilizopo za baadhi ya barabara kupidika kwa vipindi maalum pekee, baadhi ya madaraja tumeshuhudia yakibomoka hasa katika vipindi hivyo nilivyotangulia kusema hapo awali, ubora wa barabara zetu uzingatiwe kuanzia hatua za awali kwa kuangalia wakandarasi wanaopatiwa kandarasi hizo. Aidha, watumishi wetu waliopewa dhamana ya kusimamia barabara hizi wafanye kazi hiyo kwa umakini, wafanye ukaguzi wa mara kwa mara ili kuangalia maeneo yote yatakayokuwa na changamoto kuyashughulikia mara moja ili kuepusha athari kubwa zinazoweza kutokea badea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la changamoto za barabara lipo Jimboni kwangu Kibaha Vijijiini, kuna baadhi ya barabara ziko katika hali mbaya hasa kipindi cha mvua kama hiki, naiomba Serikali hasa kupidia Wakala wa Barabara kuchukua hatua za haraka hasa kwenye barabara zote zilizopo chini ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*) Jimbo la

Kibaha Vijijini kuhakikisha zinakarabatiwa na miradi kuisha kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumpongeza Rais wetu Magufuli kwa uongozi wake uliotukuka na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya pongezi, naomba kuchangia hoja iliyoko mezani kwa kutoa maoni au ushauri katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na sekta ya ujenzi; naomba kuikumbusha Serikali katika mwaka huu wa fedha kuititia Wakala wa Barabara - *TANROADS* kutekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya kilometa 56 inayounganisha Wilaya ya Longido, Mkoa wa Arusha na Wilaya ya Siha, Mkoa wa Kilimanjaro. Ujenzi wa barabara hii ni moja ya ahadi za llani ya CCM ya mwaka 2015-2020 na ni barabara muhimu kiuchumi (kilimo na utalii) na kijamii kwani pia itakuwa *bypass* kwa magari yasiyohitaji kuititia Arusha kutokea mpakani na nchi ya Kenya kuititia Namanga ama magari kutoka Moshi na Mikoa ya Kusini Mashariki ya Tanzania yanayokwenda nchi jirani ya Kenya na mataifa ya ukanda wa pembe ya Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishauri Serikali iongeze bajeti ya *TARURA* na kuziwezesha Wilaya ambazo hazina mitambo ya ukarabati wa barabara kuwa nazo ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za dharura na za kawaida inapohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hali ya sasa kwa Wilaya kama Longido ambayo haina vitendea kazi vyake inavyomiliki vya kutengeneza barabara, linapotokea hitaji la dharura la kurekebisha miundombinu ya barabara inapoharibiwa na majanga kama mafuriko, inabidi kutegemea zana za wakandarasi ambao utaratibu wa kuwa-

*engage na bajeti huwa ni kikwazo kikubwa kwa TARURA kuweza kunusuru au kutoa huduma ya kawaida ya marekebisho ya barabara za vijiji kwa ufanisi inapohitajika.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na haja ya kuwapa *TARURA* vitendea kazi; pia naomba wapewe wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, imani yangu ni kuwa *TARURA* wakiwa na mitambo na vitendea kazi muhimu pamoja na wataalam wa kutosha katika kila Wilaya, Serikali itaokoa fedha nyingi za kutengeneza barabara zake za vijiji nyenyewe kwa kutumia zana na wataalam wake badala ya kutegemea wakandarasi ambao husaini pesa nyingi kama hali ilivyo kwa sasa katika Wilaya nyingi ikiwemo na Wilaya yangu ya Longido.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa sekta ya mawasiliano, katika kujenga minara ya mawasiliano ya simu na ving'amuvi vya redio na runinga katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu, nashauri Serikali itoe kipaumbele katika maeneo yaliyo mipakani na nchi jirani tunazopakana nazo. Hili ni kwa sababu adha wanayopata Watanzania wanaoishi Wilaya za mipakani kama Wilaya yangu ya Longido ni kwamba wananchi wanajikuta wakitegemea huduma hizi muhimu kuititia mitambo ya nchi zingine jambo linalowakosesha habari muhimu za nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mantiki hiyo, katika mwaka huu wa fedha naomba Serikali watuongezee minara ya mawasiliano katika kata na vijiji vinavyopakana na mpaka na Kenya na hasa pale ambapo hakuna mawasiliano kabisa hadi leo kama Kata ya Noondoto, Vijiji vya Magadini, Wosiwosi, Matale B, Kimwati, Sinonik, Kiserian, Kitenden, Irkaswaa na Kamwanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hitaji la minara ya mawasiliano katika maeneno mbalimbali ya mipakani, naomba pia Serikali iwaelekeze makampuni husika kuhakikisha kuwa minara inayojengwa katika vijiji ambavyo

bado havijafikiwa na umeme, pamoja na kufunga mitambo ya *solar*, pia wafunge jenereta. Nasema hivi kwa sababu tuna minara ambayo imejengwa Wilayani kwangu Longido, Kata za Matale na Kamwanga ambayo inaendeshwa kwa nguvu za *solar* pekee na jua linapotua au siku za baridi, mawasiliano hukatika na wananchi kupata adha ya kukosa mawasiliano ya simu na huduma zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kuishauri Serikali ihakikishe kuwa minara yote ya mawasiliano inayojengwa inafungwa mitambo imara na yenye uwezo wa kutoa huduma za *internet* kwa kiwango cha walau 3G au zaidi. Nashauri hivi kwa sababu kwa hali ilivyo kwa sasa hivi minara mingi Wilayani kwangu ni ya kiwango cha 2G tu na hivyo kusababisha uwezo wa watumiaji wa *internet* kuweza ku-*download data* kuwa hafifu. Hili linawafanya wanafunzi wetu ambao kwa sasa wako majumbani kutokana na janga la *Corona virus* kushindwa ku *access learning materials* kwa njia za kidijitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya machache ninashukuru na ninaunga mkono hoja!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, sisi sote tuendelee kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwa Watanzania wote na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Mbulu niungane na viongozi wote kuliombea Taifa letu na dunia nzima kwa janga hilli la Corona, ewe Mwenyezi utuokoe na janga hilli la Corona sisi, uturehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi na viongozi wenzangu tuwaombee Watanzania wote waliotangulia mbele ya haki Mwenyezi Mungu awapokee katika ufalme wake usio na mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua nafasi hii kumwombea Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Serikali

nzima ya awamu ya tano kwa jinsi ilivyotekeleza llani ya CCM ya mwaka 2015/2020. Yapo mambo mengi yamefanyika katika sekta hii, mifano yake ni ujenzi wa Daraja la Magara, usanifu wa barabara ya Karatu, Mbulu, Haydom, Simiyu, Shinyanga na usanifu wa barabara ya Mbuyuni, Magara, Mbulu na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nitoe mchango wangu wa ushauri kwa Serikali katika sekta hii. Kwanza, kuna baadhi ya shule za kidato cha tano nchini bado hazijaunganishwa na Mkonga wa Taifa hali inayosababisha wanafunzi wa shule hizo kushindwa kupata masomo ya TEHAMA hivyo basi Serikali ifanye mapitio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Pili, Serikali kufanya mapitio ya uwekaji wa minara nchini kwani kuna maeneo uwekaji wake uko katika ukanda mona hali inayofanya huduma kutokufika haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Serikali ifanye usanifu wa uwanja wa ndege wa Mkoa wa Manyara kwa kuwa tayari RCC imeshapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Serikali kupitia bajeti ya Mfuko wa Mawasiliano itusaidie kupata kompyuta 240 katika niliyoomba mwaka 2019 kwa barua kwa ajili shule nane za sekondari kidato cha nne, shule hizo ambazo tayari wananchi wanajenga madarasa ya kufundishia toka mwaka 2014 kwa hiyo kuna umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mbulu naomba sana Serikali itangaze *tender* ya ujenzi wa kipande cha barabara kilometra 50 ya Mbulu, Dongobesh, Haydom. Kwa kuwa barabara hii ya Karatu, Mbulu, Haydom, Shinyanga takribani kilometra 400 ni muhimu sana kwa Mikoa ya Mara, Arusha, Manyara, Singida na Shinyanga, binafsi sisi Wabunge wa Mikoa hiyo kwa niaba ya wananchi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nianze mchango wangu kwa kmpongeza Mheshimiwa Rais

kwa kuendelea kuonesha njia katika vita hii ya janga la Corona. Hakika Mungu yu pamoja nawe na wale wote wenye nia njema na Taifa hili wako nyuma yako. Nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na Naibu Mawaziri wote kwa pamoja kwa utendaji wao mzuri katika kuwalettea maendeleo. Pongezi pia kwa watendaji wote katika Wizara hii kwa namna wanavyochapa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla naipongeza sana Serikali kwa kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika miundombinu ya nchi yetu ili kuharakisha maendeleo nchini. Naipongeza Serikali kwa *SGR*, naipongeza Serikali kwa ununuzi wa ndege, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa viwanja vya ndege, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa barabara za juu, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa meli katika Maziwa Makuu na kadhalika. Hapa Serikali inaonesha nia yake njema ya kutekeleza kwa vitendo llani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niiombe Serikali kuona umuhimu wa kuunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkao wa Lindi, sambamba na kuitoa Wilaya ya Liwale kisiwani. Kwa kuijengea barabara za Nachingwea-Liwale na barabara ya Nangurukuru-Liwale. Barabara hizi kwa Mkao wa Lindi na Wilaya ya Liwale ni barabara za kiuchumi na ni za huduma kwa wakazi wa Mkao wa Lindi. Lakini pia iko barabara inayounganisha Wilaya za Liwale, Nachingwea, Nanyumbu na Wilaya ya Tunduru. Naiomba Serikali kuona umuhimu wa kuipandisha daraja barabara hii, kutokana na umuhimu wake katika Wilaya hizo na kwa namna barabara hii ilivyo ndefu. *TARURA* hawawezi kuendelea kuihudumia barabara hii kwani tayari yenye ina sura ya barabara ya Mkao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari ya Mtwara ni muhimu sana kwa uchumi wa mikoa ya Kusini na Taifa kwa jumla. Pamoja na kuwa Serikali inafanya juhudu kubwa ya kuipanua bandari hii, lakini bado miundombinu ya bandari hii ni duni sana. Kwani bado wafanyabiashara wanapendelea sana kutumia barabara badala ya meli kwa ajili ya mizigo toka Mtwara, Songea na Lindi jambo

linalotuonesha kuwa kuna tatizo la kiutendaji au la kimiundombinu kwenye bandari hii.

Mheshimiwa Naibu Spika kwenye ujenzi wa *SGR* naiomba Serikali kuzingatia kwa makini ushauri wa Kamati wa kujenga loti zilizobaki kwa mpango wa *PPP*ili kuharakisha ujenzi wa miradi hii na kuiwezesha Serikali au kuipunguzia mzigo wa kuwahudumia wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba pia Serikali kuongeza au kuharakisha upelekaji wa fedha katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) kwani miradi mingi ya mfuko huu imekuwa ikitekelezwa kwa kusuasua kutohana na uhaba wa fedha. Mfano katika Wilaya yangu ya Liwale viko vijiji ambavyo havina mawasiliano ya simu ambavyo ni Vijiji vya Mkutano, Kikulyungu, Nahoro, Mtungunyu, Ndapata, Ngorongopa na kadhalika villvyo katika Kata za Mkutano, Nangano, Mlembwe, Mangirikiti na Mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo hapo juu naomba kuunga mkono hoja 100%.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naipongeza Wizara kwa utekelezaji wa majukumu yao pamoja na bajeti ya fungu hili inayotengewa na Wizara hii kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Ifakara-Lupiro-Malinyi-Kilosa Mpepo-Londo-Lumecha Songea ni muda mrefu sasa Serikali imekuwa ikiahidi kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Barabara hii ina umuhimu mkubwa katika kupeleka Tanzania katika uchumi wa kati kuititia viwanda kwa kuwa barabara hii unapita katika maeneo yenye rutuba na bonde zuri kwa kilimo cha kibashara. Huwezi kuwa na kilimo cha biashara kama hakuna miundombinu ya barabara na madaraja ya uhakika katika kusafirisha mazao kwenda katika soko. Aidha, miundombinu ya barabara yenye uhakika ni moja ya kivutio kikubwa kuwavuta wawekezaji wa kilimo cha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba kwa mara nyiningine tena kwa Serikali kuanza kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais John Magufuli kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Mheshimiwa Rais amekuwa akihaidi kuanza ujenzi ya barabara hii ya Ifakara - Lupiro - Malinyi - Kilosa - Mpapo - Londo -Lumecha - Songea. Ahadi hizo ametoa mara nne kuanzia 5 Septemba, 2015 akiwa Malinyi kipindi cha kampeni. Alirudia tena ahadi yake alipotembelea Mkoa wa Morogoro Aprili, 2019 Ifakara na Mji wa Kidatu alipokuja kuzindua Daraja la Magufuli liliopo katika Mto Kilombero.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Malinyi bado inakabiliana na changamoto ya mawasiliano, Kata za Biro, Itete, Ngoheranga na Kilosa Mpapo vijiji vingi katika kata hizo havina mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aldha, watoa huduma wa Airtel na Tigo katika Tarafa za Matimbira na Ngoheranga mitambo yao inaonesha imezidiwa uwezo. Mara kwa mara mitandao hii haifanyi kazi. Tunaiomba Serikali kuwasiliana na watoa huduma hao wakarabati mitambo ili waweze kuboresha huduma za mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naikumbusha Serikali yangu ifike wakati sasa kupitia bajeti hii kuondoa changamoto hizi za mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naonga mkono hoja.

**MHE. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kidogo kwenye bajeti ya Wizara hii ya Ujenzi na Uchukuzi na naomba ukubali kupokea mchango wangu kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwanza kwa kuipongeza Serikali ya awamu ya tano chini ya Rais Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi nzuri anayowafanya Watanzania kuanzia kwenye miradi ya kimkakati na kisekta hakuna Wizara hata moja ambayo

haifanyi vizuri. Rais yuko makini na Mawaziri wake wote wako makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo ameongoza mapambano ya kujikinga na maambukizi yanayotokana na mlipuko wa hili gonjwa baya linalosababishwa na virusi vya Corona (*Covid 19*).

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, sasa naomba nichangie kwenye hoja iliyoko mezani na nianze na kumpongeza Waziri Mheshimiwa Kamwelwe na Naibu Mawaziri wake pamoja na watendaji wote ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana na kuonesha ni jinsi gani Serikali imedhamiria kuendelea kutumikia Watanzania kwa kujenga na kuboresha barabara zetu katika Fungu 98 shilingi 1,766.604 trilliuni zimetengwa kutumika mwaka huu wa 2020/2021. Kule Arusha na sisi tumeonja hiyo neema kwa kujengewa barabara yenye njia nne kutoka Sakina hadi Tengeru. Sasa tunaomba awamu ya pili kutoka Tengeru hadi USA River nayo itekelezwe ili kupunguza ajali zinazotokana na msongamano.

Tunashukuru pia kwa *Western bypass*toka Ngaramtoni hadi USA River ambayo ujenzi wake umemalizika, sasa tunaomba barabara ya Malula Kibaoni hadi Kingori, Maruvango, Leguruki, Ngarenanyuki, Ngabobo, Uwiro mpaka Oldonyo Sambu nayo ipandishwe hadhi na kujengwa kwa kiwango cha lami ili iwe *Eastern bypass* ambayo itaunganisha barabara kuu za Arusha - Moshi hadi Dar es Salaam na barabara kuu ya Arusha - Namanga hadi Nairobi. Kwa kufanya hivyo, uchumi na ubora wa maisha ya wananchi wa eneo hilo la Arumeru zote mbili Mashariki na Magharibi utakuwa dhahiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimebahatika pia kutembelea nchi kadhaa za jirani nikavutiwa na sera ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami barabara za vijiji zenye urefu wa kilometra 10 ndani ya kila kijiji kinachobahatika kupitiwa na barabara kuu mpya inayojengwa. Kuiga mambo

mazuri ya wenzetu ni jambo jema. Sisi tukifanya *extension* ya namna hiyo hata kwa kilometra tano kutaleta mageuzi makubwa sana kwenye sekta ya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri. Nawapongeza pia Waheshimiwa Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu, watendaji na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa ahadi ya ujenzi wa kilometra tano za barabara za lami mjini Bagamoyo. Ujenzi umeanza na mpaka sasa mita 620 zimekamilika na mita 630 ujenzi unaendelea. Namuomba Mheshimiwa Waziri atusaidie ujenzi uanze kwa kilometra 3.75 zilizobaki hasa kwa kuzingatia kuwa ahadi hii ni ya miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, safari ya Tanzania kufika uchumi wa kati mwaka 2025 inategemea sana uwekezaji wa kimkakati katika ujenzi wa miundombinu wezeshi mfano barabara, reli, umeme na kadhalika. Serikali imeahidi kwa muda mrefu ujenzi kwa kiwango cha lami barabara zifuatazo; Tegeta - Bagamoyo, Makofia - Mlandizi - Vikumburu; Mapinga - Kibaha na Makurunge - Pangani - Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara hizo. Hoja yangu ni kuwa kwa nini kwa miradi yote hiyo minne hakuna hata mradi mmoja ambao ujenzi wake umanzia Bagamoyo!! Hii ina maana kuwa maboresho ya miundombinu ya usafirishaji Bagamoyo itasubiri kwa miaka mingi mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri utekelezaji wa miradi hii ujumuushe loti inayoanzia Bagamoyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, kuhusu ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, naomba Mheshimiwa Waziri atujulishie nini hatma ya ujenzi wa bandari hiyo? Baada ya kazi kubwa na gharama kubwa ya maandalizi ya mradi huo, sasa hivi mradi haujulikani ulipo!!

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, kuhusu mapunjo ya fidia ya baadhi ya wananchi wanaopisha mradi wa Bandari Bagamoyo. Namuomba Mheshimiwa Waziri asimamie wananchi hao walipwe. Sasa ni miaka mitano tangu wananchi hao wamehakikiwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kuhusu makazi mbadala kwa wananchi wanaopisha mradi wa bandari; wananchi hawa waliahidiwa na Serikali kupitia EPZA kuwa watapewa makazi mbadala kwa barua ya Mkurugenzi Mkuu wa EPZA ya tarehe 20.01.2014. Kijiji kizima cha Pande na sehemu ya Kijiji cha Mlingotini vinahama! Jumla ya Kaya zipatazo 460 zenye wakazi 1,670 zinahama! Wananchi hawa wakiambiwaondokeni, wanaenda kuishi wapi ukizingatia baadhi ya wananchi hao fidia zao ni ndogo sana.

Naiomba Serikali yangu adhimu iwape wananchi hawa shamba la Kidagoni kuwa makazi yao mbadala kama walivyoahidiwa na Serikali. Hii ni jamii moja ilioishi pamoja kwa miaka mingi sana. Kutowapa makazi mbadala itasambaratisha jamiii hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya na uhai na siku ya leo tukiwa hapa kujadili maendeleo ya miundombinu ya barabara nchini ambazo zimeharibika sana kutohana na mvua zilizozidi vipimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru Serikali kwa kuendeleza kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kutengeneza na kuboresha barabara hii kila mwaka ili kuweza kuitika mwaka mzima. Vilevile naishukuru Serikali kwa kuendelea kurudisha mawasiliano ya barabara zilizokatika kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kwa kutengeneza maeneo korofi na yaliyoharibika vibaya.

Mwisho naishukuru Serikali kwa kutujalia timu ya kufanya tathimini ya uharibifu wa barabara za Jimboni kwangu Morogoro Kusini Mashariki ili kufahamu uharibifu na mahitaji yake ili kuanza ujenzi wa kuzirudisha katika hali yake baada ya mvua. Nasema ahsante sana kwa niaba ya watu wa Morogoro Kusini Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuwa Jimboni ili kusikiliza na kupata shida za wananchi wake pamoja na ahadi yake ya kutengeneza barabara ya Ubena Zomozi - Kizuka kwa kiwango cha lami. Pia wajuzi wake wa ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme Mto Rufiji na kuanza kujenga na kuboresha barabara ya Ngerengere, Kiwege, Mlilingwa, Dete, Kisanga Stand Tununguo mpaka Mvua kwa kiwango cha changarawe ili kuweza kuitika mwaka mzima na kuwezesha hata magari makubwa yanayopeleka vifaa sehemu za mradi wa bwawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani na ahsante kwa Serikali naomba kushauri na kuomba mambo machache yafuatayo; kwanza, barabara ya Ngerengere - Kidunda kupandishwa hadhi kuwa barabara ya Mkoa ili kuwa chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu barabara hii ni ndefu ina urefu wa kilometa zaidi ya 75 na haijatengenezwa kwa miaka zaidi ya mitatu na haijawahi kutengenezwa yote kutokana na uwezo mdogo wa Halmashauri ilipokuwa inahudumia barabara hii na hata sasa *TARURA* bajeti yao ni ndogo sana. Bajeti ya *TARURA* kwa mwaka ni ni shilingi bilioni 1.1 ambazo hata wakitengeneza

barabara hii pekee hawawezi kutengeneza yote pamoja na madarasa na kalvati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ndio inakwenda kwenye eneo kwenye miradi mikubwa ya kimkakati ya Mkulazi Kiwanda cha Sukari ambaao mpaka sasa mitambo imekwama kwa zaidi ya wiki tatu kwenye tope lililosababishwa na ubovu wa barabara.

Naomba pia Serikali ikatoa tena timu ya tathimini kuja kukagua na kutathimini ubovu na mahitaji ya barabara hii ili iweze kujengwa hata kwa kiwango cha changarawe na kuboresha maeneo korofi na kalvati na madaraja ili iwezo kupitika.

Pili, naomba Serikali kuanza ujenzi wa barabara ya Bigwa - Kisaki kwa kiwango cha lami kama tulivyoipitisha hapa katika bajeti kwa bajeti inayotekelezwa mwaka huu wa fedha kwa sababu ni barabara yenye uchumi mkubwa kutohakana na kwenda kwenye Mbuga ya Selous, Bwawa la Nyerere, kuunganisha na Mkoa wa Pwani na Kusini kupitika moja kwa moja mpaka Rufiji. Vilevile barabara itapunguza gharama za uzalishaji na usafiri wa mazao ya kilimo ambaao ni wakulima wakubwa wa mpunga, matunda na miwa na kuongeza mapato ya wakulima na kukuza kipato chao na kuongeza uchumi wa Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naomba pia Serikali kuanza ujenzi wa barabara za Maamuzi - Luholole - Tununguo; barabara ya Mkuyuni - Ludewa mpaka Mkulazi; barabara ya Kibwaya - Mfumbwe mpaka Kiroka; barabara ya Tomondo - Tununguo; barabara ya Mbarangwe - Tununguo - Kisanga Stand; kuboresha barabara ya Kidunda - Mvuga; barabara ya Kidugalo - Visaraka - Magera - Lubumu mpaka Matuli; kujenga barabara ya Seregete B mpaka Ngese - Kwaba - Matuli na barabara ya Kwaba - Usungula ili ziweze kupitika na kurahisisha mawasiliano ya watu wetu na kuanza uchumi. Pia nikurahisisha shughuli za uwekezaji wa viwanda vinavyoendela Mkulazi na ujenzi wa Bwawa la Kidunda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(5) naongeza nusu saa. Mheshimiwa Atashasta Nditiye, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa, mto aho ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii. Awali ya yote kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai katika siku yetu hii muhimu ambayo tunajadili hotuba ya bajeti ya Wizara yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa heshima kubwa sana ya kumsaidia katika Serikali yake, lakini pia kwa kuwapa heshima kubwa sana wnanchi wa Jimbo la Muhamwe walionichagua niweze kuwatumikia kama Mbunge wa Jimbo la Muhamwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri *Engineer Kamwelwe* kwa mwongozo mbalimbali ambao ananipatia katika kufanya kazi katika Wizara. Pia siwezi kumsahau Mheshimiwa Elias Kwandikwa pacha wangu, kwa jinsi tunavyoshirikiana naye kila siku katika kuhakikisha kwamba Wizara yetu inakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru pia kwa Makatibu Wakuu wote watatu na Naibu Katibu Mkuu ambao wamekuwa wakiongozana na sisi katika hatua mbalimbali za kiutendaji kwenye Wizara yetu na kuhakikisha kwamba Wizara yetu inakwenda vizuri. Nikuhakikishie kwamba ushirikiano uliopo ndani ya Wizara ni mkubwa sana. Tunafanya kazi kama familia moja na ndio maana umesikia

hata michango ya Waheshimiwa Wabunge wengi wanapongeza kwamba Wizara yetu inakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongea kwa haraka haraka sana kwa sababu sijajua ni dakika ngapi, ningeambiwa ningeshukuru zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Una dakika saba.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa kuwa nina *portfolio* mbili; nina *portfolio* ya Uchukuzi na ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Uchukuzi nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali ambayo wameitoa. Michango ambayo inaonesha kabisa dhahiri kwamba kuna mafanikio yanayoonekana wazi kwenye sekta yetu ya Uchukuzi. Tumeona mafanikio makubwa sana kwenye Sekta ya Anga, tumeona mafanikio makubwa sana kwenye usafirishaji kwa njia ya maji, lakini pia tumeona mafanikio makubwa sana kwenye usafirishaji kwa njia ya ardhi kwa maana ya reli yetu, ile reli ya *Meter Gauge* pamoja na ile ya kisasa ya *Standard Gauge*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mbalimbali. Tunawaahidi kwamba tumejipanga kuendelea kuhakikisha tunaitumikia nchi yetu na tutatekeleza yote ambayo wametupatia ambayo tumeyachukua na kuyahifadhi kwenye *database* yetu hapa, kwamba sekta hii ya Uchukuzi inakwenda kufanya kazi inayotarajiwa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna moja ambalo ningependa nilizungumzie, tuna suala la usafiri wa majini. Katikati hapa tumekuwa tukipata ajali za hapa na pale kwenye vyombo vyetu vya usafiri wa majini. Tumekuja na mkakati kama Wizara kwa kushirikiana na Chuo cha Baharia

(*DMI*). Kwa kutengeneza sasa utaratibu ambapo sasa wanaovihudumia vyombo vile kwa maana ya Manahodha watakuwa wanatakiwa wawe *Certified* kwa kuititia vyeti vitakavyokuwa vinatambuliwa na *DMI* na kuhakikishwa na watu wa *TASAC*. Hilo tunalitekeleza kwa sababu kweli kabisa kuna ajali nyingi ambazo zinatokea nyingine tunazijua, nyingine hatuzijui. Kuna watu ambao wanaaamua tu kuendesha chombo bila kujulikana na wala hawana cheti chochote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuje tuna Chuo chetu, Chuo cha Bahari (*DMI*) kinatoa vyeti, kinatoa mafunzo mazuri sana na tunataka sasa kila atakayekuwa anaendesha chombo hicho kwa *category* mbalimbali awe anatambuliwa. Katika kufanya hivyo tunaamini kwamba tutapunguza ajali ambazo zinatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Chuo chetu cha *NIT* ambacho kimeendelea kutoa mafunzo mbalimbali. Sasa hivi tunatoa Wahandisi wa kutengeneza ndege zetu na pia tumeshaanza kutoa Marubani. Tunataka kuhakikisha kwamba katika Sekta ya Usafiri wa Anga, Usafiri wa Majini na Usafiri wa Nchi kavu tunajitosheleza kwa Wataalam mbalimbali ambao watakuwa wanatoa huduma kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna suala letu la Mamlaka ya Hali ya Hewa (*TMA*); Mamlaka imeendelea kufanya kazi nzuri sana. Nashukuru kwamba hapa hakukuwa na hoja kutoka kwa Wabunge, tumesikiliza kwa makini sana, lakini niendelee kuwashakikilia kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa inaendelea kutoa elimu na inaendelea kutoa tahadhari kwa wananchi wa Tanzania ili hali yoyote itakayokuwa inakuja wawe wanajua na wawe wanachukua tahadhari kwa haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haraka haraka kuhusu Sekta yangu ya Mawasiliano nyingine tunashukuru Mungu kwamba kwa kweli Wabunge pamoja na kwamba bado kuna sehemu chache ambazo hazijapata Mawasiliano, ni

sehemu ambazo sisi tunazifahamu kama ni asilimia sita, asilimia 94 Watanzania wanawasiliana. Sehemu nydingine nyingi sana ambazo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilaumu hapa na pale au wamekuwa wakilalamika hapa na pale ni zile sehemu ambako wananchi sasa hawataki mtandao wa *Halotel* wanataka mtandao wa *Vodacom*, wananchi hawataki *Tigo* wanataka mtandao wa *TTCL* na kadhalika na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi tutajitahidi, tutaendelea kuwashawishi Makampuni kwa sababu Sekta ya Mawasiliano kwa kiwango kikubwa inaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na Kampuni Binafsi tutaendelea kuwashawishi, kule ambako hakuna mawasiliano, au kule ambako kuna mawasiliano ambayo wananchi hawayataki, tutakuwa tunawashauri hayo Makampuni waende kuwekeza kule, lakini sisi kama Serikali tuna asilimia 94 ambako Watanzania wanawasiliana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tofauti na kama mwaka 2015 ambako kwa kadri tunafanya kampeni kuna sehemu nydingine ambazo ulikuwa unakuta zimekuwa safi kabisa au kwenye mti watu wanapanga foleni kwenda kupata mawasiliano. Kupata meseji ili aweze kujibu halafu arudi kesho yake kupata meseji tena nydingine au kupiga simu. Sasa hivi tumebadili na tunakwenda vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia kwa haraka haraka kuhusu suala la usalama kwenye mitandao. Ni kweli kwamba kuititia *TCRA* tumeendesha zoezi la kusajili laini za simu kwa alama za vidole na tunaendelea kumalizia usajili huo kwa baadhi ya makundi ya watu ambao walikuwa hawajaweza kusajili. Nikuhakikishie kwamba tukishamaliza hivi karibuni, changamoto ambayo inaendelea kidogo kidogo ya tafadhali nitumie pesa kwa kutumia namba hii, jina litatoka jina hili, itakwisha kabisa, lakini mpaka sasa hivi nikuhakikishie watu wanakamatwa, hatuwezi kutangaza kila wakati mtu anapokuuliza, lakini watu wanakamatwa na wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga kuhakikisha kwamba mawasiliano yanatuletelea maendeleo, mawasiliano yanatuletea usalama na sio vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako. Pia nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hii muhimu na ninaanza kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi ili niweze kumsaidia Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Ameendelea kuniamini, nina uhakika kwamba tunaendelea kushirikiana vyema sana na Wizara na Waziri mwenyewe. Vile vile nimshukuru Mheshimiwa Waziri Kamwele kwa Uongozi wake na kwa Maelekezo yake na kwa ushirikiano. Nina uhakika kwamba yako mambo mengi ambayo tumejifunza kuititia uongozi wake na hakika kwamba tumefanya kazi kwa kushirikiana vizuri na kuwezesha Wizara kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee niwashukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uongozi wao. Waheshimiwa Mawaziri watakumbuka kwamba ukipata nafasi ya kufanya kazi siku moja na Mheshimiwa Waziri Mkuu au Makamu wa Rais kuna jambo kubwa lazima ujifunze kwa kuona namna nzuri unavyoweza kufanya kazi kwa maelekezo yao, lakini pia kusimamia shughuli za Serikali. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa vile yupo hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru wewe na nimshukuru Mheshimiwa Spika, nina hakika kwamba

mmeliongoza vyema Bunge hili la Kumi na Moja. Yapo mambo mengi kuititia Kiti tumejifunza namna bora ya kuongoza na hakika Bunge hili limefanya kazi vizuri kuwahudumia Watanzania ambao wanajitegemea kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, niishukuru Kamati ya Miundombinu, chini ya Uongozi mahiri wa Mheshimiwa Kakoso na Makamu wake, Mheshimiwa Hawa Mchafu na Wanakamati kwa ujumla. Kwa hakika watakubaliana nami kwamba tulivyokuwa tukifanya kazi kwenye Kamati, tumeshirikiana vizuri na pia yako mengi ambayo kama Kamati ilielekeza au ilishauri na sisi kama Wizara tuliyachukua na kila wakati tumeshuhudia kwamba bajeti ya Wizara imeendelea kuwa bora kutokana na mchango ambao Kamati imetupatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru familia yangu, wapiga kura wangu wananchi wa Ushetu na Watanzania kwa ujumla. Nafahamu kwamba michango ya Watanzania kwa kulipa kodi imetuwezesha Wizara kupata fedha za kutosha kwenda kuboresha miundombinu. Mheshimiwa Waziri Mpango nakushukuru kwa sababu katika hotuba hii Waheshimiwa Wabunge tumeshuhudia tumejepata hata fedha za kuwalipa makandarasi. Shilingi bilioni 723 kwa kipindi hiki ambacho tumefanya nina uhakika imechochea kwa kiasi kikubwa sana utekelezaji wa miradi yetu. Mheshimiwa Mbunge Nachuma wakati anachangia hapa alikuwa na mashaka na barabara yake kule Mtwara lakini kwa pesa ambazo tumejepokea Mheshimiwa Waziri wa Fedha namshukuru sana miradi inaendelea kwa kasi na itakamilika kwa sababu sasa tuna fedha hakuna madeni ambayo tunadaiwa na wakandarasi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru watendaji wa Wizara, Makatibu Wakuu wako hapa; ndugu yangu hapa Mwakalinga na Makatibu wengine yuko Chamuriho, Dkt. Chaula lakini pia mama Sasabo ambaye amestaafu na watendaji wote, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Jim Yonaz. Nasema hivyo kwa sababu katika uongozi wa Mheshimiwa Waziri hapa

Kamwele kuna wakati mwagine tumefanya kazi kwa kushirikiana, kuna wakati kazi zingine zilikuwa kwenye sekta nyingine Uchukuzi na Mawasiliano lakini nilipopewa nafasi ya kwenda kufanya kazi na Makatibu hawa kwenye sekta nyingine tulifanya kazi vizuri. Nawashukuru sana na naamini kwamba tumeshirikiana vizuri ndiyo maana mambo yameendelea kwenda vyema.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru watendaji wa taasisi mbalimbali. Naweza kutoa ushuhuda kwamba wako watendaji wengine kwenye mikoa wakisimamiwa na hawa walioko Makao Makuu, mwaka huu tumekuwa na mvua nydingi, wako wataalam walikesha kwenye madaraja, nawapongeza sana kwa sababu ni uzalendo, waliona ni muhimu sana tuwatumikie Watanzania ili tuhakikishe wananchi hawa wanakwenda kwenye shughuli zao za maendeleo popote pale walipokuwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Mwanza au baadhi ya maeneo nataka nitoe mfano maji yameongezeka sana. Ukienda Mkao wa Manyara ukipa ile barabara kutoka pale Mogitu kwenda Haydom nilikwenda juzi utaona kuna mabwawa makubwa yamezaliwa ambayo hatutegemei kwamba yatakauka. Tumelazimika kwenda kufanya matengenezo ya dharura, unakuwa na kilometra 6, kilometra 9 kukwepa sehemu ambayo maji yamekuja kutokana na mvua nydingi lakini watendaji hawa hata bila kusubiri fedha kutokana na fedha tulizonazo kwa utaratibu uliokuwepo kwa usimamizi wa Makatibu Wakuu tumeenda kujenga barabara kwa dharura ili kuhakikisha Watanzania hawa wanapita. Kwa hiyo, nataka nishuhudie kwamba kuna kazi kubwa imefanyika. (*Makoff*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Singida kwa shemeji yangu, naona yuko hapa Mheshimiwa Mwigulu, ukiona ile barabara inaenda Mgungila kule kuna kilometra nzima ya lami imemezwa na maji na hatutegemei maji haya yataondoka lakini wenzetu wa *TANROADS* wameenda kutengeneza barabara mbadala ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao. Yako maeneo mengi nilitaka

nitumie nafasi hii kuwashukuru sana watendaji hawa kwa sababu umahiri wetu hauwezi kutokea kama watendaji hawa hawafanyi kazi na kutekeleza majukumu yao vizuri. Kwa hiyo, nawapongeza na kuwashaukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka nizungumzie mambo mawili tu; naamini mengi waliyoyazungumza Waheshimiwa Wabunge tutayajibu kwa maandishi lakini nilitaka nizungumze hili la *TEMESA*. *TEMESA* inalo jukumu la kufanya matengenezo ya magari na mitambo, kusimamia usimikaji wa umeme, kusimamia *ICT*na vivuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ilizungumzwa hapa kuhusu shughuli za utengenezaji wa magari kwamba kumekuwa na gharama kubwa. Nataka niseme tu kwamba kuna hatua nzuri ambazo tumezichukua kama Wizara kwa maana ya kuanzisha karakana mpya katika mikoa milpya Ikiwemo Mikoa ya Songwe, Geita na Katavi, hivyo tumeendelea kuboresha huduma. Pia tumeanzisha karakana katika maeneo ya Wilaya ambayo ni mbali na Makao Makuu ya Mikoa. Tumeanzisha karakana kule Ifakara, Same na Kahama na tunaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kama Wizara tumenunua hizi *mobile shop* kwa maana ya kupeleka huduma maeneo ya mbali. Tunayo magari maalum ambayo yana mitambo na vifaa maalum, sasa tunaweza tukahamisha mitambo ile na wataalam wale wakaenda sehemu ambayo tunaweza kwenda kuhudumia ili kupunguza zile gharama ambazo zilikuwa zinatokana na umbali wa watu wetu kwenda kupata huduma. Kwa maana hiyo, nataka niseme tu kwamba yako mambo mengi ambayo tunaendelea kuyafanya ili kuboresha huduma kutockana na majukumu ambayo yako chini ya *TEMESA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho nizungumze jambo ambalo Mheshimiwa Silinde alilizungumza hapa. Kwanza naamini kwamba wananchi wa Mombasa wanatambua kazi nzuri iliyo fanywa na Serikali kwenda kuwajenjea daraja kubwa la Mombasa. Miaka iliyo pita mimi nimefika Mombasa

historia niliyokuwa napewa watu wengi walipoteza maisha, mali nydingi zilipotea katika daraja hili sasa tumekamilisha daraja hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naijuliza kama siyo maono ya Mheshimiwa Rais wetu ya kujenga madaraja makubwa haya ikiwepo daraja la Momba na madaraja mengine ambayo yametajwa katika hotuba wakati wa mvua hizi nydingi hali ingekuwaje? Kwa hiyo, unaona kabisa Mheshimiwa Rais wetu kwa maono yake tumeenda tumejenga madaraja makubwa na yamekuwa msaada mkubwa kipindi hiki cha mvua. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Silinde wananchi wa Momba wanafahamu namna Serikali hii ilivyowatendea vyema. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na hili, alikuwa anahitaji sisi kama Wizara tuseme namna gani Wizara yetu imeleta *impact* kwenye maendeleo. Nataka nimwambie kwamba asome tu taarifa za *NBS*, Ofisi ya Takwimu ataona anachoulizia. Kwa mfano, mwaka 2019, Sekta ya Ujenzi imechangia ukuaji wa uchumi kwa asilimia 13.2, ukisoma kwenye taarifa imeelezwa wazi. Kwa hiyo, akienda kule ataona ni namna gani Wizara imechangia katika suala analolizungumzia kwa sababu yako mambo mengine ambayo ni *direct*, mengine siyo *direct*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya Ujenzi imesaidia kwenye viwanda, biashara, kilimo, huduma za jamii hata kwenye kodi maana wakandarasi walivyolipwa wamelipa kodi. Pia imesaidia kwenye utalii, ajira za moja kwa moja, mama lishe, baba lishe na watu wengine. Angekuwa hapa ningewambia wakati mwingine anahitaji kujifunza kidogo ili tumuoneshe namna nzuri ya kupata data aone ni namna gani Sekta hii ya Ujenzi imechangia katika uchumi wa nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja asilimia 100. Ahsante sana. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (mtoa hoja) ili ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye kwa rehema zake nyingi Bunge lako Tukufu limejadili hoja niliyoiwasilisha kwa upana na kwa umakini kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, nitumie fursa hii pia kuwashukuru sana wapiga kura wangu wa Jimbo la Katavi kwa juhudhi na ushirikiano wao walionipa katika kipindi chote cha miaka mitano cha uongozi wangu katika Jimbo la Katavi. Jitihada hizo na ushirikiano huo hakika umetuwezesha kwa pamoja kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa ajili ya kuboresha maisha yetu kijamii na kiuchumi. Nawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini na kwa maelekezo na miongozo yake ambayo imenisadia sana katika kipindi chote cha utumishi wangu. Tangu aliponiteua na kunipa dhamana ya uongozi katika Serikali ya Awamu ya Tano nikiwa Naibu Waziri na Waziri wa Maji na mpaka sasa Waziri katika Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Aidha, nitumie fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maelekezo na miongozo yake ambayo imenisadia wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika kipindi chote cha miaka mitano. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake anaoendelea kutuonesha wasaidizi wake katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku Bungeni, namshukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nitumie fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa ushirikiano mlionipatia kwa kipindi chote wakati wa utekelezaji wa majukumu yangu mbalimbali ya Serikali hapa Bungeni.

Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wao wa dhati walionipatia kuititia Wizara nilizozihudumia katika kipindi cha miaka mitano nikiwa Naibu Waziri na hivi sasa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwashukuru pia Wenyeviti na wajumbe wa Kamati zote za Bunge kwa kufanya kazi karibu na Wizara yangu. Kipekee nimshukuru Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Selamani Moshi Kakoso pamoja na wajumbe wake ambao wameongoza Wizara yangu vizuri katika utekelezaji wa miradi ambayo imenisaidia kwenye Sekta ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Naahidi kwamba Wizara itazingatia masuala yote yaliyoshauriwa na Kamati hiyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Elias John Kwandikwa, Mbunge na Naibu Waziri (Sekta ya Ujenzi); Mheshimiwa Mwandisi Atashasta Nditiye, Mbunge Naibu Waziri (Uchukuzi na Mawasiliano), Makatibu Wakuu, Mbunifu Majengo Elius Asangalwisye Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Mwandisi Dkt. Leonard Madaraka Chamuriho (Uchukuzi) pamoja na Dkt. Maria Leticia Sasabo aliyekuwa Katibu Mkuu wa Sekta ya Mawasiliano ambaye amestaafu lakini pia Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Jim Yohaz. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Idara, Vitengo, Wenyeviti wa Bodii zilizo chini ya Wizara, Viongozi wa Taasisi na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano mzuri ambao wamenipatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushukuru na kutambua michango ya washirika mbalimbali wa maendeleo katika utekelezaji wa programu na mipango mbalimbali ya Wizara. Washirika hao ni kama nilivyowataja kwenye hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kuwatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika bajeti yangu. Waheshimiwa Wabunge wanne walichangia wakati wa majadiliano ya mjadala wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu; Waheshimiwa 28 wamechangia katika bajeti hii inayoendelea, hatukupata mchango wa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi punde Waheshimiwa Naibu Mawaziri wa Wizara yangu wamejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia maeneo yao ya kisekta. Nawashukuru sana kwa jinsi ambavyo wamejibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nihitimishe kwa kujibu hoja za kisekta pamoja na kutoa ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizojitekeza kwa ufupi sana. Kwa ujumla wake tu Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia uharibifu wa barabaraa ambaao umetokana na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha ambazo zilianza tarehe 1 Oktoba, 2019.

Waheshimiwa Wabunge ni kwamba kweli barabara zimeharibika na mvua bado inaendelea kunyesha lakini Wizara yangu pamoja na Serikali tuko makini, tunasubiri mvua hizi ziishe na tathmini inaendelea kufanyika ili tuweze kupata fedha kwa ajili ya kuzirudisha kwenye hali yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nishukuru sana michango ya Waheshimiwa Wabunge ambaao wamesema tusije tukaathiri bajeti tuliyonayo kwa kukata kule kwenye bajeti na kwenda kufanya matengenezo hayo. Niwashukuru sana, tutakuwa makini kwa kushirkiana na Wizara ya Fedha tutajitahidi kuhakikisha kwamba tunarejesha huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu uliotolewa na Mheshimiwa Selemani Kakoso nimeona amezungumzia utoaji wa fedha za maendeleo. Nishukuru sana Hazina wametoa zaidi ya asilimia 82 ya fedha za maendeleo hasa katika barabara. Pia wamegusa ununuzi wa mabehewa na vichwa vyta treni kwa

ajili ya *SGR*. Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za ununuzi wa *rolling stock*. Aidha, Fedha zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2020 na 2021. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wamezungumzia wadau wa bandari kukutana. Wizara inaanadaa kikao cha wadau wote wa bandari kitakachofanyika mwishoni wa mwezi Mei, 2020. Hata hivyo, tulishaanza kukutana kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge hasa waliotoka maeneo yenye maziwa wamezungumzia ukarabati wa meli na hasa Ziwa Tanganyika. Tumetenga bajeti katika mwaka huu wa fedha ili tuhakikishe pamoja na kujenga meli mpya ya mizigo na abiria lakini lazima tukarabati MV Mwongozo pamoja na MV Liemba ambayo imekuwepo muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo haya, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021 yenye jumla ya shilingi 4,784,874,417,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja yetu imeungwa mkono. Kwa hiyo, kwa utaratibu wetu nimeona hapa Waheshimiwa Wabunge wameshapiga kura na kwa idadi ya kura zilizopigwa Wabunge wengi wameikubali na kuipitisha bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kwa hivyo, nitangaze kwamba Bunge limeshakubali na kuipitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi,  
Uchukuzi na Mawasiliano kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/  
2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

### **MATUMIZI YA KAWAIDA**

Fungu 62 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Uchukuzi.....Sh.90,710,109,000

Fungu 68 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Mawasiliano..... Sh. 4,654,466,000

Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Ujenzi.....Sh. 38,774,425,000

### **MIPANGO YA MAENDELEO**

Fungu 62 – Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Uchukuzi.....Sh.3,062,148,636,000

Fungu 68 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Mawasiliano..... Sh.11,000,000,000

Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na  
Mawasiliano - Ujenzi.....Sh.1,577,586,781,000

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba  
yenu, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa  
Waziri, Naibu Mawaziri na watendaji wao kwa kazi nzuri  
wanayoifanya kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wengi  
wamepongeza hapa maeneo yao mmeyapitia, pia Kamati  
yetu imeeleza mambo makubwa ambayo wameyaona na  
miradi mikubwa ambayo wameiona pia wametoa  
mapendekezo kwa niaba ya Bunge.

Niwashukuru sana Kamati yetu kwa kazi nzuri  
mliyoifanya kutembelea miradi hiyo pia kutoa  
mapendekezo mbalimbali ambayo Mheshimiwa Waziri na  
wasaidizi wake wameahidi kuyafanya kazi. Kwa hiyo,  
tunawashukuru sana kwa kazi hiyo na Waheshimiwa

Wabunge wote mliochangia mawazo yenu pia naamini yatawasaidia upande wa Serikali maadam hii bajeti imepitishwa basi wataweza kuyafanya kazi.

Waheshimiwa Wabunge, nina mambo matatu kwa haraka, moja ni mwongozo ulikuwa umeombwa na Mheshimiwa Amina Mollel kuhusu jambo ambalo yeye ameliona huko kwenye mitandao mimi sijalionia lakini anaeleza kwamba yuko mtu anayetuhumu Wabunge wa CCM kwamba ni wezi. Pia ameleeza kwamba huyu mtu ambaye taarifa zake sasa anazo Mheshimiwa Amina Mollel pia amemkashifu Mheshimiwa Rais.

Sasa hili la kutuhumu Bunge ama Wabunge wa CCM Bunge lina utaratibu wake, halitahitaji kutolewa mwongozo hapa. Taarifa hiyo nimwombe Mheshimiwa Amina Mollel alipeleke Ofisi ya Spika ili iwe rahisi kulfanyia kazi kwa kadri uzito wake utakavyoonekana ili tutumie Kanuni zetu za Bunge kushughulika na huyo ambaye anachafua Wabunge wa CCM. (*Makof!*)

Jambo lingine la kuhusu kumkashifu Mheshimiwa Rais, nadhani vyombo vyaya ulinzi na usalama vitakuwepo huko nje. Kwa hiyo, vimtafute huyo mtu na ashtakiwe kwa makosa hayo ya jinai kama ambavyo amefanya hilo kosa.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ni kuhusu mambo mengi yamezungumzwa hapa ndani lakini nalazimika kutoa ufanuzi kidogo kuhusu vifo vyaya Waheshimiwa Wabunge vilivyotokea hapa karibuni na watu kujaribu kuhuishwa ugonjwa uliopo sasa kwa maana ya *Corona* na kwamba hawa Wabunge kwamba wamekuwa pengine na huo ugonjwa ama wakiashiria kwamba wamekuwa na ugonjwa fulani.

Waheshimiwa Wabunge, sisi sote ni viongozi tunafahamu ugonjwa wa mtu ni siri yake yeye peke yake akitaka sana ni yeye na daktari. Sasa hatuwezi kufika mahali tukaanza kulazimishana kwamba mtu aseme ugonjwa wake ni nini ama mtu mwingine amsemee mtu

mwagine kwamba amekufa na ugonjwa gani. Wale walioumwa hata na hivi virusi wametangaza wao wenyehe hakuna mahali Serikali inasema nani amekufa na ugonjwa gani kwa sababu kila mtu ana ugonjwa wake na ugonjwa ni siri ya mtu, kama ameama kusema hilo ni suala lake, kama hakusema mpaka mauti imechukua ameondoka nayo siri yake yeye na daktari, haimuhusu mtu mwagine.

Kwa hiyo, hakuna mahali tutafika kama Bunge kuanza kutangazia Wabunge fulani amekufa na kifo fulani, hilo halitowezekana. Kwa hiyo, likae hivyo, nadhani tutakuwa tumefuata miongozo yote ambayo inawataka wenzetu kwenye eneo la afya kufanya hivyo na sisi tusingetaka kuingia kwenye eneo hilo la kujifanya sisi watangazaji wa watu wamefariki na kitu gani ama mtu fulani anaumwa ugonjwa fulani, kila mtu atasema yeye akiona inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, lingine kwa ufupi pia ni vizuri Waheshimiwa Wabunge kufuatilia kwa makini sana hasa Kiongozi wetu wa nchi anapozungumza. Unapokuwa umechukua mambo yaliyozungumzwa nje ya muktadha unapelekea wewe wenyehe kwanza kujikosesha heshima na pia kumkosea heshima Kiongozi wetu Mkuu wa nchi.

Kwa hiyo, tusikilize kwa makini yale anayoagiza na tufuate hayo, tusijifanye kila mtu sasa ni mwamba kwenye eneo lake na yeye basi anaweza kuwa Rais, hapana.

Waheshimiwa Wabunge, nchi ina Rais mmoja na anavyotoa maelekezo yeye ndiye Kiongozi wa nchi hii na amepewa dhamana kwa kipindi hiki chote yeye peke yake. Hakuna mtu mwagine sehemu nyininge anaweza na yeye akajifanya ni Rais akaanza kutoa maelekezo yake, akishasema Rais ameshasema na amemaliza mpaka atakapobadilisha yeye. Nafikiri sisi kama Wabunge tunafahamu anachozungumza Mheshimiwa Rais ni sheria. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho lakini si kwa umuhimu, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Lameck Mwigulu Nchemba kwa uteuzi alioupara. Sisi tunakupongeza sana kwa yote ambayo umeyafanya lakini tunakuamini pia kama ambavyo Mheshimiwa Rais amekuamini na sisi tunakupokea na tunaamini kwamba tutaendelea kushirikiana katika hiki kipindi kilichobaki, nakupongeza sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa nane mchana.

*(Saa 12.21 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 5 Mei, 2020 Saa Nane Kamili Mchana)*